# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 9 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. ROSE C. TWEVE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu tuendelee.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 165

**Uanzishaji wa Wilaya ya Bukene**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI (K.n.y. MHE. SELEMANI J. ZEDI)** aliuliza:-

Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Tabora *(RCC)* mwaka 2014 ilikubali ombi la wananchi wa Wilaya ya Nzega la kutaka kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Bukene hasa ikizingatiwa kuwa Jimbo la Bukene lina vigezo vyote vinavyohitajika kwa uanzishwaji wa Wilaya na ombi hili lilipelekwa TAMISEMI ili kufanyiwa kazi.

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa maamuzi ya *RCC* ya kuomba uanzishwaji wa Wilaya mpya ya Bukene?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Tabora uliwasilisha maombi ya kuanzishwa kwa Wilaya ya Bukene baada ya kupitishwa na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kilichofanyika tarehe 29 Mei, 2015. Kikao hicho kilijadili pendekezo la kuanzisha Mkoa mpya wa Ngega sambamba na kuanzisha Wilaya mpya ya Bukene. Aidha, tarehe 26 Februari, 2016 Katibu Tawala Mkoa wa Tabora aliandikiwa barua yenye Kumb. Na. BD. 310/365/31 ya tarehe 26/02/2016 ili kufanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa katika maombi hayo. Tayari mkoa umefanyia kazi upungufu huo na kuwasilisha taarifa kwa barua ya tarehe 11 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kina unafanyika sambamba na maombi ya maeneo mengine. Aidha, timu ya wataalam imefanya zoezi kubwa la uhakiki wa vigezo na taratibu *(physical verification)* kwa maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu mapendekezo hayo kwa kuzingatia Ibara ya 2(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Napenda sasa katika majibu yake angeweza kufafanua kwa jinsi ambavyo barua ilivyokuwa imeelekeza, kwa sababu

tunavyojua katika kikao chetu cha *RCC* pamoja na uanzishwaji wa Wilaya mpya ya Bukene pia kulikuwa na maombi ya Wilaya mpya ya Manonga.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria MheshimiwaWaziri atuambie; je, mchakato huo utaenda sambamba pamoja lakini turahisishiwe katika kuanzishiwa Mkoa wetu wa Tabora kwa sababu Mkoa wa Tabora ni mkubwa katika mikoa yote iliyobakia kwa sasa, una kilometa zaidi ya 75,000 na tumeshaona baadhi ya mikoa mingine imegawanywa kama Mkoa wa Mbeya, Arusha na Shinyanga. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri atuhakikishie uharakishaji wa kugawa huu mkoa ili kurahisisha kupeleka maendeleo kwa wananchi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, kwa sababu maombi haya yalivyokuja, lengo kubwa lilikuwa ni kuanzisha Mkoa mpya wa Nzega ambao uliainisha mkoa huo utakuwa na Wilaya nne. Ilipendekezwa kwamba kutakuwa na Wilaya hii mpya ya Bukene, Wilaya kongwe ya Nzega, Wilaya ya Igunga, halikadhalika na Wilaya mpya ya Manonga. Kwa hiyo, huo ndiyo mchakato wenyewe ulivyokuwa katika pendekezo lile. Ndiyo maana nimesema kwamba kulikuwa na mapungufu kadhaa, baadaye sasa ofisi yetu ikapeleka mrejesho kwa Katibu Tawala wa Mkoa na wameshafanyia kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema kwamba *physical verification* imeshaenda kufanyika, sasa kilichobakia ni kwamba iko katika mchakato wa kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais naye atafanya maamuzi, lakini tukiwa na angalizo kwamba na Mheshimiwa Rais alifika pale Tabora, kuna mazungumzo aliyazungumza. Kwa hiyo, yeye mwenyewe atapima ataona nini kifanyike kuhakikisha kwamba jambo linafanikiwa kwa kadri yeye mwenyewe atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya hayo yote ili mradi kufanya jambo hili kwa matakwa yenu na Mheshimiwa Rais aweze kufanya maamuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha na Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, kwa tatizo lililoko Nzega huko ni sawasawa na tatizo lililoko Serengeti. Sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya ya Serengeti kwa ukubwa wake; je, ina-*qualify* kuigawa kuwa Wilaya mbili?

**MWENYEKITI:** Naona swali lingine hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri kama unaweza, basi kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *qualification* ya Wilaya inategemea vigezo kadhaa ikiwepo *population* ya watu, ikiwepo *area size* na mambo mengine. Kwa hiyo, kwa sababu ombi hilo hatuna rasmi katika ofisi yetu, maana ingekuwepo limefika, tungeenda kufanya uhakiki kuangalia, je, vile vigezo vyote vya kuanzisha Wilaya mpya vinakidhi au vipi? Ndiyo tungeweza kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hili naomba niliache kwa wananchi wa Serengeti wenyewe watafanya maamuzi kwa kadri watakavyoona inafaa na sisi kwa mujibu wa ofisi yetu, itakwenda kufanya tathmini kama hilo litkuja kuangalia kama nini kinafanyika. Ila tufahamu wazi kwamba Serengeti japokuwa eneo ni kubwa lakini idadi ya watu ni wachache, kwa sababu eneo kubwa sana liko katika sehemu ya hifadhi. Kwa hiyo, mambo hayo yote tutayazingatia. Lengo kubwa ni mustakabali wa nchi yetu iwe vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Wilaya ya Bunda ni Wilaya

kubwa na ina majimbo matatu ya uchaguzi, ikiwemo Bunda, Bunda Mjini na Mwibara; na kwa kuwa tayari Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, miaka saba sasa iliyopita tulishaamua Mwibara iwe Halmashauri ya Wilaya lakini mpaka leo Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia mambo ya uchambuzi na vigezo; je, ni lini mambo ya uchambuzi na vigezo vitafikiwa ili Jimbo la Mwibara sasa miaka saba tangu wananchi wameomba iweze kupatiwa Halmashauri yake?

**MWENYEKITI:** Naona leo maswali yote ya nyongeza ni tofauti na maswali ya msingi. Mheshimiwa Naibu naomba kama unaweza jibu tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kangi Lugola amehamisha goli, lakini hakuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Mheshimiwa Kangi alivyosema Jimbo la Mwibara, kwanza anafahamu kwamba zamani kwanza walikuwa na majimbo mawili pale, lakini walikuwa na Halmashauri moja, baadaye wakagawanyika tukapata majimbo matatu na Halmashauri mbili; Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Bunda Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyokuwepo ni kwamba haya majimbo mawili; Jimbo la Mwibara na Jimbo la Bunda Vijijini ukiangalia jiografia yake, haiko sawasawa. Unatoka Jimbo la Mheshimiwa Boniphace Getere, unaenda katika Jimbo la Mheshimiwa Bulaya, halafu unaenda tena Jimbo la Mheshimiwa Kangi Lugola.

Mwenyekiti Mwenyekiti, haya majimbo mawili ambayo ni kwa upande mmoja Magharibi na mmoja Mashariki, katikati kuna Jimbo lingine lakini haya majimbo mawili ni Halmashauri moja. Hili sasa tuseme kwamba inawezekana kuna mapungufu yaliyofanyika kule mlipokuwa mnafanya maamuzi kwamba Jimbo hili ligawanyike vipi, ndiyo changamoto kubwa iliyokuwepo hapo. Kwa hiyo, kikubwa zaidi tuseme kwamba mchakato ule ulikwenda lakini tulipata majimbo haya mawili ya Mji na Bunda Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaelekeza, pale itakapoonekana kuna mahitaji ya ziada hasa katika maeneo yale inaonekana kuhudumia Halmashauri ile katika Majimbo mawili ambayo yako sehemu mbili tofauti ni changamoto kubwa, basi mtaleta maombi haya ili tujadili kwa pamoja nini kifanyike. Lengo kubwa ni kuwapatia wananchi huduma ya karibu katika maeneo yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante Naibu Waziri. Tuendelee na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, sasa aulize swali lake.

Na. 166

**Kukwama kwa Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia - Madaba**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza:-

Miradi ya maji inayojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia katika vijiji vya Lilondo na Maweso imekwama kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, licha ya miradi hiyo kutumia fedha nyingi na nguvu kubwa za wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha miradi hiyo?

(b) Je, ni lini miradi hiyo itakamilika ili kutatua kero za maji kwa wananchi wa vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji ya Maweso na Lilondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ni kati ya miradi iliyoibuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea

katika mpango wa vijiji kumi kwa kila Halmashauri chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Aidha, utekelezaji wa miradi hii imekuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea kutokana na kuwa illibuliwa na kuanza kutekelezwa wakati Madaba ikiwa ni sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Maweso kwa mujibu wa mkataba una gharama ya shilingi 546,792,163.2. Jumla ya shilingi 109,771,259 zimetumika kumlipa mkandarasi. Vilevile, mradi wa Lilondo kwa mujibu wa mkataba una gharama ya shilingi 1,048,875,254 na jumla ya shilingi 224, 491,637.25 zimetumika kumlipa mkandarasi. Hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Songea imewasilisha hati ya madai ya wakandarasi wa miradi hiyo na Wizara imetuma jumla ya shilingi 101,444,072 ili kuwalipa wakandarasi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima kuu ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Hivyo, Serikali kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa itahakikisha inapeleka fedha kwa kadri zinavyopatikana katika miradi hii kulingana na hati za madai zilizohakikiwa na Halmashauri, Sekretarieti ya Mkoa na Wizara ili iweze kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Madaba sasa ipo kisheria na tayari kumekuwa na mgawanyo wa mali na miradi mbalimbali kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na Songea; na kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Songea ipo mbali sana kijiografia na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba; kwa nini sasa miradi isikabidhiwe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ili iweze kusimamiwa kwa ukaribu na kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa vile yapo mabomba ambayo yalinunuliwa kwa kupitia mradi huu na mkandarasi na kwa miaka zaidi ya miwili yapo nje, yapo juani, yanazidi kuwakiwa jua na yanapoteza ubora; kwa nini sasa Wizara isimshauri mkandarasi kwa kushirikiana na Halmashauri ili yale mabomba sasa yaweze kufukiwa katika njia ambazo zimekusudiwa na mradi huu ili miradi midogo midogo ya maji ambayo wananchi wameianzisha na wanaiendeleza iweze pia kuingia kwenye mtandao huu na kuanza kutoa huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, miradi hii iliibuliwa ikiwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea na sasa hivi Madaba sasa ni Halmashauri. Anasema, kama vitu vingi vimeshagawiwa tayari, kwa nini ile miradi ibakie kuwa Songea? Hatuna tatizo na hilo na halitakuwa la kwanza. Kuna Halmashauri nyingi mpya. Kwa hiyo, kama wameshakamilika, basi utuletee barua kuomba hilo na Wizara itakubaliana na hiyo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba kuna mabomba ambayo yameshanunuliwa na mkandarasi na yanaungua na jua; kwa nini yasifukiwe ili wananchi wapate maji?

Mheshimiwa Mhagama, kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 ulitengewa zaidi ya shilingi milioni 800 ambayo matumizi yake inapanga Halmashauri yenyewe. Naomba tu kushauri kwamba Halmashauri yako basi watumie hizo fedha kwa sababu mnazo ili waweze; ama kwa kutumia nguvu ya wananchi ama huyo mkandarasi basi, kwa nini asiyafukie kwa sasa na hela inatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Mheshimiwa tuwasiliane ili tuweze kulijadili hili kwa pamoja, mabomba haya yafukiwe haraka wananchi wapate huduma ya maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Bilago, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Mhagama, matatizo yaliyoko Madaba yanafanana moja kwa moja na matztizo yaliyoko Jimbo la Ndanda. Kwenye bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri utakumbuka zilitengwa fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kupeleka *MANAWASA* ili kununua viunganishi pamoja na mabomba ambayo yangeweza kupeleka maji katika kata za Chikukwe, kijiji cha Maparagwe pamoja na kijiji cha Chikunja. Wananchi walikubali watajitolea nguvu zao, lakini mpaka sasa hivi mabomba yale hayajakwenda.

Je, unaweza kutueleza ni lini Serikali itapeleka pesa hiyo, wakati tumebakisha siku chache tu kumaliza mwaka wa bajeti? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa kwamba Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Mbwinji pale Masasi, kupitia Mamlaka ya *MANAWASA.* Juzi juzi hapa Mheshimiwa Mbunge tuliwasiliana, walileta andiko na andiko hilo tayari limesapitishwa ili *MANAWASA* waweze kusaini mkataba kwa ajili ya *procurement* ya hivyo vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kwa maana ya Wizara imeshaidhinisha kwa hiyo, ni kazi ya Mkurugenzi wako sasa kusaini mkataba na mkandarasi yule ambaye mmempa kazi. Ile kazi ni ya kununua vifaa; vifaa vile ni kitu cha wiki mbili vitakuwa vimeshanunuliwa na mkishamaliza, kwa utaratibu wetu, mnaleta *certificate* tunatoa hela, mkandarasi analipwa. Kwa hiyo, kama *MANAWASA* watafanya haraka, hela hiyo lazima mtaipata katika huu mwaka wa fedha.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililoko Madaba linafanana sana na tatizo lililoko Jimbo la Buyungu. Wilaya ya Kakonko ina miradi ya maji ya Mradi wa *World Bank* katika vijiji vya Muhange, Katanga na Nyagwijima kata ya Mgunzu. Miradi ile inaendelea kusuasua na wananchi hawanufaiki na miradi ile wakati fedha zilitolewa na fedha hizo ni za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Kauli ya Serikali ni lini miradi hiyo itakamilishwa ili wananchi wa Muhange, Katanga na Nyagwijima waweze kupata maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bilago mwenyewe ni shahidi, Serikali imetoa fedha. Utekelezaji wa miradi unafanywa na Halmashauri. Katika hiyo Halmashauri, Mheshimiwa Mbunge wewe ni Diwani kule, hebu naomba tusaidiane kusimamia hao Wakandarasi waweze kukamilisha hii miradi. Tatizo la hela halipo, hela tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Halmashauri ya Kakonko na sisi Madiwani na Mheshimiwa Mbunge, tuwasimamie Wakandarasi ipasavyo ili miradi iweze kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo cha mabondeni ni kilimo ambacho ni cha asili na kimezoeleka na wananchi, hasa wa Mikoa ya Iringa, Njombe, Songea na kinajulikana kwa jina la ukulima wa vinyungu, sasa hivi

kimezuiwa kutokana na kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji; na kwa kuwa, kilimo hicho ndiyo kimekuwa kikitumika kwa muda mrefu.

Je, Serikali ili kuwanufaisha wananchi wa vijiji vya Lukani, Kihesa Mgagao, Lulanzi, Idete, Kimala, Boma la Ng'ombe, wameweka mikakati gani mbadala kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanaendelea kulima kilimo kisasa? Imejipangia mikakati gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa lazima tukubaliane kwamba ili tuwe na maji endelevu ya kuweza kuwatosheleza Watanzania ni lazima tutunze vyanzo vya maji. Katika utunzaji wa vyanzo vya maji, kuna watu ambao kwa miaka mingi kama anavyosema wamekuwa wanalima kilimo cha vinyungu; maana yake wanalima kwenye vyanzo vya maji. Sasa mikakati ya kuweza kuwatafutia shughuli mbadala ni lazima muwe shirikishi kati ya Halmashauri na Serikali. Haiwezi kuwa Serikali tu inawapelekea kwamba mtafanya hiki, kwa hiyo, ni lazima iwe shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kukaa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo tuweze kuona shughuli nyingine ambayo wanaweza wakafanya nyingine tofauti na uharibifu wa vyanzo vya maji. Kulingana na sheria yetu, ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji, haturuhusiwi kufanya kazi yoyote, kufuga mifugo au kulima ili tuwe na maji na rasilimali ya kutosha kuwapelekea Watanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwenye bajeti ya mwaka huu hakutupatia pesa kwa ajili ya mradi mkubwa ambao uko kwenye usanifu. Naomba awaeleze wananchi wa Jimbo la Kyerwa, mradi huu utakapokuwa umekamilika kwa ajili ya usanifu.

Je, yuko tayari kuhakikisha anawapatia wananchi wa Jimbo la Kyerwa maji safi na salama kwa sababu maji ni tatizo Wilaya ya Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Mheshimiwa Bilakwate ilipata shilingi milioni 200 na fedha hizo tayari zimeshatumika kuboresha chanzo cha maji kwenye kijiji kimoja eneo la mjini na tayari maji yanapatikana. Pia, kupitia vyanzo vingine vya Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji, tayari tumesaini mkataba wa usanifu ambao ukikamilika, umelenga kuvipatia vijiji zaidi 57 maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kesho tunawasilisha bajeti kwenye Bunge hili na katika bajeti hiyo tayari utaona wewe mwenyewe ni nini tumetenga ambacho kitahakikisha kwamba baada ya kukamilisha mradi wa usanifu, basi ujenzi utaanza bila wasiwasi wa aina yoyote.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 167

**Mradi wa Maji Ng'apa – Manispaa ya Lindi**

**MHE. HASSANI S. KAUNJE** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Ng'apa ambao upo Manispaa ya Lindi ulikusudiwa kuwahudumia wakazi wa Lindi Mjini tangu mwezi Mei, 2015, lakini mpaka sasa mradi huo haujakamilika.

Je, ni lini mradi huo utakamilishwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Ng'apa unagharamiwa na Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya kupitia Benki ya Maendeleo ya *KfW* kwa gharama ya *Euro* milioni 11.56. Ujenzi wa mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi ajulikanaye kwa jina la *Overseas Infrastructure Alliance* kutoka nchini India. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ufungaji wa pampu katika visima ambavyo vimeshachimbwa na vina uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 7,500 kwa siku; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ujenzi wa matenki mawili ya kuhifadhi maji; ujenzi wa nyumba ya wafanyakazi, karakana, ghala, nyumba ya walinzi; ujenzi wa mabwawa ya kusafisha maji na ununuzi wa gari moja la majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mradi huu ulitegemewa kukamilika mwezi Mei, 2015. Sababu kuu zilizosababisha kutokamilika kwa mradi huu ni kutolipwa kwa wakati kwa fidia na kasi ndogo ya mkandarasi katika ujenzi wa mradi. Hadi sasa Serikali imefanikiwa kuwalipa waathirika wote wa mradi waliokuwa wamefanyiwa tathmini. Kwa upande wa mkandarasi, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kulingana na masharti ya mkataba, ikiwemo kumkata fedha za adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua mbalimbali zilizochukuliwa zimewezesha utekelezaji wa mradi kufikia asilimia 85 kwa sasa na mradi unategemea kukamilika mwezi Julai, 2017.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. HASSANI S. KAUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naibu Waziri yuko tayari kuwaambia wananchi wa

Lindi kumwambia Mbunge wao na Mheshimiwa Rais kwamba ahadi ya Mheshimiwa Waziri wake ya kwamba mradi huu utakamilika tarehe 3 Julai, 2017 kwamba, itatekelezwa kama walivyoahidi? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri awe tayari kuweza kunifikishia salamu zangu za pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na yeye mwenyewe kwa kuweza kukamilisha mradi mwingine pacha na huo wa kijiji cha Chikondi. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kunifikishia salamu zangu hizo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge, ahadi ya Mheshimiwa Waziri itatekelezwa na nikwambie tu kwamba ni siku kumi tu zimepita nimeenda Lindi, nimeenda kukagua ule mradi, nimekuta vifaa vyote vilivyokuwa vinatakiwa kwenye mradi vimewasili na tayari kuna kundi kubwa ambalo liko pale linafunga na mabomba yaliyobaki yanakamilishwa na eneo ambalo kutokana na mvua kubwa mabomba yalifumuliwa, linarekebishwa. Kwa hiyo, uwe na uhakika kabisa kwamba maji yatatoka na inawezekana hiyo tarehe 3 au kabla ya tarehe 3 Julai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge wamecheka, hawakujua wewe una maana gani? Ni kwamba baada ya ziara ya Mheshimiwa Rais, tuliamua kuchimba kisima kingine ili kuongeza uwezo wa upatikanaji wa maji Lindi na kisima kile tayari kimekamilika, na mimi mwenyewe nimeenda kukagua juzi. Tumekuwa na matatizo kidogo yaliyokuwa yamejitokeza kuhusiana na ukataji wa huduma ya umeme kwenye mitambo, ambapo jana tumekaa nao kikao; tunatarajia kulikamilisha mapema. Kwa hiyo, Mheshimiwa nikuhakikishie

kwamba huduma ya maji Lindi inafika na Mheshimiwa Waziri yupo humu ndani, ameshasikia salamu zako. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Muda ni mfupi lakini nitawapa wawili tu sasa hivi. Mheshimiwa Willy Qambalo na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mamlaka ya Maji ya Mji wa Karatu *(KARUWASA)* ina kisima kimoja na kisima hicho kimeharibika na ni miezi miwili wananchi hawana huduma ya maji; na Mamlaka hiyo iko katika kundi la Mamlaka Daraja la C ambalo zinapata ruzuku kutoka Serikalini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kuokoa kisima hicho ili wananchi waendelee kupata huduma hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea Karatu na nilikuta kweli kisima hicho kilikuwa kimepata shida ya pampu. Akiba ya fedha niliyoikuta kwenye Mamlaka ya Karatu ilikuwa shilingi milioni tano na tulitoa maelekezo kwamba ashirikiane na Mamlaka ya Arusha ili waweze kum-*support* kupata pampu nyingine. Sasa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu imekuwa ni muda kidogo, naomba tuwasiliane baadaye, nitafanya mawasiliano na Mamlaka ya Arusha kuona wamefikia wapi ili kurudisha ile huduma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tulikubaliana, viko visima vitatu ambavyo tayari vimeshachimbwa na Serikali, tuhakikishe kwamba, kwenye bajeti tunayoitoa tuwekee miundombinu na kuweka pampu ili kuhakikisha wananchi wa Karatu wanapata maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mji mkongwe wa Mbulu ni mji wa zamani. Umekumbwa na tatizo kubwa la maji hivi karibuni, lakini tatizo hili la miradi ya maji kusuasua katika utekelezaji limeikumba Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Serikali mwaka huu ilitenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa maji Mbulu Mjini. Mradi huu hadi sasa utaratibu umeshafanyika wa tenda kwa kupitia Mamlaka ya Maji Mji wa Babati, lakini hakuna hatua iliyofikiwa umebaki mwezi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika Mheshimiwa Naibu Waziri mwenye dhamana, alifika Mbulu akafanya ziara. Mradi wa Maji ulioko katika kijiji cha Moringa Daudi una takribani miaka minne, hadi sasa mradi huo umeshindikana kukamilika na mkandarasi alimdanganya Mheshimiwa Naibu Waziri alipotembelea *site.*

Je, ni hatua gani ichukuliwe kwa mkandarasi wa namna hii ambaye alimdanganya Mheshimiwa Waziri hadi leo ni miezi minne hajakamilisha mradi huo, ambapo aliahidi mbele ya Mheshimiwa Naibu Waziri wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba nijibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa Kanuni. Maana ameuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za mkataba zinashughulikiwa kwa masharti yaliyoko ndani ya mkataba. Kwa hiyo, naomba tuwasiliane mimi na wewe ili tuone huyu mkandarasi ni wapi ambapo ameteleza tuweze kushauri. Kwa sababu mkataba huo umesainiwa na Halmashauri yake, Wizara ya Maji na Umwagiliaji iko tayari kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunashauriana ili kumfanya huyu Mkandarasi aweze kutekeleza miradi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la kutokamilika kwa miradi ya maji kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara linaonekana kuwa sugu na moja ya chanzo chake ni wakandarasi kutokaa *site;* na mfano mzuri Naibu Waziri anajua ni miradi ya maji ya Jimbo langu, maeneo ya Ingawali, Linoha, Nyangamala, Namangale na maeneo mengine; tatizo kubwa ni kwamba hawa Wakandarasi hawakai *site;* wanakwenda mnapokwenda kufanya ziara. Msipoenda na wao wanarudi Dar es Salaam, ndiyo maana miradi hii haikamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni hatua gani mnachukua ambazo zitasaidia hawa wakandarasi wakae *site* ili miradi ikamilike kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea kwenye Jimbo lake na huo mradi mkubwa niliutembelea na siku nilipokuwepo pale ni kweli mkandarasi alikuwepo. Kama kuna hilo tatizo la mkandarasi kutokukaa kwenye eneo la kazi yake na mkataba tunao na vifungu vya mkataba viko ndani ya mkataba, wasiwasi wangu ni kwamba wale wanaosimamia mkataba hawachukui hatua za kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge nitawasiliana nawe ili tumpigie Mkurugenzi simu tumwulize kama hilo linatokea. Nami vifungu navijua kwa sababu nimesimamia mkataba, tumwelekeze kitu cha kufanya.

**MWENYEKITI:** Inatosha. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, sasa aulize swali lake.

Na. 168

**Upatikanaji wa Boti za Polisi**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeimarisha kwa kuweka boti kwa ajili ya *Police Marine* maeneo mengi ya mito, maziwa na hata baharini ili kuzuia au kudhibiti ajali zinapotokea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hiyo katika Mikoa au Wilaya ambazo hazijapata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kupeleka huduma za boti kwa ajili ya Polisi Wanamaji ili kuzuia, kudhibiti ajali kwa awamu katika mikoa yote na Wilaya ambazo hazijapata huduma pale uwezo wa kibajeti utakapoimarika.

Aidha, muda huu ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili huduma hizo ziweze kupatikana, huduma hiyo ya Polisi Wanamaji itatolewa na vituo vya Wanamaji waliopo karibu kwa kufanya doria kwenye maeneo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Khatib Kai, swali la nyongeza.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejengeka dhana ya askari wa KMKM kule Zanzibar kujiona wao peke yao ndio wenye haki ya kufanya doria baharini, jambo ambalo hupelekea askari hawa ambao ni askari *Marine* ambao wamepata mafunzo maalum kujiona wametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka wa askari wa *Police Marine* - Pemba kupata boti ili aweze kufanya doria ya haraka ambayo itaweza kuokoa usalama kwa Pemba lakini kwa Watanzania kwa jumla? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Jimbo langu la Micheweni, raia wema na raia wenye kupenda amani idumu nchi hii wamewahi kushika boti za Kisomali zaidi ya mara mbili; na boti hizi zinapofanyiwa upekuzi zimegundulika na maganda ya risasi.

Je, kwa kuwa askari wa *Marine* Pemba wanasema kila mwezi hutolewa mafuta lita 500 kwa ajili ya doria baharini, utakubaliana na mimi sasa kwamba ni vema *Police Marine* - Pemba kuwa na boti ya doria ili kuweza kuimarisha ulinzi wa baharini, lakini pia kuweza kunusuru usalama wa nchi hii na raia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa *Police Marine* - Pemba Micheweni kuwa na boti yake. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nilizungumza kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Wilaya zote ambazo zinapaswa kuwa na boti, polisi wanapatiwa kadri hali ya kibajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ndiyo azma ya Serikali na pale ambapo bajeti itakapokuwa inaruhusu, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na askari wa KMKM, Jeshi la Polisi kutokana na kutokuwa na vifaa vya kutosha ikiwemo uchache wa boti zilizomo katika maeneo mballimbali nchini, hufanya kazi kwa ushirikiano na vyombo vingine vya usalama nchini ikiwemo Kikosi cha KMKM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme Mheshimiwa Mbunge ana bahati kwamba katika Wilaya yake ajue kwamba Jeshi la Polisi limekosa boti kwa wakati huu, lakini zipo boti za KMKM ambazo zinasaidiana na Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa pamoja kusimamia ulinzi katika upande wa bahari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Suleiman na Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ajali za baharini zimekuwa nyingi sana siku hizi na kadhalika majanga ya baharini *(disasters)* naiuliza Serikali: Je, imejipangaje kwa kujenga vituo karibu na bahari na pia kutumia sayansi ya kileo, yaani kutumia kama *drowns* ili kuweza kubaini haraka sehemu zilizofikwa na mabalaa na kuweza kutoa huduma ya mwanzo haraka sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha usalama katika maeneo ya bahari hasa pale ajali zinapotokea. Ndiyo maana kwa kulitambua hilo, Serikali imeamua kuunda kikosi kazi cha *coast guard* ambapo Jeshi la Polisi ni taasisi mojawapo ambayo imo katika kikasi hicho. Kwa pamoja na mambo mengine, kikosi hicho kinaangalia masuala yote yanayohusu uokoaji pale majanga yanapotokea ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya kisasa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba niiulize swali kwenye swali namba 169 kuhusu Magereza ya Kondoa, samahani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Wilaya ya Mafia imezungukwa na bahari na hakuna *Police Marine* na kuna matishio ya Maharamia wa Kisomali. Je, ni lini sasa Serikali itafikiria uwezekano wa kuleta doria ya *Police Marine* katika Kisiwa cha Mafia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mafia ni kati ya maeneo ambayo tumeyawekea kipaumbele katika kuimarisha usalama katika maeneo ya bahari. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalitambua hilo; na pale ambapo hali ya bajeti itakaporuhusu, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 169

**Mwingiliano wa Gereza na Hospitali ya Mkoa Iringa**

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Gereza la Wilaya ya Iringa ambalo lipo jirani na Hospitali ya Mkoa wa Iringa limekuwa likisababisha usumbufu kwa wananchi wanaotembea kwa miguu hasa nyakati za usiku.

Je, Serikali ina mpango gani kwa kuondoa mwingiliano wa shughuli za kijamii na shughuli za gereza hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamindi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yalikuwepo malalamiko ya wananchi kupata usumbufu wa kuingia na kutoka Hospitali ya Mkoa wa Iringa ambapo barabara ya kuingia inapita mbele ya lango la Gereza la Iringa. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Iringa katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, hasa baada ya kufungwa kwa barabara inayopita mbele ya gereza kuelekea hospitalini kwa watumiaji wa magari ilikutanisha uongozi wa Manispaa ya Mkoa wa Iringa na uongozi wa Jeshi la Magereza mkoani humo na kutoa maangizo yafuatayo:-

Moja, uongozi wa Manispaa ya Iringa kuandaa barabara mbadala itakayotumiwa na wananchi wanaokwenda hospitalini kwa kutumia gari; pili, uongozi wa Manispaa uandae ramani ya ukuta utakaozuia matumizi ya barabara inayopita gerezani kwa kutumia gari. Ukuta huo ulilengwa kuzuia magari kutoka eneo ambalo waenda kwa miguu wangepita bila kuingilia shughuli za gereza; na tatu, baada ya kupatikana ramani, uongozi wa gereza ulitakiwa kujenga ukuta huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza tayari limeshatekeleza maagizo hayo kwa kujenga ukuta unaotenganisha barabara ya watembea kwa miguu wanaokwenda hospitali kwa kutumia eneo la mbele ya gereza ili wasiingiliane na shughuli za gereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeshatekeleza agizo la kujenga barabara mbadala inayotumiwa na wananchi wanaokwenda

hospitalini na magari. Hata hivyo, pamoja na kujengwa kwa barabara mbadala, gereza limeendelea kuruhusu magari yanayokwenda hospitalini kutumia barabara hiyo mbele ya gereza kwa wakati wa dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamwindi, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. *Issue* siyo kujenga ukuta kuzuia mwingiliano kati ya wananchi wanaokwenda hospitali na magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao vya *RCC* Mkoa wa Iringa, makubaliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ilikuwa kupatiwa eneo mbadala ili Hospitali ya Mkoa wa Iringa ambayo sasa ni Hospitali ya Rufaa iweze kupanuliwa. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ilitekeleza agizo la vikao vya *RCC,* Magereza walipewa eneo mbadala ambalo liko katika eneo la Mlolo na Serikali kuanzia mwaka 1998 na 2000 imelipa fidia kwa wananchi wote waliokuwa wanamiliki eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali, kama Serikali imeshawalipa wananchi fidia na eneo liko pale kubwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhamishia matumizi ya Gereza pale, eneo lile ni dogo, Hospitali ya Rufaa inatakiwa iendelezwe na *TANROADS* waliokuwepo pale wameshaondoka, wamepisha eneo hilo kwa ajili ya eneo la Hospitali. Ni lini Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaondoa Jeshi la Mageraza pale ambapo ni eneo linalowatunza wafungwa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, akubaliane na mimi kwamba Mheshimiwa Mwigulu amekuja Iringa ameona hali halisi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naomba swali.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, ni lini sasa magereza wataondoa matumizi yao pale na kuachia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, na sisi kama Wizara tunakubaliana naye kwa asilimia 100 ya mapendekezo yake aliyoyasema. Niweke sawa sawa hivyo, maana yake nilikuwa naona Mheshimiwa Ritta Kabati hapa anajiandaa kusimama; sasa ili alielewe ni kwamba Wizara inaelewa kwamba kati ya hospitali na gereza kinachotakiwa kuondoka pale mjini ni gereza na siyo hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hospitali ile inahitaji upanuzi, Wizara inakubaliana na gereza kuhama pale na kwenda kwenye eneo lingine ambalo na lenyewe liko ndani ya mji lakini pembeni kidogo kilometa kama saba kutoka pale mjini ili kuweza kuwa na nafasi ambayo hata kiusalama itaruhusu mazingira yale kuwa salama zaidi ya kutunza wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichojibu Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba wakati jambo hilo halijafanyika, kuna hatua za mpito ambazo tunazifanya zikiwemo hizo za barabara ile kupitika kwa dharura pamoja na masuala ya ukuta aliyoyasemea. Kadri bajeti inavyoruhusu na taratibu nyingine za ndani ya Wizara ya kutumia nguvu kazi inayoendelea, mpango ni huo huo kuhamisha gereza na kuacha fursa kwa Hospitali ya Mkoa kuweza kuwa na nafasi ya kutosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza. Gereza la Kondoa linahudumia Wilaya

ya Chemba na Wilaya ya Kondoa. Gereza hili limejengwa mwaka 1919, lina hali mbaya sana.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa pengine hata Waziri aende tu aone pale kama kweli hawa wafungwa bado ni binadamu, lakini wanaishi kwenye mazingira mabaya sana. Askari wana hali mbaya sana, hata Mkuu wa Gereza anatembea na boda boda. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari hata kwenda tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mwaliko wa Mheshimiwa Juma Nkamia na mara kwa mara amekuwa mstari wa mbele kuunga mkono jitihada na mahitaji yanayotakiwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani ikiwepo nyumba za Polisi, nyumba za Askari Magereza, Zimamoto pamoja na Uhamiaji. Kwa hiyo, sina tatizo na kwenda Wilayani kwake pamoja na Wilaya jirani ya kondoa ili kuweza kujiridhisha na mazingira hayo ili kuweza kuweka utekelezaji mzuri zaidi wa ujenzi wa gereza ili wafungwa pamoja na askari waweze kufanya kazi katika mazingira ya usalama zaidi. Nitafanya hivyo baada ya bajeti yetu kuwa imepita.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.170

**Ahadi ya Serikali kuimarisha Huduma za Ugani na Mafunzo**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Serikali kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 iliahidi kuimarisha huduma za ugani na

mafunzo kwa kuongeza udahili wa Maafisa Ugani wa Uvuvi kutoka 1200 hadi 2500 kwa mwaka ili kuwepo Maafisa Ugani kwa ngazi ya kata na kuimarisha huduma za uvuvi na ufugaji samaki.

(a) Je, ni lini mkakati wa utekelezaji wa suala hili ambao utatoa ajira nyingi kwa vijana utaanza?

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuzishirikisha Halmashauri nyingi katika kuhamasisha uchimbaji wa mabwawa na ufugaji wa samaki hasa katika maeneo yenye ukame ili kuongeza lishe bora na pia ajira kwa vijana?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kuongeza za udahili ili kuongeza Maafisa Ugani wa Uvuvi ulianza kwa Wizara kuimarisha Wakala wa Elimu ya Mafunzo na Uvuvi *(FETA)* katika Kampasi zake za Mbegani (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), *Mwanza South* (Mwanza). Vilevile ili kuongeza udahili wa wanafunzi Serikali itakamilisha ujenzi wa kampasi za Mkindani (Mtwara), Gabimori (Rorya) ifikapo mwaka 2019 ambapo kwa ujumla vyuo vyote vitadahili wanafunzi 2,200 kwa mwaka ukilinganisha na wanafunzi 1,200 wanaodahiliwa kwa mwaka hivi sasa. Vyuo hivyo vinazalisha wataalam wa uvuvi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ambapo hupata ajira Serikalini, sekta binafsi na wengine hujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imechimba visima virefu 101 kwa ajili ya kujaza maji kwenye mabwawa ya kufugia samaki na malambo 1,381 kwa ajili ya kunyweshea mifugo ambayo pia hupandikizwa samaki. Mabwawa hayo yamechimbwa katika Halmashauri mbalimbali nchini hususan maeneo kame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu wa kuwezesha ufugaji wa samaki unafanywa kupitia mkakati wa kuendeleza ufugaji katika sekta ya uvuvi 2010. Mkakati wa Taifa wa kuendeleza ufugaji wa samaki na viumbe wengine kwenye maji wa 2009 na Mpango Mkuu wa Sekta ya Uvuvi wa mwaka 2002 *(The Fisheries Master Plan, 2002).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mkakati wa ufugaji wa samaki umepewa kipaumbele katika mpango wa kuendeleza Sekta ya Kilimo (A*SDP-2)* utakaoanza hivi karibuni. Mikakati yote inatekelezwa chini ya Mpango wa *D by D,* yaani Ugatuaji wa Madaraka ambapo utekelezaji wake unafanywa kwa ushirikiano na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara inatafiti na na kusambaza teknolojia rahisi za ufugaji wa samaki ili kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika ufugaji wa samaki kwa kuongeza ajira, lishe na kipato nchini ikiwemo wananchi wanaoishi kwenye maeneo kame.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangoye, swali la nyongeza.

**MHE. MARIA N. KANGOYE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kutoka Serikalini, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa sheria inawataka wavuvi wanaovua katika Ziwa Victoria wakiwemo wavuvi wa Mkoa wa Mwanza kutumia nyavu za inchi sita hadi saba ambazo hazikidhi mahitaji ya uvuvi katika maji ya kina kirefu. Je, Serikali ina mpango gani ya kupitia upya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1973, sheria ambayo ilitungwa kabla hata samaki aina ya sangara hawajapandizwa ndani ya Ziwa Victoria na kuwa imepitwa na wakati? *(Makofi)*

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri na Mbunge wangu wa Jimbo la Buchosa, ni lini utakuwa tayari kuja Mkoani Mwanza kukaa na wadau ili kuweza kusikiliza kero zao na changamoto zinazowakumba katika uvuvi ndani ya Ziwa Victoria? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Namba 22 na maboresho ya kanuni zake kama yalivyofanywa imeweka aina za nyavu ambazo zinaruhusiwa kutumika katika maji baridi, kwa maana ndani ya maziwa yetu; na aina za nyavu ambazo zinaruhusiwa kutumika katika uvuvi baharini. Sasa utafiti ambao umefanywa na wataalamu wetu kwa muda mrefu ulibaini kwamba nyavu zenye matundu *size* ya chini ya inchi sita zinasababisha uvuvi kutokuwa endelevu ndani ya maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii imezingatia pia aina za samaki waliomo Ziwani na imewekwa ili kuhakikisha kwamba samaki aina kadhaa hawatoweki na aina nyingine wanaendelea kuzaana kwa ajili ya matumizi ya wavuvi wenyewe na watu wengine wanaohusika na suala hili la uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokifanya, mimi binafsi nimeshakutana na wavuvi wa Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine, siyo mara moja, mara kadhaa na mara ya mwisho tulichokubaliana ni kwamba utafiti wa pamoja ufanyike tena kuangalia *mesh size* na lile suala la kuunganisha nyavu yaani *double* tatu, *double* tisa na kadhalika, ili tuweze kujua kwa kushirikiana ni njia gani sahihi ya kuendesha uvuvi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukutana na hawa wavuvi, mimi nakutana nao kila mara ninapokuwa Jimboni. Ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf na Mheshimiwa Mama Ishengoma.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri katika swali la msingi (b); katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Serikali ilisema ilizalisha vifaranga milioni 20 na kuwapa wafugaji wa

samaki ili kuweza kuzalisha samaki. Sasa katika bajeti ya mwaka 2015/2016 na 2016/2017 ingawa haijaja, sijasikia Serikali ikisema tena kwamba wamepeleka vifaranga vingapi vya samaki kwa ajili ya wakulima. Je, mpango ule uli-*fail* ndio ikawa haikuja tena au ulifanikiwa? Kama ulifanikiwa ni kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa nchi yetu wa kuzalisha vifaranga vya samaki umeongezeka sana hasa baada ya sekta binafsi kuingia katika biashara hii ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki. Sasa hivi Morogoro, Dar es Salaam, Mkuranga na Mwanza kuna uwezo mkubwa tu wa watu binafsi kuzalisha vifaranga vya samaki hadi kufikia vifaranga milioni karibu 36. Kwa hiyo, tunaendelea tu kuhimiza na kutoa elimu kwa watu wenye nia ya kujiingiza katika biashara hii ya uzalishaji wa vifaranga waendelee kufanya hivyo ili kukidhi mahitaji makubwa ambayo yanazidi kuongezeka hapa nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ni mpango wa Serikali kuanzisha Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya: Je, kuna mkakati gani wa kuanzisha mkondo wa kilimo na uvuvi katika kila Chuo cha *VETA* kinachoanzishwa kwenye Wilaya zetu ili kuongeza Maafisa Ugani hawa wa kilimo na uvuvi ambao wanaweza kufanya kazi kwenye vijiji vyetu na kuinua kilimo chetu na uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Ishengoma ni zuri sana. Nitaiagiza mamlaka yetu ya *FETA* iwasiliane na *VETA* kuona ni namna gani wanaweza kushirikiana katika kutekeleza wazo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Najielekeza hapo kwenye wavuvi. Kwa kuwa wavuvi katika Ziwa Victoria nyavu wanazotumia wanazinunua madukani na Serikali ipo na bandari ipo; Serikali ituambie ni lini itayafunga yale maduka yanayouza nyavu zisizotakiwa kuvuliwa na lini itaweza kuleta sheria hapa Bungeni kuzuia viwanda vinavyozalisha nyavu zinazosababishia wavuvi hasara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Jumuiya anapomuuliza mdhamini wake inakuwa shida kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupambana na uvuvi haramu kwa ujumla, Serikali sasa hivi inachokifanya, inashambulia maeneo yote, yaani hatuendi kwa wavuvi peke yao, tunamchukulia hatua yeyote aliyeko katika ule mnyororo wa thamani wa uvuvi kwa maana kwamba mzalishaji wa zana haramu, msambazaji, mtunzaji, mhifadhi na yeyote. Kwa hiyo, anayeuza akipatikana anachukuliwa hatua kama mhalifu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tumekwenda hatua zaidi hata ya kudhibiti uingizwaji wa nyavu nchini, acha wenye viwanda ambao tunawakagua mara kwa mara na kwa kweli mwenye kiwanda hapa nchini akipatikana anazalisha nyavu zisizoruhusiwa tunachukua leseni yake na kufunga kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunakagua hata uingizaji, kwa sababu wako watu wanaagiza nyavu kutoka nchi za nje kwa kisingizio kwamba zinapita Tanzania zinakwenda nchi nyingine, lakini baada ya kuwa wamesha-*clear* pale bandarini, wanafanya maarifa hizi nyavu zikifika mpakani Tunduma au pengine, zinarudi nchini. Kwa hiyo, hata hawa sasa hivi tunashughulika nao, tunahakikisha wanatoka nje ya mipaka yetu na hizo nyavu zao. Tukimkamata tunamchukulia hatua kama sheria inavyotaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 171

**Kuipa Kipaumbele Sekta ya Uvuvi**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** aliuliza:-

Sekta ya Uvuvi ni muhimu kwa uchumi wa nchi, sekta hii ikiwezeshwa ina uwezo angalau kufikisha shilingi bilioni 12 kama kipato kwa mwaka:-

Je, ni lini na kwa vipi Serikali itaipa kipaumbele Sekta ya Uvuvi nchini ili kuboresha utendaji na kuongezea nchi kipato?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Uvuvi ili iweze kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa kupitia mikakati na mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Aidha, kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi, ambayo

pamoja na mambo mengine inalenga kuboresha miundombinu ya uvuvi, ikiwemo bandari ya uvuvi na kuimarisha ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2015/ 2016, Serikali kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilikusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 19 ambayo ni zaidi ya asilimia 100 ya lengo la bilioni 18 ilizokuwa imepangiwa kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeandaa kanuni za kusimamia uvuvi katika Bahari Kuu ya Tanzania ambapo zimetoa fursa kwa meli kubwa za uvuvi zinazovua bahari kuu kushusha samaki katika Bandari ya Dar es Salaam (Gati Na. 6) na Zanzibar (Gati Na. 3). Aidha, samaki wanaovuliwa bila kukusudiwa *(by-catch)* watashushwa katika bandari hizo ambapo itatochea uzalishaji wa samaki nchini, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa ajira na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza mapitio ya Mpango Kabambe wa Uvuvi *(Fisheries Master Plan)* wa mwaka 2015 kwa lengo la kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mpango ili kuchangia katika kuongeza usalama wa chakula, lishe, ajira, kuchangia uchumi wa nchi pamoja na kuongeza pato la Taifa. Aidha, Sekta ya Uvuvi imepewa kipaumbele katika Programu ya Kuendeleza Kilimo awamu ya pili *(ASDP II)* ambayo utekelezaji wake unaanza mwaka 2017/2018 hadi 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Semesi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilitegemea Wizara itaonesha angalau *trend* ya mapato kutoka kwenye shughuli za uvuvi angalau miaka mitano au kumi tuone kwamba inaendaje, ila wametoa tu mfano kwa mwaka wa 2015/2016. Ukiangalia mapato kutoka uvuvi 2016/2017 huu mwaka uliokwisha, walikuwa na pungufu *almost* shilingi bilioni tisa kwa sababu walipata tu shilingi bilioni 10. Sasa Serikali haioni kwamba

sasa ni wakati muafaka wa kuamka na kuweka vipaumbele katika Sekta hii ya Uvuvi ili kujiongezea mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mfano tu, bajeti ya maendeleo inayotengwa katika Sekta ya Uvuvi, mwaka 2016 na mwaka huu 2017 ni sifuri. Kwa hiyo, ina maana shughuli za doria, mikakati ya kujenga Bandari ya Uvuvi au kuboresha Bandari ya Uvuvi haipo, kujikita zaidi katika kuongeza mapato katika *deep sea fisheries,* haipo; hii mikakati yote haipo; zaidi kuna *project* moja tu ya *SWIOFish* ndiyo ambayo imesimama ambapo fedha zake kutoka *World Bank* ni za mikopo. Sasa Serikali haioni kwamba hawako *fair* kwa wavuvi, shughuli za uvuvi na yenyewe pia inajinyima mapato ambayo yangetuletea maendeleo katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante*. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Sekta ya Uvuvi imepewa kipaumbele katika Programu ya Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili *ASDP II* na katika Programu hii, yote anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, yamo. Ni programu itakayoanza mwaka huu wa fedha mpaka mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kwamba haoni mikakati yoyote ya kuendeleza sekta hii ya uvuvi; mkakati lazima utengenezewe mazingira ili uweze kutekelezwa. Kwa hiyo, tusingeweza kupanga mambo ya uvuvi wa bahari kuu bila kuwa na *legal framework* ambayo inatuwezesha kutekeleza yale tunayotaka kufanya. Kwa hiyo, tulichoanza nacho ni kubadilisha kanuni za uvuvi wa bahari kuu ili sasa yale tutakayopanga kuyafanya, yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kusisitiza hapa kwamba akisoma kanuni na natumaini ameshazisoma; ataona wazi kwa vipi sasa hivi tutabadilisha sana sura ya

Sekta ya Uvuvi wa bahari kuu hapa nchini na manufaa yataanza kuonekana. Sasa hivi tunapozungumza, wavuvi wa bahari kuu ambao wameomba kukata leseni kwa masharti mapya wapo wengi, wamekwishafika 30 na kadhaa hivi. Kwa hiyo, tuanze tu kutegemea kwamba manufaa makubwa ya uvuvi yataonekana hapa nchini na hicho kinachoitwa *blue economy* utakishuhudia kinatokea hivi karibuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Tunamalizia Wizara hii na Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 172

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege**

**MHE. BONNAH M. KALUWA** aliuliza:-

Mwaka 1995 Serikali ilifanya uthamini wa wananchi wa Kata ya Kipawa ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam ambapo baadhi ya wananchi hao walilipwa fidia lakini kuna baadhi ambao mpaka sasa bado hawajalipwa fidia hiyo na hawajui ni lini watalipwa.

Je, Serikali imejipanga vipi kuwalipa wananchi hao ambao hawajalipwa ili waweze kupisha upanuzi wa uwanja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ilifanya uthamini wa mali za wananchi ili kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Dar es Salaam mwishoni mwa miaka ya 1990. Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya upanuzi huo ni Kipawa, Kigilagila na Kipunguni. Kutokana na gharama za fidia na uhaba wa fedha, Serikali imekuwa ikilipa fidia kwa wakazi hao kwa awamu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ililipwa mwaka 2009/2010 kwa wakazi wapatao 1,500 wa eneo la Kipawa ambao walilipwa fidia zilizofikia shilingi bilioni 18 na zoezi hili lilikamilika Januari, 2010. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ililipa shilingi bilioni 12 za fidia kwa wakazi 864 wa eneo la Kigilagila na malipo yalikamilika Januari, 2011. Mwaka 2013/2014 Serikali ililipa shilingi bilioni 1.2 ikiwa ni fidia kwa wakazi 59 kati ya wakazi 801 wa eneo la Kipunguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa ni wakazi 742 wa Kipunguni ndio ambao hawajalipwa fidia zao zenye thamani ya takriban shilingi bilioni 19. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya kulipa fidia wananchi wa Kipunguni. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni 30 ili kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi hao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba nimekuwa nikiuliza hili swali na leo hili ni swali la tatu; lakini pia Naibu Waziri alikuja kuongea na wananchi wa Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni kuhusiana na mambo ya fidia na akawaahidi atarudi. Mpaka sasa hivi ni mwaka mmoja Mheshimiwa Waziri hajawahi kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri; kwa kuwa wananchi hawa walifanyiwa tathmini mwaka 1995, leo ni miaka 22: Je, atawalipa kwa kutumia tathmini gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, namwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hawa wananchi...

**MWENYEKITI:** Maswali mawili tayari Mheshimiwa Bonnah. Kuna la kwanza uliuliza Mheshimiwa Waziri atakuja lini na hilo la pili.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Ah, hapana.

**MWENYEKITI:** Tayari tumemaliza Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nabadilisha la kuja...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeshamaliza, acha tuendelee na Naibu Waziri. *(Kicheko)*

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba, hawa wananchi wamesimamisha maendeleo kwa muda mrefu; aseme hapa leo katika Bunge hili kwamba: Je, waendelee na maendeleo yao mpaka watakapopata hizo pesa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli niliahidi nitarudi, lakini nilimwambia nitarudi nikiwa na majibu sahihi. Sikusema mwaka mmoja, niliwaambia ni katika kipindi cha miaka mitatu tatizo hilo tutalitatua. Naona umeshaona tofauti, toka pale nilipofika, mwaka huu tumeshatenga shilingi bilioni tano na mwaka ujao tumeshatenga shilingi bilioni 30. Unaona kabisa kwamba nitakaporudi kule, nitarudi kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kwamba tunalipa kwa tathmini gani? Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalipa kwa tathmini ile

iliyofanyika pamoja na *interest* ya miaka yote hiyo. Ndivyo sheria za fidia zinavyotuongoza, kwamba kuanzia mwaka uliofanya tathmini ukizidisha miezi sita hujalipa, kuna *interest* inaingia na kadri utavyoendelea kuchelewa ndivyo *interest* inavyoingia. Ndiyo maana kama umeona gharama inayodaiwa iliyopo katika kitabu kile cha tathmini ni shilingi bilioni 19, lakini fedha tutakazolipa ni zaidi ya shilingi bilioni 35, ina maana ni kwa sababu ya kuongeza *interest* ambayo ni kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 173

**Kuboresha Reli ya Tanga**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU** aliuliza:-

Reli ya Tanga inategemewa sana kiuchumi kwa usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, ni kiunganishi hadi Bandari ya Tanga:-

Je, ni lini Serikali itaboresha na kuijenga kisasa kwa kiwango cha *Standard Gauge* ili iongeze uchumi na kuleta maendeleo?

**NAIBU WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa reli ya Tanga katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo nchini Tanzania. Mpango wa Serikali uliopo ni kuunganisha Bandari ya Tanga na Bandari mpya ya Mwambani kwenye reli ya *Standard Gauge* ya Ukanda wa Kati *(Central corridor)*

kupitia reli ya njia panda ya Ruvu hadi njia panda ya Mruazi ambayo inaunganisha reli ya kati na reli ya Tanga hadi Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa kina *(detailed engineering design)* wa reli ya kutoka Tanga hadi Arusha (kilometa 438) umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuanza ujenzi wa reli ya Tanga hadi Arusha kwa kiwango cha Kimataifa. Aidha, Mhandisi Mshauri, Kampuni ya *HP Gauff* ya Ujerumani inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali, yaani *feasibility study and preliminary engineering design* kati ya Arusha na Musoma pamoja na matawi ya kwenda Engaruka na Minjingu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa ujenzi wa reli hii ya Tanga ambao utahusisha mpaka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Mara una umuhimu ambao utaongeza mizigo sana kwenye reli hii. Tunahitaji iwe reli ya kisasa kutokana na viwanda ambavyo vinategemewa kujengwa kwenye ukanda huo ukitilia maanani kwamba Mkoa wa Tanga sasa hivi tuna viwanda vingi vya simenti na kuna kiwanda kikubwa sana ambacho kitaanza kujengwa karibuni kwa ajili ya simenti na ukitilia maanani kwamba kuna bomba la mafuta ambalo linatoka Hoima kule Uganda mpaka Bandari ya Tanga. Bandari ya Tanga imeshaanza kuboreshwa. Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Mheshimiwa Waziri linaonekana ni lepesi na halina uzito, nataka kujua kuna mikakati gani ambayo imeshafanyika na Serikali kuweza kutafuta hizo fedha za kuanza ujenzi wa reli hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, sasa hivi kuna changamoto kubwa katika Bandari ya Tanga ukitilia maanani kwamba Bandari ya Mombasa wameshajenga reli

ya *standard gauge* ambayo inatoka Mombasa inakwenda Nairobi mpaka Kisumu na Tororo mpaka Kampala. Sasa sisi bado hatujaanza hiyo kazi; Mheshimiwa Waziri anaonaje suala la kuhusisha sekta binafsi katika utaratibu wa *PPP* ili tuweze kupata mwekezaji wa kujenga reli hii kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Balozi, Mheshimiwa Mbunge kwamba reli hii ya Tanga – Arusha – Musoma ni muhimu sana na ni lazima tuifanye kazi hii kwa haraka. Anafahamu na nampongeza tu kwa kazi kubwa ya kufuatilia shughuli hii pamoja na Wabunge wengine wa Mkoa wa Tanga, kwamba reli hii imeshaanza kufanyiwa kazi na hatua ya kwanza kuifanyia kazi ni kufanya hiyo *feasibility study* na *detailed design.* Nashukuru kazi hii imekamilika na tunatarajia tumlipe Mkandarasi tupate taarifa ili tukishapata hiyo taarifa yake tuweze kuanza sasa hatua za kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wake kwamba katika hatua hizi za kutafuta fedha ni pamoja na kutumia mfumo wa *PPP.* Tunakubali ushauri wenu, mmetushauri hilo na sisi tumekubali kwamba tutahakikisha tukishapata ile taarifa tutaanza hatua madhubuti za kufuata Sheria ya *PPP* ili ujenzi huo uanze haraka kwa sababu tukisema tujenge kwa hela zetu, reli zote hizi ambazo tunaenda nazo kwa sasa hatutaweza kwa muda mfupi. Kwa hiyo, nadhani ni wazo sahihi na tunashukuru sana kwa ushauri wenu, tutatumia njia hiyo ya *PPP.*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 174

**Ongezeko la Nauli Katika Sekta ya Usafiri wa Anga**

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Kukua kwa soko huria katika utoaji wa huduma za anga nchini kumevutia na hivyo kuimarisha Sekta ya Usafirishaji wa abiria na mizigo. Baadhi ya Mashirika ya Ndege yamekuwa yakitoza nauli kubwa na hivyo kuongeza mzigo kwa watumiaji:-

Je, Serikali inatoa kauli gani dhidi ya ongezeko la nauli lisiloendana na uhalisia inayotozwa na baadhi ya Mashirika ya Ndege?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na sekta nyingine, nauli za ndege hutozwa kutegemeana na nguvu ya soko katika njia husika. Mpango uliopo ni kuongeza ushindani katika njia husika ili kupunguza nauli. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kutoa leseni kwa watoa huduma za usafiri wa anga ili kuleta ushindani kwa kutoa huduma zilizo bora na kutoza nauli ambazo abiria wanazimudu. Aidha, mamlaka huingilia kati kisheria kuweka kiwango kikomo pale tu inapoonekana kuna ukiritimba na wananchi wanaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubaliana kuwa nauli kwa baadhi ya njia zilikuwa juu kutokana na kuwa na mtoa huduma mmoja. Baada ya Kampuni ya Ndege *ATCL* kuanza kutoa huduma katika njia hizo, nauli za ndege

zimeshuka kutokana na ushindani. Kwa mujibu wa Ibara ya 25 ya Sheria ya Usafiri wa Anga *(Civil Aviation Act, Revised Edition of 2006),* Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA)* itaendelea kufuatilia kuchukua hatua pale inapobainika kuwa hakuna ushindani wa kutosha na wananchi wanatozwa nauli kubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ambaye umeuliza swali kwa niaba, kama una swali la nyongeza.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na kwamba Serikali inanunua ndege na kuikodisha *ATCL,* hata hivyo umiliki huu wa ndege uko kwa Wakala wa Ndege za Serikali. Kwa maana hiyo basi, *ATCL* inakodisha hizi ndege. Sasa je, *ATCL* inatoa malipo yoyote kwa Serikali kwa ajili ya kukodisha ndege hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwamba mpaka sasa hivi Serikali inaisimamia *management* pamoja na Bodi ya *ATCL,* kwa maana hiyo *ATCL* haina mamlaka huru ya kutekeleza shughuli zake za utawala. Sasa swali langu ni kwamba, Serikali ina mpango gani wa kuiachia *management* na Bodi ya *ATCL* ili iweze kufanya mamlaka yake kwa uhuru na kuweza kufanya shughuli za kibiashara kwa ajili ya kuipatia Serikali mapato ambayo itakuwa ni faida endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna malipo yanayolipwa na *ATCL* kwa mmiliki wa ndege, lakini nadhani Mheshimiwa Lathifah anafahamu, mmiliki wa ndege, *TDFA,* inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali na kwa upande mwingine mwendesha ndege au mkodishaji wa ndege hizo ni *ATCL* ambaye naye anamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Hiyo haifanyi *ATCL* apunguze nguvu katika kuhakikisha

kwamba anafuata shughuli za biashara na hatimaye analipa gharama za kukodisha ndege hizo. Kwa hiyo, zinalipwa na takwimu tu bahati mbaya sina, ukizitaka nitakuletea uone hadi sasa *ATCL* wameshalipa kiasi gani kwa *TDFA* ambao ndege zao wamezikodisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhuru wa bodi na *management,* nimhakikishie Mheshimiwa Lathifah, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni moja kati ya Wizara zinazohakikisha taasisi zake zinazofanya shughuli za kibiashara zinafanya shughuli kibiashara na haziingiliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hizo zikiwa ni pamoja *ATCL,* haiingiliwi, bodi ina mamlaka kamili ingawa tu wanalalamika kuna vikao vingi sana vya taasisi za Kiserikali na taasisi za Bunge, lakini hizi zote ni kwa mujibu wa sheria. Sheria za Bunge zinawataka wao wawajibike Bungeni kila wanapotakiwa kuwajibika na Sheria za Msajili wa Hazina zinawataka wao wawajibike kwa Msajili wa Hazina kila wanapoona kwamba wanahitaji kuwajibika, lakini huko siyo kuingilia uhuru wao. Taasisi hizi zinatekeleza wajibu wao kwao, wao wanaendelea kuwa huru katika kufanya maamuzi yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swlai dogo la nyongeza. Kwa kuwa kukua kwa soko huria katika utoaji wa huduma ya anga nchini, hivyohivyo naweza nikaambatanisha na kukua kwa elimu yetu kuwa huria na nilikuwa nataka tu kupata maelekezo ya Wizara juu ya huria hii ya kutokana na elimu yetu ya Tanzania kuwa huria, hali iliyosababisha baada ya kutoka kwa uhakiki wa vyeti feki imepelekea baadhi ya Madaktari, Walimu, Watumishi, taarifa zao kuonekana ni *incomplete.* Hii ni kwa sababu ya elimu yetu kuwa huria. Sasa naiomba Serikali itoe maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, kuna watumishi sasa wanaelekea Dar es Salaam kwenda kuhakiki *incomplete* zao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba nakata kujua: Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya wafanyakazi ambao taarifa iliyotoka juzi ya uhakiki wa vyeti vyao, hasa wale wote walioandikiwa *incomplete?* Serikali hasa Wizara hii ya Elimu ituelekeze, maana leo hii watu wanasafiri wengi kwenda kuhakiki vyeti vyao vya *Form Four. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni hilo nalielekeza kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu hapa ni mada huria na elimu yetu ni huria, naomba Wizara ya Elimu itoe tamko juu ya kadhia hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba tumekuwa tukitoa elimu huria ili kuwezesha maeneo mbalimbali ya ajira kuweza kupata wataalam wanaohitajika. Katika suala hili la watu kusafiri kuhusiana na kuhakiki vyeti vyao, napenda tu kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makundi makuu matatu ambayo yameendana na uhakiki uliofanyika. Kuna kundi la kwanza la vyeti feki au vyeti vya kughushi, kundi hili kama kuna yeyote anayeona kwamba hajaridhika, anachotakiwa kufanya siyo kusafiri, bali ni kukusanya vyeti vyake halali na kumwona mwajiri wake ambaye ni *DED* (Mkurugenzi wa Halmashauri) au Katibu Tawala wa Mkoa ili

apeleke huo ushahidi wake na viweze kuwasilishwa. Vitawasilishwa kwa Katibu Mkuu, Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kundi lingine, hili analolizungumza la *incomplete* (vyeti visivyokamilika). Yawezekana wakati wa kuwasilisha, mtu aliwasilisha labda vyeti vya Chuoni, vyeti vya Kidato cha nne au cha sita hakuwasilisha; au vyeti vingine vinavyohusiana. Kwa hiyo, anachotakiwa kufanya ni vilevile, kupeleka vile vyeti ambavyo vilikuwa havijawasilishwa kwa hao waajiri wake ambao ni Mkurugenzi wa Halmashauri au *RAS* (Katibu Tawala wa Mkoa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi la tatu la vyeti vyenye utata. Vyeti vyenye utata unakuta kwamba cheti kimoja kimetumika na watu zaidi ya mmoja. Kwa hali hiyo inabidi lazima kumfahamu ni yupi mwenye cheti halisi. Wanachotakiwa kufanya ni kila mtu anayeamini ndiye mwenye cheti hicho, hao ndio wanaotakiwa kusafiri, waende *NECTA* ili sasa wakahakikiwe na kujulikana mwenye cheti chake ni yupi kwa sababu haiwezekani cheti kimoja kikatumika na mtu zaidi ya mmoja. Huo ndiyo ufafanuzi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tumemaliza muda wetu wa maswali, najua mna maswali mengi ya nyongeza lakini muda hauturuhusu na siwezi kuwaridhisha wote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, tumefika mwisho wa maswali. Kipindi hiki ni kipindi cha matangazo na hapa leo nina matangazo mawili.

Kwanza ni wageni walipo Bungeni asubuhi hii. Tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiongozwa na Meja Jenerali Projest Rwegasira ambaye ni Katibu Mkuu; Ndugu Ernest Mangu, Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi; Ndugu Dkt. Juma Malewa, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza; Ndugu

Thobias Andengenye, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Dkt. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. Wakuu hawa wameambatana na Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali vilivyopo chini ya Wizara hiyo. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Pili, kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge, ambao ni familia yake na wanachama wenzake. Ndugu Neema Godbless, mke wake; Ndugu Salum Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA, Zanzibar; na Ndugu Haleluya Natai, Katibu wake. *(Makofi)*

Mwisho, tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Wote kwa pamoja tunawakaribisha. *(Makofi)*

Kuna tangazo moja hapa, ambapo Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika eneo la *basement* leo siku ya Jumanne, tarehe 9, Mei, 2017 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, kabla ya ibada hiyo tutakuwa na chakula cha pamoja na mtumishi wa Mungu Mtume na Nabii Mwingira ambaye atahudumu katika ibada hiyo. Mara baada ya ibada hiyo pia mtumishi wa Mungu atakuwa na faragha na Waheshimiwa Wabunge wanawake. *(Makofi)*

Katibu, tunaendelea.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, tunaanza...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Nitapokea miongozo miwili kwa leo kutokana na muda. Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Lema.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Why front only?*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kwa nini siyo huku nyuma?

**MWENYEKITI:** Ni wawili tu hao leo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jana Taifa letu lilikuwa linapita katika kipindi kigumu baada ya kuwapoteza vijana wetu ambao walipata ajali kule Arusha, lakini Mheshimiwa Rais wa nchi yetu amekuwa akisisitiza kwamba wakati huu siyo wakati wa kampeni, tushirikiane tuijenge nchi yetu na tuheshimiane wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jana katika tukio lile lililokuwa linaendelea pale Arusha, shule iliyopoteza watoto waliofariki ni ya Arusha Mjini lakini kwa masikitiko makubwa, katika *protocol* ya kutoa pole kwa wafiwa, Meya wa Jiji la Arusha, Mbunge wa Jiji la Arusha hawakupewa hiyo heshima ya kuwapa pole waliofiwa na sisi ndiyo Wabunge wa kuchaguliwa tunaowawakilisha wananchi. Je, ni haki? Pamoja na *ambulance* ambayo imekuwa *donated* na Mbunge katika eneo lile, imeambiwa itoke kwa sababu tu ina jina lake. Hii ni pamoja na *ambulance* ya Mheshimiwa Nassari ambazo zote zilikuwa zinafanya kazi. Je, ni haki kwa Waheshimiwa Wabunge ambao Mheshimiwa Rais amekuwa akisema tushirikiane tuache siasa, kitendo kilichofanywa jana na *protocol* ya yeyote aliyeongoza katika Mji wa Arusha, ni halali kwa kupuuza kazi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hapo hapo, kwamba jana gari za kubeba wagonjwa ambazo zimekuwa *donated* kwenye Halmashauri ya Meru na Jimbo la Arusha Mjini ziliondolewa kwenye *stadium* kwa sababu ubavuni kuna maandishi 'gari hizi zimetolewa mchango kwa hisani ya watu wa Arusha na Mbunge wa Arusha Mjini Godbless Lema na Mheshimiwa Nassari, Jimbo la Arumeru Mashariki'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu tu tunamheshimu sana Mama Samia lakini mambo kama hayo huwa hayatokei mbele yetu. Tunaomba Mwongozo wako. Kama kwenye msiba Madiwani wa Jiji la Arusha wanakuwa *sidelined,* Mbunge na Meya waliofiwa ambao tunapaswa kupokea wageni, tunakatazwa hata kutoa salamu za rambirambi kwa sababu ya siasa; gari za wagonjwa zinaondolewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kufanya siasa au tunaviambia vizazi vinavyokua vijipange viende msituni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Nimemaliza miongozo, nilisema miwili na nimepokea miongozo yote miwili na nitaitolea majibu baadaye. Tuendelee Katibu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Mwenyekiti!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Mwenyekiti!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:** ...kwamba Bunge sasa likubali...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *We are working here.*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Hoja za Serikali, Waziri wa Mambo ya Ndani...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Tunafanya kazi hapa. *Why?*

**MWENYEKITI:** ...naomba sasa aje awasilishe Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake...

**MBUNGE FULANI:** Sugu acha fujo.

**MWENYEKITI:** ...kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa dakika ambazo hazipungui 60.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *We are working here.*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini wewe!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *No, no, no, we are working here.*

**MBUNGE FULANI:** Zumbukuku huyo!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *We are working here.*

**MBUNGE FULANI:** Zumbukuku huyo!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MBUNGE FULANI:** Sugu acha bangi!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje ya Mambo ya Ulinzi na Usalama sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2016/2017 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda, naomba hotuba yangu yote kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba iingie kwenye *Hansard* kwa kuwa nitasoma muhtasari tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusoma hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Vile vile nimshukuru Mungu kipekee kwa kunijaalia mtoto wiki iliyopita tena wa kike, baada ya watoto wawili wa kiume na mmoja wa kike sasa nina *fifty fifty* kwenye familia yangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniteua kuwa Waziri katika Wizara hii nyeti inayosimamia usalama wa nchi. Naahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuhakikisha kuwa hali ya usalama nchini inaendelea kuimarika ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya kiuchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi pamoja na viongozi wako, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzako kwa kuendesha na kusimamia vema shughuli za Bunge. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa

Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maoni yenu yanayolenga kuboresha utendaji wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti Balozi Adadi Rajabu, Mbunge wa Muheza, kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2017/2018. Naishukuru Kamati hiyo kwa maelekezo, ushauri na maoni ambayo mara zote yamelenga kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kutoa pole kwa familia na wananchi kwa ujumla waliopatwa na matatizo kama ambavyo Bunge lako limekuwa katika kipindi hicho tangu lilipotokea kwa kupotelewa na wanafunzi wetu, watoto wetu pamoja na familia nyingine ambavyo zimepatwa na matatizo ya aina hiyo katika vipindi tofauti tofauti tangu Julai, 2016 hadi Machi, 2017. Kipekee natoa pole kwa ndugu walioguswa na matatizo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya wajibu mkubwa na muhimu wa Serikali ni kulinda usalama wa raia pamoja na mali zao na kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinaendelea kuwepo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeendelea kutekeleza wajibu huo kwa kusimamia sheria, kupambana na kudhibiti uhalifu wa aina yoyote unaoweza kuathiri hali ya amani pamoja na utulivu pamoja na shughuli za maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla. Hali ya usalama hapa nchini imeendelea kuwa tulivu licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali za hapa na pale ambazo Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kulikuwa na matukio makubwa ya uhalifu

56,913 ambapo matukio 53,850 yaliripotiwa kutoka Tanzania Bara na matukio mengine 3,063 yaliripotiwa kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha makosa hayo yameongezeka kwa 7% ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali ikiwepo kuongezeka kuyafichua makosa ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa makubwa ya jinai yamegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali pamoja na makosa ya kimaadili ya jamii. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi hapa nchini yalikuwa kama ifuatavyo, yakiwemo makosa dhidi ya binadamu 10,089, makosa ya kuwania mali 29,476 na makosa dhidi ya maadili yakiwa 17,348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya matukio 2,470 ya mauaji yalitokea na watu 2,532 waliuawa; na kati ya hao wanaume wakiwa 2,067 na wanawake 465. Idadi kubwa ya mauaji ilitokea kwenye matukio yaliyohusisha wizi wa mifugo, ujambazi, imani za kishirikina, wivu wa mapenzi, unyang'anyi wa pikipiki pamoja na magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio hayo yalijitokeza kwa wingi zaidi katika Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Mbeya, Kagera, Geita na Dodoma. Upelelezi wa kesi hizi umeendelea na watuhumiwa zaidi ya 1,000 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na katika mwaka 2017/2018, Jeshi litaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na uhalifu huo pamoja na kuendelea kuelimisha jamii umuhimu wa kuzingatia Sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 silaha 410 na risasi 2,262 zilikamatwa na aidha kulikuwa na matukio 576 ya ujambazi wa kutumia

silaha yaliyoripotiwa katika vituo mbalimbali hapa nchini na matukio hayo yalijitokeza kwa wingi katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Morogoro, Mara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mikoa ya Kipolisi; Ilala, Kinondoni, Tarime (Rorya) na Pwani. Watuhumiwa 306 waliopatikana na silaha haramu walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa tarehe 24 Januari, 2017, Wizara ya Mambo ya Ndani iliteketeza jumla ya silaha 5,608 zilizokuwa zinasalimishwa na nyingine zilizopatikana katika mazingira ya uhalifu kuanzia mwaka 2013 hadi 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuhimiza wananchi wote wanaomiliki silaha kinyume cha Sheria wazisalimishe kwenye vituo vya Polisi vilivyo karibu nao au kwenye Ofisi za Watendaji wa Kata. Kinyume cha hapo, Jeshi litaendelea kufanya doria, misako na operesheni za mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha kwamba wote wanaomiliki silaha kinyume cha Sheria wanadhibitiwa na wanafikishwa katika mkono wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupambana na wimbi la umiliki wa silaha haramu, Jeshi la Polisi lilianzisha zoezi la uhakiki wa silaha mwezi Machi, 2016 ambapo hadi mwezi Machi mwaka huu, asilimia 63.20 ya silaha zilikuwa zimehakikiwa. Katika zoezi hilo, jumla ya silaha 486 zilisalimishwa kutokana na kutomilikiwa kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wamiliki wote wa silaha kuhakikisha kwamba silaha zao zinahakikiwa katika muda uliopangwa na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote ambao hawatafuata utaratibu huo na tutafuta leseni zao kama watakuwa hawamiliki silaha kwa uhakiki uliokua umetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya usalama barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya matukio 6,500 ya usalama barabarani yaliripotiwa hapa nchini na katika matukio hayo jumla ya ajali 1,552

zilisababisha vifo 2,372 na watu 6,074 kujeruhiwa. Takwimu zinaonesha kupungua ajali hizo kwa 7% ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia Sheria za Usalama Barabarani ambapo kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya madereva 6,500 wa magari mbalimbali pamoja na waendesha pikipiki 5,865 ambao walikamatwa na kupelekwa Mahakamani kwa kukiuka Sheria za Usalama Barabarani, walichukuliwa hatua za Kisheria. Katika mwaka 2017/2018 Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia Sheria za Usalama Barabarani, kuelimisha jamii kuzingatia taratibu za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali ya ajali barabarani, tumebainisha makosa ama sababu za ajali ikiwemo uzembe, ulevi, mwendokasi pamoja na ubovu wa vyombo. Tumefanyia kazi kuhusu mwendokasi, hatua zilishachukuliwa, lakini kwa kuzingatia hali hiyo sasa na madhara makubwa yanayojitokeza kutokana na ajali hizo, Serikali inakusudia kuanzisha ukaguzi wa lazima kwa magari yote ili kubaini magari mabovu yasiyostahili kuwepo barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa hivi sasa, kipaumbele kinawekwa kwenye magari ya abiria pekee na nawaomba wananchi wote ambao wanamiliki magari watoe ushirikiano punde mamlaka husika zitakapoanza kutekeleza zoezi hili ili kuondoa magari yasiyostahili kuwa barabarani, yanayosababisha ajali kuendelea kuwepo barabarani na kusababisha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa tarehe 20 Novemba, 2015 kufuatia hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge rasmi la Kumi na Moja na maelekezo hayo kwa nyakati tofauti amekuwa akiyatoa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya kilogramu 16 za madawa ya

kulevya aina ya *cocaine* pamoja na kilogramu 37 na gramu 118 za *Heroine* zilikamatwa na watuhumiwa 1,241 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani kama Mheshimiwa Rais alivyosisitiza katika ufunguzi wa Bunge na kama ambavyo amesisitiza katika maeneo mengine alipoongelea masuala ya vita ya madawa ya kulevya na vita hiyo ni endelevu, haina ukomo mpaka pale biashara haramu hiyo itakapokuwa imekomeshwa ili kuwa na hatima njema ya vijana wetu na Taifa letu kwa ujumla. Aidha, katika kipindi hicho kilo 36,337 na gramu 426 za bangi zilikamatwa na watuhumiwa 12,691 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mara nyingi wamesema, kumekuwepo na tatizo la wananchi kubambikwa kesi. Hatua stahiki za kukabiliana na malalamiko ya wananchi kubambikwa kesi zimechukuliwa, ambapo Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kupokea malalamiko na kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko hayo yameendelea kupokelewa katika Ofisi za Wakuu wa Polisi wa Wilaya, Mikoa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi 2017, Jeshi la Polisi limepokea malalamiko 206, ongezeko la malalamiko 138 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Jeshi la Polisi lilichukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa Watendaji ambao walifanya makosa hayo ikiwemo kufukuzwa kazi kwa Askari 14 na Maafisa wawili na kushushwa vyeo kwa Askari wanne pamoja na Askari sita kupewa adhabu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeimarisha utaratibu na usimamizi wa utendaji katika kushughulikia malalamiko mbalimbali yanayofikishwa katika vituo vya Polisi na kutoa miongozo ya mara kwa mara kwa Wakuu wa Vituo

pamoja na Wapelelezi ili kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba wanyonge wanapata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongozo hiyo ni pamoja na; kusimamia kwa karibu upelelezi wa mashauri yote kabla ya kuyapeleka kwa Mwanasheria wa Serikali; kushirikiana kwa pamoja kati ya wapelelezi na waendesha mashtaka kutoka hatua za awali hadi hatua za juu ili mwisho wa kesi iweze kutendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandishwaji Vyeo kwa Askari; mapendekezo ya upandishwaji vyeo kwa Askari yameendelea kuzingatia uwepo wa nafasi, bajeti, sifa pamoja na miundo ya Kitaasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, jumla ya Askari 4,604 walipandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali wakiwepo Askari 4,000 wa Jeshi la Polisi na waliosalia wa vikosi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya madai ya Askari, Serikali imelipa madeni ya watumishi jumla ya Shilingi bilioni 14.8 katika mwaka wa fedha 2016/2017 na madeni hayo ni ya kipindi cha mwaka 2014/2015 ambayo yalitokana na malimbikizo ya posho za likizo pamoja na safari za kikazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea na kusambaza miongozo unayotoa ufafanuzi kuhusu Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, pamoja na kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uraia wa watu wanaotiliwa mashaka. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Serikalini imetoa tafsiri ya uraia wa Tanzania kwa kuzaliwa na hivyo kuondoa mkanganyiko uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu imeendelea kusimamia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka

2016. Ili kutatua changamoto za kiutendaji zinazojitokeza katika utoaji wa vibali vya kazi na ukaazi, Wizara hizi mbili zimekubaliana kuyafanyia kazi hayo ili kuweza kupunguza matatizo yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais la tarehe 23 Julai, 2016 la Serikali kuhamia Dodoma, Wizara imewahamisha jumla ya watumishi 45 kwa awamu ya kwanza. Aidha, watumishi wengine wataendelea kuhamia kulingana na mpango uliopo na katika bajeti ya mwaka huu 2017/2018, jumla ya Shilingi bilioni 4.7 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Ofisi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi bilioni 867 na kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 47 zikiwa ni za miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 500 zikiwa ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2017 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 644.8 ikiwa ni sawa na asilimia 74 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 293.8 na ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na upotevu wa mapato unaotokana na mianya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliongezea Jeshi la Polisi rasilimali watu na rasilimali fedha, katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Jeshi la Polisi iliajiri Askari wapya 3,164 kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi. Ajira hizi ni katika kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya CCM, Ibara ya 146 ya mwaka 2015/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa makundi maalum; Ibara ya 146 ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 - 2020 pamoja na mambo mengine inaelekeza kutoka elimu kwa umma dhidi ya imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi. Katika kipindi kuanzia Julai, 2016 hadi Machi 2017 jumla ya watu 164 waliuwawa, kati ya hao wanawake wakiwa 96 na wanaume wakiwa 68. Mchanganuo wa matukio hayo kwa mikoa yameonyeshwa katika aya ya 43 ukurasa 23 katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kutoa taarifa kuwa kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 hapakuwa na tukio lolote la mauaji ama kujeruhiwa lililoripotiwa linalohusisha vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Katika mwaka 2027/2018, Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti na kuzuia mauaji ya wazee, vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi pamoja na makundi mengine maalum ili kuweza kudhibiti vitendo hivyo vya kikatili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha makazi ya askari, katika kukabiliana na changamoto hiyo ya makazi ya askari, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ukarabati na miradi ya ujenzi wa nyumba katika mikoa mbalimbali. Kwa upande wa Jeshi la Polisi, miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari imeendelea katika Mikoa ya Njombe, Musoma, Mwanza, Kagera pamoja na Dar es Salaam. Hatua za awali zimeendelea kwa ajili ya maandalizi ya miradi mingine ambapo nyumba za makazi ya askari familia 4,136 na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza punde fedha zitakapokuwa zimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba fedha za ujenzi wa kuboresha makazi ya askari familia 320 unaanza mara moja. Hadi Machi, 2017 jumla ya shilingi bilioni 5 tayari zilishatolewa kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Uhamiaji, ujenzi wa majengo umeendelea ambapo katika Mkoa wa Pwani ujenzi umefikia asilimia 97, ujenzi wa nyumba ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza umefikia zaidi ya asilimia 94, ujenzi wa nyumba ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma umefikia zaidi ya asilimia 92, ujenzi katika Mkoa wa Lindi umefikia zaidi ya asilimia 76. Katika Mkoa wa Geita mradi umefikia wastani wa asilimia 50 pamoja na mikoa mingine ambapo kwa Dar es Salaam ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali unaendelea na umeshazidi asilimia 65 pamoja na nyumba zingine tano za Makamishna wa Idara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Polisi ambapo Kituo cha Polisi Daraja A - Ludewa (Njombe) umefikia asilimia 60, Kituo cha Polisi Daraja B - Mkokotoni (Unguja) asilimia 60, Kituo cha Polisi Daraja C - Mtambaswala (Nanyumbu -Mtwara) kimefikia asilimia 85 na Kituo cha Polisi Daraja B - Newala (Mtwara) kimefikia asilimia 85. Vilevile Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi linaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Rungwe pamoja na maeneo mengine kama ambavyo imeainishwa katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali linaendelea na ujenzi wa kituo kipya cha Polisi Daraja A - Oysterbay, Dar es Salaam ambao umekamilika kwa zaidi ya asilimia 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2017 Serikali ilisaini mkataba pamoja na Serikali ya Watu wa China kuhusu upanuzi wa Chuo cha Polisi - Moshi. Mkataba huo ni msaada ambao utawezesha ujenzi wa majengo matatu yenye madarasa 13 yanayoweza kuchukua wanafunzi 500 na ofisi sita, mabweni manne yenye uwezo wa kuishi wanafunzi 300. Mkandarasi wa Kampuni ya Jiang Su Jiang Du Construction Group Limited imeshaanza maandalizi ya ujenzi huo ambapo unatarajiwa kukamilika mwaka 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa uhalifu hapa nchini, usalama wa raia na mali zao kama nilivyotangulia kusema umeendelea kudumishwa kwani ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Taifa na ya wananchi. Katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Polisi limeendelea kulinda na kudumisha amani na utulivu kupitia doria, misako na operesheni maalum zinazofanyika. Matukio ya ujambazi wa kutumia silaha yenye kuhusisha mauaji katika siku za hivi karibuni ni yale yaliyohusisha mauaji ya Askari wa Jeshi la Polisi pamoja na uporaji wa silaha yaliyojitokeza katika Mkoa wa Pwani hususani katika Wilaya ya Kibiti. Itakumbukwa kuwa tarehe 13 Aprili, 2017 katika eneo la Mkenge, Wilaya ya Kibiti, Mkoani Pwani askari nane waliokuwa kazini waliuwawa kwa kushambuliwa na kundi la majambazi wenye silaha kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio hilo, askari mmoja alijeruhiwa na silaha nne kuporwa. Uvamizi wa askari waliopo kazini na kuuwawa ni mwendelezo wa matukio yaliyowahi kujitokeza katika baadhi ya vituo vya polisi pamoja na baadhi ya benki. Serikali kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama itaendelea kuwabaini wote waliojihusisha na vitendo hivyo haramu pamoja na washirika wao ili kuweza kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, haitafumbia macho matukio ya aina hiyo na itahakikisha kuwa watuhumiwa wote wanakamatwa na wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria. Ni suala la muda tu, kama kuna wanaojidanganya kwamba wanaweza wakafanya jambo la aina hiyo na wakaendelea kutamalaki wanajidanganya. Serikali haitaruhusu hata kwa sekunde uhalifu wa aina hiyo kuweza kutawala katika maeneo yetu ya wananchi.

Nawaomba wananchi waendelee kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za wahalifu na uhalifu ili kuendelea kudumisha amani na usalama hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la matukio makubwa ya uhalifu katika Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji, katika mwaka 2017/2018 Serikali inatarajia kuanzisha Mkoa mpya wa Kipolisi katika maeneo hayo kusogeza huduma ya polisi karibu zaidi na wananchi na kurejesha amani na utulivu katika maeneo hayo ukizingatia jiografia yao iko pembeni. Wilaya ya Mafia nayo itakuwa ndani ya mkoa huo mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Polisi liliendelea kushirikiana na Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuzuia mauaji, kujeruhi ama kuharibu mali kunakosababishwa na migogoro ya wakulima na wafugaji. Jumla ya matukio 42 ya migogoro yaliripotiwa kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti uvunjifu wa amani kutokana na migogoro hiyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama imefanya mikutano katika mikoa mbalimbali na kuweka utaratibu ambao utashughulikia kwa haraka migogoro hiyo inapojitokeza kabla haijawa na madhara makubwa. Katika mwaka 2017/2018 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na Kamati hizo pamoja na mamlaka nyingine ili kuzuia matukio ya migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linaendelea kuimarisha na kuboresha zana za kazi za kisasa ambapo matengenezo makubwa ya heelikopta yamefanyika na magari 77 kutoka Kampuni ya Ashok Leyland kwa ajili ya kazi mbalimbali ya Jeshi la Polisi yamepatikana. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 tunategemea kupokea magari mengine 596 ili kuweza kurahisisha shughuli za kazi zetu za Wizara yetu. Ikumbukwe kwamba magari hayo yakija, yatakuja huko kwenye Wilaya zetu na hivyo itawapunguzia kazi ambazo mmekuwa mkizifanya za kusaidia vituo vyetu vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya

kurekebisha wafungwa magerezani kwa kupitia programu mbalimbali za mafunzo ya darasani, ya kidini, ya michezo, ya ushauri nasaha na stadi za kazi. Stadi za kazi zinazotolewa ni pamoja na maeneo ya ujenzi, viwanda, kilimo, mifugo pamoja na utunzaji wa mazingira. Tumeorodhesha miradi tuliyonayo katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Jeshi la Magereza litaendelea na programu za kurekebisha wafungwa kwa kuhudumia miradi mbalimbali kama tulivyobainisha katika kitabu cha hotuba kwa urefu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uimarishaji wa viwanda, kuitikia dira iliyotolewa na Mheshimiwa Rais, Jeshi la Magereza limeendelea na programu za urekebishaji wa wafungwa kupitia viwanda vidogo vidogo kwa kuwapatia stadi za kazi za useremala katika Magereza ya Ukonga, Uyui, Arusha na utengeneza wa sabuni katika Gereza la Ruanda kule Mbeya. Pia utengenezaji wa viatu katika Gereza la Karanga lililoko kule Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba bidhaa zinazotengenezwa na taasisi hizi ni nzuri na ni za kiwango cha juu. Kama hapa Bungeni hivi ukiondoa viatu vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na vya Mheshimiwa Hussein Mwinyi ambaye ni kaka yangu, hakuna mwingine ana viatu vingine vizuri kama mimi hapa kama mnavyoniona. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza linaendelea kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuingia ubia pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na taasisi zingine. *NSSF* inawekeza katika kilimo cha miwa na kufufua Kiwanda cha Sukari katika Gereza la Mbigiri kule Morogoro; *PPF* inawekeza katika Kiwanda cha Viatu kama ambavyo nimetoka kusema. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Magereza linatarajia kuanzisha viwanda vipya katika Gereza la Ukonga kwa kutengeneza kofia ngumu na Kiwanda cha Useremala katika Gereza la Isanga hapa

Dodoma ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetengwa kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upanuzi na ukarabati wa miundombinu, katika mwaka 2016/2017 Jeshi la Magereza liliendelea na jitihada za kupunguza msongamano kwa kuanzisha ujenzi wa mabweni mawili ya wafungwa katika Gereza la Ruangwa (Lindi), kufanya ukarabati wa majengo ya miundombinu katika Magereza ya Kilosa, mahabusu Morogoro, Mpwapwa ambako ujenzi wake umekamilika Lindi na Bagamoyo na kuanza ujenzi mwingine kule Geita. Aidha, ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali umefanyika sambamba na ukarabati wa mfumo wa maji katika Magereza ya Keko pamoja na Segerea.

Mhesshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo pamoja na viwanda vidogo vidogo kama ambavyo tumeelezea kwa kirefu katika kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya utawala, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Magereza yameendelea kutolewa ambapo zaidi ya askari 1,612 wa Jeshi la Magereza walipatiwa mafunzo hayo. Kati ya hao askari watano walipata mafunzo nchini Morocco na 880 wanaendelea na mafunzo katika vituo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa upatikanaji wa zana za kisasa, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Magereza limepanga kununua mashine 20 za viwanda ambavyo vitakuwa hapa Dodoma; ununuzi wa mashine 3 kwa ajili ya uzalishaji pamoja na mashine moja ya uchakataji wa chumvi katika Gereza la Lindi kule Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana pia na masuala ya msongamano magerezani, programu ya adhabu mbadala ya kifungo cha gerezani cha nje hutekelezwa katika Makao Makuu ya Wizara. Programu hiyo inahusisha

upatikanaji wa taarifa za uchunguzi wa kijamii. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya taarifa za kijamii 2,376 ziliandaliwa na wafungwa zaidi ya 1,995 walinufaika na programu hiyo. Kwa sasa Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ina uwezo wa kuwatoa gerezani au mahakamani wafungwa zaidi ya 6,000 wenye sifa za kutumikia vifungo vya nje ambao wanagharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.3 kwa mwaka. Gharama hii ikiwa ni kwa ajili ya chakula na huduma zingine magerezani. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa na kinaokolewa na kinaenda kutumika katika shughuli zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Uhamiaji, hali ya ulinzi na usalama mipakani, Serikali imeendelea kutoa huduma kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka hapa nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya wageni 1,032,978 waliingia nchini ukilinganishwa na wageni 1,187,000 walioingia nchini katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya wageni 881,000 waliotoka nchi jirani waliingia ukilinganishwa na wageni milioni 1.2 walioondoka nchini katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa uhamiaji haramu, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya watuhumiwa 9,581 wa uhamiaji haramu walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 6,600 waliokamatwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Hivyo idadi ya wahamiaji haramu waliokamatwa imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 45. Aidha, katika kipindi hicho Watanzania 5,923 walirudishwa nchini, kati ya hao 253 ni *stow aways* na 5,670 ni Watanzania waliokuwa wakiishi nchini Msumbiji kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibali vilivyotolewa vya wageni wakaazi, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi 2017, jumla ya wageni 11,559 walipewa vibali vya ukaazi na mchanganuo wake tumeuonesha katika aya ya 98 ukurasa wa 52 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utoaji wa hati za kusafiria, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya *passport* 55,573 zilitolewa kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali ukilinganisha na *passport* 85,758 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Idara ya Uhamiaji imeanza kuandaa mazingira ya utekelezaji wa mfumo wa uhamiaji mtandao kwa kufanya marekebisho ya mitambo ya utoaji wa *passport* ili kuwezesha kutoa *passport* za kieletroniki kama ilivyo katika makubaliano ya Wakuu wa Nchi za Jumuiya za Afrika Mashariki katika kikao kilichofanyika Uenyekiti ulipokuwa chini ya Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutekeleza mradi huo kwa awamu kwa kuanza na masuala ya *passport.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto hapa nchini. Jumla ya maeneo 54,961 yalikaguliwa katika kipindi husika. Aidha, zoezi hili limeendelea sambamba na utoaji elimu ya kujikinga na majanga ya moto na namna ya kutumia vifaa vya kuzimia moto. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Jeshi la Polisi, samahani ni Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea na ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga zinazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unisamehe nimetaja Jeshi la Polisi ni kwa sababu niliwahi kuombo polisi nilipomaliza sekondari. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matukio ya moto na majanga; katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshiriki kuzima moto na kufanya maokozi katika matukio 1,509 kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, kutokana na kukukithiri kwa matukio ya moto katika shule za bweni, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kipindi hicho limefanya operesheni maalum na kutoa

mafunzo kwa shule za bweni 210 hapa nchini. Katika mwaka 2017/2018, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Jeshi la Zimamoto licha ya changamoto za vitendea kazi wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa na kwa ufanisi mkubwa ndio maana tunaona katika maeneo mengine uokozi umefanyika kabla ya madhara makubwa. Ili kuendeleza ufanisi huo katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea misaada ya vifaa vya kuzimia moto kutoka Ujerumani yenye thamani ya *Euro* 45,000. Aidha, Wizara inakamilisha utaratibu wa ununuzi wa magari ya kuzimia moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Jeshi la Zimamoto litaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa magari ya kuzimia moto pamoja na vifaa vingine vya kuzimia moto na uokoaji ambapo zaidi ya shilingi 3,000,000,000. Pia Wizara imeanza majadiliano ya awali ya mikopo yenye masharti nafuu kutoka nchi ya Ubelgiji pamoja na Austria kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzimia moto na vifaa vingine vya uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* inaendelea kutekeleza lengo la Ibara ya 145(f) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 ya kuendelea kuhakikisha kuwa tunatoa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania. Hadi kufikia Machi, 2017, *NIDA* imesajili na kuwatambua jumla ya wananchi 8,551,259 na wageni 8,412 katika mikoa yote hapa Tanzania Bara. Katika kuongeza wigo wa kukamilisha zoezi hilo kwa nchi nzima, Serikali imehamishia miundombinu ya taarifa za Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenda *NIDA* ambapo uhakiki wa taarifa hizo unaendelea na hatua hiyo itaongeza idadi

ya wananchi waliosajiliwa na kuruhusu matumizi mapana ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imefanikisha zoezi la kuwasajili na kuwahakiki watumishi wa umma 507,026 ambapo mfumo wa taarifa wa *NIDA* na ule wa taarifa za kiutumishi imeanza kubadilishana taarifa. Hatua hii itaiwezesha Serikali kulipa mishahara kwa watumishi sahihi na taarifa za watumishi kuendelea kuhuishwa kila mara. Aidha, mfumo wa Vitambulisho vya Taifa umeanza kufanya kazi pia katika tasisi za kibenki ikiwemo *CRDB*, *Bank of Africa* na *Barclays*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, NIDA itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar ambapo Watanzania takribani 22,000,000 wanatarajiwa kusajiliwa na kupewa Vitambulisho vya Taifa ifikapo mwezi Desemba, 2018. Aidha, mamlaka itakamilisha ujenzi wa ofisi 13 za Wilaya ambapo itaweka mitandao ya mawasiliano na tayari imeshaweka katika Wilaya 135 ili kurahisisha utumiaji wa taarifa za wananchi kutoka Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za wakimbizi, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na wadau wengine imeendelea kutoa hifadhi na huduma kwa wakimbizi kutoka nchi jirani hususan zile za Maziwa Makuu ikiwemo Burundi pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kutafuta suluhuhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi hawa. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2017 idadi ya wakimbizi ilikuwa 340,835 na wamehifadhiwa katika kambi za wakimbizi za Nyarugusu, Nduta, Mtendeli zilizoko Mkoa wa Kigoma na wengine katika makazi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Februari, 2017 Serikali ilisitisha utaratibu wa kupokea wakimbizi bila ya kuwahoji na kuendelea na utaratibu wa kawaida wa kila

mkimbizi kuhojiwa na Kamati Maalum ya Kitaifa ya kujadili maombi ya wanaoomba hifadhi. Lengo la utaratibu huu wa kuwahoji kila mmoja anayeomba ukimbizi ni kuhakikisha kuwa Serikali inatoa hifadhi kwa wakimbizi wanaostahili kutokana na kuimarika na hali za kiusalama katika nchi walizokuwa wanatoka wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali iliahidi kutekeleza miradi iliyokuwa inalenga kupunguza athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kiholela kwa ajili kupata nishati ya kupikia, fito za kujengea pamoja na kuhamasisha upandaji wa miti katika maeneo ndani ya makambi. Katika kutekeleza azma hiyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kushirikiana na *UNHCR* imeanza utekelezaji wa mradi wa kutumia majiko ya gesi kupikia badala ya kuni katika makambi ya Nyarugusu kwa awamu ya kwanza ambapo mitungi ya gesi 3,216 imegawiwa kwa wakimbizi. Mradi huu utakuwa unafanyika kwa awamu hadi kufikia kambi zote za wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mradi wa matumizi ya majiko ya gesi, miche ya miti 1,481,592 imekuzwa na kupandwa ndani ya makambi na maeneo yanayozunguka makambi. Aidha, ujenzi wa nyumba 15,664 ambazo zilitumia tofali mbichi na kuezekwa kwa bati badala ya kutumia fito za miti ambazo zilikuwa zinachangia kwa kiwango kikubwa uharibifu wa mazingira unaendelea. Vilevile majiko sanifu 59,924 yaligawiwa kwa kila nyumba katika kambi za wakimbizi Nyarugusu, Nduta pamoja na Mtendeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ya usalama katika baadhi ya maeneo ya nchi za Burundi imeimarika, Serikali inapendekeza kuwepo na mazungumzo kati yake na Serikali ya Burundi pamoja na Shirika linalohudumia wakimbizi kuwezesha wakimbizi watakaopenda kurejea kwao kwa hiyari waweze kufanya hivyo ili wakajenge na nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vita ya usafirishaji wa

binadamu, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu iliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 17 ya makosa ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na kuwafikisha mahakamani ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Vilevile wahanga 20 wa biashara hiyo waliokolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti hiyo pia inaratibu mafunzo yaliyotolewa kwa maafisa 60 kutoka kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria hiyo ikiwemo Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo kwa namna ya kupeleleza, kuendesha na kutoa maamuzi sahihi dhidi ya makosa ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili wa vyama vya kijamii na vya kidini; katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi 2017, Wizara ilipokea jumla ya maombi 296 ya usajili wa vyama vya aina hiyo. Kati ya maombi hayo, jumla ya vyama 162 vimepewa usajili, maombi ya vyama 124 yanashughulikiwa na maombi ya vyama kumi yalikataliwa kutokana na kukosa sifa na kati ya hayo, vyama vitano ni vya kidini na vyama vitano ni vyama vya kijamii. Tumewaelekeza wale ambao kukosa kwao sifa si kutokana na kukosa vigezo vya kimaadili ama kuhatarisha usalama waweze kurekebisha na kuwa na sifa hizo. Tumeweka mipaka kwenye vile vitu ambavyo havivumiliki kwa vyama vinavyoomba na kwa vyama ambavyo vipo vikikosa sifa hizo ambazo hazivumiliki sisi kama Wizara hatutavivumilia na tutavifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na shughuli za usajili, Wizara imeanza kuchukua hatua kama nilivyosema kuvifutia vyama visivyotekeleza wajibu wao kulingana na Sheria Na.13 ya vyama hivyo na vyama 13 vilishapewa kusudio hilo la kufutiwa. Katika mwaka 2017/2018 Wizara itaendelea na usajili na uhakiki wa vyama vya kijamii na vyama vya kidini ili kuwa na kanzidata yenye taarifa sahihi za vyama

vilivyolengwa ambavyo vinafuata masharti ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sheria, kanuni na mikakati inayohusu Wizara, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imekamilisha uandaaji wa mpango mkakati wa kipindi cha mwaka 2016/2017 - 2020/2021 ambapo ni msingi wa utekelezaji wa malengo ya Wizara na uandaaji wa mpango wa bajeti katika mwaka wa fedha wa sasa. Aidha, rasimu ya mpango wa kudhibiti vihatarishi kwa mwaka 2016/2017 - 2020/2021 umeandaliwa kwa lengo la kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imekamilisha rasimu ya mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Jeshi la Polisi *(The Tanzania Police Force Act of 2017)*na mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Usajili na Utambuzi wa Watu ya mwaka wa 2017 *(The Registration and Identification of Persons Act, 2017).* Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara itaendelea kuboresha sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kuoanisha baadhi ya sheria zinazotumika katika Idara zingine zilizoko ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ajira mpya na upandishaji wa vyeo, kwa mwaka 2017/2018 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeweka mapendekezo ya jumla ya watumishi 7,317 na kati ya hao watumishi 105 ni wa Makao Makuu, Askari Polisi 5,772 na Askari wa Uhamiaji 1,140. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara inatarajia kuajiri watumishi 4,339 Makao Makuu ya Wizara ikiwa ni 26; Jeshi la Polisi 2,573; Jeshi la Magereza 500; Jeshi la Zimamoto na Ukoaji 600; Idara ya Uhamiaji 600 na *NIDA* watumishi 40. Aidha, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi na askari watakaopata sifa kulingana na miundo ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kuongoza Wizara hii. Kipekee namshukuru

sana Katibu Mkuu - Meja Jenerali Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu - Balozi Hassan Simba Yahya kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu na utendaji wa kazi kwa Wizara hii nyeti inayohusu usalama wa raia. Nawashukuru wakuu wa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nikianza na Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi - Bwana Ernest Mangu, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza -Dkt. Juma Malewa, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - Bwana Thobias Andengenye, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji - Dkt. Anna Makakala na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - Bwana Andrew Massawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru ma Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi - Bwana Abdulrahmani Kaniki, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Idara, Vitengo, Sehemu mbalimbali, Askari pamoja na wafanyakazi wote wanaowezesha majukumu ya Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi kuwa na ufanisi. Wao wanapofanya kazi nzuri, mimi nakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani mzuri na wao wakifanya kazi mbaya mimi nitakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani mbaya. Kwa kuwa sitegemei kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani mbaya, nawashukuru sana na nawaombea waendelee kuchapa kazi hivi hivi ili na mimi niendelee kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani mzuri. Ni Wizara niliyoipenda tangu nikiwa mtoto, nilikuwa napenda wanavyofanya na wanavyopendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natoa shukrani zangu kwa nchi wahisani wakiwemo China ambao wametusaidia Chuo cha Polisi, India, Korea, Marekani, Misri, Ujerumani, Morocco, Uturuki na taaasi zingine na mashirika mbalimbali ya kimataifa, taasisi za kidini pamoja na vyombo vya habari na wananchi kwa misaada mbalimbali ambayo wametoa katika utendaji wa kazi lakini pia katika uendeshaji wa Ofisi zetu kwa maana ya vitendea kazi pamoja na kujitolea katika masuala ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa naishukuru familia yangu na kama nilivyosema namshukuru na *a new*

*born* aliyeniwezesha kuwa na *fifty fifty* kwenye familia. Nawashukuru na wananchi wa Jimbo langu la Iramba kwani imani yao kwangu na ushirikiano wanaonipa umewezesha kunifanya niendelee kutekeleza majukumu haya kwa uhuru na muda mwingi kuuweka kwenye kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia, Wizara itaendelea kuweka mipango bora ya kudhibiti matukio ya uhalifu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola hapa nchini na vyama vya kimataifa pamoja na kuwashirikisha wananchi ili kuhakikisha kwamba uhalifu unadhibitiwa na hali ya usalama inaimarika hapa nchini. Hakuna ushirika wa aina yoyote wa waovu utakaoweza kushinda haki. Tutajitahidi kama Serikali na kama Wizara kuhakikisha tunatembea katika dira iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu katika mikoa yetu wanaposafiri, wanapokuwa kazini na wanapokuwa majumbani wanakuwa hawana hofu kuhusu usalama wao pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 930,396,817,000 kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; kati ya fedha hizo shilingi 890,388,452,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 367,706,884,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 522,681,568,000 ni mishahara na shilingi 40,008,365,000 zikiwa ni fedha za miradi ya maendeleo na kati ya fedha hizo shilingi 39,700,000,000 zikiwa ni fedha za ndani na shilingi 308,365,000 zikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2016/17 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2017/18.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniteua kuwa Waziri katika Wizara hii nyeti inayosimamia usalama wa nchi. Naahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuhakikisha kuwa hali ya usalama nchini inaendelea kuimarika ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Job Y. Ndungai (Mb.) pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika Dkt. Tulia Ackson (Mb.) kwa kuendesha na kusimamia vema shughuli za Bunge. Pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maoni yao yanayolenga kuboresha utendaji wa Wizara.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo

ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2017/18. Naishukuru Kamati hiyo kwa maelekezo, ushauri na maoni yanayolenga katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii kutoa pole kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na matetemeko ya ardhi, mafuriko, ajali za barabarani, majini na nchi kavu katika kipindi chote kutoka mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017.

## B. HALI YA USALAMA NCHINI

7. ***Mheshimiwa Spika*****,** moja ya wajibu mkubwa na muhimu wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kuwepo nchini. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeendelea kutekeleza wajibu huo kwa kusimamia sheria; kupambana na kudhibiti uhalifu wa aina zote unaoweza kuathiri hali ya amani na utulivu ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

8. ***Mheshimiwa Spika*****,** hali ya usalama nchini imeendelea kuwa tulivu licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama ongezeko la vyombo vya moto (pikipiki na magari), utandawazi, kuongezeka kwa watu mijini, kuongezeka kwa mbinu za uhalifu, migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo Jeshi la Polisi limekuwa likikabiliana nayo. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kulikuwa na matukio makubwa ya uhalifu wa jinai 56,913 ambapo makosa 53,850 yaliripotiwa kutoka Tanzania Bara na mengine 3,063 yaliripotiwa kutoka Zanzibar.

9. ***Mheshimiwa Spika*****,** takwimu zinaonyesha makosa hayo yameongezeka kwa asilimia 7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Ongezeko hilo

linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukuaji wa miji, utandawazi na kuongezeka kwa mbinu mpya za uhalifu. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vya ndani na nje ya nchi pamoja na wananchi ili kuhakikisha hali ya usalama na utulivu inaendelea kudumishwa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, makosa makubwa ya jinai yamegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi nchini yalikuwa kama ifuatavyo: makosa dhidi ya binadamu 10,089; makosa ya kuwania mali 29,476; na makosa dhidi ya maadili ya jamii yalikuwa 17,348. Aidha, jumla ya watuhumiwa 52,353 wa makosa makubwa ya jinai walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha doria, misako, kushirikisha jamii na kutoa elimu kwa umma ya namna ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu.

**11.** ***Mheshimiwa Spika*****,** mauaji ni mojawapo ya makosa dhidi ya binadamu yanayoendelea kutokea kutokana na sababu mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya matukio 2,470 ya mauaji yalitokea na watu 2,532 waliuawa ambapo wanaume ni 2,067 na wanawake 465. Idadi kubwa ya mauaji ilijitokeza kwenye matukio yaliyohusisha wizi wa mifugo, ujambazi, imani za kishirikina, wivu wa kimapenzi, unyang'anyi wa pikipiki na magari pamoja na ulevi. Matukio hayo yalijitokeza kwa wingi katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Mbeya na Tabora. Upelelezi wa kesi hizi unaendelea na watuhumiwa 1,619 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na uhalifu huo pamoja na kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

**12.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 silaha 410 na risasi 2,262 zilikamatwa

kwa mchanganuo ufuatao: gobore 217 na risasi 361; *shotgun* 62 na risasi 386; *FN* 8, bastola 49 na risasi 403; *Sub Machine Gun (SMG)* 27 na risasi 1,025; *Semi Automatic Rifle (SAR)* moja (1) na risasi 9; *Mark iv* 12 na risasi 33, *Rifle* 32 na risasi 31; risasi 14 za *G3* na AK47 mbili (2). Aidha, kulikuwa na matukio 576 ya ujambazi wa kutumia silaha yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi nchini katika kipindi hicho. Matukio hayo yalijitokeza kwa wingi katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Morogoro, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tabora, Mikoa ya Kipolisi ya Ilala, Kinondoni na Tarime – Rorya. Watuhumiwa 306 waliopatikana na silaha haramu walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**13.** ***Mheshimiwa Spika*,** itakumbukwa kuwa tarehe 24 Januari, 2017 Jeshi la Polisi liliteketeza jumla ya silaha 5,608 zilizosalimishwa na nyingine zilizopatikana katika mazingira ya uhalifu kuanzia mwaka 2013 hadi 2016. Miongoni mwa silaha zilizoteketezwa ni *pistol - 21, toy pistol - 21, shotgun - 606, rifle - 300*, *gobore - 4,487, SMG - 166, G3 - 01, FN rifle - 03 na SAR - 03.* **Aidha, nachukua nafasi hii kuhimiza wananchi wanaomiliki silaha kinyume cha sheria wazisalimishe kwenye vituo vya Polisi au Ofisi za Watendaji wa Kata na Vijiji**. Katika mwaka 2017/18 Jeshi litaendelea kufanya doria, misako na operesheni za mara kwa mara kwa lengo la kuwabaini waingizaji na watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria ili kudhibiti vitendo vya uhalifu nchini.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na wimbi la umiliki haramu wa silaha nchini Jeshi la Polisi lilianzisha zoezi la uhakiki wa silaha mwezi Machi, 2016 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 asilimia 63.20 ya silaha zilizosajiliwa zilikuwa zimehakikiwa. Katika zoezi hilo jumla ya silaha 486 zilisalimishwa kutokana na kutomilikiwa kihalali ambazo ni *pistol - 16, rifle - 18, shotgun - 161, SMG - 24, G3 - 1* na magobore 266 katika mikoa mbalimbali nchini.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeongeza muda wa uhakiki mpaka tarehe 30 Juni, 2017 ili kutoa nafasi kwa wamiliki wa silaha ambao hawakupata nafasi ya kuhakiki silaha zao kwa muda uliotolewa awali.

**Natoa rai kwa wamiliki wa silaha kuhakiki silaha zao kwa muda uliopangwa vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufuta leseni zao za kumiliki silaha.**

**Hali ya Usalama Barabarani**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya matukio 6,500 ya usalama barabarani yaliripotiwa nchini. Katika matukio hayo jumla ya ajali 1,552 zilisababisha vifo vya watu 2,372 na watu 6,074 kujeruhiwa. Takwimu zinaonesha kupungua kwa ajali hizo kwa asilimia 7 kwani katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16 kulikuwa na jumla ya ajali za barabarani 7,006 zilizoripotiwa ambapo watu 2,589 walipoteza maisha na watu 7,536 walijeruhiwa. Kwa ujumla ajali nyingi kati ya hizo zimesababishwa na uzembe wa madereva, kutozingatia sheria za usalama barabarani, mwendo kasi, ulevi pamoja na ubovu wa magari na miundombinu.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia sheria za usalama barabarani ambapo kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya madereva 6,500 wa magari mbalimbali na waendesha pikipiki 5,865 ambao walikamatwa na kupelekwa mahakamani kwa kukiuka sheria za usalama barabarani.

**18.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ajali za barabarani kwa kushirikiana na wadau wengine kama Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Shule za Udereva zilizosajiliwa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kuongeza idadi ya askari wa usalama barabarani; kuendeleza zuio la magari ya abiria kusafiri baada ya saa 4 usiku; kudhibiti mwendo kasi kwa kuweka vituo vya ukaguzi wa ratiba za magari ya abiria; kuimarisha

doria na ukaguzi wa magari barabarani; kufuta leseni za madereva wanaosababisha ajali kubwa; kuzuia leseni kwa kipindi maalum kwa madereva wanaofanya makosa madogo; kutoa elimu ya usalama barabarani kwa njia za redio na luninga kwa madereva na jamii yote; na kuhakikisha wamiliki wa vyombo vya usafiri wanaajiri madereva wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha.

**20.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia sheria za usalama barabarani na kuelimisha jamii kuzingatia sheria na taratibu hizo.

**C. UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MHE. RAIS WA AWAMU YA TANO**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoyatoa tarehe 20 Novemba, 2015 kupitia hotuba yake ya ufunguzi rasmi wa Bunge la 11 pamoja na maelekezo mengine aliyoyatoa kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo:

**Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini**

**22.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya kilogramu 16 na gramu 223 za *cocaine* pamoja na kilogramu 37 na gramu 118 za *heroine* zilikamatwa na watuhumiwa 1,241 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Aidha, katika kipindi hicho kilo 36,337 na gramu 426.76 za bangi zilikamatwa na watuhumiwa 12,691 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa operesheni mbalimbali za kupambana na uingizaji, usambazaji na ulimaji wa bangi zinaendelea nchi nzima kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na raia wema. Aidha, Jeshi

la Polisi litaendelea kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa katika kubaini waingizaji na wasambazaji wa dawa za kulevya nchini.

**Kutatua Tatizo la Wananchi Kubambikizwa Kesi**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua stahiki za kukabiliana na malalamiko ya wananchi kubambikiwa kesi zimechukuliwa, ambapo Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kupokea malalamiko na kuyashughulikia. Malalamiko hayo yameendelea kupokelewa katika Ofisi za Wakuu wa Polisi za Wilaya na Mikoa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dar es Salaam.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jeshi la Polisi limepokea malalamiko 206, ambapo malalamiko 203 ni ya kutoka kwa wananchi na malalamiko matatu (3) ni ya ndani ya Jeshi. Takwimu zinaonesha ongezeko la malalamiko 138 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka 2015/16, ambapo kulikuwa na jumla ya malalamiko 68, kati ya hayo, malalamiko 64 yalitoka kwa wananchi na malalamiko manne (4) yalikuwa ni ya ndani ya Jeshi la Polisi.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Jeshi la Polisi lilichukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa watendaji ambao walifanya makosa hayo kwa kuwafukuza kazi askari 14 na maafisa wawili (2); kuwashusha vyeo askari wanne (4); na askari sita (6) walipewa adhabu nyingine.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeimarisha utaratibu na usimamizi wa utendaji katika kushughulikia malalamiko mbalimbali yanayofikishwa vituoni kwa kutoa miongozo mara kwa mara kwa wakuu wa vituo na wakuu wa upelelezi.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongozo hiyo ni pamoja na: kusimamia kwa karibu upelelezi wa mashauri yote kabla ya kuyapeleka kwa wanasheria wa Serikali; kushirikiana kwa pamoja kati ya wapelelezi na waendesha mashtaka kutoka hatua za awali za upelelezi mpaka hatua ya mwisho wa

kesi mahakamani; na kuendelea kusimamia na kudhibiti vitendo vya utovu wa nidhamu na ukiukaji wa maadili vinavyofanywa na baadhi ya wapelelezi kwa kuweka mfumo maalum wa kupokea taarifa za siri kutoka kwa wananchi juu ya wapelelezi wasio waadilifu.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na miongozo hiyo, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa askari juu ya madhara ya kuwabambikia kesi wananchi, imeimarisha ushirikiano na wananchi kwa kufanya vikao nao ili kuwajengea imani waweze kutoa taarifa kwa viongozi pale wanapofanyiwa vitendo wasivyoridhika navyo, pia imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa Haki Jinai na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika hatua mbalimbali za mashauri ya jinai na inaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi kuanzia ngazi ya Makao Makuu ya Polisi, Mikoa, Wilaya na Vituo ili kubaini ubambikizwaji wa kesi kwa wananchi. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia na kufuatilia nidhamu ya askari ili kuwa na watendaji wenye weledi.

**Upandishwaji Vyeo kwa Askari**

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inapandisha vyeo askari kutokana na sifa na muundo wake wa kiutumishi. Mapendekezo ya upandishwaji vyeo yameendelea kuzingatia uwepo wa nafasi, bajeti, sifa binafsi kama inavyobainishwa katika miuundo na elimu kuwa kigezo cha ziada. Katika mwaka 2016/17, jumla ya askari 4,604 walipandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali ambapo askari 4,137 ni wa Jeshi la Polisi na askari 467 ni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

**Malipo ya Madai ya Askari**

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya madai ya askari, Serikali imelipa madeni ya watumishi jumla ya Shilingi 14,872,010,390 kwa mwaka 2016/17 kwa mchanganuo ufuatao: Jeshi la Polisi Shilingi 6,205,212,689.14; Jeshi la Magereza Shilingi

7,510,430,711; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Shilingi 751,869,659.36; na Idara ya Uhamiaji Shilingi 404,497,330. Madeni hayo ni ya kipindi cha mwaka 2014/15 ambayo yalitokana na malimbikizo ya posho za likizo na safari za kikazi ndani na nje ya nchi.

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Jeshi la Polisi limeimarisha Kitengo cha Uhasibu kwa kuongeza watendaji na lina mipango ya kuanzisha kanda za malipo *(Payroll Points)* ili kuhakiki madai ya askari kwa haraka. Hadi kufikia mwezi Januari, 2017 askari wapya 3,164 wote walikuwa wamelipwa mishahara yao na malimbikizo ya posho zao za chakula ambazo hawakuwa wamelipwa tangu waanze kazi. Pia, suala la mapunjo ya mishahara ya watumishi yanayotokana na watumishi/askari kupandishwa vyeo limeanza kushughulikiwa kwa awamu baada ya zoezi la uhakiki wa watumishi kukamilika.

### Kuzingatia Sheria katika Kutoa Hati za Uraia

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeandaa na kusambaza mwongozo unaotoa ufafanuzi kuhusu Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995 iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2002, pamoja na kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uraia wa watu wanaotiliwa mashaka. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetoa tafsiri ya uraia wa Tanzania kwa kuzaliwa na hivyo kuondoa mkanganyiko uliokuwepo.

### Vibali vya Kuishi Nchini kwa Wageni

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu imeendelea kusimamia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016, ili kutatua changamoto za kiutendaji zinazojitokeza katika utoaji wa vibali vya kazi na ukaazi. Aidha, Wizara

imeandaa utaratibu maalum wa kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa vibali vya ukaazi vinavyotolewa.

### Utekelezaji wa Mpango wa Kuhamia Dodoma

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia agizo la Mhe. Rais la tarehe 23 Julai, 2016 la kuhamishia Makao Makuu ya Serikali katika Mji wa Dodoma, Wizara imewahamisha jumla ya watumishi 45 katika awamu ya kwanza. Aidha, watumishi wengine wataendelea kuhama kulingana na mpango uliopo. Katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2017/18 jumla ya Shilingi 4,700,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa ofisi kama ifuatavyo: Jeshi la Polisi Shilingi 100,000,000, Jeshi la Magereza 2,200,000,000, Idara ya Uhamiaji Shilingi 200,000,000 na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Shilingi 2,200,000,000.

## D. MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/17, UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) PAMOJA NA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/18

### Mapato na Matumizi

**36.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa. Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi 867,190,349,608.87. Kati ya fedha hizo, Shilingi 47,923,421,105 zilikuwa ni za miradi ya maendeleo, Shilingi 500,056,492,105 zilikuwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 319,210,436,398.87 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zake.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2017 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 644,862,980,215.64 sawa na asilimia 74 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Shilingi 13,466,336,364 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 28 ya bajeti ya maendeleo,

Shilingi 366,462,364,559 zilikuwa ni Mishahara na Shilingi 264,934,279,292.64 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Pia, Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 178,339,863,952.10 ikiwa ni maduhuli sawa na asilimia 62 ya lengo la Shilingi 289,946,031,504.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 293,822,132,859. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na kutumia mifumo ya kieletroniki.

**Kuliongezea Jeshi la Polisi Rasilimali Watu na Rasilimali Fedha**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeajiri jumla ya askari wapya 3,164 kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi. Ajira hizi ni katika kutekeleza **Ibara ya 146 (i) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020** inayoelekeza Serikali kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha.

**Maslahi ya Watendaji**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuboresha maslahi ya watendaji wa vyombo vya usalama kwa kuwapatia *ration allowance* za kila mwezi kwa wakati kama **Ibara ya 146 (ii) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020** inavyoelekeza. Aidha, Serikali imeanza kuwapatia askari wa Jeshi la Polisi fedha ya msamaha wa kodi kwa mwezi. Katika mwaka 2017/18 Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya maslahi ya watendaji wa vyombo vya usalama ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Kushiriki katika Kuimarisha Amani na Usalama katika Nchi Mbalimbali**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza **Ibara ya 146 (iv) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020,** Wizara

inashiriki katika majukumu ya kiusalama na amani kwenye nchi mbalimbali kwa kupeleka askari wake. Lengo likiwa ni kuwezesha majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa. Katika mwaka 2016/17, jumla ya askari 102 wa Jeshi la Polisi wanashiriki katika operesheni za ulinzi wa amani za Umoja wa Mataifa katika nchi mbalimbali, ambapo Sudan - Darfur kuna askari 87, Sudan - Abyei askari sita (6), Sudani Kusini askari wawili (2), Marekani – New York askari mmoja (1) na Lebanon askari sita (6).

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, jumla ya maafisa 155 walifaulu mtihani wa usaili uliofanyika tarehe 20 Februari, 2017 na wanasubiri kwenda kushiriki majukumu hayo nje ya nchi. Kwa upande wa Jeshi la Magereza wapo askari wawili (2) Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na wanne (4) Sudan Kusini.

**Usalama wa Makundi Maalum na Ulinzi Shirikishi**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** **Ibara 146 (v) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 –2020,** pamoja na mambo mengine inaelekeza kutoa elimu kwa umma dhidi ya imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya watu 164 waliuawa, kati ya hao wanawake ni 96 na wanaume 68. Matukio hayo yalitokea Mikoa ya Geita 7, Iringa 4, Kagera 5, Kigoma 12, Mbeya 4, Mwanza 13, Njombe 17, Rukwa 5, Shinyanga 11, Simiyu 5, Singida 3, Songwe 21 na Tabora 57. Kufuatia matukio hayo watuhumiwa 161 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi pia limeendelea kuimarisha mpango wa ulinzi shirikishi na kushirikiana na wadau mbalimbali nchini katika kutoa elimu kwa umma kuhusu imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua kali za kisheria zimeendelea kuchukuliwa kwa wote wanaobainika kujihusisha na uhalifu wa aina hii. **Napenda kutoa taarifa**

**kupitia Bunge hili kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 hapakuwa na tukio lolote la mauaji au kujeruhiwa lililoripotiwa kuhusiana na vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ualbino.**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti na kuzuia mauaji ya wazee, watu wenye ualbino na makundi mengine maalum ili kudhibiti vitendo hivyo nchini. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kuacha mila, desturi na imani potofu zinazosababisha madhara kwa makundi hayo.

**Kushirikiana na Mataifa Mengine na Asasi za Kimataifa katika Kupambana na Uhalifu**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Mataifa mengine na vyombo vingine vya kimataifa vikiwemo Shirika la Polisi la Kimataifa *(INTERPOL*) na Mashirika ya Kipolisi ya Kanda za Kusini na Mashariki mwa Afrika (*SARPCCO* na *EAPCCO*) kama **Ibara 146 (vi) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020** inavyoelekeza katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka. Katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Jeshi la Polisi imefanya operesheni za pamoja na nchi za *SARPCCO* na *EAPCCO* ambapo jumla ya watuhumiwa 193 walikamatwa kwa makosa mbalimbali na wote wamefikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kupambana na kudhibiti uhalifu wa aina zote ikiwemo makosa yanayovuka mipaka kwa kushirikiana na mataifa mengine na asasi za kimataifa pamoja na kufanya doria, misako na operesheni maalum za mara kwa mara za nchi kavu na majini.

**Kuboresha Makazi kwa Askari**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya makazi ya askari, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa nyumba katika

mikoa mbalimbali. Kwa upande wa Jeshi la Polisi miradi ifuatayo ya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari inaendelea katika mikoa ya: Njombe (Ludewa) familia 12; Mara (Musoma) familia 24; Mwanza (Mabatini) familia 24; na Kagera (Buyekera) familia 12. Aidha, hatua za awali zinaendelea kwa ajili ya maandalizi ya mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi ya familia 4,136 za askari na utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2017/18.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jeshi la Magereza kazi za ujenzi wa block 12 za magorofa kwa ajili ya familia 320 za askari umeanza kwa kukamilisha ujenzi wa misingi ya block zote na kazi ya kupandisha kuta inaendelea. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya **Shilingi 5,000,000,000** zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi huo.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii **kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuhakikisha kuwa fedha hizo zimetolewa ili kuboresha makazi ya askari.** Katika mwaka 2017/18, Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa nyumba hizo pamoja na kuanza ujenzi wa nyumba 50 za makazi ya askari katika Gereza Isanga – Dodoma.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Idara ya Uhamiaji inaendelea kujenga ofisi, ambapo katika Mkoa wa Pwani ujenzi umefikia asilimia 97 na kazi inayofanyika kwa sasa ni kumalizia kazi za nje. Aidha, ujenzi wa nyumba ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza umefikia asilimia 94 na Mkandarasi anavuta umeme pamoja na kazi za kumalizia *(finishing phase).* Kazi nyingine iliyofanyika ni ujenzi wa nyumba ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma ambao umefikia asilimia 92 na Mkandarasi anamalizia kazi ndogo ndogo. Katika Mkoa wa Lindi mradi umefikia asilimia 76 na kazi inayofanyika kwa sasa ni kuweka mifumo ya umeme, TEHAMA na viyoyozi.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine inayoendelea chini ya Idara ya Uhamiaji ni kama ifuatavyo:

Mkoa wa Geita mradi umefika wastani wa asilimia 50 na kazi inayofanyika kwa sasa ni kuweka paa; Mkoa wa Mtwara mradi umeendelezwa kwa asilimia 23 na kazi inayofanyika kwa sasa ni kumwaga jamvi la ghorofa ya pili; ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika eneo la Masaki – Dar es Salaam upo katika wastani wa asilimia 65 na kazi inayofanyika kwa sasa ni kupiga plasta; na ujenzi wa nyumba tano (5) za Makamishna wa Uhamiaji Mtoni Kijichi (Dar es Salaam), ambapo mkandarasi anafanya kazi za nje na kuweka umeme na maji. Katika mwaka 2017/18 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutekeleza miradi hiyo ya ujenzi wa makazi kulingana na upatikanaji wa fedha.

### Miradi ya Ujenzi wa Ofisi na Vituo vya Polisi

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea na ujenzi wa vituo vya Polisi katika Mikoa ifuatayo: Kituo cha Polisi Daraja A Ludewa, Njombe kimefikia asilimia 60; Kituo cha Polisi Daraja B Mkokotoni, Unguja (asilimia 60); Kituo cha Polisi Daraja C Mtambaswala, Nanyumbu Mtwara (asilimia 85); na Kituo cha Polisi Daraja B Newala, Mtwara (asilimia 85).

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi linaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya, Rungwe na Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya, Chunya ambayo imetekelezwa kwa asilimia 80; ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Mbweni – Dar es Salaam (asilimia 80); ujenzi wa Kituo cha Polisi Madale – Dar es Salaam (asilimia 95); na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja C Kiluvya – Dar es Salaam (asilimia 55). **Natumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa maeneo husika kwa kujitolea kwao katika ujenzi wa ofisi na vituo hivyo vya Polisi**.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (Police Force Corporation Sole) linaendelea na kazi zifuatazo: ujenzi wa Kituo Kipya cha Polisi Daraja A Oysterbay – Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia 92; ujenzi wa nyumba 23 za makazi ya maofisa wa juu wa Polisi – Mikocheni ambao umekamilika kwa asilimia 95; na

ujenzi wa nyumba za familia 330 Kunduchi, Dar es Salaam ambao umekamilika kwa asilimia 86.

**Upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi**

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Machi, 2017 Serikali ilisaini mkataba na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi. Mkataba huo ni msaada ambao utawezesha ujenzi wa majengo matatu (3) yenye madarasa 13 na kuweza kuchukua wanafunzi 500, ofisi sita (6) na mabweni manne (4) yenye uwezo wa kuishi wanafunzi 300. Mkandarasi Kampuni ya Jiang Su Jiang Du Construction Group Limited imeanza maandalizi ya ujenzi huo ambao unatarajiwa kukamilika Julai, 2019.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa jumla wa Wizara, maeneo mengine yaliyotekelezwa kupitia Idara Kuu ambazo ni Jeshi la Polisi (Fungu 28), Jeshi la Magereza (Fungu 29), Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Fungu (14), Idara ya Uhamiaji (Fungu 93) na Makao Makuu ya Wizara inayojumuisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Fungu 51 ni kama ifuatavyo:

**JESHI LA POLISI**

**Udhibiti wa Uhalifu Nchini**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa raia na mali zao umeendelea kudumishwa kwani ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Taifa na maendeleo ya wananchi. Katika mwaka 2016/17, Jeshi la Polisi linaendelea kulinda na kudumisha amani na utulivu kupitia doria, misako na oparesheni maalum zilizofanyika nchi nzima.

**Kuanzisha Mkoa Mpya wa Kipolisi Rufiji**

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, matukio ya ujambazi wa kutumia silaha yenye kuhusiana na mauaji ya askari wa Jeshi la Polisi pamoja na uporaji wa silaha yameendelea kujitokeza katika Mkoa wa Pwani, hususan katika Wilaya ya Kibiti. Itakumbukwa tarehe 13 Aprili, 2017 katika eneo la Mkenge

Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani askari nane (8) waliokuwa kazini waliuawa baada ya kushambuliwa na kundi la majambazi wenye silaha. Katika tukio hilo askari mmoja alijeruhiwa na silaha nne (4) aina ya *SMG* na *Long range* tatu (3) ziliporwa.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, uvamizi wa askari waliopo kazini na kuuawa ni muendelezo wa matukio yaliyowahi kutokea katika vituo vya polisi, malindo na baadhi ya benki. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama itaendelea kuwabaini wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo haramu pamoja na washirika wao ili kuwachukulia hatua stahiki za kisheria.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, natumia nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa **Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama haitafumbia macho matukio ya aina hiyo na itahakikisha kuwa watuhumiwa wote wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria.** Nawaomba wananchi waendelee kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za wahalifu na uhalifu ili kuendelea kudumisha amani na usalama nchini.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la matukio makubwa ya uhalifu katika Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji katika mwaka 2017/18 Serikali inatajaria kuanzisha Mkoa Mpya wa Kipolisi Rufiji ili kusogeza huduma ya polisi karibu zaidi na wananchi na kurejesha amani na utulivu katika maeneo hayo. Wilaya ya Mafia nayo itakuwa ndani ya Mkoa huo mpya.

**Utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Jeshi la Polisi**

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi limeanza kutekeleza Mpango wa Kuboresha Usalama wa Jamii *(Community Safety Initiave - CSI)* kwa kuanzia na Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni. Mpango huo ni wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2018/19 na umelenga katika

maeneo makuu manne ambayo ni: kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa polisi; kuboresha utoaji wa huduma; kuboresha mawasiliano na ushirikishwaji wa jamii katika utendaji wa polisi; na utafutaji wa rasilimali kutoka vyanzo mbalimbali.

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango huo ni kuwa na Vituo vya Polisi vinavyohamishika vitatu (3) katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha uhalifu ambayo ni Masaki, Oysterbay na Manzese. Lengo la vituo hivyo ni kuwawezesha askari kufika katika sehemu za matukio kwa haraka. Aidha, kituo cha kisasa cha miito ya mawasiliano *(Call Centre)* katika Mkoa wa Dar es Salaam kimeimarishwa na kinawarahisishia wananchi kutoa taarifa za matukio na kuwawezesha askari kufika katika eneo la tukio ndani ya dakika 15.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine ya mpango huo ni kufungwa kwa vifaa maalumu *(Global Position System - GPS)* katika magari yote ya Polisi ya Mkoa wa Kipolisi Kinondoni kwa ajili ya kudhibiti na kufuatilia wahalifu na uhalifu. Maboresho hayo yanatarajiwa kuanza kutekelezwa nchi nzima kwa kuanzia na mikoa yenye matukio makubwa ya uhalifu ambayo ni Arusha, Dodoma, Geita na Mwanza pamoja na Mikoa ya Kipolisi ya Ilala na Temeke.

### Kudhibiti Uvunjifu wa Amani Unaotokana na Migogoro ya Wakulima na Wafugaji

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/17 Jeshi la Polisi limendelea kushirikiana na Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuzuia mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya wakulima na wafugaji. Jumla ya matukio 42 ya migogoro yaliripotiwa kutoka Mikoa ifuatayo: Arusha (2), Dodoma (2), Geita (2), Kagera (2), Kigoma (2), Manyara (2), Mbeya (3), Morogoro (8), Mtwara (1), Lindi (1), Pwani (8), Rukwa (1), Simiyu (2), Singida (1), Songwe (1), Tabora (1) na Tanga (3).

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kudhibiti uvunjifu wa amani unaotokana na migogoro hiyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa limefanya mikutano katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mbeya, Mara, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani na Shinyanga. Kupitia mikutano hiyo Jeshi la Polisi limetoa elimu kwa wananchi kuhusu njia mbalimbali za kuiepuka na kuikabili migogoro hiyo. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na kamati hizo pamoja na mamlaka nyingine ili kuzuia matukio ya migogoro ya wakulima na wafugaji nchini.

### Mafunzo kwa Askari wa Jeshi la Polisi

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwaongezea ujuzi wa utendaji kazi jumla ya askari 956 wa Jeshi la Polisi wa vyeo mbalimbali walihudhuria mafunzo ya huduma bora kwa jamii, mbinu za upelelezi na mafunzo ya mbinu mbalimbali za kijeshi. Kati ya hao, askari 137 walipata mafunzo nje ya nchi kwa ufadhili wa nchi za Marekani (55), India (5), China (25), Morocco (30), Misri (19), Uingereza (2), Japan (1) na askari 819 wamepata mafunzo ndani ya nchi zikiwemo kozi zilizofadhiliwa na nchi za Marekani, Canada, Korea Kusini, Ujerumani na Uturuki.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi lilifanya Kikao cha Kazi kuanzia tarehe 27 hadi 29 Machi, 2017 mjini Dodoma kwa lengo la kutathmini utendaji wake. Kikao hicho kilihusisha Maafisa Waandamizi wa Makao Makuu ya Polisi (Dar es Salaam na Zanzibar) na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi. Kauli Mbiu ya kikao hicho ilikuwa ni ***"Zingatia Maadili Tunapopambana na Uhalifu ili Kuimarisha Usalama kwa Maendeleo ya Taifa"****.* Kupitia kikao hicho, Maazimio mbalimbali yalitolewa kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Jeshi la Polisi nchi nzima.

### Kuboresha Vitendea Kazi katika Jeshi la Polisi

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi, limeendelea kuimarisha na kuboresha zana za kazi za kisasa ambapo

matengenezo makubwa ya Helkopta yamefanyika. Aidha, magari 77 kutoka Kampuni ya *Ashok Leyland* kwa ajili ya kazi mbalimbali za Jeshi la Polisi yamepatikana kupitia ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na India. Magari mengine 596 yanatarajiwa kuwasili mwaka 2017/18.

**Usimamizi wa Nidhamu kwa Askari**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi linaendelea kuwatambua maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuwapa tuzo na zawadi. Jumla ya askari na watumishi raia 200 wamepewa tuzo kwa utendaji mzuri na kuliletea sifa Jeshi la Polisi katika nyanja mbalimbali. Aidha, fedha taslimu Shilingi 20,280,000 zilitolewa kwa watendaji 26, vyeti 119 na barua za pongezi 55 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mara, Tanga, Lindi, Geita, Katavi na Kikosi cha Ujenzi.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kuwatambua na kuwatunuku zawadi Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi raia watakaoendelea kufanya majukumu yao kwa ufanisi na ubora wa hali ya juu.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia nidhamu, Jeshi la Polisi limechukua hatua za kinidhamu kwa askari waliokiuka sheria za maadili ya kijeshi. Katika mwaka 2016/17 askari 14 na maofisa wawili (2) wamefukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali yakiwemo: rushwa, wizi, kubaka, utoro kazini, kughushi nyaraka na kujipa likizo. Aidha, wakaguzi na maofisa 16 walipewa barua za kujieleza, sita (6) walipewa barua za onyo, kumi (10) walishtakiwa na wanne (4) walishushwa vyeo.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi pia litaendelea kufanya uhakiki wa kina kwa ajira za askari wapya waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na kuomba kujiunga na Jeshi la Polisi ili kuwa na askari wenye nidhamu

na moyo wa dhati wa kulitumikia Taifa. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia nidhamu kwa askari wake ili kuongeza tija na ufanisi.

## JESHI LA MAGEREZA

### Programu za Urekebishaji wa Wafungwa

**76.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2016/17 Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza jukumu la kurekebisha wafungwa magerezani kwa kupitia program mbalimbali za mafunzo ya darasani, dini, michezo, ushauri nasaha na stadi za kazi. Stadi za kazi zilizotolewa ni pamoja na maeneo ya ujenzi, viwanda, kilimo, mifugo na utunzaji wa mazingira. Aidha, kupitia urekebishaji kwa stadi za kazi, ng'ombe wa nyama 8,381, ngombe wa maziwa 2,726, mbuzi 3,274, kondoo 503 pamoja na mifugo mingine iliendelea kuhudumiwa kwa kuboresha huduma mbalimbali za mifugo kama vile chanjo, dawa za tiba na huduma za kuogeshea mifugo kwenye Magereza yote yaliyo na mifugo.

**77.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza litaendelea na program za kurekebisha wafungwa kwa kuhudumia jumla ya Ng'ombe wa nyama 9,958 na Ng'ombe wa maziwa 3,351, Mbuzi 3,898 na Kondoo 589 pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa kununua chanjo na tiba pamoja na kuboresha mashamba ya malisho.

### Uimarishaji wa Viwanda vya Ndani

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeendelea na program za urekebishaji wafungwa kupitia viwanda vidogo vidogo kwa kuwapatia stadi za kazi kama vile: useremala katika Magereza ya Ukonga (Dar es Salaam), Uyui (Tabora) na Arusha (Arusha); utengenezaji wa sabuni katika Gereza la Ruanda (Mbeya); utengenezaji wa viatu katika Gereza la Karanga (Kilimanjaro); sanaa za mikono na uchongaji wa vinyago katika Gereza la Lilungu (Mtwara);

ushonaji wa nguo katika Magereza ya Ukonga (Dar es Salaam) na Butimba (Mwanza); utengenezaji na uchakataji wa chumvi katika Gereza la Lindi (Lindi) na Lilungu (Mtwara).

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeendelea kuimarisha Viwanda vidogo vidogo kwa kuingia ubia na Mifuko ya Hifadhi za Jamii ya National Social Security Fund (NSSF) na Parastatal Pensional Fund (PPF). NSSF imewekeza katika kilimo cha miwa na kufufua Kiwanda cha Sukari katika Gereza Mbigiri – Morogoro na PPF imewekeza katika Kiwanda cha Viatu, ambapo itafanya upanuzi wa kiwanda kwa kujenga kiwanda kipya cha kuchakata ngozi katika Gereza la Karanga – Kilimanjaro. Ubia huu utaboresha zaidi shughuli za uzalishaji mali zikiwemo bidhaa za sukari, viatu na ngozi na hivyo kutekeleza kwa vitendo jitihada za Serikali za kuelekea katika Uchumi wa Viwanda.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza linatarajia kuanzisha viwanda vipya katika Gereza Ukonga – Dar es Salaam kwa kutengeneza Kofia ngumu (Helmet) na kiwanda cha useremala katika Gereza la Isanga (Dodoma), ambapo jumla ya Shilingi 1,600,000,000 zimetengwa kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda hivyo.

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilifanya ziara ya kutembelea viwanda vya nguo vya Namera Group of Industries (T) Limited (ambao ni muungano wa Namera Company Limited & Nida Garments Company Limited), 21st Century (Morogoro), Sunflag (Arusha) na Tanzania – China Friendship Textile Company Limited (URAFIKI – Dar es Salaam) ili kuona uwezekano wa kuzalisha sare za askari ndani ya nchi badala ya kuagiza sare hizo nje ya nchi. Baada ya ziara hiyo, viwanda hivyo viliwasilisha sampuli za vitambaa kwa Maboharia Wakuu wa Majeshi kwa ajili ya kuangaliwa ubora wake. Hatua hii ni miongoni mwa mkakati wa kukuza viwanda vya ndani.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo Ofisi ya Boharia Mkuu wa Serikali imeridhika na ubora wa viatu vinavyozalishwa na baadhi ya viwanda nchini kwa matumizi

ya askari. Viwanda hivyo ni Open Sanit kilichopo Tabata, Ital Shoes cha Kigamboni na Kiwanda cha Viatu cha Jeshi la Magereza kilichopo Gereza la Karanga Moshi.

**Ukarabati wa Majengo na Miundombinu ya Magereza**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza linatarajia kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza pamoja na makazi ya askari yaliyoharibika na tetemeko la ardhi Mkoani Kagera na mvua kali katika Magereza ya Kanegere (Geita), Bariadi (Simiyu), Mahabusu ya Morogoro na Mkono wa Mara (Morogoro), Manyoni (Singida), Lindi, Ubena na Kibiti (Pwani).

**Upanuzi, Ukamilishaji, Ukarabati na Ujenzi wa Mabweni ya Wafungwa**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Jeshi la Magereza limeendelea na jitihada za kupunguza msongamano kwa kuanza ujenzi wa mabweni mawili (2) ya wafungwa katika Magereza ya Ruangwa – Lindi; kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza ya Kilosa, Mahabusu ya Morogoro, Mpwapwa, Lindi na Bagamoyo; kuanza ujenzi wa jengo la utawala pamoja na kukamilisha ujenzi wa bweni moja (1) katika Gereza la Chato – Geita. Aidha, ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali umefanyika sambamba na kukarabati mfumo wa maji taka katika Magereza ya Keko na Segerea.

**Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza**

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (Prison Corporation Sole) limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na viwanda vidogo vidogo. Aidha, Shirika limepokea zabuni ya kutengeneza samani za ofisi za Waheshimiwa Wabunge zenye thamani ya Shilingi 2,807,127,174.50 ambapo mpaka sasa jumla ya Majimbo 18 yamepokea samani hizo. Pamoja na hilo, kazi

ya utengenezaji wa madawati 30,000 imekamilika na yanaendelea kusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza linatarajia kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi na nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi.

**Mafunzo katika Jeshi la Magereza**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya utawala, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za magereza na taaluma mbalimbali yanaendelea kutolewa kwa watumishi na askari 1,612 wa Jeshi la Magereza. Kati ya hao, askari watano (5) walipata mafunzo nchini Morocco kwa ufadhili wa Serikali ya nchi hiyo pamoja na askari na watumishi raia 880 wanaendelea na mafunzo katika vyuo mbalimbali ndani ya nchi katika vyuo vya Magereza.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo hayo yatasaidia kuongeza weledi na kuwajengea uwezo wa kiutendaji katika Jeshi la Magereza na pia kusimamia vema program za urekebishaji wa wafungwa magerezani. Katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza linatarajia kutoa mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa askari 1,530.

**Upatikanaji wa Zana za Kisasa katika Jeshi la Magereza**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza limepanga: kununua mashine ishirini (20) za Kiwanda kipya cha Seremala katika Gereza la Isanga (Dodoma); ununuzi wa mashine tatu (3) kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya mawese na mise katika Kambi ya Kimbiji (Dar es Salaam); na mashine moja (1) ya uchakataji chumvi katika Gereza la Lindi (Machole).

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza linategemea kupata mkopo wa matrekta 50 kutoka Shirika la Maendeleo ya Taifa (National Development Corporation – NDC) ambayo yatatumika katika kilimo kwenye mashamba ya Magereza ya Mollo (Rukwa); Songwe, Katai (Ruvuma); Kitengule (Kagera); Arusha; Kwitanga (Kigoma); Kambi Kimbiji (Dar es Salaam); Mugumu (Mara); Ubena (Pwani); na Idete, Kingolwira na Mbigiri (Morogoro). Upatikanaji wa zana hizo utasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao kwa lengo la kuanza kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa magerezani.

**Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Hifadhi ya Mazingira na Upandaji miti ambao unatekelezwa na Jeshi la Magereza kwa ufadhili wa *Tanzania Forest Fund* unaendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya miti 1,107,220 ilipandwa katika Magereza ya Mgagao na Isupilo – Iringa, Gereza la Mkwaya – Ruvuma, Gereza la Msalato - Dodoma, Gereza la Bariadi – Simiyu na Kambi ya Ihanga – Njombe.

**PROGRAMU YA ADHABU MBADALA YA KIFUNGO CHA GEREZANI**

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani hutekelezwa kupitia Makao Makuu ya Wizara. Program hiyo inahusisha upatikanaji wa Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 2,376 ziliandaliwa na kuwezesha wafungwa 1,995 kunufaika na Programu ya Adhabu Mbadala ya Vifungo, ambapo wanaume ni 1,642 na wanawake ni 353. Miongoni mwa wafungwa hao, 456 wametumikia adhabu ya Probesheni na wafungwa 1,539 wametumikia adhabu ya Huduma kwa Jamii kwa kufanya kazi za kijamii kwenye Taasisi za Serikali. Hivyo, kupunguza gharama za uendeshaji katika magereza na taasisi husika. Aidha, wafungwa 794

wamemaliza adhabu zao na kurudishwa kwenye jamii kuungana na familia zao.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ina uwezo wa kuwatoa Gerezani/Mahakamani na kuwasimamia wafungwa 6,000 wenye sifa za kutumikia vifungo vya nje kwa mwaka. Kuendelea kuwepo kwa wafungwa 6,000 magerezani wenye sifa za kutumikia vifungo vya nje kunaigharimu Serikali takriban Shilingi 3,285,000,000 kwa mwaka ikiwa ni gharama za chakula za kuwahudumia wakiwa magerezani. Kiasi hicho cha fedha kingeweza kuokolewa endapo wafungwa hao wangetumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kutumikia adhabu mbadala katika Wizara na Taasisi za Umma.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia umuhimu huo Serikali katika mwaka 2017/18 imetenga jumla ya Shilingi 1,045,586,000 ili kuongeza idadi ya wafungwa wanaotumikia vifungo nje ya magereza hadi kufikia takribani wafungwa 4,000.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza wigo wa matumizi ya adhabu mbadala nchini, katika mwaka 2017/18 Wizara inatarajia kuongeza mikoa saba (7) iliyokuwa imebaki ambayo ni Kigoma, Rukwa, Katavi, Lindi, Ruvuma, Kagera na Simiyu. Hivyo, kufanya mikoa yote ya Tanzania Bara kutekeleza programu hiyo.

## IDARA YA UHAMIAJI

### Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa huduma kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini kwa mujibu wa Sheria za Uhamiaji. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya wageni 1,032,978 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,187,490 walioingia nchini katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya wageni 881,478 walitoka nchini

ikilinganishwa na wageni 1,199,995 waliotoka nchini katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16.

### Udhibiti wa Wahamiaji Haramu

**97.** ***Mheshimiwa Spika****,* ili kudhibiti wahamiaji haramu nchini, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya watuhumiwa 9,581 wa uhamiaji haramu walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 6,600 waliokamatwa katika kipindi Julai, 2015 hadi Machi, 2016. Hivyo, idadi ya wahamiaji haramu waliokamatwa imeongezeka kwa asilimia 45. Aidha, katika kipindi hicho Watanzania 5,923 walirudishwa nchini kati yao 253 ni *stow aways* na 5,670 ni Watanzania waliokuwa wakiishi nchini Msumbiji kinyume cha utaratibu.

### Vibali Vilivyotolewa kwa Wageni Wakaazi

**98.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017*,* jumla ya wageni 11,259 wamepewa vibali vya ukaazi kwa mchanganuo ufuatao: Vibali Daraja "A" 2,474 ikilinganishwa na vibali 1,152 mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia 114; Vibali Daraja "B" 6,736 ikilinganishwa na vibali 7,709 mwaka 2015/16 na Vibali Daraja "C" 2,049 ikilinganishwa na vibali 3,723 mwaka 2015/16.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** vibali Daraja B na C vimepungua kutokana na zoezi la uhakiki wa uhalali wa utoaji wa vibali husika. Vibali hivyo vimetolewa kwa wageni wawekezaji, wageni waliopata ajira katika kampuni mbalimbali na walioingia nchini kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za uhamiaji. Vilevile, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya Hati za Mfuasi 650 na Hati za Msamaha 1,427 zilitolewa.

### Utolewaji wa Pasipoti na Hati nyingine za Safari

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya pasipoti 55,573 zilitolewa kwa

Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali ikilinganishwa na pasipoti 85,758 zilizotolewa katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016. Kati ya pasipoti zilizotolewa, pasipoti za kawaida ni 54,503 pasipoti za Afrika Mashariki ni 785, pasipoti za Kibalozi 229 na pasipoti za kiutumishi ni 56. Aidha, katika kipindi hicho Hati za Dharura za Safari 80,445 zilitolewa.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imeanza kutekeleza mfumo wa uhamiaji mtandao (*e – immigration*) kwa kufanya maboresho katika mtambo wa utoaji Pasipoti ili kuweza kutoa pasipoti za kielektroniki. Aidha, katika mwaka 2017/18 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutekeleza mradi wa Uhamiaji Mtandao, kwa awamu kwa kuanza kutoa pasipoti za kielektroniki (*e - passport*).

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika hatua ya kukamilisha mfumo wa kulipia huduma mbalimbali za uhamiaji kwa njia ya ki-elektroniki. Mfumo huo utawawezesha wateja kulipia huduma hizo kwa njia ya simu sambamba na mifumo mingine iliyopo. Kwa sasa Idara ya Uhamiaji inafanya majaribio ya mfumo huo kwa kulipia baadhi ya huduma zake kama vile Hati za Ukaazi na Pasipoti. Aidha, mfumo huu utakapokamilika utaongeza udhibiti wa maduhuli ya Serikali.

**Wageni Walioomba na Kupewa Uraia wa Tanzania**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 wageni 110 kutoka katika mataifa yafuatayo walipewa uraia: India (64), Yemeni (15), Umoja wa nchi za Falme za Kiarabu (5), Burundi (4), Kenya (5), Rwanda (5), Uingereza (3), Somalia (2), Congo (2), Ujerumani (1), Nigeria (1), Zambia (1), Poland (1) na Lebanon (1).

**Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine**

**104.** ***Mheshimiwa Spika*,** Watanzania 35 waliukana uraia wao baada ya kujipatia uraia wa mataifa mengine

katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017. Mchanganuo wa Mataifa walikopata uraia ni kama ifuatavyo: Ujerumani (7), Uingereza (2), Norway (10), Sweden (3), Canada (1), Afrika Kusini (1), Zambia (1), Uganda (2), Marekani (1), Ureno (1), India (4), Botswana (1) na Srilanka (1). Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357 Toleo la Mwaka 2002, watu hao wamepoteza hadhi ya kuwa raia wa Tanzania.

**Mafunzo katika Idara ya Uhamiaji**

**105.** ***Mheshimiwa Spika*,** jumla ya askari 35 wa Idara ya Uhamiaji walipata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Kati ya hao, 10 walihudhuria mafunzo nchini Morocco na 25 nchini China kwa ufadhili wa Serikali za nchi hizo.

**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga ya Moto**

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto nchini. Jumla ya maeneo 54,961 yalikaguliwa katika kipindi husika. Aidha, zoezi hili linaenda sambamba na utoaji elimu ya kujikinga na majanga ya moto na namna ya kutumia vifaa vya kuzimia moto.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea na ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga mengine inazingatiwa.

**Matukio ya Moto na Majanga Mengine**

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshiriki kuzima moto na kufanya maokozi katika matukio 1,509 kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha, kutokana na kukithiri kwa matukio ya moto katika shule za bweni, Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji katika kipindi hicho limefanya operesheni maalum na kufanikiwa kutoa mafunzo kwa shule za bweni 210 nchini.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za zimamoto na uokoaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo luninga, redio na magazeti. Aidha, elimu itaendela kutolewa kuhusu ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto kwenye maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu zikiwemo shule, masoko, vituo vya mabasi, vivuko na taasisi mbalimbali.

### Ununuzi wa Zana na Vifaa vya Kuzimia Moto

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea msaada wa vifaa mbalimbali vya kuzimia moto kutoka Ujerumani vyenye thamani ya Euro 45,000. Aidha, Wizara inakamilisha taratibu za ununuzi wa magari mawili (2) ya kuzimia moto.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Jeshi la Zimamoto litaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa magari manne (4) ya kuzimia moto pamoja na vifaa vingine vya kuzimia moto na uokoaji, ambapo Shilingi 3,500,000,000 zimetengwa. Pia, Wizara imeanza majadiliano ya awali ya mikopo yenye masharti nafuu kutoka nchi za Ubelgiji (Euro milioni 19) na Austria (Euro milioni 5) kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzimia moto na vifaa vya maokozi.

### Mafunzo katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kuwapatia mafunzo ya ualimu wa uwanjani askari 18 na maafisa watatu (3) katika Chuo cha Maafisa - Magereza, Ukonga. Pia, jumla ya watumishi 10 wanahudhuria mafunzo ya kisasa ya kuzima moto na uokoaji nchini Morocco kwa ufadhili wa nchi hiyo, kati ya hao maafisa ni wanne (4) na askari ni sita (6).

## MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

### Kuendelea na Zoezi la Uandikishaji na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imeendelea kutekeleza lengo la **Ibara 145 (f) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020 la kuendelea kuandikisha na kutoa Vitambulisho vya Taifa.** Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 NIDA imesajili na kutambua jumla ya wananchi 8,551,259 na wageni 8,412 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza wigo wa kukamilisha zoezi hilo nchi nzima, Serikali imehamisha miundombinu ya taarifa za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwenda NIDA, ambapo uhakiki wa taarifa zilizochukuliwa unaendelea. Hatua hii itaongeza idadi ya wananchi waliosajiliwa nchini na kuruhusu matumizi mapana ya Vitambulisho vya Taifa.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imefanikisha zoezi la kuwasajili na kuwahakiki watumishi wa umma 507,026 ambapo mfumo wa taarifa wa NIDA na ule wa taarifa za kiutumishi na mishahara Serikalini *(Human Capital Management Information System – HCMIS)* imeanza kubadilishana taarifa. Hatua hii itaiwezesha Serikali kulipa mishahara kwa watumishi sahihi na taarifa za watumishi kuendelea kuhuishwa kila mara. Aidha, Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa umeanza kufanya kazi katika baadhi ya Benki nchini kama CRDB, Bank of Africa na Barclays.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, NIDA imenunua scanner 478 na imefunga mtandao wa mawasiliano katika wilaya 84 za mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mamlaka inaendelea na ufungaji wa mtandao wa mawasiliano katika wilaya 67 pamoja na

kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa.

**117.** ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2017/18 NIDA itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo Watanzania milioni 22.7 wanatarajiwa kusajiliwa na kupewa Vitambulisho vya Taifa ifikapo mwishoni mwa mwezi Desemba, 2018. Aidha, Mamlaka itakamilisha ujenzi wa ofisi 13 za wilaya, itakamilisha uwekaji wa mtandao wa mawasiliano katika wilaya 135 ili kurahisisha utumaji wa taarifa za wananchi kutoka wilayani, itakamilisha kituo cha uchakataji, uzalishaji na utunzaji wa kumbukumbu (*Data centre*) na kituo cha uokozi wakati wa majanga (*Disaster recovery centre*).

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Mamlaka inatarajia kukarabati ofisi za usajili kwa baadhi ya wilaya na ununuzi wa vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya kuunganisha mtandao wa mawasiliano. Aidha, Mamlaka itakamilisha utaratibu utakaoruhusu taasisi na mashirika mengi zaidi kutumia mfumo huu kupata taarifa sahihi za watu na kupunguza urasimu katika utoaji huduma.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) na wadau wengine, imeendelea kutoa hifadhi na huduma kwa wakimbizi kutoka nchi jirani, hususan zile za Maziwa Makuu za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kutafuta suluhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi hao. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2017 idadi ya wakimbizi nchini ilikuwa ni 340,835 na wamehifadhiwa katika kambi za Nyarugusu, Nduta, Mtendeli zilizoko Mkoani Kigoma, wengine katika makazi ya Katumba, Mishamo, Ulyankulu na Chogo (hawa ni wale waliokosa fursa ya kupata uraia wa Tanzania).

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kupokea wakimbizi wapya kutoka katika nchi za Burundi na

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Awali, wakimbizi kutoka Burundi walikuwa wakipokelewa moja kwa moja kwenye kambi bila ya kufanyiwa mahojiano ya kina kutokana na kuingia kwa makundi makubwa kwa sababu ya machafuko ya kisiasa yaliyokuwa yanaendelea nchini kwao.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, imebainika kuwa hali ya usalama nchini Burundi imeimarika kwa sasa na wengi wa wakimbizi hawa wanakimbilia Tanzania kwa sababu za kiuchumi, hususan kutokana na ukame ulioikumba sehemu kubwa ya nchi hiyo na kusababisha njaa.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na hali hiyo, mwezi Februari, 2017 Serikali ilisitisha utaratibu wa kuwapokea na kuwasajili wakimbizi bila ya kuwahoji kwa kina (*prima facie recognition*) na kuendelea na utaratibu wa kawaida wa kila mkimbizi kuhojiwa na Kamati Maalumu ya Kitaifa ya Kujadili Maombi ya Waomba Hifadhi (*National Eligibility Committee*). Lengo la utaratibu huu wa kumhoji kila muomba hifadhi ya ukimbizi ni kuhakikisha kuwa Serikali inatoa hifadhi ya ukimbizi kwa wanaostahili tu.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2016/17 Serikali iliahidi kutekeleza miradi inayolenga kupunguza athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kiholela kwa ajili ya kupata nishati ya kupikia, fito za kujengea na kuhamasisha upandaji wa miti katika maeneo ya ndani ya kambi na maeneo yanayozunguka kambi hizo. Katika kutekeleza azma hiyo, **napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Wizara, kwa kushirikiana na UNHCR imeanza kutekeleza mradi wa kutumia majiko ya gesi kupikia badala ya kuni katika kambi ya Nyarugusu kwa awamu ya kwanza, ambapo mitungi ya gesi 3,216 imegawiwa kwa wakimbizi.** Mradi huu utakuwa unafanyika kwa awamu hadi kufikia kambi zote za wakimbizi.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mradi wa matumizi ya majiko ya gesi, miche ya miti 1,481,592 imekuzwa na kupandwa ndani ya kambi na maeneo yanayozunguka kambi hizo. Aidha, ujenzi wa nyumba 15,664 ambazo

zitatumia tofali mbichi na kuezekwa kwa mabati badala ya kutumia fito za miti ambazo zinachangia katika uharibifu wa mazingira unaendelea. Vilevile, majiko sanifu 59,924 yaligawiwa kwa kila nyumba katika kambi za Wakimbizi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeli.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya kambi za wakimbizi. Pia, Wizara itaanza kutekeleza mradi wa matumizi mbadala ya mkaa katika kambi za wakimbizi, kufuatia kukamilika kwa utafiti wa upatikanaji wa malighafi za uzalishaji.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na UNHCR na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) inaendelea kutekeleza mradi wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambao wanaishi katika kambi ya Nyarungusu, ambapo kuanzia Julai, 2016 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2017 wakimbizi 6,545 walikuwa wamehamishiwa nchini humo.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mpango wa kuwapeleka wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo nchini Marekani, wakimbizi 227 walihamishiwa katika nchi za Australia (23), Canada (197), Uingereza wawili (2) na Sweden watano (5). Hata hivyo, sababu ya kuwahamishia wakimbizi nchi hizo ni kuzipunguzia mzigo nchi zenye wakimbizi wengi ikiwemo Tanzania.

**128.** ***Mheshimwa Spika,*** kwa kuwa hali ya usalama katika baadhi ya maeneo nchini Burundi imeimarika, Serikali imependekeza kuwepo kwa mazungumzo kati yake na Serikali ya Burundi pamoja na UNHCR. Lengo likiwa ni kuwawezesha wakimbizi watakaopenda kurejea kwao kwa hiari na kusaidiwa kujenga maisha mapya katika nchi yao ya asili.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 UNHCR kwa kushirikiana na NIDA imeanza zoezi la kuwasajili wakimbizi wanaoishi nchini. Katika hatua ya awali zoezi

litahusisha kuwapatia namba za utambuzi ili kubana mianya ya wakimbizi kudanganya na kusajiliwa kama raia. NIDA imepanga kutekeleza zoezi hilo kabla ya kuanza usajili wa raia wa Tanzania katika Mkoa wa Kigoma ambako kuna kambi nyingi za wakimbizi. Lengo ni kuwapatia wakimbizi hao Vitambulisho vya Taifa vitakavyowawezesha kupata huduma mbalimbali wanazostahili.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuwapatia wakimbizi hati za utambulisho pamoja na kusaidia utambulisho ni kutekeleza mikataba ya kimataifa ambapo wakimbizi wanapaswa wawe na hati muhimu.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilitoa uraia kwa wakimbizi 162,156 wenye asili ya Burundi walioingia nchini mwaka 1972 na kupangiwa kuishi katika makazi ya Katumba, Mishamo mkoani Katavi na Ulyankulu mkoani Tabora. Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa utangamanisho (*local integration*), ambao utawahamasisha raia hao kuhamia katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Kutokana na hali hiyo, Serikali inaendelea kuiomba Jumuiya ya Kimataifa kutimiza wajibu wake katika kutekeleza mradi wa utangamanisho kwa kuchangia rasilimali zinazohitajika kuwezesha raia hao kuwa sehemu ya jamii watakayohamishiwa.

**VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu iliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 17 wa makosa ya biashara haramu ya usafirishaji binadamu na kuwafikisha mahakamani ili kuchukuliwa hatua za kisheria. Vilevile, wahanga 20 wa biashara hiyo waliokolewa, kusaidiwa na hatimaye kuunganishwa na familia zao.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekretarieti hiyo pia iliratibu mafunzo yaliyotolewa kwa maafisa 60 kutoka kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria,

ambavyo ni Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna ya kupeleleza, kuendesha na kutoa maamuzi sahihi dhidi ya makosa ya biashara haramu ya binadamu.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Sekretarieti imejipanga kuendelea kuratibu uendeshaji wa mafunzo kwa maofisa kutoka vyombo vinavyosimamia sheria na wadau wengine wanaotekeleza sheria ya kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu. Sekretarieti pia itapitia sheria zinazotoa mwanya kwa wale wanaojihusisha na biashara haramu ya usafirishaji binadamu na kupendekeza kwa Serikali maeneo ya kufanyiwa marekebisho.

## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilipokea malalamiko 392 kutoka kwa wananchi wakilalamikia utendaji wa vyombo vya kijeshi ndani ya Wizara. Aidha, Wizara ilifanya uchunguzi wa malalamiko hayo na jumla ya malalamiko 182 yalipatiwa ufumbuzi na wahusika kujulishwa na mengine 210 yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa. Katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi na watumishi wa Wizara pamoja na kufanya uchunguzi wa kina ili kuweza kubaini ukweli wa malalamiko hayo na kuchukua hatua stahiki.

## USAJILI WA VYAMA VYA KIJAMII NA VYA KIDINI

**136.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilipokea jumla ya maombi 296 ya usajili wa vyama. Kati ya maombi hayo jumla ya vyama 162 vimepewa usajili, maombi ya vyama 124 yanashughulikiwa na maombi ya vyama 10 yamekataliwa kutokana na kukosa sifa, kati ya hivyo vitano (5) ni vya kidini na vitano (5) ni vya kijamii.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** sanjari na shughuli za usajili, Wizara imeanza kuchukua hatua za kuvifutia usajili vyama visivyotekeleza wajibu wao kulingana na sheria, ambapo vyama 13 vimepewa taarifa ya kusudio la kuvifuta. Katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea na usajili na uhakiki wa vyama vya kidini na kijamii ili kuwa na kanzi data yenye taarifa sahihi za vyama kwa lengo la uanzishwaji wake.

## SHERIA, KANUNI, MIKAKATI INAYOHUSU WIZARA

**138.** ***Mheshimwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Wizara imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati kwa kipindi cha 2016/17 - 2020/21 ambao ni msingi wa utekelezaji wa malengo ya Wizara na uandaaji wa mpango na bajeti kwa kila mwaka wa fedha. Aidha, Rasimu ya Mpango wa Kudhibiti Vihatarishi *(Risk Register)* kwa mwaka 2016/17 – 2020/21 imeandaliwa kwa lengo la kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa maeneo hatarishi.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imekamilisha Rasimu za Mapendekezo ya Kutunga Sheria Mpya ya Jeshi la Polisi Tanzania *(The Tanzania Police Force Act, 2017)* na Mapendekezo ya Kutunga Sheria Mpya ya Usajili na Utambuzi wa Watu *(The Registration and Identification of Persons Act, 2017).* Katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea kuboresha sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi.

## MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA AJIRA MPYA

### Mafunzo kwa Watumishi wa Wizara

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuwaongezea ujuzi watumishi waliopo Makao Makuu ya Wizara kwa kuwawezesha kupata mafunzo ndani ya nchi. Katika mwaka 2016/17 watumishi kumi (10) walipatiwa mafunzo ndani ya nchi katika fani za makarani masijala, katibu muhtasi pamoja na fani ya usafirishaji.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara inatarajia kuwapeleka mafunzoni ndani ya nchi jumla ya watumishi 141 wa kada mbalimbali waliopo Makao Makuu ya Wizara. Kati ya hao, watumishi 120 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 21 mafunzo ya muda mrefu.

**Ajira Mpya kwa Mwaka 2017/18 na Upandishwaji Vyeo**

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ujumla wake inatarajia kuwapandisha vyeo jumla ya watumishi 7,317. Kati ya hao watumishi 105 ni wa Makao Makuu ya Wizara; askari 5,772 wa Jeshi la Polisi; na askari 1,440 wa Idara ya Uhamiaji.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 4,339 (Makao Makuu ya Wizara 26, Jeshi la Polisi 2,573, Jeshi la Magereza 500, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 600, Idara ya Uhamiaji 600 na NIDA 40). Aidha, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi na askari kadiri watakavyopata sifa kulingana na miundo yao ya kiutumishi.

**MAPAMBANO DHIDI YA MAAMBUKIZI YA VVU/UKIMWI**

**144.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2016/17 Wizara imeendelea na juhudi mbalimbali za kupambana na janga la UKIMWI zikiwemo za kuboresha huduma za upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU) na ushauri nasaha ili kuhakikisha huduma hizo zinawafikia watumishi, askari, wafungwa na familia za askari na zinapatikana bure pamoja na kampeni za upimaji wa hiari wa mara kwa mara. Aidha, fedha za kila mwezi kwa askari na watumishi raia wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa ajili ya kuimarisha afya zao dhidi ya magonjwa nyemelezi ziliendelea kutolewa.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Wizara kwa kushirikiana na Asasi ya John Snow Inc (*JSI – Aids Free)* ilitoa mafunzo kwa watumishi 55 ambao watakuwa waelimishaji wa masuala ya UKIMWI katika magereza nchini.

**146.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea kutoa huduma kwa watumishi waathirika wa VVU na UKIMWI kulingana na miongozo ya Serikali. Aidha, watumishi wataendelea kuhamasishwa kupima afya zao mara kwa mara ili kuweza kupata matibabu na ushauri nasaha pale watakapogundulika kuwa na VVU/UKIMWI pamoja na magonjwa mengine yasiyoambukiza.

**SHUKRANI**

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni kwa kunipa ushirikiano katika kuongoza Wizara hii. Kipekee nawashukuru Katibu Mkuu Meja Jenerali Projest A. Rwegasira na Naibu Katibu Mkuu, Balozi Hassan S. Yahya kwa kusimamia vema utekelezaji wa majukumu na utendaji kazi wa Wizara hii nyeti inayohusu usalama wa nchi.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara nikianza na Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Bw. Ernest J. Mangu; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Dkt. Juma A. Malewa; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bw. Thobias E. Andengenye; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala; na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Bw. Andrew W. Massawe. Pia, nawashukuru Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi Bw. Abdulrahmani O. Kaniki, Makamishna; Makamishna Wasaidizi; Wakuu wa Idara, Vitengo na Sehemu; askari na wafanyakazi wote kwa utendaji wao uliowezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninatoa shukrani zangu kwa nchi wahisani ikiwemo Serikali za Nchi za China, India, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ujerumani, Morocco, Uturuki na Taasisi na Mashirika mbalimbali ya ACSA, ADRA, AIRD, AU, CCBRT, CDF, CEMDO, Danish Refugee Council, DFID, EAC, EAPCCO, EU, GTI, Hanns Seidel Foundation, Help Age

International, INTERPOL, IOM, IRC, John Snow Inc (*JSI – Aids Free)* OXFAM, Pharm Access, Plan International, REDESO, SADC, SARPCCO, Save the Children International, TRCS, TWESA, UNDP, UNFPA, UN – WOMEN, UNHCR, UNICEF, WFP, WLAC, TAWLA, TAYOA, TACAIDS, World Vision Tanzania, Taasisi za dini, vyombo vya habari, wananchi pamoja na wadau wengine kwa kutoa taarifa na misaada mbalimbali ambayo imesaidia katika utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa naishukuru familia yangu, ndugu, marafiki na wananchi, hususan wa Jimbo langu la Iramba Magharibi kwa imani yao kwangu na ushirikiano wao katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya jimbo letu.

## E. HITIMISHO

**151.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara itaendelea kuweka mipango bora ya kudhibiti matukio ya uhalifu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola nchini na vya kimataifa pamoja na kuwashirikisha wananchi ili kuhakikisha uhalifu unadhibitiwa na hali ya usalama inaimarika nchini.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 930,396,817,000** kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2017/18. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 890,388,452,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 367,706,884,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 522,681,568,000** ni Mishahara. **Shilingi 40,008,365,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo **Shilingi 39,700,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 308,365,000** ni fedha za nje.

**153.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hoja imeungwa mkono. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aje kuwasilisha taarifa yake. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa na kuweza kuwasilisha taarifa hii ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naungana na wananchi wote kutoa pole kwa tukio kubwa ambalo lilitokea huko Mkoani Arusha na kupoteza watoto wetu na baadhi ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naungana na Wanatanga kutoa pole kwa wananchi wote wa Mkoa wa Tanga kutokana na mafuriko makubwa ambayo yametokea usiku wa leo na kusababisha msongamano wa magari mkubwa sana, kubomoka kwa nyumba na madhara mengine makubwa sana. Nawahakikishia kwamba tumeshatoa taarifa Serikalini na suala hilo linachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapa pole sana wananchi wa Jimbo langu la Muheza kutokana na ajali ambayo imetokea juzi usiku na wananchi wanne kufariki na pia usiku wa jana kutokana na mafuriko hayo kupoteza baadhi ya watu ambao idadi yao bado sijaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe taarifa ya Kamati ya Mambo ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na naomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge *(Hansard)* kama sitaweza kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi yaWizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa utaratibu wa kibajeti, inahusisha mafungu matano fungu la kwanza ni Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu la 28 - Jeshi la Polisi, Fungu la 29 - Jeshi la Magereza, Fungu la 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* na Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017 kuanzia tarehe 22 - 24 Machi, 2017, naomba kutoa taarifa hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Kamati ilitembelea Mradi Na. 6311 kuhusu ukamilishaji wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto eneo la Mchicha - TAZARA mjini Dar es Salaam na pia iliangalia kuhusu mradi wa ununuzi wa magari mawili ya zimamoto. Kuhusu Jeshi la Polisi Mradi Na. 6107 - *Offenders Management Information System (OMIS)* na *Digital Mobile Radio* katika Jeshi la Polisi na mradi ufungaji wa *lift* katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Aidha, Kamati pia ilitembelea Mradi kuhusu Vitambulisho vya Taifa ambao uko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani - Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi hicho, Kamati yangu ilikagua mradi wa uwekezaji eneo la Polisi Oysterbay *Dar es Salaam City Project*. Mradi huu ni wa ubia kati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mwekezaji ambaye ni *Mara World Tanzania Limited*. Katika mradi huu,

Shirika la Uzalishaji Mali ya Polisi limetoa ardhi na mwekezaji atajenga majengo yote. Aidha, wakati wa ukaguzi huo, Kamati ilielezwa kuwa ardhi ya eneo hilo la mradi na majengo yote yatakayojengwa katika eneo hilo yatakuwa mali ya Shirika la Uzalishaji Mali ya Polisi na mwekezaji atakuwa mpangaji. Mradi huo Kamati iliridhika na kwa kweli mradi ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezwa kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji katika miradi hiyo. Naomba nianze kutoa taarifa hii kwa kueleza kuwa kutopatikana kwa fedha kutoka Hazina kulikuwa ni changamoto kubwa sana katika utekelezaji wa miradi. Kwa sababu hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi matatu kama ambavyo nitayaeleza hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo haikutekelezwa kabisa, kwa mfano miradi Na.6311 kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto uliotengewa shilingi bilioni 2 na mradi kuhusu ufungaji wa *lift* katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi uliotengewa shilingi milioni 300. Miradi ambayo ilitekelezwa kwa kiwango kisichokamilika, kwa mfano, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ulitengewa shilingi bilioni 30 lakini fedha ambazo zilipokelewa ni shilingi bilioni 12.7 sawa na asilimia 45.5 ya fedha zilizoidhinishwa. Mradi kuhusu ununuzi wa magari mawili ya zimamoto ulitengewa shilingi bilioni 1.5 lakini zilipokelewa shilingi milioni 117,045,000 sawa na asilimia 0.07

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo haikupelekewa fedha za maendeleo lakini ikatekelezwa kwa kutumia fedha za matumizi mengine na fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, kwa mfano mradi wa *Digital Mobile Radio* katika Jeshi la Polisi. Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Machi, 2017 mikoa 13 ilikuwa imeshaunganishwa na mfumo wa *Digital Mobile Radio* kwa kila Wilaya na Mikoa mingine nane kwa baadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa ukamilifu kunaathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo;

(ii) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unahitaji kuboreshwa zaidi;

(iii) Kutumia fedha za matumizi mengine kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Mpango Kazi wa Wizara na Taasisi za Serikali;

(iv) Upo umuhimu wa Serikali kuwa na miradi mingi inayotekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na wawekezaji ili kuwa na miradi ambayo utekelezaji wake ni wa uhakika; na

(v) Manufaa ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekanaka pale tu Serikali itakapotoa fedha zote kwa wakati na kwa ukamilifu kama ilivyoidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ni kwamba uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi cha Oktoba, 2016 na Januari, 2017 na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi 289,969,629,604. Hadi mwezi Februari, 2017 Kamati ilielezwa kuwa kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni shilingi 116,546,675,737 ambayo ni asilimia 54 tu ya makadirio ya makusanyo katika kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,uchambuzi wa Kamati kuhusu ukusanyaji wa mapato unaonyesha mambo matano yafuatayo:-

(i) Makusanyo kuhusu Jeshi la Zimamoto yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 12.24 lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limechangia asilimia 14;

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Polisi yalikusudiwa kuchangia asilimia 24.4 lakini taarifa inaonyesha kuwa makusanyo yamechangiwa kwa asilimia 27.3;

(iii) Jeshi la Magereza yalikusudiwa kukusanya asilimia 0.9 lakini taarifa ya makusanyo inaonekana kwamba imechangia asilimia 0.5;

(iv) Wizara iliyokusudiwa kuchangia asilimia 0.1 makusanyo yanaonyesha yamechangiwa kwa hiyo hiyo 0.1;

(v) Makusanyo ya Jeshi la Uhamiaji yalikusudiwa kuchangia kwa asilimia 63 lakini makusanyo yanaonesha kwamba asilimia ambayo imechangiwa 58.1 ya kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii na kubaini yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 64.3 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara;

(ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2017 asilimia 98 ilikuwa ni kwa ajili ya

matumizi ya kawaida na asilimia 2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo; na

(iii) Hadi kufikia mwezi Februari pia Wizara ilikuwa imepokea asilimia 66.5 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na asilimia 28 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo ni dhahiri kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni ya kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi bado hauridhishi kabisa. Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri mpango na ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa na yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kama yafuatayo:-

(i) Kusimamia usalama wa raia na mali zao;

(ii) Kusimamia marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya magereza na katika maeneo ya jamii;

(iii) Kutoa huduma za zimamoto na uokoaji;

(iv) Kudhibiti uingiaji na utokaji nchini kwa raia na wageni;

(v) Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa; na

(vi) Kutoa huduma kwa wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umeonyesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatatekelezeka kwa ufanisi endapo tu Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uichambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka 2017/2018 Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 293,822,132,859 hii ni sawa na asilimia 32.9 ya makadirio ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa lengo la makusanyo unaonekana kwenye jedwali kama ilivyo kwenye kitabu chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya makusanyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yameongezeka kwa asilimia 1.4 ikilinganishwa kwa makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(ii) Fungu la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 12.1 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 12;

(iii) Fungu la Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 25.1 ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo ilitegemewa kukusanya asilimia 24;

(iv) Fungu Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya kiasi cha asilimia 0.9 kwa mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na asilimia hizo hizo kwa mwaka uliopita;

(v) Wizara asilimia 0.4 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo ilitegemewa kukusanya asilimia 0.1; na

(vi) Uhamiaji ilitegemewa kukusanya asilimia 61.5 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa ongezeko dogo la makadirio ya makusanyo kwenye baadhi ya mafungu limezingatia mafungu ambayo yalifanya vizuri kwenye makusanyo katika mwaka wa fedha unaoishia.

Mhesimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni shilingi 930,396,817,000. Kati ya fedha hizo shilingi 522,681,568,000 ni mishahara na shilingi 367,706,884,000 ni matumizi mengineyo na shilingi 40,008,365,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeongezeka kwa shilingi 65,561,877,149.13 sawa na ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na bajeti iliyopita ya mwaka 2016/2017;

(ii) Asilimia 4.3 ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na asilimia 56.2 ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 39 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo;

(iii) Wakati bajeti kuu ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Fedha tarehe 28 imeongezeka kwa asilimia 1.5, bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya miradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia 16; *(Makofi)*

(iv) Wakati asilimia 38 ya bajeti kuu kwa mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, asilimia 4.3 ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo;

(v) Wakati mwaka 2016/2017 asilimia 36 ya bajeti ya Wizara hii ilikuwa ni kwa ajili ya uendeshaji, mwaka 2017/2018 asilimia 39.5 ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili kugharamia uendeshaji wa shughuli;

(vi) Pamoja na kwamba Serikali haikutoa shilingi bilioni mbili zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lililopo *TAZARA*, Serikali haijatenga kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo hilo katika mwaka wa fedha 2017/2018; na

(vii) Pamoja na kwamba kazi ya ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali katika Gereza la Segerea haikufanyika kutokana na kutokutolewa shilingi bilioni moja zilizoidhinishwa na Bunge, kwa mwaka huu wa fedha, Serikali haijatenga fedha yoyote kwa ajili ya shughuli hiyo katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa mapendekezo na ushauri wa jumla kwa mafungu yote na ushauri mahsusi kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa jumla kuhusu upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara na mafungu yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ukamilifu na kwa wakati ili kutekeleza kikamilifu miradi iliyopangwa. Hadi kufikia robo ya tatu ya

mwaka huu unaoishia, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 28 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo, jambo ambalo limeathiri ratiba na mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo.

(ii) Miradi yote iliyokuwa imetengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017 na ambayo haijakamilika ipewe kipaumbele kwenye utekelezaji wake kabla ya kuanza kutekeleza miradi mingine mipya katika mwaka wa fedha 2017/2018. Hii itaiwezesha Serikali kuwa na miradi michache lakini iliyokamilika na yenye tija kwa Serikali na Taifa. *(Makofi)*

(iii) Pamoja na nia njema ya Serikali kuhamia Dodoma, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutekeleza miradi yote iliyokuwa imeanza kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam, kwa mfano mradi wa ukamilishaji wa Jengo la Makao Makuu ya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahsusi kuhusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itafute uwezekano wa kutoa shilingi bilioni mbili zilizotengwa katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji uliokwama tangu 2013. Hii itasaidia kukamilisha jengo hilo haraka na hivyo kuokoa shilingi milioni 30 zinazolipwa kila mwezi ambapo kwa mwaka ni shilingi milioni 360, kwa ajili ya kodi ya pango ya Makao Makuu ya Jeshi hilo;

(ii) Serikali ikamilishe mchakato wa marekebisho ya Sheria Na. 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kuboresha ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Jeshi hilo; na

(iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi hili kuwa na vifaa hususan dawa na magari ya kuzimia moto. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Hazina itoe shilingi 1,382,955,000 ambazo hazijatolewa kwa ajili ya kununua magari mawili ya zimamoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hii itawezesha Jeshi la Zimamoto kutekeleza kwa

ufanisi jukumu lake la msingi la kutoa huduma bora ya zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Polisi, tuna ushauri ufuatao:-

(i) Lihakikishe kwamba amani na utulivu katika Mkoa wa Pwani inaendelea kuimarika. Aidha, Jeshi litumie mbinu na taaluma za kipolisi kuhakikisha kwamba uhalifu huo ambao uko katika Mkoa wa Pwani unakomeshwa kwa kukamata wote wanaojihusisha na vitendo hivyo. Kamati ilitoa taarifa yake na imeipeleka kwenye Serikali na naamini Waziri ameipata na inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

(ii) Mipango ya kiutawala na uendeshaji ya Jeshi la Polisi kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yake katika Mkoa wa Pwani inabidi uboreshwe kiutendaji;

(iii) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Polisi kibajeti na vifaa ili Jeshi hilo liwe na ufanisi na mafanikio katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao ikiwemo kukabiliana na matukio ya mauaji na vihatarishi vya amani na usalama hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mbali na makosa ya uhalifu wa mauaji Kamati inashauri:-

(i) Serikali ikamilishe haraka mchakato wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani ili kupunguza ajali za barabarani ambazo zimeongezeka kwa kasi kubwa na ambazo zimepoteza maisha ya raia wetu. Hili lina ushahidi wa wazi kabisa ambapo juzi tu hapa tumepoteza watoto wetu wengi na ajali nyingine mbalimbali zimetokea. Kwa hiyo, sheria hii ni muhimu sana iletwe katika Bunge hili ili tuweze kufanyia marekebisho labda tunaweza tukapunguza ajali hizi ambazo zinaendelea. *(Makofi)*

(ii) Serikali isimamie usalama wa raia na mali zao katika maeneo yote ya migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kuweka mikakati madhubuti ya kumaliza migogoro hiyo.

Hii itawahakikishia wananchi usalama wao na mali zao katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza, tuna ushauri ufuatao:-

(i) Serikali kupitia Hazina ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kulipa madeni yote ya Magereza yaliyohakikiwa yenye jumla ya shilingi 63,805,279,064. Hii itapunguza kasi ya kuzaliana kwa madeni na kuepusha migogoro inayoweza kutokea kati ya Jeshi hilo na wazabuni au Jeshi na watumishi wake.

(ii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na vitendea kazi vya kisasa ili kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya ulinzi, usalama, uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali. *(Makofi)*

(iii) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa kwa mwaka wa fedha unaoishia 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali iliyopo Gereza la Segerea. *(Makofi)*

(iv) Serikali iendelee kutekeleza programu za adhabu mbadala kwa wafungwa ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani. Aidha, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuwezesha Mpango wa Huduma kwa Jamii. Hadi kufikia mwezi Februari 2017 Serikali ilikuwa imetoa asilimia 9.9 tu ya fedha zote ambazo ziliidhinishwa.

(v) Serikali ianze utaratibu wa kusafirisha mahabusu kwenda mahakamani na kurudi gerezani kwa kununua na kupeleka mabasi katika Mikoa yote Tanzania ambayo haina utaratibu huo. Hii itasaidia mahabusu wengi kupata haki zao za kisheria kwa wakati. Serikali ione umuhimu wa kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya magereza.

(vi) Serikali iendelee na juhudi za kuliwezesha Jeshi la Magereza kuimarisha viwanda mbalimbali ikiwemo viwanda vya useremala, ngozi na sukari. Aidha, juhudi zaidi ziongezwe

kuliwezesha Jeshi hili kibajeti na kununua vifaa vya kilimo vya kisasa ili liweze kujiendesha lenyewe.

(vii) Kufuatia Serikali kufuta utaratibu wa majeshi kumiliki maduka yasiyotoza ushuru *(Duty Free Shops)* na badala yake kuanzisha utaratibu wa kutoa fedha, Serikali itoe fedha zote kwa Jeshi la Magereza kama ilivyofanya kwa majeshi mengine kwa utaratibu huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kuhusu Fungu la Wizara ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani iratibu ushirikiano wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama katika kutekeleza mikakati ya pamoja ya vyombo hivyo katika kudhibiti ipasavyo matukio yote yanayohatarisha usalama wa raia na mali zao nchini.

(ii) Serikali ione umuhimu wa kukamilisha mradi wa Vitambulisho vya Taifa ambao ulipaswa kukamilika Desemba 2016, kwa kutoa shilingi 17,239,710,636 ambazo bado hazijatolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

(iii) Serikali kupitia Hazina itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kudhibiti vitendo vya ujambazi, unyang'anyi na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe. Hadi kufikia Februari, 2017 Wizara ilikuwa imetoa shilingi milioni 362 kati ya shilingi bilioni 1.8 ambayo ni asilimia 19.9 tu kwa ajili ya operesheni za kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji, tunashauri:-

(i) Serikali iendelee kutekeleza mpango wa kuwarudisha makwao wahamiaji haramu walioko magerezani ili kupunguza gharama ya kuwahudumia na kupunguza msongamano magerezani.

(ii) Serikali iliwezeshe kibajeti kufanya misako na doria ili kuwabaini na kuwaondosha wahamiaji haramu hapa nchini.

(iii) Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya *passport* na malighafi iongezwe ili kukidhi mahitaji halisi ya utoaji wa huduma za *passport* na hati za dharura za kusafiria; na

(iv) Rangi ya pasi ya kusafiria ya kidiplomasia ibadilishwe kutoka nyeusi inayotumika sasa hivi kuwa nyekundu kama ilivyo katika nchi nyingine. *(Makofi)*

Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilishwa kwa taarifa hii, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, pia napenda kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, namshukuru pia Katibu Mkuu, Meja Jenerali Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Yahya Simba pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango mkubwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Katiba. *(Makofi)*

Mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati za Bunge. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii ambao wamefanya kazi kubwa sana Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe. Pia Bi. Grace Wambura, Bi. Olando kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa utaratibu wa kibajeti, inahusisha Mafungu matano (5) yafuatayo:- Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28- Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza, Fungu 51- Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa-NIDA; na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kueleza mpangilio wa Taarifa hii ninayoiwasilisha kwa kutaja sehemu zake kuu nne. Sehemu hizo ni:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

### 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara tatu inazozisimamia ikiwewo Wizara hii, kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi, 2017.

Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi mitano (5) iliyoidhinishiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kutekelezwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**a) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

i) Mradi Na. 6311 kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya Jeshi la Zimamoto, eneo la Mchicha- TAZARA jijini Dar es Salaam.

ii) Mradi Na. 6582 kuhusu ununuzi wa magari mawili ya kuzimia moto.

**b) Fungu 28- Jeshi la Polisi**

i) Mradi Na. 6107 kuhusu *Offenders Management Information System* (OMIS) na *digital mobile radio* katika Jeshi la Polisi nchini.

ii) Mradi Na. 6302 kuhusu ufungaji wa *lift* katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi jijini Dar es Salaam.

**c) Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Mradi Na. 6501 kuhusu Vitambulisho vya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi hicho, Kamati yangu ilikagua mradi wa uwekezaji eneo la Polisi *Oysterbay* (Dar City Project). Mradi huu ni wa ubia kati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mwekezaji ambaye ni Mara *World Tanzania Limited*. Katika mradi huu, Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi limetoa ardhi na mwekezaji atajenga majengo yote. Aidha, wakati wa ukaguzi huo, Kamati ilielezwa kuwa ardhi ya eneo la mradi na majengo yote yatakayojengwa katika eneo hilo yatakuwa mali ya Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi na mwekezaji atakuwa mpangaji**.**

**2.2 Matekeo ya Ukaguzi**

**Mheshimwia Spika,** baada ya kueleza kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji katika Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nianze taarifa hiyo kwa kueleza kuwa kutopatikana kwa fedha kutoka Hazina kulikuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi. Kwa sababu hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Miradi umegawanyika katika makundi matatu kama inavyoelezwa hapa chini.

**Mheshimiwa Spika,** kundi la kwanza ni Miradi ambayo haikutekelezwa kabisa. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hazikutolewa kabisa. Mfano wa miradi hiyo ni mradi Na. 6311 kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya Jeshi la Zimamoto uliotengewa **shilingi**

**Bilioni 2** na Mradi Na. 6302 kuhusu ufungaji wa *lift* katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi uliotengewa **shilingi Milioni 300**.

**Mheshimiwa Spika,** kundi la pili ni Miradi ambayo ilitekelezwa kwa kiwango kisichokamilika. Sababu iliyoelezwa ni kutolewa kwa fedha pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi wa Vitambulisho vya Taifa unaotekelezwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Kamati ilijulishwa kuwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni **shilingi Bilioni 30**. Hata hivyo, taarifa ilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2017, mradi huu ulikuwa umepokea kiasi cha **shilingi Bilioni 12.7** sawa na asilimia 42.5 ya fedha zilizoidhinishwa. Vilevile, Mradi Na. 6582 kuhusu ununuzi wa magari mawili ya kuzimia moto ulitengewa **shilingi Bilioni 1.5**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 mradi huu ulikuwa umepokea **shilingi 117,045,000.00** sawa na asilimia 0.7 tu ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kutokutolewa kwa fedha za miradi kwa ukamilifu kuliathiri utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la tatu ni miradi ambayo haikupelekewa fedha za maendeleo lakini kutokana na umuhimu wake ilitekelezwa kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) pamoja na fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo. Mfano wa mradi huo ni mradi Na. 6107 wa *Digital Mobile Radio* katika Jeshi la Polisi. Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2017, mikoa kumi na tatu (13)[1] ilikuwa imeshaunganishwa na mfumo wa *digital mobile radio* kwa kila Wilaya, na mikoa mingine 8 kwa baadhi ya Wilaya.

### 2.3 Maoni kuhusu Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

______________

[1]Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Magharibi, Dar es Salaam, Pwani, Katavi, Shinyanga, Geita, Tarime Rorya, Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera

(i) Kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa ukamilifu kunaathiri ratiba ya utekelezaji wake;

(ii) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unahitaji kuboreshwa zaidi;

(iii) Kutumia fedha za matumizi mengineyo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Mpango Kazi wa Wizara/ Taasisi za Serikali;

(iv) Upo umuhimu wa Serikali kuwa na miradi mingi inayotekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na Wawekezaji ili kuwa na miradi ambayo utekelezaji wake ni wa uhakika;

(v) Manufaa ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekanaka pale tu Serikali itakapotoa fedha zote kwa wakati na kwa ukamilifu kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ulizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi cha Oktoba, 2016 na Januari 2017, na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya **shilingi 289,966,629,604**. Hadi mwezi Februari 2017, Kamati ilielezwa kuwa kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni **shilingi 156,543,675,737.91 sawa** na asilimia 54 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebainisha mchanganuo wa makusanyo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 hapa chini.

**Jedwali Na.01: MCHANGUO WA MAPATO**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 14 - Zimamoto | 35,500,003,000 | 12.24 | 21,890,990,000 | 14 |
| 28 - Polisi | 70,915,650,000 | 24.4 | 42,724,555,842 | 27.3 |
| 29 – Magereza | 2,619,335,504 | 0.9 | 840,617,933.70 | 0.5 |
| 51- Wizara | 226,601,100 | 0.1 | 114,458,087 | 0.1 |
| 93- Jeshi la Uhamiaji | 180,705,040,000 | 63 | 90,973,053,875.21 | 58.1 |
| **JUMLA** | **289,966,629,604** | **100** | **156,543,675,737.91** | **100** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Makusanyo ya Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 12.24 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 14 limechangia kwa asilimia 14 ya kiasi kilichokusanywa;

(ii) Makusanyo ya Fungu 28- Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 24.4 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 28 limechangia kwa asilimia 27.3 ya kiasi kilichokusanywa;

(iii) Makusanyo ya Fungu 29- Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.9 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 29 limechangia kwa asilimia 0.5 ya kiasi kilichokusanywa;

(iv) Makusanyo ya Fungu 51- Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.1 na Taarifa ya Makusanyo ilionesha Fungu 51 limechangia kwa asilimia 0.1 ya kiasi kilichokusanywa;

(v) Makusanyo ya Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 63 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 93 limechangia kwa asilimia 58.1 ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mafungu yote matano ni wa kuridhisha. Hadi kufikia mwisho wa robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 wastani wa makusanyo ulikuwa ni zaidi ya asilimia 50 ya lengo lililowekwa.

### 3.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka hazina

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara nyingi. Kwa kuzingatia jambo hilo Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2017. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari 2017, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 64.3 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.

(ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2017, asilimia 98 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(iii) Hadi kufikia mwezi Februari 2017, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 66.5 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na asilimia 28 ya bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi huo, ni dhahiri kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo bado hauridhishi. Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri mpango na ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kusimamia usalama wa raia na mali zao;

(ii) Kusimamia marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya magereza na katika maeneo ya jamii;

(iii) Kutoa huduma za zimamoto na uokoaji;

(iv) Kudhibiti uingiaji na utokaji nchini kwa raia na wageni;

(v) Utoaji wa vitambulisho vya Taifa; na

(vi) Kutoa huduma kwa wakimbizi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonyesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatatekelezeka kwa ufanisi endapo tu Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 293,822,132,859 sawa na asilimia 32.9 ya makadirio ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa lengo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

**Jedwali Na.02: MAKADIRIO YA MAPATO**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO |
|---|---|---|
| Fungu 14 - Zimamoto na uokoaji | 35,500,003,000 | 12.1 |
| Fungu 28 - Jeshi la Polisi | 73,600,000,000 | 25.1 |
| Fungu 29 - Jeshi la Magereza | 2,645,528,859 | 0.9 |
| Fungu 51 – Wizara | 1,226,601,100 | 0.4 |
| Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji | 180,800,000,000 | 61.5 |
| **Jumla** | **293,822,132,859** | |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Makadirio ya makusanyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yameongezeka kwa asilimia 1.4 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia;

(ii) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 12.1 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 12;

(iii) Fungu 28- Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 25.1 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 24;

(iv) Fungu 29- Jeshi la Magereza linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha asilimia 0.9 na mwaka 2016/ 2017 lilitegemewa kwa asilimia hizo hizo;

(v) Fungu 51- Wizara linategemewa kukusanya asilimia 0.4 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.1;

(vi) Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 61.5 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 63.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa ongezeko dogo la makadirio ya makusanyo kwenye baadhi ya mafungu limezingatia mafungu ambayo yalifanya vizuri kwenye makusanyo katika Mwaka wa Fedha unaoishia.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mhesimiwa Spika,** Maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni **shilingi 930,396,817,000/=.** Kati ya fedha hizo shilingi **522,681,568,000/=** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 367,706,884,000/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 40,008,365,000/=** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imeongezeka kwa shilingi 65,561,877,149.13 sawa na ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(ii) Asilimia 4.3 ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 56.2 ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 39.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo;

(iii) Wakati bajeti kuu ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa fedha tarehe 28 Machi, 2017, imeongezeka kwa asilimia 1.5 Bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya mradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia 16;

(iv) Wakati asilimia 38 ya bajeti kuu kwa mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya Maendeleo, asilimia 4.3 ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo;

(v) Wakati mwaka 2016/2017 asilimia 36.8 ya bajeti ya wizara hii ilikuwa ni kwa ajili ya uendeshaji (OC), mwaka 2017/2018 asilimia 39.5 ya bajeti ya wizara hii ni kwa ajili kugharamia uendeshaji wa shughuli (OC);

(vi) Pamoja na kwamba Serikali haikutoa shilingi Bilioni 2 zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la makao makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lililopo TAZARA- Dar es Salaam, Serikali haijatenga Kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo hilo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

(vii) Pamoja na kwamba kazi ya ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali katika Gereza la Segerea haikufanyika kutokana na kutokutolewa shilingi Bilioni moja zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali haijatenga fedha yoyote kwa ajili ya shughuli hiyo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili Randama za mafungu matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa mapendekezo na ushauri wa jumla kwa mafungu yote na ushauri mahsusi kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

### 5.1 Ushauri wa Jumla

#### 5.1.1 Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara na Mafungu yake

i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ukamilifu na kwa wakati ili kutekeleza kikamilifu miradi iliyopangwa. Hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha unaoishia, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 28 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo, jambo ambalo limeathiri ratiba na mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo.

ii) Miradi yote iliyokuwa imetengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na ambayo haijakamilika ipewe kipaumbele kwenye utekelezaji wake kabla ya kuanza kutekeleza miradi mingine mipya katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hii itaiwezesha Serikali kuwa na miradi michache lakini iliyokamilika na yenye tija kwa Serikali na Taifa kwa ujumla.

iii) Pamoja na nia njema ya Serikali kuhamia Dodoma, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutekeleza miradi yote iliyokuwa imeanza kutekelezwa katika jiji la Dar es Salaam, kwa mfano mradi wa ukamilishaji wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

### 5.2 Ushauri Mahsusi

#### 5.2.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

i) Serikali itafute uwezekano wa kutoa shilingi Bilioni 2 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji uliokwama tangu Mwaka 2013. Hii itasaidia kukamilisha jengo hilo haraka na hivyo kuokoa shilingi milioni 30 zinazolipwa kila mwezi ambapo kwa mwaka ni milioni 360, kwa ajili ya kodi ya pango ya Makao Makuu ya Jeshi hilo;

ii) Serikali ikamilishe mchakato wa marekebisho ya Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji ili kuboresha ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Jeshi hilo; na

iii) Serikali itenge Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi hili kuwa na vifaa hususan madawa na magari ya kuzimia moto. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Hazina itoe shilingi 1,382,955,000 ambazo bado hazijatolewa kwa ajili ya kununua magari mawili ya zimamoto kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Hii itawezesha Jeshi la Zimamoto kutekeleza kwa ufanisi jukumu lake la msingi la kutoa huduma bora za zimamoto na uokoaji.

### 5.2.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia matukio ya uhalifu kuendelea kutokea mara kwa mara nchini hususan matukio ya uhalifu wa mauaji ya wananchi, viongozi wa Serikali za Mitaa na Askari Polisi katika Mkoa wa Pwani, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Jeshi la Polisi nchini lihakikishe kwamba amani na utilivu katika Mkoa wa Pwani inaendelea kuimarika. Aidha, Jeshi litumie mbinu na taaluma za kipolisi kuhakikisha uhalifu huo unakomeshwa kwa kukamata wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

ii) Mipango ya kiutawala na uendeshaji ya Jeshi la Polisi kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yake katika mkoa wa Pwani iboreshwe kiutendaji;

iii) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Polisi kibajeti na vifaa ili Jeshi hilo liwe na ufanisi na mafanikio katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao ikiwemo kukabiliana na matukio ya mauaji na vihatarishi vya amani na usalama.

**Aidha mbali na makosa ya uhalifu wa mauaji Kamati inashauri:-**

iv) Serikali ikamilishe haraka mchakato wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani ili kudhibiti na kupunguza ajali za barabarani ambazo zimeongezeka kwa kasi kubwa na kupoteza maisha ya raia wetu.

v) Serikali isimamie usalama wa raia na mali zao katika maeneo yenye migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kuweka mikakati madhubuti ya kumaliza migogoro hiyo. Hii itawahakikishia wananchi usalama wao na wa mali zao katika maeneo hayo.

**5.2.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Jeshi la Magereza limekuwa likipewa ukomo mdogo wa bajeti usiozingatia mahitaji halisi pamoja na kupelekewa fedha pungufu katika migao ya kila mwezi, Kamati inashauri ifuatavyo:-

i) Serikali kupitia Hazina ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kulipa madeni yote ya Magereza yaliyohakikiwa yenye jumla ya shilingi 63,805,279,064.31. Hii itapunguza kasi ya kuzaliana kwa madeni na kuepusha migogoro inayoweza kutokea kati ya Jeshi na wazabuni, au Jeshi na watumishi wake;

ii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na vitendea kazi vya kisasa ili kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya ulinzi, usalama, uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali;

iii) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali iliyopo kaika Gereza la Segerea;

iv) Serikali iendelee kutekeleza program za adhabu mbadala kwa wafungwa ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani. Aidha, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa

na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuwezesha Mpango wa Huduma kwa Jamii. Hadi kufikia mwezi Februari 2017, Serikali ilikuwa imetoa asilimia 9.9 tu ya fedha zilizoidhinishwa;

v) Serikali ianzishe utaratibu wa kusafirisha mahabusu kwenda mahakamani na kurudi Gerezani kwa kununua na kupeleka mabasi katika mikoa yote Tanzania ambayo haina utaratibu huo. Hii itasaidia mahabusu wengi kupata haki zao za kisheria kwa wakati;

vi) Serikali ione umuhimu wa kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya askari magereza. Kwa sasa Jeshi linaupungufu wa nyumba 10,526 sawa na asilimia 71.4 ya mahitaji kamili na hivyo askari wengi kulazimika kuishi nje ya kambi jambo ambalo lina athari katika masuala ya ulinzi na usalama;

vii) Serikali iendeleze juhudi katika kuliwezesha Jeshi la Magereza kuanzisha/ kuimarisha viwanda mbalimbali kiwemo viwanda vya useremala, ngozi na sukari. Aidha, juhudi zaidi ziongezwe kuliwezesha Jeshi hili kibajeti na kununua vifaa vya kilimo vya kisasa ili liweze kujiendesha lenyewe;

viii) Kufuatia Serikali kufuta utaratibu wa majeshi kumiliki maduka yasiyotoza ushuru (Duty free shops) na badala yake kuanzisha utaratibu wa kutoa fedha, Serikali itoe fedha hizo kwa Jeshi la Magereza kama ilivyofanya kwa majeshi mengine yenye utaratibu huu.

### 5.2.4 Fungu 51- Wizara

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia matukio ya utekaji/ mauaji katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuhatarisha usalama wa raia na mali zao, Kamati inashauri:-

i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi iratibu ushirikiano wa vyombo vya Ulinzi na Usalama katika kutekeleza mikakati ya pamoja ya vyombo hivyo katika kudhibiti ipasavyo matukio yote yanayohatarisha usalama wa raia na mali zao nchini;

ii) Serikali ihakikishe kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea kuzingatia kufanya kazi kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu katika kuchunguza na kukamata watuhumiwa wa matukio hayo. Hii itawezesha vyombo hivyo kukamata wahusika halisi na pia itaepusha malalamiko ya kukamatwa kwa raia wasiokuwa na hatia;

**Aidha, Kamati inashauri:-**

iii) Serikali ione umuhimu wa kukamilisha mradi wa vitambulisho vya Taifa ambao ulipaswa kukamilika Mwezi Disemba 2016, kwa kutoa shilingi 17,239,710,636 ambazo bado hazijatolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwa Mwaka 2016/2017;

iv) Serikali kupitia Hazina itoe fedha zote zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kudhibiti vitendo vya ujambazi, unyang'anyi na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe. Hadi kufikia mwezi Februari 2017, Wizara ilikuwa imetoa shilingi 362,512,900 kati ya shilingi 1,823,201,000 sawa na asilimia 19.9 tu kwa ajili ya operesheni za kupambana na uhalifu wa aina hiyo.

### 5.2.5 Fungu 93- Idara ya Uhamiaji

i) Serikali iendelee kutekeleza mpango wa kuwarudisha makwao wahamiaji haramu walioko Magerezani ili kupunguza gharama za kuwahudumia na kupunguza msongamano Magerezani;

ii) Serikali iliwezeshe kibajeti Fungu 93 kufanya misako na doria ili kuwabaini na kuwaondosha wahamiaji haramu na raia wengine wa kigeni wasiotakiwa nchini;

iii) Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya pasipoti na malighafi zake iongezwe ili kukidhi mahitaji halisi ya utoaji wa huduma ya pasipoti na hati za dharura za kusafiria; na

iv) Rangi ya hati za kusafiria za kidiplomasia ibadilishwe kutoka nyeusi inayotumika sasa kuwa nyekundu kama ilivyo katika nchi nyingine.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
6. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
7. Mhe. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
8. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
9. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
10. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb
11. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
12. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
13. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
14. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb
15. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
16. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
17. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb
18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
19. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb
20. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb
21. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
22. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
23. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb
24. Mhe. Stephene J. Masele, Mb
25. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
26. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
27. Mhe. Khamisi Yahya Machano, Mb
28. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Katibu Mkuu Meja Jenerali Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu Balozi Yahya Simba pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, Bi. Grace Wambura, Bi. Chiku Ramadhani na Bi. Irene Olando kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu**, Mb**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,**
**ULINZI NA USALAMA**
09 Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Balozi Adadi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamkaribisha Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba nisome maelekezo ya Spika kuhusu Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya fedha kwa Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika anasema, "Nimepitia hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Godbless Lema kuhusiana na maoni ya Kambi hiyo kwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Nimejiridhisha kwamba kuna maeneo ambayo kwa ujumla wake yanapingana na maudhui ya Kanuni ya 64(1) na yalishatolewa maamuzi katika mkutano huu kuwa hayakubaliki kuingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa mantiki hiyo, nimeelekeza kwamba maelezo hayo yaondolewe na hata nakala za hotuba zitazowasilishwa hapa Bungeni na kugawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote hazitakuwa na maneno hayo isipokuwa hotuba zitaonyesha kwamba kuna maneno yameondolewa. Aidha Msemaji wa Kambi Rasmi atakaposema hotuba yake atatakiwa kuzingatia maelezo haya niliyoyatoa na sio kusoma maeneo yaliyoondolewa." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kutoa maoni ya kambi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa pole na salamu zetu za rambirambi kwa wazazi, familia na uongozi wa shule kwa wanafunzi 32, walimu na dereva wa shule ya Lucky Vincent waliopoteza maisha Mkoani Arusha mnamo tarehe 6 Mei, 2017 katika maeneo ya Rhotia Marera, wakiwa njiani kuelekea Wilayani Karatu kwa ajili ya mitihani ya ujirani mwema kujipima uwezo na shule ya wenzao. Msiba huu ni mzito na janga kubwa kwa Taifa na kupoteza hazina kubwa ya vijana waliokuwa na ndoto kubwa ya kulitumikia Taifa, ni msiba ambao umegusa moyo wa kila Mtanzania na watu wote ulimwenguni na hivyo kutuunganisha pamoja kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mwakilishi halali wa wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini mahali ambapo msiba ule wa Kitaifa umetokea, nilinyimwa kwa makusudi nafasi ya kutoa salamu za rambirambi pale uwanja wa Sheikh Amri Abeid, kwa wafiwa, Watanzania wote na wapiga kura wangu kwa siasa za chuki dhidi yangu zilipewa uzito mkubwa kuliko ubinadamu.  Hii ni ishara mbaya kwa Taifa na ni wazi kwamba tofauti zetu za kisiasa zinaweza kutufikisha pabaya kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nakushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kuguswa na msiba huu mzito na kuamua kutoa mchango mkubwa wa rambirambi kiasi cha shilingi milioni 100 kwa familia za wafiwa wote. Watu wa Arusha kwa pamoja wamenituma niwaletee salamu zangu za shukrani kwa Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa salamu zake kwa wakazi wa Arusha zilizosilishwa na Makamu wetu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikamatwa mwezi wa kumi mwaka 2016 nje ya Ukumbi wa Bunge. Safari yangu ya kupelekwa magereza ilianza kwa matisho makubwa. Nilikamatwa na askari wasiopungua watano. Tulianza safari kuelekea Arusha na kuwasili Kondoa majira ya saa 4 usiku

ambapo niliwekwa rumande Kituo cha Polisi Kondoa mpaka saa 8 usiku na kisha kuchukuliwa mpaka kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Mjijini Arusha ambapo safari yangu ya mateso na huzuni ilikamilika kwa mimi kukaa jela kwa zaidi ya miezi minne kwa kosa tu la kuota ndoto na kuona maono niliyopewa na Mwenyezi Mungu. Kwa dhati ya moyo wangu sifa, utukufu na heshima, narudisha shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wale wote walionijali wakati nilipokuwa magereza. Namshukuru kipekee mke wangu Neema kwa maombi yake na ujasiri wake, watoto wangu Allbless, Brilliant, Terrence na Precious Mawazo. Precious Mawazo ambaye baba yake mzazi Alphonce Mawazo hayupo kwani aliuawa kikatili katika mazingira ya kisiasa kwa kosa tu la kuwa mfuasi wa siasa za upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru marafiki zangu wafungwa na mahabusu niliowaacha Gereza Kuu Arusha kwa upendo na uenyeji wao wenye ukarimu katikati ya mateso mengi, ulionifundisha mengi na kumjua Mungu zaidi. Sitaacha kuwaombea hata siku moja tangu nimetoka gerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru viongozi wangu wa chama, Mwenyekiti wetu wa Taifa, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, viongozi wote wa UKAWA na wengine wote waliokuja kunisalimu nilipokuwa magereza bila kusahau viongozi wa dini zote na wanachama wote wa CHADEMA na wanachama na viongozi wa CCM ambao hawakujali kuitwa wasaliti kwa kujali utu, upendo kuliko chuki za kisiasa na utengano. Aidha, niwashukuru wanachama WA CCM waliothubutu kuja kuniona lakini wakaogopa, naweza nikaelewa hofu yao na inatupa picha Taifa linakwenda wapi, pia wao nawaombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa na changamoto nyingi sana, changamoto kubwa ya msingi ni hali ya usalama wa nchi

ambayo ni muhimu ikiwezekana hekima zetu zikajikita kwenye mjadala wake na kutafuta ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama wa nchi, maadili ya familia na mapambano dhidi ya rushwa. Jambo hili linalohusu maadili nilianza kulisema katika hotuba yangu ya mwaka 2016/2017, kuwa ukitaka kuhakikisha hali ya usalama wa Taifa hili ni sharti jamii na Serikali kwa ujumla iwekeze nguvu zake katika malezi yenye maadili bora yatakayojenga familia zetu ili kuunda Taifa imara kabisa Afrika na duniani kote. Nilisema hapa mwaka jana na nitanukuu kuwa:-

*"Taifa lolote Duniani msingi wake ni familia, hivyo njia sahihi ya Taifa kuwa na usalama wa kweli katika Jamii ni muhimu Serikali ikajua kuwa Jamii ni Familia, kuongelea hali ya usalama na amani ya Nchi yetu bila kuongelea maadili ya familia zetu ni kupotosha fikra zetu."*

Na pia *"ukweli ni kwamba familia yenye maadili, wajibu na inayomcha Mungu ni jamii bora itakayozalisha Raia wema wenye wajibu na tija kwa Taifa, hatuwezi kuwa na Nchi yenye nidhamu na ustawi pasipo kuwa na familia zenye wajibu katika malezi."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inaamini kuwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, *paragraph* hiyo imeondolewa, nakukumbusha tena kwa mara nyingine.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hata hii hamtaki?

**MWENYEKITI:** Unaendelea kwenye mifumo ya kutoa haki nchini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**WABUNGE FULANI:** Kaeni.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mambo ya utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema maelezo tumeshatoa, naomba tuyaheshimu na tuheshimiane ili tuendelee vizuri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, naomba uendelee kwa mujibu wa taarifa ambayo nimeisoma mbele yenu ambayo imetolewa na Spika na maamUzi yakishatolewa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utaratibu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ungesikiliza kwanza utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema naomba uendelee pale ambapo tumeachia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba mkae tafadhali, tuendelee Mheshimiwa Lema.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Tusikilize suala la utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Ester Bulaya mkae tuendelee na hotuba tukishamaliza kama tuna la kusema tutasema lakini maelekezo ambayo tumeyatoa hatuwezi kuyabadilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hatuwezi kuendelea wakati suala linahusu sasa hivi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kuhusu utaratibu ni haki kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Mheshimiwa ameomba hapa.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Lema amalize kusoma.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wenyewe unahusu suala la sasa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mnyika ameomba kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba basi mkae chini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Angesimama upande wa Serikali mngemnyima? *Fair* itendeke Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini. Waheshimiwa Wabunge tafadhali naomba Mheshimiwa Lema aendelee kumalizia hotuba yake.

**MHE. JOHN MNYIKA:** Kuhusu suala la utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae, tafadhali Mheshimiwa Lema endelea.

**MHE. JOHN MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utaratibu kabla hajaendelea kwa sababu linahusu suala linaloendelea hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Mtoe nje!

**MWENYEKITI:** Mwongozo umeshatolewa mwanzo, kwa hiyo, naomba aendelee.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Ester kaa chini wewe.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WABUNGE FULANI:** Watoe nje.

**MWENYEKITI:** Nawaomba mkae chini kwa mara ya mwisho, Mheshimiwa Lema endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utaratibu kabla hajaendelea.

**MWENYEKITI:** Nazungumza tena kwa mara ya mwisho, naomba mkae chini Mheshimiwa Lema aendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Utaratibu unahusu kabla hajaendelea.

**MWENYEKITI:** Hakuna ambalo linahitaji utaratibu kwa hapo maelezo nimeshayatoa mwanzo, naomba Mheshimiwa Lema aendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Tufuate Kanuni hizi.

**WABUNGE FULANI:** Watoe nje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema naomba uendelee.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa suala la rushwa ni suala linalohusu zaidi maadili. Hata hivyo, Kambi Rasmi Bungeni hairidhishwi kabisa na jitihada za Serikali katika kukabiliana na rushwa kwani viongozi wakuu wa nchi wameonekana waziwazi wakisema...**[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

**MWENYEKITI:** Anayoyazungumza Mheshimiwa Lema yameondolewa.

**WABUNGE FULANI:** Rushwa, rushwa imeondolewa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Jamani rushwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Lema anatakiwa aendelee kuanzia mifumo ya kutoa haki nchini.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Woga huo.

**MBUNGE FULANI:** Mnaogopa hata rushwa?

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi ni shida, Mwigulu anaweza kuja akasoma kipande hiki. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tatizo si msomaji, tatizo ni maneno ambayo yameondolewa, naomba tuelewane na unielewe. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini muda wangu utalindwa lakini kila mnachopanda mtavuna, tena mbele ya macho yetu, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika japokuwa ukweli huo unapata vikwazo vingi kwamba haki huzaa amani. Katika Taifa ni muhimu tukajua kwamba wingi wa silaha, ukubwa wa majeshi hauwezi kuwa sababu ya kuwepo kwa amani. Katika Taifa lenye uonevu na ukimya ukatawala kwa sababu ya mabavu ya dola Taifa hilo liko kwenye hatari kubwa ya migogoro ya kijamii kwani njia pekee

ya kutunza amani ni mifumo ya kutoa haki nchini ikajua kwamba haki huzaa amani ikiwa ni pamoja na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa hili haki ina mgogoro mkubwa katika maeneo mbalimbali ya utaoji haki nchini. Ni muhimu kwamba ukimya huu uliopo sasa ukatazamwa kama uvumilivu unaoweza kufikia ukomo na kukata tamaa. Ukienda sehemu mbalimbali zinazotoa haki kuanzia Serikalini, Mahakamani, Bungeni, Polisi na sehemu nyingine ambazo kwa asili hutakiwa kutoa haki utakuta kuna uonevu, unyanyasaji na ukandamizaji wa hali ya juu ambao unakusanya hasira za watu ndani ya mioyo yao kama inavyotokea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi kuendelea kupuuza maneno kama haya kwa sababu yanatolewa na upande wa pili wa waleta maoni, lakini ipo siku tutakumbukwa kwa ukweli huu tunaousema ndani ya Bunge hili. Uonevu na ukandamizaji katika Taifa hili imekuwa ni sehemu ya maisha ya kila siku ya Mtanzania. Mimi ni mfano hai wa uonevu huo, Mheshimiwa Lijualikali ni mfano wa uonevu huo, Mheshimiwa Lissu ni mfano wa uonevu huo na familia ya marehemu Mawazo ni mfano wa uonevu huo, familia ya Ben Saanane ni mfano wa uonevu huo, Msafiri Mbwambo aliyeuawa na kuchinjwa shingo maeneo ya *USA River* na waliomuua kutoroka wakiwa wamefungwa pingu mbele ya Polisi wanne wenye *SMG*. *(Makofi)*

MheshimiwaMwenyekiti, hawa ni wale ambao nimewakumbuka kuwataja, lakini ukienda magerezani, mahabusu, mahakamani, hospitalini hata makaburini kwa waliokufa na kila mahali panapotolewa huduma za umma zinazohusu Watanzania utakutana na vilio na mateso kutoka kwa watu wengi sana wanaodhulumiwa haki zao. Angalau kila familia katika Taifa hili ukiachilia watawala wa Serikali ya CCM hii inaweza ikasimulia huzuni na mateso wanayokutana nayo kila siku katika mifumo ya utoaji haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mateso na huzuni zao haziwafundishi watu hao kuwa waoga japokuwa wanaonekana ni waoga kama hatua za haraka zisipochukuliwa na Serikali kwa kuganga mioyo yao kwa kutenda haki ipo siku Taifa letu litakuwa na historia mbaya kwa kuwa watu hao wanaandamana ndani ya mioyo yao wakati miguu yao imezuiwa kuandamana kudai haki kutokana na vitisho vya zana za kivita. Ni ajabu mtu anapoandamana kudai maji ya kunywa anakabiliwa na mtutu wa bunduki. Ni jambo la kushangaza chama cha siasa kinapotaka kudai haki ya msingi ya kutaka kuandamana na kufanya mikutano ambayo ni haki yao kikatiba na kisheria wanakamatwa na kufunguliwa kesi zilizobatizwa jina la “Uchochezi”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini mambo haya ni ya muda tu, kwani haki haijawahi kushindwa na kila mpigania haki ni mpenzi wa Mungu. Ni hakika yetu kuwa kila mtu atavuna anachopanda. Ni maombi yetu kwa nia njema kabisa kwamba Serikali hii ijitahidi kutenda mema ili watoto wenu na wajukuu wenu wakute Taifa lenye misingi ya kuheshimu haki na utu. Kwani huo ndiyo urithi mnaopaswa kuacha kwa watoto wenu na sio nyumba na magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kusema siku za nyuma kwenye moja ya mchango wangu kuwa CCM ikitawala muda wote lakini ikatawala kwa haki, heri na baraka utawala wao unapaswa kuheshimiwa. Lengo Letu kama Wapinzani si tu kuiondoa CCM madarakani bali ni kuhakikisha kuwa CCM inatawala katika misingi ya haki na kheri kwa nyie ndio watawala kwa sasa. Mnapokosea ninyi sio CCM inayopata hasara bali ni Taifa zima ndilo linalopata hasara na sisi na ninyi ni miongoni mwa wananchi wa Taifa hili. Haki huinua Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la uhalifu unaotakana na uchumi duni. Amani ya Taifa hili itategemea pia hali ya uchumi wa Taifa hili. Kama ilivyo hivi sasa katika mzunguko wa fedha nchini ni ishara kwamba jitihada za

ziada zinapaswa kufanyika juu ya uchumi na biashara ili kuongeza tija na maisha bora miongoni mwa Watanzania na kupunguza uhalifu unaosababishwa na njaa na ukosefu wa kipato halali. Tatizo kubwa la mzunguko hafifu wa fedha linatokana na kauli za viongozi mbalimbali wa Serikali ambazo zimesababisha mashaka makubwa katika uwekezaji wa biashara katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ni busara kubana matumizi lakini ni muhimu zaidi ikajulikana kwamba, matumizi ya kila siku ya Serikali na jamii ndiyo chanzo cha mzunguko wa fedha katika jamii. Hivyo, sera za Serikali katika uchumi wa nchi sharti zizingatie hali ya usalama wa maisha ya wananchi wake kwa kuruhusu mzunguko halali wa fedha katika maeneo mbalimbali ya kibiashara ikiwa ni pamoja na Serikali hii kulipa madeni ya wazabuni mbalimbali wanaoidai Serikali kwa muda sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio la ongezeko la uhalifu unaotokana na njaa na mabadiliko ya tabia ya nchi. Ni muhimu Taifa kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ikajenga uwezo wake wa kuona picha kubwa katika Taifa ya kuangalia visababishi vinavyotishia hali ya usalama ndani ya nchi, ikiwemo suala la tishio la mabadiliko ya tabia ya nchi. Hivyo, kazi muhimu sana ya Wizara ya Mambo ya Ndani ni kuzuia kuporomoka kwa amani sasa na katika siku za baadaye. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa hali ya mabadiliko ya tabia nchi na hali ya nchi duniani na Tanzania kwa ujumla ni moja ya sababu zinazoweza kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani katika siku za usoni kwa kuwa tabia ya nchi imebadilika sana hivyo kupelekea ongezeko la njaa kutokana na uzalishaji duni wa chakula cha kutosha kupitia kilimo kinachosuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wote tunakubaliana kuwa mtu mwenye njaa ni mtu mwenye hasira. Hivyo, ili kukabiliana na uhalifu unaosababishwa na njaa na tafrani nyingine za kimazingira, ni muhimu sasa Serikali ikaweka malengo muhimu katika utunzaji wa misitu na

upandaji miti ili kukabiliana na changamoto hizi kwa siku za usoni. Vilevile Serikali ni muhimu sana ikaongeza bajeti katika Wizara inayoshugulikia mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliangalia suala la usalama wa chakula, mabadiliko ya tabia nchi kama suala la usalama wa raia na mali zao. Hivyo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliingize katika sera na mipango yake kama suala mtambuka la kiusalama. Mathalani Jeshi la Magereza kupitia mashamba yake yatumiwe kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na kuhakikisha kwamba usalama wa chakula unakuwepo muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mateso na mauaji ya raia wasiokuwa na...

**MWENYEKITI:** Haimo na hiyo Mheshimiwa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hii nayo Mwenyekiti hutaki, pia ukurasa wa 12 na 13 hutaki, haya Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia bora ya kupambana na ujambazi nchini. Ni ukweli usiopingika kuwa kumekuwa na viashiria vya wazi kabisa vya matendo ya kigaidi katika nchi yetu. Hata hivyo, ni uhalifu ambao unahitaji utaalam wa hali ya juu na hekima katika kukabiliana nao. Ni rai yetu kuwa suala la ugaidi halihitaji tu operesheni maalum na muhimu katika kuwasaka magaidi mahali popote walipo pia ni muhimu zaidi ikafamika kwa nini sasa sura na hali hii ya matukio ya kigaidi yanaanza kujitokeza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia Jeshi la Polisi likikabiliana na matukio mbalimbali ya kiuhalifu, mengine yenye sura za ujambazi na mengine yenye sura za kigaidi. Ni muhimu sana Jeshi la Polisi likajua changamoto wanazopitia za kiusalama ndani ya nchi yetu, haziwezi kutatuliwa kwa wingi wa askari waliopo na

wingi wa silaha zilizopo bali wanahitaji kujenga mahusiano mazuri baina ya Jeshi hilo na raia wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha kuwa tunajali mahusiano mema baina ya Jeshi la Polisi na raia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na raia wote wa Tanzania kulaani vikali matukio ya mauaji ya Askari Polisi wetu ambayo miaka ya hivi karibuni yamekuwa yakijirudia na Serikali bado haijatoa taarifa za kina juu ya kujirudia kwa mauaji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa inapokuja kwenye masuala ya kuzuia vyama vya upinzani visifanye mikutano ya kikatiba, maandamano na mikutano ya hadhara kwa nyakati mbalimbali Jeshi limekuwa jepesi kutumika kisiasa kuzuia mikusanyiko hiyo kwa kisingizio cha 'taarifa za kiintelijensia' kuwa kungeweza kutokea vurugu. Hata hivyo, inapokuja katika suala la kuzuia mauaji ya Askari hao hao basi uwezo wao wa kunusa taarifa na kuzuia mauaji yasitokee unakuwa ni duni. Huu ni ushahidi tosha kuwa intelijensia ya Jeshi letu la Polisi ni dhaifu kwa sababu za kujiingiza katika siasa badala ya kuangalia maslahi mapana ya kitaifa na kuzingatia weledi wa kazi ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia matukio hayo yasitokee na kutokomeza kabisa vikundi hatarishi vya usalama wa nchi hii, huu ndio wakati ambao Idara ya Usalama wa Taifa pamoja na Intelijensia ya Jeshi letu la Polisi ingetumika ipasavyo kubaini matukio hayo na kuyazuia kabla hayajatokea lakini hali imekuwa ni tofauti. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mara moja kuitumia Idara ya Usalama wa Taifa na Jeshi la Polisi kwa maslahi ya kisiasa na ikajielekeza katika matumizi ya vyombo hivyo kuzuia matukio ya mauaji ya Askari na viongozi wa Serikali za Mitaa kama ilivyotokea katika Wilaya ya Kibiti. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulipatia Jeshi la Polisi zana za kisasa za kupambana na makundi ya kigaidi, kijambazi na makundi mengine ya kihalifu yenye mrengo wa uporaji wa silaha na mauaji ya askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kitengo cha Upelelezi; takribani miaka 20 iliyopita, hakujawahi kufanyika Mafunzo Maalum ya Upelelezi *(CID Course)*. Hivyo basi, ndiyo sababu katika matukio yanayohitaji uweledi wa intelijensia Jeshi la Polisi limekuwa likijitokeza kama Kikundi cha Mapambano yaani *Operation Force*. Aidha, Jeshi la Polisi badala ya kutengewa bajeti ya kununua magari ya washawasha na kuwamwagia maji hayo raia wasiokuwa na silaha, basi ilipatie Jeshi hilo fedha za kutosha kununua zana za kisasa za kiuchunguzi na kutenga fedha maalum kwenye Mfuko wa Fedha za Upelelezi ambao uko kishera *(Criminal Investigation Fund)* ili kutoa nguvu na uwezo wa upelelezi kufanyika kwa kina hasa kipindi ambapo ulimwengu unakabiliwa na uhalifu wa aina mbalimbali unaozidi zana na ujuzi uliopo. Ni aibu kwa Taifa kwamba Serikali imekuwa haitoi fedha hizo ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na hivyo kufanya shughuli za upelelezi kuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magereza yetu hapa nchini watuhumiwa wengi wa ugaidi ni pamoja na viongozi wa dini na unaposhindwa kukamilisha upelelezi haraka wa kesi hizi, unaweza ukaleta mgogoro mkubwa wa kimatabaka ya dini kwa wasio na hatia kuona kwamba kuna mkakati wa dhati wa kuonea na kudhalilishana. Maneno haya yanasemwa na ili yasisemwe ni bora mkakamilisha upelelezi haraka ili kila mtu avune alichopanda kwa haki na sio kwa hila na ulaghai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magereza mbalimbali nchini kuna watuhumiwa wa kesi za ugaidi walioshikiliwa kwa muda sasa. Katika Gereza Kuu la Arusha mahabusu wa kesi za ugaidi wanaanza kuhesabu mwaka wa nne wakiwa mahabusu bila upelelezi wa kesi zao kukamilika. Wakati wa kukamatwa kwao, wengine waliuawa na wengine wameachwa na vilema vya kudumu vya kukatwa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za wafungwa, mahabusu na watuhumiwa wa makosa mbalimbali nchini. Kama ambavyo jamii iliyoko uraiani ina haki zake ndivyo ilivyo

kwa mahabusu na wafungwa. Sio lugha rahisi sana kueleweka kwa watu ambao hawajawahi kuwa magereza na ndio sababu nilipotoka magereza nilimwomba Mungu angalau kila Mbunge apite jela kwa miezi isiyopungua miwili na bado ni maombi yangu tena yenye msisitizo kwa Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosa uhuru ni adhabu kubwa sana duniani na anayeijua ni huyo anayekuwa hana uhuru. Moja ya huzuni kubwa waliyo nayo watuhumiwa katika Taifa hili ni ucheleweshwaji wa kesi. Ni kawaida sana mtuhumiwa kujikuta yuko magereza kwa muda mrefu wakati mwingine zaidi hata ya miaka sita akisuburi kesi au upelelezi kukamilika, haya ni mateso makubwa sana. Ni muhimu sasa Bunge lako Tukufu likatunga Sheria ya kuwepo na kikomo cha upelelezi katika makosa yote ya jinai tofauti na sasa ambapo baadhi ya makosa mengi ya jinai hayana kikomo cha upelelezi na hivyo kuwafanya watuhumiwa kukaa ndani muda mrefu bila mashauri yao kusikilizwa na kuongeza tabu na huzuni katika maisha yao na msongamano wa mahabusu magerezani unaolipelekea pia Taifa hili kupata hasara kubwa ya kuwatunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutana na vijana wengi nilipokuwa mahabusu, nilitumia muda mwingi kuongea nao na hivi ndivyo walivyosema:-

*“Mheshimiwa Mbunge ili kuzuia rushwa na uonevu unaofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na ofisi ya DPP ni muhimu Wabunge wakaondoa vikwazo vya dhamana kwenye makosa yote ya jinai kama ilivyo Kenya na Uganda, kwani ubambikiwaji wa kesi unafanywa kwenye makosa yasiyokuwa na dhamana ili watuhumiwa waweze kufikiria kutoa rushwa kubwa. “(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nao kwa asilimia zote, katika Taifa la Kenya makosa yote yana dhamana isipokuwa uhaini; Uganda makosa yote yana dhamana ikiwemo uhaini; Tanzania orodha ya makosa yasiyokuwa na dhamana ni mengi lakini hata yenye

dhamana siku hizi pia yanaweza kuzuiliwa dhamana kwa kitu kinachoitwa ‘Hati ya Mwendesha Mashtaka” *(Certificate of DDP).* Japokuwa kuna hukumu ya hivi karibuni ya Mahakama Kuu iliyoitangaza Hati ya *DPP* kuwa ipo kinyume cha Katiba kwa kuzuia dhamana kwa watuhumiwa lakini ofisi ya *DPP* imeendelea kuidharau hukumu hiyo ya Mahakama na endapo *DPP* akijisikia kukuwekea hati hiyo maana yake ujue kwamba unaanza kesi ya kupigania dhamana yako kwenye mashtaka hata yenye nafasi ya dhamana kisheria, jambo ambalo limesababisha mateso mengi na kuongeza msongamano wa watuhumiwa magerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakili Median Mwale ambaye *AG* anamfahamu vizuri anaanza mwaka wa saba magereza bila shauri lake kukamilika, bado ni mahabusu na aliniambia maneno haya:-

*“Mheshimiwa Mbunge nimekaa sana magereza, nimechoka sana mwili wangu na roho yangu, nimezuiwa hata kuzaa na sijui kesi yangu itakwisha lini. Ningetamani shauri hili liishe, kwani hata kama ningekutwa na hatia katika shauri hili ningekuwa nimeshafungwa na kumaliza kifungo changu. Nashukuru umekuja magereza na pengine Christmas utaweza kuwa nasi na ukitoka nenda ukawatetee mahubusu, wafungwa na Askari jela”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakili Mwale aliendelea kuniambia kuwa:-

*“Bunge linapotunga sheria linapaswa kuwa makini, kwa mfano; kesi inayonikabili mimi ya Money Laundery inamkabili pia kijana mmoja anaitwa Masawe yupo humu ndani, anakabiliwa na shitaka la Money Laundery la dola 1,900 lakini amekaa jela zaidi ya miezi 15 kwa sababu shtaka hili halina dhamana na adhabu yake ukikutwa na hatia ni kati ya miaka 4 na 7, wakati huo huo mtu anayetuhumiwa kunajisi au kubaka kosa ambalo adhabu yake ni miaka 30 jela au kifungo cha maisha, anapewa dhamana akisubiri shauri lake kukamilika. Wabunge mnapoletewa Miswada ya Sheria na Serikali, mnapimaje haya mambo? Sheria za nchi*

*zinahitaji rehema ili kujenga dhana ya urekebishaji na sio mateso yasiyolenga dhana ya urekebishaji" (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza kuoneka jambo rahisi mtu kukaa jela miaka saba bila kesi yake na upelelezi kukamilika, Waheshimiwa Wabunge nawaomba tena, niko chini ya miguu yenu, vaeni utu na viatu vya watu hawa na familia zao, ni mateso na huzuni sana. Mimi najua na kila siku nawaombea kwa Mungu. Hivyo chanzo muhimu kinachosababisha msongamano na mateso magerezani ni ofisi ya *DPP*, sheria mbovu zisizozingatia utu na ucheleweshwaji wa upelelezi kutoka katika Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma *(DPP)* tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali zenye nia ovu ya kutumia Mahakama ndivyo sivyo *(DPP abuse of Courts)* kupindisha haki kwa makusudi katika kesi mbalimbali, hususani kuzuia haki ya dhamana kwa watuhumiwa ambao hawajatiwa hatiani na mahakama. *DPP* akiiwakilisha Serikali hudiriki kufanya hivyo hata katika makosa ambayo kisheria watuhumiwa wana haki ya dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta Bungeni haraka iwezekanavyo mabadliko ya sheria mbalimbali kandamizi kuhusu mienendo ya makosa ya jinai ili sheria zote katika mwenendo wa makosa ya jinai iakisi utu na urekebishaji ili kupunguza mateso kwa binadamu. Aidha, tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Kitengo cha Upelelezi cha Jeshi la Polisi na bajeti ya Mahakama ya Tanzania inakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi, wepesi, uharaka, weledi wa hali ya juu, uzingatiaji wa maadili, haki na utu wa binadamu bila kuwa na njaa na tamaa ya rushwa na ucheleweshaji wa mashauri mahakamani ambao unatokana na ufinyu wa bajeti kwa sasa. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa maslahi ya Waendesha Mashtaka ya Serikali, watumishi wote wa Mahakama na Askari Polisi wote

yanazingatiwa vizuri ili kuwapa utulivu katika kazi ya kutenda haki na sio vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharamia dhidi ya siasa na demokrasia nchini. Siasa safi na demokrasia ya kukuza amani nchini. Misingi ya amani katika Taifa inategemea siasa safi na demokrasia huru. Ushindani wetu wa kisiasa unapokosa siasa safi na demokrasia huru ni dhahiri kwamba Taifa halitaweza kuepuka uvunjifu wa amani unaopunguza kasi ya maendeleo na mshikamano wa Taifa. Katazo la mikutano ya hadhara na kazi za siasa katika nchi sio tu ni hatari kwa vyama vya siasa vinavyozuiwa kufanya kazi zake za siasa na chama dola bali ni hatari kwa demokrasia ya chama dola hicho pia kinachozuia kazi za siasa kwa vyama vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa vyama vya siasa vinavyowakilisha maoni ya aina mbalimbali ni nguzo muhimu ya usalama wa Taifa hili. Kitendo cha Serikali ya CCM kupuuza nguzo hiyo ni kuamua kwa makusudi kuliingiza Taifa katika majanga ya chuki yanayoweza kuliingiza Taifa katika migogoro isiyokwisha. Ni wajibu wa chama kilichopo madarakani kuhakikisha ukuaji wa demokrasia kuwa ni silaha muhimu ya amani katika nchi na sio kupuuza demokrasia, kudhalilisha vyama vingine visiyokuwa na dola kama CCM inavyofurahia kufanya kule visiwani Zanzibar na hapa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa CCM ndani ya Bunge unaweza kutumika kupuuza hata maoni haya muhimu. Mwandishi Voltaire aliyeishi kati ya mwaka 1694 na 1778 katika moja ya maandiko yake aliwahi kusema kuwa, *"It is dangerous to be right when the government is wrong"* akimaanisha kuwa "ni hatari kuwa sahihi wakati Serikali haipo sahihi". Hiki ndicho kinachowakuta raia wote wa Tanzania leo hii. Katika Serikali ya Awamu hii ya Tano tumeona na kuthibitisha namna ambavyo demokrasia na wanademokrasia wanavyopita katika wakati mgumu katika maisha yao ya siasa ya kila siku. Dhambi ya kuua demokrasia hapa nchini msidhani kuwa itaishia kuangamiza upinzani,

bali italitafuna Taifa na itaingia hadi ndani ya chama chenu CCM na wakati huo ukiwadia hakuna kati yenu au watoto wenu atakayesalimika. *Only time will tell*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari leo kwa Mtanzania kuthubutu kuwa na maoni tofauti na yale ya Serikali. Kusikiliza maoni yasiyofanana na mtazamo wako na usiyoyapenda ni busara na pia ni dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wengi waliopotezwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, hii pia huipendi? *Okay*, nisije nikakukwaza na mimi nakupenda, nakuheshimu ngoja niruke. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Njia bora za kuzuia ukatili wa vyombo vya dola nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jeshi la Polisi likituhumiwa kufanya mauaji haliwezi kujichunguza lenyewe na kutoa maamuzi lenyewe; basi sharti kuwe na chombo huru kitakachosimamia Jeshi la Polisi. Kwa muktadha huo wa kulifanya Jeshi letu la Polisi kuzingatia sheria ya Jeshi hilo, sheria nyingine na Katiba ya nchi yetu na kuachana kabisa na kujirudia kwa makosa ya uadilifu wa Jeshi la Polisi katika kusababisha mauaji na ukatili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuzingatia ushauri uliotolewa na wadau wa Haki za Binadamu kwa kuleta Muswada wa Sheria katika Bunge lako Tukufu utakaounda chombo maalum cha kuangalia utendaji kazi wa haki ndani ya Jeshi la Polisi.

Chombo ambacho kitafanya uchunguzi na kuwawajibisha Maafisa wa Polisi ambao wamejihusisha na mauaji na utekaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea ushauri ambao tumekuwa tukiutoa mara kwa mara kwa Serikali ambao haujawahi kufanyiwa kazi juu ya kuundwa kwa Mahakama ya Korona *(Coroners Court)* kwa mujibu wa sheria inayotoa mamlaka ya kuchunguza vifo vyenye utata *(Inquest Act)*. Mfano wa kifo ni kama kile cha Marehemu Alphonce Mawazo ambapo mpaka sasa hakuna taarifa mahsusi juu ya kifo hicho ambazo zimetolewa na mamlaka ya Serikali huku ikijulikana wazi kwamba Mawazo aliuwawa mchana kweupe huko Busanda, Mkoani Geita mbele ya Kituo cha Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi za kuzuia uhalifu nchini kwa njia ya bajeti. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi 5.3 kama bajeti ya maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Kwa mujibu wa randama ya Wizara, Fungu la 28 la Jeshi la Polisi hadi kufikia mwezi Februari, 2017 fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Serikali ilikuwa ni jumla ya shilingi milioni 40 sawa na asilimia moja tu ya bajeti yote ya maendeleo iliyotengwa na Bunge. Hii ni aibu kubwa na ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti Askari Polisi wanapotekeleza wajibu wao hupiga, hutesa na hata kuteka nyara wananchi na wakati mwingine kusababisha ulemavu hata kifo kutokana na kukosa mafunzo ya kushughulika na ulinzi wa raia na mali zao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachelea kusema kuwa hali hii ni kutokana na bajeti finyu ya maendeleo ambayo ingetumika kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Askari hao. Kitendo cha Serikali kutopeleka fedha za maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Polisi kinapunguza weledi wa Jeshi la Polisi kutokana na kukosa mafunzo muhimu ya kuendesha kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu sababu

za kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kwa Jeshi hili ili kutekeleza majukumu yake mahsusi ya ulinzi wa raia na mali zao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa kitendo cha kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kinalifanya Jeshi Polisi kushindwa kuwekeza kwenye intelijensia pamoja na mafunzo ya kuimarisha weledi na hivyo kuzuia matukio kama yale ya kuuawa kwa Askari wa Jeshi Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha usalama wa barabarani. Wakati Wizara ya Mambo ya Ndani inawasilisha makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka huu wa fedha, Taifa limepatwa na mshtuko mkubwa sana juu ya ajali mbaya iliyotokea huko Karatu, Mkoani Arusha na kusababisha vifo vya watoto wa shule ya Msingi Lucky Vincent ya Jijini Arusha ambapo walimu wawili na dereva wa gari na wanafunzi 32 wote walipoteza maisha hapo hapo. Siyo muhimu tena kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kuja na takwimu za idadi ya vifo na ulemavu unaotokana na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ziko wazi kwamba watu wanapoteza maisha kila uchwao. Pamoja na sheria kali za usalama barabarani kutungwa, ni muhimu sasa masuala yanayohusu usalama barabarani yakaanza kufundishwa kuanzia shule za msingi mpaka katika vyuo vya elimu ya juu kwani usalama wa barabarani hauhusu gari peke yake bali inahusu pia namna sahihi ya matumizi ya barabara kwa kila mmoja wetu na watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayo taarifa kwamba mafunzo ya Askari wa Usalama Barabarani *(Traffic)* hayajafanyika kwa muda mrefu na hivyo Askari wengi wa Barabarani wanafanya kazi kwa mazoea badala ya utaalam. Hii ndio sababu kazi yao imekuwa ni ya kuvizia hadi kufikia kupanda juu ya miti na kamera za tochi huku wakiamini kuwa kosa la barabarani ni mwendo kasi peke yake. Hawana uwezo wa kufanya uchambuzi wa kina hata juu ya matatizo ya mifumo ya magari kwa undani. Leo hii Kitengo hicho cha *Traffic* kinatumika kukusanya mapato, kazi ya *TRA* badala ya

kutumika kuelimisha jamii juu ya usalama barabarani jambo ambalo ndio dhima ya uanzishwaji wa kitengo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaasa wananchi wote Tanzania wawe makini katika chaguzi zinazokuja, kwani vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani ni sehemu ya majanga mengi yanayotokana na Serikali hii ya Awamu ya Tano kushindwa kusimamia ustawi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi duni ya Askari Polisi na Magereza. Askari wetu wanahitaji mazingira bora na maslahi bora wawapo kazini. Nguzo ya kwanza ya ulinzi kwa askari ni yeye kuwa na amani, askari wasiokuwa na maslahi bora ni hatari kwa usalama wa Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kucheza na maslahi ya askari wetu na kuanza kuwalipa mishahara vizuri na posho zote zilizoko kisheria kama ambavyo wanafanya kwa watumishi wengine wa umma kama Wabunge na Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia msongamano wa mahabusu na wafungwa na bajeti ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia randama ya bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo Fungu 29 ya mwaka 2017/2018 na kubaini kuwa bajeti ya maendeleo iliyopelekwa katika Jeshi la Magereza na Serikali mpaka mwezi Februari, 2017 ni asilimia 6 tu ya bajeti yote ya fedha za maendeleo ya Jeshi la Magereza ambazo ziliziidhinishiwa na Bunge ilikuwa ni shilingi bilioni tatu na fedha zilizotolewa ni Sh.190,000,000 peke yake. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza nchini limenukuliwa likitoa lawama kwa Serikali kutokana na kuruhusu msongamano magerezani bila kuwa na juhudi zozote za kutatua shida hiyo. Ikumbukwe kuwa magereza

nchi hii yana uwezo wa kuhifadhi wahalifu 29,000 kwa siku lakini anapokea wastani wa wahalifu kati ya 35,000 mpaka 38,000. Katika randama ya Fungu 29 - Jeshi la Magereza limeitupia Serikali lawama likisema kuwa msongamano huu unafanya tusiweze kutoa huduma ipasavyo kutokana na fedha kidogo zinazotolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti kama unavyosemekana kwenye randama unasababisha kutofanikiwa kwa masuala mbalimbali ya kimaendeleo ya jeshi hilo kama ifuatavyo:-

(i) Ukosefu wa nyumba za maafisa na maaskari;

(ii) Upungufu wa vyombo vya usafiri;

(iii) Upungufu wa watumishi;

(iv) Madeni ya watumishi shilingi bilioni 23 na wazabuni shilingi bilioni 44;

(v) Ukosefu wa ofisi stahiki za Wakuu wa Magereza wa Mikoa; na

(vi) Uhaba wa madawa na vifaa vya tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nilivyokwenda Gereza Kuu Kisongo nilikuta hawana hata kompyuta mimi ndiyo niliyewanunulia kompyuta nikiwa mahabusu mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza kwa mwaka wa fedha 2018 limeomba fedha za bajeti ya maendeleo shilingi bilioni saba sawa na ongezeko la asilimia 58 la bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji Serikali inawezaje kuleta hapa ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa asilimia 58 zaidi kuliko ile bajeti ya mwaka wa fedha unaoenda kuisha kama siyo kulihadaa Jeshi la Magereza kuwa watapatiwa bajeti kubwa wakati uwezo wa Serikali kutoa fedha haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza vyema Sheria ya *Parole* na utekelezaji wake uzingatie kuwaachia huru wafungwa ambao wameshatumikia vifungo virefu gerezani badala ya wale ambao wamehukumiwa miaka michache na wanaachiwa kwa *parole* kila mara. Uzoefu unaonesha kuwa wafungwa wa vifungo vidogo wanaoachiwa kwa *parole* ni wafungwa wanaorudiarudia makosa kulikoni wale ambao tayari wameshakaa magereza muda mrefu na hutamani uhuru kwa shauku kubwa. Endapo jambo hili litafanyika kila mara na kwa wakati litapunguza msongamano magerezani hasa kwa wale wenye vifungo virefu ambao kimsingi huwa tayari wamejifunza na kujirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa Bodi ya *Parole* ifikie mahali iwaachilie wafungwa wote waliofungwa wakati wa Nyerere, wakati wa Mwinyi, wakati wa Mkapa hata wakati wa Kikwete ambao wana zaidi ya miaka 10 mpaka 15 magerezani. Kwani ni imani ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa watu hawa wamejifunza vya kutosha. Mtu amekaa jela miaka 25, ana miaka zaidi ya miaka 65, akipata msamaha kisha akawa huru kweli mtu huyo anaweza kuwa mhalifu tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haki pia nyingine ya mahabusu ni pamoja na maisha yao ya ndani ya kila siku, ni maisha ya huzuni kwao pamoja na wafungwa. Chakula sio kizuri, malazi ni ya shida kubwa, selo yenye uwezo wa kuchukua watu 35 wanaweza kulala hata watu 80, mawasiliano ya ndugu zao ni tabu kwani hata leo Magereza Tanzania wanatumia kanuni zilizoachwa na Mkoloni kuendesha masuala ya Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna unyanyasanyaji wa aina mbalimbali ambao maneno hayawezi kutosha kueleza katika hotuba hii, unaotokana na tabia za Askari na mfumo mbovu wa Kanuni za Uendeshaji Magereza. Kwa mfano, wafungwa na mahabusu kuvuliwa nguo zote na kupanua makalio yao kwa ajili ya kupekuliwa mara watakapoingia

magerezani wakati hasa wanapokwenda Mahakamani na wakati wa kurudi ikiwa ni pamoja na kutoka kwenye shughuli nyingine mbalimbali mara zote wanakuwa chini ya ulinzi wa Askari. Vitendo vinavyofanywa na Jeshi la Magereza hapa nchini kuwavua nguo mahabusu na wafungwa si cha kibinadamu ni utekelezaji wa mikakati ya kishetani. Ni tendo la aibu sana kwa wazee na vijana wanapokusanyika kufanyiwa hivi hadharani hata Askari wanapofanya kazi hii nao wanatia huzuni bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Jeshi la Magereza kuacha mara moja udhalilishaji dhidi ya utu wa ubinadamu. Pia Serikali itenge fedha za vifaa vya kisasa kwa ajili ya upekuzi wa mahabusu na wafungwa katika Magereza yote nchini kwa kutumia mbinu za kisasa ambazo hazitwezi utu wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imetambua ugumu wa mawasiliano uliopo ndani ya mahabusu na magereza. Hivyo, tunaitaka Serikali kuweka simu maalum (*call box)* ili kurahisisha mawasiliano baina ya ndugu, Mawakili, mahabusu na wafungwa walioko magerezani. Mawasiliano jela kutoka kwa mahabusu au wafungwa kwenda kwa ndugu au jamaa ni magumu sana wakati wenzetu wa Kenya wamefikia mahali hata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, hiyo ni kengele ya pili malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Naam.

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi ya mwisho kengele ya pili imeshalia muda wako umekwisha.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mwenyekiti Mwenyekiti, sijakusikia.

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie sentensi yako ya mwisho muda wako umemalizika.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nakwenda kwenye hitimisho na mengine yote yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni siyo chuki dhidi ya Serikali iliyopo madarakani bali ni msaada wa fikra mbadala ambao Serikali inapaswa kuuzingatia kwa Taifa hili letu sote. Tunaweza tukataja mikakati mbalimbali ya kuelimisha umoja na mshikamano wa Taifa hili, lakini ukweli unabakia kwamba umoja na mshikamano hautajengwa na matangazo ya luninga wala machapisho ya magazetini, isipokuwa upendo ukishamiri miongoni mwetu haki, utu, usawa vitakuwa ni sehemu ya maisha yetu. Kwa hiyo, kama tunafikiria kwa dhati usalama wa nchi hii, ni lazima tukubali kwamba utu wetu ni bora kuliko rangi za vyama vyetu, utu wetu ni bora kuliko vyeo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ya hivi karibuni ya viongozi wakuu wa nchi kuanza kujenga utengano kati ya jamii ni jambo la hatari linalopaswa kupigwa vita na kila mtu mwenye akili timamu. Kauli za viongozi ni muhimu katika kujenga mshikamano wa Taifa kwani kama baba alivyo ndivyo watoto watakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeongelea masuala ya *DPP* na Ofisi ya *DCI* kwa kirefu. Ni muhimu tukatambua kwamba maana ya usalama wa Taifa hili utajengwa kwa uhuru kamili wa mahakama zetu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nilikuomba sentensi moja...

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, kwa sababu mfumo wa kikatiba na uteuzi wa watendaji wa mahakama zetu bado haupo huru kwa kiwango cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia moja ya sababu zinazopelekea mapinduzi yaliyosababisha machafuko Ufaransa ni wananchi kukosa imani na mahakama. Hivyo, kuwa na mhimili imara wa Mahakama...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema imetosha na imeeleweka na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda uliopo ni mdogo, naomba nisome maneno ya mwanaharakati aliyepinga utumwa Bw. Frederick Douglass aliyeishi kati ya mwaka 1818 hadi 1895 alipata kusema maneno haya, nitanukuu, namalizia Mwenyekiti. *(Makofi)*

*“Where justice is denied, where poverty is enforced...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema imetosha na unapigiwa makofi kwa wingi hapo, kwa hiyo naona imetosha.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upendo, haki na usawa ndio silaha ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema imetosha na unapigiwa makofi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI, MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha za wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nitumie fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa pole na salamu zetu za rambirambi kwa wazazi, familia na uongozi wa shule kwa wanafunzi 32, walimu na dereva wa Shule ya Lucky Vincent waliopoteza maisha mkoani Arusha mnamo tarehe 6 Mei, 2017 katika maeneo ya Rhotia Marera, wakiwa njiani kuelekea wilayani Karatu kwa ajili ya mitihani ya ujirani mwema kujipima uwezo na shule ya wenzao. Msiba huu ni mzito na janga kubwa kwa Taifa kupoteza hazina kubwa ya vijana waliokuwa na ndoto kubwa ya kulitumikia Taifa, ni msiba ambao na umegusa moyo wa kila Mtanzania na watu wote ulimwenguni na hivyo kutuunganisha pamoja kama Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, nikiwa mwakilishi halali wa wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini mahali ambapo msiba ule wa Kitaifa umetokea, nilinyimwa kwa makusudi nafasi ya kutoa salamu za rambirambi pale uwanja wa Sheikh Amri Abeid, kwa wafiwa, Watanzania wote na wapiga kura wangu kwani siasa za chuki dhidi yangu zilipewa uzito

mkubwa kuliko ubinadamu. Hii ni ishara mbaya kwa taifa na ni wazi kwamba tofauti zetu za kisiasa zinaweza kutufikisha pabaya kama taifa.

Hata hivyo nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Bunge zima kwa pamoja kwa kuguswa na msiba huu mzito na kuamua kutoa mchango mkubwa wa rambirambi kiasi cha shilingi milioni 100 kwa familia zote za wafiwa wote. Watu wa Arusha kwa pamoja wamenituma nikuletee salamu zao za shukrani na kwa Bunge lako tukufu. Aidha, namshukuru pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa salamu zake kwa wakazi wa Arusha zilizosilishwa na Makamu wetu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu.

**Mheshimiwa Spika,** Nilikamatwa mwezi wa Kumi mwaka 2016 nje ya Ukumbi wa Bunge Safari yangu ya kupelekwa magereza ilianza kwa matisho makubwa. Nilikamatwa na Askari Polisi wasiopungua watano. Tulianza safari kuelekea Arusha na kuwasili Kondoa majira ya saa 4 usiku ambapo niliwekwa rumande kituo cha Polisi Kondoa mpaka saa 8 usiku na kisha kuchukuliwa mpaka kufikishwa kituo kikuu cha Polisi jijini Arusha; ambapo safari yangu ya mateso na huzuni ilikamilika kwa mimi kukaa jela kwa zaidi ya miezi 4, kwa kosa tu la kuota ndoto na kuona maono niliyopewa na mwenyezi Mungu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati ya moyo wangu sifa na utukufu, heshima, nazirudisha kama shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na nchi kwa kunijalia afya njema.

**Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru wale wote walionijali wakati nilipokuwa magereza. Namshukuru Kipekee mke wangu Neema kwa maombi yake na ujasiri wake, watoto wangu Allbless, Brilliant, Terrence na Precious Mawazo. Precious Mawazo ambaye baba yake mzazi Alphonce Mawazo hayupo kwani aliuawa kikatili katika mazingira ya kisiasa kwa kosa la kuwa mfuasi wa siasa za upinzani.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru marafiki zangu wafungwa na mahabusu niliowaacha Gereza Kuu Arusha kwa upendo na uwenyeji wao wenye ukarimu katikati ya mateso mengi, ulionifundisha mengi na kumjua Mungu zaidi. Sijaacha kuwaombea hata siku moja tangu nimetoka gerezani.

**Mheshimiwa Spika,** pia nawashukuru viongozi wangu wa chama, Mwenyekiti wetu wa Taifa, Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe, viongozi wote wa UKAWA, na wengine wote waliokuja kunisalimu nilipokuwa magereza bila kusahau viongozi wa dini zote, na wanachama wote wa CHADEMA na wanachama na viongozi wa CCM ambao hawakujali kuitwa wasaliti kwa kujali utu, upendo kuliko chuki za kisiasa na utengano. Aidha, niwashukuru viongozi wa CCM waliothubutu kuwaza kuja kuniona lakini wakaogopa, ninaweza nikaelewa hofu yao na inatupa picha Taifa linakwenda wapi. Pia wao nawaombea.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa na changamoto nyingi sana, changamoto kubwa ya msingi ni hali ya usalama wa nchi ambayo ni muhimu ikiwezekana hekima zetu zikajikita kwenye mjadala wake na kutafuta ufumbuzi wa haraka.

## 2.0 HALI YA USALAMA WA NCHI

### 2.1 Maadili ya Familia na mapambano dhidi ya rushwa

**Mheshimiwa Spika**, Jambo hili linalohusu maadili nilianza kulisema katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2016/2017 kuwa ukitaka kuhakikisha hali ya usalama wa Taifa ni sharti jamii na serikali kwa ujumla iwekeze nguvu zake katika malezi yenye maadili bora yatakayojenga Familia zetu ili kuunda Taifa imara kabisa Afrika na duniani kote.

Nilisema hapa mwaka jana na nitanukuu kuwa;

*"Taifa lolote Duniani msingi wake ni familia , hivyo njia sahihi ya Taifa kuwa na usalama wa kweli katika Jamii ni muhimu Serikali ikajua kuwa Jamii ni Familia, kuongelea hali ya usalama na amani ya Nchi yetu bila kuongelea maadili ya familia zetu ni kupotosha fikra zetu."*

Na pia *"ukweli ni kwamba familia yenye maadili, wajibu na inayomcha Mungu ni jamii bora itakayozalisha Raia wema wenye wajibu na tija kwa Taifa, hatuwezi kuwa na Nchi yenye nidhamu na ustawi pasipo kuwa na familia zenye wajibu katika malezi."* Mwisho wa kunukuu.

***[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]***

### 2.2 Mifumo wa Kutoa Haki Nchini

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika ijapokuwa ukweli huo unapata vikwazo vingi kwamba haki huzaa amani. Kama Taifa ni muhimu tukajua kwamba wingi wa silaha, ukubwa wa majeshi hauwezi kuwa sababu ya kuwepo kwa amani katika Taifa. Katika Taifa lenye uonevu na ukimya ukatawala kwa sababu ya mabavu ya dola, Taifa hilo lipo kwenye hatari kubwa ya migogoro ya kijamii. Kwani njia pekee ya kutunza amani ni mifumo ya kutoa haki nchini ikajua kwamba haki huzaa amani.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Taifa hili haki ina mgogoro mkubwa katika maeneo mbalimbali ya utoaji haki nchini. Ni muhimu kwamba ukimya huu uliopo sasa ukatazamwa kama uvumilvu unaoweza kufikia ukomo na kukata tamaa. Ukienda Sehemu mbalimbali zinazotoa haki kuanzia Serikalini, Mahakamani, Polisi na sehemu nyingine ambazo kwa asili hutakiwa kutoa haki, utakuta kuna uonevu, unyanyasaji na ukazamizaji wa hali ya juu ambao unakusanya hasira za watu ndani ya mioyo yao.

**Mheshimiwa Spika**, ni rahisi kuendelea kupuuza maneno kama haya kwa sababu yanatolewa na upande wa pili wa waleta maoni. Lakini ipo siku tutakumbukwa kwa ukweli huu tunaosema ndani ya Bunge hili. Uonevu na

ukandamizaji katika Taifa hili imekuwa ni sehemu ya maisha ya kila siku ya Watanzania. Mimi ni Mfano hai wa uonevu huo, Mhe. Lijualikali ni mfano wa uonevu huo, Mhe. Lissu ni mfano wa uonevu huo, familia ya Marehemu Alphonce Mawazo ni mfano wa uonevu huo. Familia ya Ben Saanane ni mfano wa uonevu huo. Msafiri Mbwambo aliyeuawa kwa kuchinjwa shingo maeneo ya USA River na waliomuua kutoroka wakiwa wamefungwa pingu mbele ya Polisi wanne wenye SMG.

**Mheshimiwa Spika**, hawa ni wale ambao nimewakumbuka kuwataja lakini ukienda Magerezani, Ukienda Mahabusu, Ukienda Mahakamani, Mahospitalini na makaburini na kila mahali panapotolewa huduma za umma zinazowahusu Watanzania utakutana na vilio na mateso kutoka kwa watu wengi sana wanaodhulumiwa haki zao. Angalau kila familia katika Taifa ukiachilia watawala wa Serikali hii ya CCM hili inaweza ikasimulia huzuni na mateso wanayokutana nayo kila siku katika mifumo ya utoaaji haki.

**Mheshimiwa Spika**, mateso na huzuni zao haziwafundishi watu hawa kuwa waoga, japokuwa wanaonekana ni waoga, kama hatua za haraka zisipochukuliwa na Serikali kwa kuganga mioyo yao kwa kutenda haki ipo siku Taifa letu litakuwa na historia mbaya kwa kuwa watu hawa wanaandamana ndani ya mioyo yao wakati miguu yao imezuiwa kuandamana kudai haki kutokana na vitisho vya zana za kivita. Ni ajabu mtu anapoandamana kudai maji ya kunywa anakabiliwa na mtutu wa bunduki. Ni jambo la kushangazwa chama cha siasa kinapotaka kudai haki yao ya msingi ya kutaka kuandamana na kufanya mikutano ambayo ni haki yao kikatiba na kisheria wanakamatwa na kufunguliwa kesi zilizobatizwa jina la “Uchochezi”.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaamini mambo haya ni kwa muda tu, haki haijawahi kushindwa na kila mpigania haki ni mpenzi wa Mungu. Ni hakika yetu kuwa kila mtu atavuna anachopanda. Ni maombi yetu kwa nia njema kabisa kwamba Serikali hii ijitahidi kutenda wema ili watoto wenu

na wajukuu wenu wakute Taifa lenye misingi ya kuheshimu haki na utu. Kwani huo ndio urithi mnaopaswa kuacha kwa watoto wenu na sio nyumba na magari.

**Mheshimiwa Spika**, Nilishawahi kusema huko nyuma kwenye moja ya mchango wangu kuwa CCM ikitawala muda wote lakini ikatawala kwa haki, heri na baraka utawala wao unapaswa kuheshimiwa. Lengo Letu kama Wapinzani si tu kuindoa CCM madarakani bali ni kuhakikisha kuwa CCM inatawala kwa haki na heri kwa nyie ndio watawala kwa sasa. Mnapokosea ninyi sio CCM inayopata hasara bali ni taifa ndio linalopata hasara, na sisi na ninyi ni miongoni mwa wananchi wa Taifa hili. Haki Huinua Taifa.

### 2.3 Ongezeko la Uhalifu unaotakana na uchumi duni

**Mheshimiwa Spika**, amani ya Taifa hili itategemea pia hali ya uchumi wa Taifa. Kwa hali ilivyo hivi sasa katika mzunguko wa fedha nchini ni ishara kwamba jitihada za ziada zinapaswa kufanyika juu ya uchumi na biashara ili kuongeza tija na maisha bora miongoni mwa Watanzania na kupunguza uhalifu unaosababishwa na njaa na ukosefu wa Kipato halali.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo kubwa la mzunguko hafifu wa fedha linatokana na kauli za viongozi mbalimbali wa Serikali ambazo zimesababisha mashaka makubwa katika uwekezaji wa biashara maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ni busara kubana matumizi lakini ni muhimu zaidi ikajulikana kwamba, matumizi ya kila siku ya Serikali na jamii ndio chanzo cha mzunguko wa fedha katika jamii. Hivyo sera za Serikali katika uchumi wa nchi sharti zizingatie hali ya usalama wa maisha ya wananachi wake kwa kuruhusu mzunguko halali wa fedha katika maeneo mbalimbali ya kibiashara, ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya wazabuni mbalimbali wanaoidai Serikali kwa muda sasa.

**2.4 Tishio la Ongezeko la Uhalifu unaotokana na Njaa na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi.**

**Mheshimiwa spika,** Ni muhimu Taifa kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ikajenga uwezo wake wa kuona picha kubwa katika Taifa ya kuangalia visababishi vinavyotishia hali ya usalama wa ndani ya nchi, ikiwemo na suala la tishio la mabadiliko ya Tabia ya Nchi. Hivyo kazi muhimu sana ya wizara ya mambo ya ndani ni kuzuia kuporomoka kwa amani sasa na katika siku za baadae. Kambi Rasmi ya upinzani bungeni inaona kuwa hali ya mabadiliko ya hali ya nchi duniani na Tanzania kwa ujumla ni moja ya sababu zinazoweza kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani katika siku za usoni kwa kuwa tabia ya nchi imebadilika sana hivyo kupelekea ongezeko la njaa kutokana na uzalishaji duni wa chakula cha kutosha kupitia kilimo kinachosuasua.

**Mheshimiwa Spika,** Ni kweli kabisa wote tunakubaliana kuwa mtu mwenye njaa ni mtu mwenye hasira, hivyo ili kukabiliana na uhalifu unaosababishwa na njaa na tafrani nyingine za kimazingira, ni muhimu sasa Serikali ikaweka malengo muhimu katika utunzaji wa misitu na upandaji miti ili kukabiliana na changamoto hizi kwa siku za usoni , na vile vile serikali ni muhimu sana ikaongeza bajeti katika wizara inayoshugulikia mazingira nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliangalia suala la Usalama wa Chakula na Mabadiliko ya tabia ya nchi kama suala la usalama wa raia na mali zao, hivyo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliingize katika Sera na mipango yake kama suala mtambuka la kiusalama. Mathalani jeshi la Magereza kupitia mashamba yake yatumiwe kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na kuhakikisha usalama wa chakula unakuwepo muda wote.

***[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]***

**2.6 Njia bora za kupambana na ugaidi na ujambazi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli usiopingika kuwa kumekuwa na viashiria vya wazi kabisa vya matendo ya kigaidi katika Nchi nyetu. Hata hivyo ni uhalifu ambao unahitaji utaalamu wa hali ya juu na hekima katika kukabiliana nao , ni rai yetu kuwa suala la Ugaidi halihitaji tu operation maalumu na muhimu katika kuwasaka magaidi mahali popote walipo lakini pia ni muhimu zaidi ikafamika kwanini sasa sura ya hali hii ya matukio ya kigaidi yanaanza kujitokeza Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia jeshi la Polisi likikabiliana na matukio mbalimbali ya kiuhalifu, mengine yenye sura za ujambazi, na mengine yenye sura za kigaidi. Ni muhimu sasa jeshi la Polisi likajua changamoto wanazopitia za kiusalama ndani ya nchi yetu, haziwezi kutatuliwa kwa wingi wa askari waliopo na wingi wa silaha zilizopo, **bali wanahitaji kujenga mahusiano mazuri baina ya Jeshi hilo na raia wote kwa ujumla.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuonesha kuwa tunajali mahusiano mema baina ya jeshi la Polisi na raia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na raia wote wa Tanzania kulaani vikali matukio ya mauaji ya Askari Polisi wetu ambayo miaka ya hivi karibuni yamekuwa yakijirudiarudia na Serikali bado haijatoa taarifa za kina juu ya kujirudia kwa mauaji hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa mnamo tarehe 13 Julai, 2015 Kituo cha Polisi cha Sitakishari kilichopo Ukonga jijini Dar es Salaam kilivamiwa na watu ambao walidhaniwa kuwa ni majambazi, wakafanya mauaji ya Polisi na raia wetu na kupora silaha na kutokomea kusikojulikana.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 13 Aprili, 2017 Askari Polisi 8 waliuawa kikatili na **'watu wasiojulikana'** katika eneo la Jaribu Mpakani, Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani huku wauaji

hao wakipora silaha tisa kati ya hizo SMG sita zikiwa na risasi 30 kila moja na long range tatu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwezi Februari, 2017 Afisa wa Upelelezi wa Wilaya (OC CID) wa Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani, Mrakibu wa Polisi, Peter Kubezya, Afisa wa Misitu ambaye alikuwa Mkaguzi wa Kituo cha Ukusanyaji mapato ya ushuru katika Kijiji cha Jaribu, Peter Kitundu na Rashid Mgamba ambaye ni Mlinzi/Mgambo wakiuawa kwa kupigwa risasi kichwani na begani na walikufa papo hapo eneo la tukio.

**Mheshimiwa Spika,** Gazeti la Mtanzania la tarehe 15 Aprili, 2017 liliripoti kuwa mwezi Mei, 2016 Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyambunda, Said Mbwana, aliuawa kwa risasi. Oktoba, 2016, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho hicho cha Nyambunda Ally Milandu, aliuawa kwa kupigwa risasi na watu wanne. Novemba, 2016 wenyeviti wawili wa Vitongoji wa Kijiji hicho hicho, waliuawa kwa kupigwa risasi. Mwezi Januari, 2017 watu ambao Jeshi la Polisi hadi sasa halijawafahamu waliomuua mfanyabiashara, Oswald Mrope kwa kumpiga risasi mbele ya familia yake. Februari 3, 2017 watu wasiojulikana walivamia nyumba ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Jaribu, Bakari Msanga na kuichoma moto huku yeye mwenyewe akifanikiwa kuwatoroka.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa wauaji wa Askari Polisi hulenga kupora Silaha na kutokomea nazo kusikojulikana na haijafahamika kwa nini viongozi wa Serikali za Mitaa wengi wameuawa katika maeneo hayo ya ukanda wa kuanzia mkoa wa Pwani mpaka Lindi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua mchango wa Jeshi la Polisi katika kustawisha amani katika maeneo ya ukanda huo na nchi nzima kwa ujumla isipokuwa Jeshi linapokosa zana za kisasa na rasilimali za kutosha kuendesha operesheni za kutokomeza kabisa mauaji hayo ya askari na viongozi wa Serikali za Mitaa basi linashindwa kabisa kumaliza tatizo hilo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi kuwa inapokuja kwenye masuala ya kuzuia vyama vya upinzani visifanye mikusanyiko ya kikatiba, maandamano na mikutano ya hadhara, kwa nyakati mbalimbali Jeshi limekuwa jepesi kutumika kisiasa kuzuia mikusanyiko hiyo kwa kisingizio cha 'taarifa za kiintelijensia' kuwa kungeweza kutokea vurugu. Lakini inapokuja katika suala la kuzuia mauaji ya askari hao hao basi uwezo wao wa kunusa taarifa na kuzuia mauaji yasitokee unakuwa duni. Huu ni ushahidi tosha kuwa 'intelijensia ya jeshi letu la Polisi' ni dhaifu kwa sababu za kujiingiza katika siasa badala ya kuangalia maslahi mapana ya kitaifa na kuzingatia weledi wa kazi yao.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzuia matukio hayo yasitokee na kutokomeza kabisa vikundi hatarishi vya usalama wa nchi, huu ndio wakati ambao Idara ya Usalama wa Taifa pamoja na intelijensia ya Jeshi letu la Polisi ingetumika ipasavyo kubaini matukio hayo na kuyazuia kabla hayajatokea, lakini hali imekuwa tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mara moja kuitumia Idara ya usalama wa Taifa na Jeshi la Polisi kwa maslahi ya kisiasa na ijielekeze katika matumuzi ya vyombo hivyo kuzuia matukio ya mauaji ya askari na viongozi wa Serikali za Mitaa kama ilivyojitokeza katika Wilaya ya Kibiti.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulipatia Jeshi la Polisi zana za kisasa za kupambana na makundi ya kigaidi, kijambazi na makundi yote ya kihalifu yenye mrengo wa uporaji wa silaha na mauaji ya askari wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi kitengo cha Upelelezi takribani miaka 20 iliyopita, hakujawahi kufanyika mafunzo maalumu ya Upelelezi (CID Course). Hivyo Basi ndio sababu katika matukio yanayohitaji uweledi wa Intelijensia Jeshi la Polisi limekuwa likijitokeza kama Kikundi cha Mapambano (Operation Force).

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Jeshi la Polisi badala ya kutengewa bajeti ya kununua magari ya washawasha na kuwamwagia maji hayo raia wasiokuwa na silaha, basi ilipatie Jeshi hilo fedha za kutosha kununua zana za kisasa za Kiuchunguzi, na Kutenga fedha maalumu kwenye Mfuko wa fedha za Upelelezi ambao uko kishera (Criminal Investigation Fund) ili kutoa nguvu na uwezo wa upelelezi kufanyika kwa kina hasa kipindi hiki ambapo ulimwengu unakabiliwa na uhalifu wa aina mbalimbali unaozidi zana na ujuzi uliopo. Ni aibu kwa Taifa kwamba Serikali imekuwa haitoi fedha hizo ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na hivyo kufanya shughuli za upelelezi kuwa ngumu sana.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu upelelezi wa washitakiwa wa makosa haya ukaendeshwa kwa haraka iwezekanavyo ili kuepuka kukaa na mahabusu wengi magerezani wenye hatia za makosa ya mbali mbali na kumbe hawakufanya makosa wanayotuhumiwa nayo; kwani unapochanganya watu wema na wabaya ni rahisi watu wema wakawa wabaya. Kwa hiyo namna pekee ya kuwatenganisha ni upelelezi kukamilika haraka na haki kutolewa mapema iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Magereza yote Nchini watuhumiwa wengi wa Ugaidi ni pamoja na viongozi wa dini, unaposhindwa kukamilisha upelelezi haraka wa kesi hizi, unaweza ukaleta mgogoro mkubwa ma kimatabaka ya dini kwa wasio na hatia kuona kwamba kuna mkakati wa dhati wakuoneana na kudhalilishana na maneno haya yanasemwa na ili yasisemwe ni bora mmakamilisha upelelezi haraka ili kila mtu avune alichopanda kwa haki na sio hila na ulaghai.

**Mheshimiwa Spika,** katika magereza mbalimbali nchini kuna watuhumiwa wa kesi za ugaidi walioshikiliwa kwa muda sasa. Katika Gereza kuu la Arusha Mahabusu wa Kesi za Ugaidi wanaanza kuhesabu mwaka wa nne wakiwa mahabusu bila upelelezi wa kesi zao kukamilika. Wakati wa kukamatwa kwao, wengine waliuwawa na wengine wameachwa na vilema vya kudumu (kukatwa miguu).

**Mheshimiwa Spika,** swali la kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inalouliza ni je kwanini upelelezi wa mashauri yao mpaka leo unachukua muda mrefu? kwa matendo yote yale ya kuwakata miguu, kuwatesa na kuua baadhi ilikuwa ni wazi kuwa Polisi angalau wanaushaidi asilimia tisini (90) lakini mpaka leo kesi zao bado zinatajwa tu , ni tafsiri mbaya katika haki, haki inapochelewa kuamuliwa ni wazi kuwa visasi na chuki inaweza kujengwa kwa ufasaha zaidi. Ni muhimu sasa upelelezi wa makosa haya na mengine mengi ukakamilika mapema ili haki ionekane imetendeka , lakini kuwaweka watu rumande wasio na hatia na wenye hatia kwa muda mrefu ni ugaidi dhidi ya haki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ikamilishe upelelezi haraka iwezekanavyo ili anayestahili adhabu apate adhabu na asiyestahili aachiliwe akaungane na familia yake.

### 2.7 Haki za Wafungwa, Mahabusu na Watuhumiwa wa Makosa Mbalimbali nchini

**Mheshimiwa spika,** Kama ambavyo jamii iliyoko uraiani ina haki zake ndivyo ilivyo kwa mahabusu na wafungwa. Sio lugha rahisi sana kueleweka kwa watu ambao hawajawahi kuwa magereza na ndio sababu nilipotoka magereza nilimuomba Mungu angalau kila Mbunge apite jela kwa miezi isiyopungua miwili na bado ni maombi yangu tena yenye msisitizo kwa Mungu.

**Mheshimiwa Spika,** kukosa uhuru ni adhabu kubwa sana Duniani na aneyeijua ni yule anayekuwa hana uhuru, moja ya huzuni kubwa waliyo nayo watuhumiwa katika Taifa hili ni ucheleweshwaji wa kesi , ni kawaida sana mtuhumiwa kujikuta yuko magereza kwa muda mrefu wakati mwingine zaidi hata ya miaka 6 akisuburi kesi au upelelezi kukamilika , haya ni mateso makubwa sana.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu sasa Bunge lako tukufu likatunga sheria ya kuwepo na kikomo cha upelelezi katika makosa yote ya jinai tofauti na sasa ambapo baadhi ya makosa mengi ya jinai hayana kikomo cha upelelezi na hivyo kuwafanya watuhumiwa kukaa ndani muda mrefu bila

mashauri yao kusikilizwa na kuongeza taabu na huzuni katika maisha yao na msongamano wa mahabusu magerezani unaolipelekea pia Taifa kupata hasara kubwa ya kuwatunza.

**Mheshimiwa Spika,** nimekutana na vijana wengi nilipokuwa mahabusu, nilitumia muda mwingi kuongea nao na hivi ndivyo walivyosema *"Mhe. Mbunge ili kuzuia rushwa na uonevu unafanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na ofisi ya DPP ni muhimu Wabunge wakaondoa vikwazo vya dhamana kwenye makosa yote ya jinai kama ilivyo Kenya na Uganda, kwani ubambikiwaji wa kesi unafanywa kwenye makosa yasiokuwa na dhamana ili watuhumiwa waweze kufikiria kutoa rushwa kubwa "*

**Mheshimiwa Spika,** nakubaliana nao kwa asilimia zote , Kenya makosa yote yana dhamana isipokuwa uhaini , Uganda makosa yote yana dhamana ikiwemo uhaini , Tanzania orodha ya makosa yasiokuwa na dhamana ni mengi , lakini hata yenye dhamana siku hizi pia yanaweza kuzuiliwa dhamama kwa kitu kinachoitwa " HATI YA MWENDESHA MASHITAKA" **(Certificate of DDP)**. Japokuwa kuna hukumu ya hivi karibuni ya mahakama kuu iliyoitangaza hati ya DPP kuwa ipo kinyume cha Katiba kwa kuzuia dhamana kwa watuhumiwa, lakini ofisi ya DPP imeendelea kuidharau hukumu hiyo ya Mahakama na endapo DPP akijisikia kukuwekea hati hiyo maana yake ujue kwamba unaanza kesi ya kupigania dhamana yako kwenye mashitaka hata yenye nafasi ya dhamana kisheria, jambo limesababisha mateso mengi na kuongeza msongamano wa watuhumiwa magerezani.

**Mheshimiwa Spika**, Wakili Median Mwale anaanza mwaka wa saba magereza bila shauri lake kukamilika, bado ni mahabusu na aliniambia maneno haya "Mheshimiwa Mbunge nimekaa sana magereza, nimechoka sana mwili wangu na roho yangu, nimezuiwa hata kuzaa, na sijui kesi yangu itaisha lini, ningetamani shauri hili liishe, kwani hata kama ningekutwa na hatia katika shauri hili ningekuwa nimeshafungwa na kumaliza kifungo changu, nashukuru umekuja magereza na pengine Christmas utaweza kuwa

nasi na ukitoka nenda ukawatetee Mahubusu , wafungwa na Askari jela"

**Mheshimiwa Spika,** Wakili Mwale, aliendelea kuniambia kuwa;

*"Bunge linapotunga sheria linapaswa kuwa makini, kwa mfano; kesi inayonikabili mimi ya Money Laundery inamkabili pia kijana mmoja anaitwa Masawe yupo humu ndani, anakabiliwa na shitaka la Money Laundery la dola 1,900 lakini amekaa jela zaidi ya miezi 15 kwa sababu shitaka hili halina dhamana na adhabu yake ukikutwa na hatia ni kati ya miaka 4 na 7, wakati huo huo mtu anayetuhumiwa kunajisi au kubaka kosa ambalo adhabu yake ni miaka 30 jela au kifungo cha maisha, anapewa dhamana akisubiri shauri lake kukamilika, wabunge mnapoletewe miswada ya sheria na Serikali, mnapimaje haya mambo? Sheria za nchi zinahitaji rehema ili kujenga dhana ya urekebishaji na sio mateso yasiyolenga dhana ya urekebishaji"*

**Mheshimiwa Spika,**inaweza kuoneka jambo rahisi mtu kukaa jela miaka saba bila kesi yake na upelelezi kukamilika, waheshimiwa Wabunge nawaomba tena niko chini ya miguu yenu vaeni utu na viatu vya hawa watu na familia zao , ni mateso na huzuni sana , Mimi najua , kila siku ninawaombea kwa Mungu. Hivyo chanzo muhimu kinachosababisha msongamano na mateso magerezani ni ofisi ya DPP, Sheria mbovu zisizozingatia utu, na ucheleweshwaji wa upelelezi kutoka Jeshi la Polisi.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma (DPP) tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali zenye nia ovu ya kuitumia mahakama ndivyo sivyo ***[DPP abuse of Courts]*** kupindisha haki kwa makusudi katika kesi mbalimbali, hususani **kuzuia haki ya dhamana** kwa watuhumiwa ambao hawajatiwa hatiani na mahakama; DPP akiiwakilisha Serikali hudiriki kufanya hivyo hata katika makosa ambayo kisheria watuhumiwa wana haki ya kupata dhamana..

**Mheshimiwa Spika**, akisoma hukumu kukemea ***tabia ya Serikali kupitia DPP kuitumia mahakama kupindisha haki***, hukumu ambayo nimeambatanisha katika hii hotuba, katika ukurasa wake wa tisa (9), Mhe. Jaji S.M Maghimbi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, katika iliyokuwa Kesi ya Rufani ya Jinai Na. 135 ya mwaka 2016 tarehe 3 Machi, 2017 alisema na nitanukuu;

*"It is after the bail conditions have been set that in the eyes of the laws, we can lawful conclude that the respondent was actually granted bail and should have only been detained thereafter he failed to fulfill the bail conditions so set. The right of appeal of the aggrieved party would have hence accrued AFTER the bail conditions were set and NOT before that has argued by the appealant"*

Jaji Maghimbi aliendelea kusema kuwa;

*"The records are that after the objection to bail was overruled, instead of proceeding to set the bail conditions as required by the law,* ***the trial magistrate erroneously the appealant herein to enterfere with the court process by prematurely lodging the purpoted notice to appeal"***

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia DPP walikuwa wanaufahamu ukweli uliotolewa na hukumu ya Mhe. Jaji Maghimbi, lakini waliamua kwa makusudi kuipigisha Mahakama Sarakasi haramu ambazo hazipo kisheria ili kuendelea kumweka Mtuhumiwa mahabusu kwa muda wa miezi minne.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mara moja kuitumia ofisi ya DPP kuingilia utaratibu wa kimahakama kutoa dhamana kwa watuhumiwa mbalimbali. Aidha, kwa sababu Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma ni mtumishi wa umma na analipwa msharaha na Watanzania ambao yeye anaitumia ofisi yake kupindisha haki za wananchi, basi achukuliwe hatua kali za kinidhamu ikiwemo kufutwa kazi, na kufunguliwa mashitaka mahakamani kwa kosa la kuidhalilisha Serikali yetu katika

kesi hii ambayo dhamana ilikuwa wazi kama alivyohukumu Jaji Maghimbi katika hitimisho lake akisema, nitanukuu;

***"Given the leghth of time that the respondent was so detained in remand custody, I further find it just that I step in the shoes of the trial court and proceed to finalize the grant of bail to the respondent by setting the conditions hereinunder"*** mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika**, nayasema haya kwa sababu mara kadhaa ofisi hii imekuwa ikiarifu Mahakama kuwa hawana nia ya kuendelea na shauri la jinai ambalo lipo Mahakamani, lakini mara ya mtuhumiwa kuachiwa huru na Mahakama Jeshi la Polisi limekuwa likiwakamata tena watuhumiwa na kuwaweka kizuini na baadae kurudia makosa yaleyale ambayo upande wa Jamhuri umeiarifu Mahakama kuwa hawana nia ya kuendelea na shauri lililpo Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, hata pale shauri linapofutwa au Jamhuri kueleza kuwa hawana nia ya kuendelea na shauri husika bado wanawakamata watuhumiwa kwa makosa yaleyale. Ni kweli kuwa kifungu cha 225 (5) cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai (CPA) kinaeleza kuwa kuachiwa na Mahakama haitawazuia Jamhuri kumkamata mtuhumiwa, lakini mamlaka haya yametumika vibaya kama kigezo cha kuwakomoa wananchi waliowengi ambao wanaachiwa na Mahakama.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuleta Bungeni haraka iwezekanavyo marekebisho ya Sheria Mbalimbali kandamizi kuhusu mienendo ya makosa ya jinai ili sheria zote katika mwenendo wa makosa ya jinai iakisi utu na urekebishaji ili kupunguza mateso kwa binadamu. Aidha, tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa kitengo cha Upelelezi cha Jeshi la Polisi, na Bajeti ya Mahakama ya Tanzania inakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi, wepesi, uharaka, weledi wa hali ya juu, uzingatiaji wa maadili, haki na utu wa binadamu bila kuwa na njaa na tamaa ya rushwa

na ucheleweshaji wa mashauri mahakamani unaotokana na ufinyu wa bajeti kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa maslahi ya Waendesha Mashitaka ya Serikali, Watumishi wote wa Mahakama na Askari Polisi wote yanazingatiwa vizuri ili kuwapa utulivu katika kazi ya kutenda haki na sio vinginevyo.

## 3.0 UHARAMIA DHIDI YA SIASA NA DEMOKRASIA NCHINI

### 3.1 Siasa safi na Demokrasia ya kukuza amani nchini

**Mheshimiwa Spika,** Msingi ya amani katika Taifa inategemea siasa safi na **demokrasia huru**. Ushindani wetu wa kisiasa unapokosa siasa safi na demokrasia huru ni dhahiri kwamba Taifa halitaweza kuepuka uvunjifu wa amani unaopunguza kasi ya Maendeleo na mshikamano katika Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katazo la mikutano ya hadhara na kazi za siasa katika nchi sio tu ni hatari kwa vyama vya siasa vinavyozuiwa kufanya kazi zake za siasa na chama dola bali ni hatari kwa demokrasia ya chama dola hicho pia kinachozuia kazi za siasa kwa vyama vingine.

**Mheshimiwa Spika,** uwepo wa vyama vya siasa vinavyowakilisha maoni ya aina mbalimbali ni nguzo muhimu ya usalama wa Taifa hili. Kitendo cha Serikali ya CCM kupuuza nguzo hiyo ni kuamua kwa makusudi kuliingiza Taifa katika majanga ya chuki yanayoweza kuliingiza Taifa katika migogoro isiyoisha. Ni wajibu wa chama kilichopo madarakani kuhakikisha ukuaji wa demokrasia kuwa ni silaha muhimu ya amani katika nchi na sio kupuuza demokrasia, kudhalilisha vyama vingine visiyokuwa na dola kama CCM inavyofurahia kufanya sasa kule visiwani Zanzibar na hapa Tanzania bara.

**Mheshimiwa Spika,** wingi wa CCM ndani ya Bunge, unaweza kutumika kupuuza hata maoni haya muhimu, Mwandishi Voltaire aliyeishi kati ya mwaka 1694 na 1778 katika moja ya maandiko yake aliwahi kusema kuwa "**It is dangerous to be right when the government is wrong"** akimaanisha kuwa **"ni hatari kuwa sahihi wakati Serikali haipo sahihi"** Hiki ndicho kinachowakuta raia wote wa Tanzania leo hii. Katika Serikali ya awamu hii ya tano tumeona na kuthibitisha namna ambavyo demokrasia na wanademokrasia wanavyopita katika wakati mgumu katika maisha yao ya siasa ya kila siku. Dhambi ya kuua demokrasia hapa nchini msidhani kuwa itaishia kuangamiza upinzani, bali italitafuna Taifa, na itaingia hadi ndani ya chama chenu CCM na wakati huo ukiwadia hakuna kati yenu au watoto wenu atakayesalimika. Only Time will Tell.

**Mheshimiwa Spika,** ni hatari leo hii kwa Mtanzania kuthubutu kuwa na maoni tofauti na yale ya Serikali. Kusikiliza mawazo yasiyofanana na mtazamo wako na usiyoyapenda ni busara na pia ni dhahabu.

**Mheshimiwa Spika,** wote ni mashahidi dhidi ya mateso wanayopitia viongozi mbalimbali wa kisiasa katika Taifa hili kwa kuwa na mitizamo tofauti na ya wale waliokalia viti vya utawala kwa wakati huu.

***[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]***

## 5.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 5.1 Njia bora za kuzuia Ukatili wa Vyombo vya Dola nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Ripoti ya mwaka 2016 ya '*Mtazamo wa hali ya haki za kiraia na kisiasa Tanzania*

*2016'* iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, asilimia 81 ya Mikoa yote nchini imepata alama mbaya kabisa za ukiukwaji wa haki ya kuishi. Ripoti hiyo inasema kuwa, ninanukuu; *"..Alama hizi za chini zimesababishwa na mambo muhimu kadhaa, kama vile matukio ya polisi kufanya ukatili na kutumia nguvu kupita kiasi wakati wa kukamata watu wanaohisiwa kufanya uhalifu, muda mwingine kusababisha kifo,….haki ya kuishi inaonekana kuhatarishwa na mauaji na ukatili mikononi mwa vyombo vya dola…."*

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Jeshi la Polisi likituhumiwa kufanya mauaji haliwezi kujichunguza lenyewe na kutoa maamuzi lenyewe; basi sharti kuwe na chombo huru kitakacholisimamia Jeshi la Polisi. Kwa muktadha huo wa kulifanya Jeshi letu la Polisi kuzingatia sheria ya Jeshi hilo, Sheria nyingine na Katiba ya nchi yetu na kuachana kabisa na kujirudia kwa makosa ya uadilifu wa Jeshi la Polisi katika kusababisha mauaji na ukatili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuzingatia ushauri uliotolewa na wadau wa Haki za Binadamu kwa kuleta muswada wa Sheria katika Bunge lako tuko utakaounda chombo maalumu cha kuangalia utendaji kazi wa haki ndani ya Jeshi la Polisi, chombo ambacho kitafanya uchunguzi na kuwawajibisha maafisa wa polisi ambao wamejihusisha na mauaji, utesaji au ukatili.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea ushauri ambao tumekuwa tukiutoa mara kwa mara kwa Serikali ambao haujawahi kufanyiwa kazi juu ya kuundwa kwa Mahakama ya Korona (Corners Court) kwa mujibu wa Sheria inayotoa mamlaka ya kuchunguza vifo vyenye utata (Inquest Act) kuchunguza vifo vyenye utata kama kile cha Marehemu Alphonce Mawazo, ambapo mpaka sasa hakuna taarifa mahususi juu ya kifo hicho ambazo zimetolewa na mamlaka za serikali huku ikijulikana wazi kuwa Mawazo aliuwawa mchana kweupe huko Busanda Mkoani Geita.

### 5.2 Jinsi za Kuzuia Uhalifu nchini kwa Njia ya Bajeti ya Jeshi La Polisi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi 5,370,041,105 kama Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Kwa mujibu wa randama ya Wizara, Fungu 28 Jeshi la Polisi, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Serikali ilikuwa ni jumla ya Shilingi milioni 40 sawa na asilimia 1 tu ya bajeti yote ya maendeleo iliyotengwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa nyakati tofauti Askari Polisi wanapotekeleza wajibu wao hupiga, hutesa na hata kuteka nyara wananchi na wakati mwingine kusababisha ulemavu hata kifo kutokana na kukosa mafunzo ya kushughulika na ulinzi wa raia na mali zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachelea kusema kuwa hali hii inaweza kutokana na bajeti finyu ya maendeleo ambayo ingetumika kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Askari hao. Kitendo cha Serikali kutopeleka fedha za maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Polisi kinapunguza weledi wa jeshi hilo kutokana na kukosa mafunzo muhimu ya kuendesha kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu sababu za kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kwa Jeshi hili ili kuendelea na majukumu yake mahususi ya ulinzi wa raia na mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kitendo cha kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kinalifanya Jeshi Polisi kushindwa kuwekeza kwenye intelgenisia pamoja na mafunzo ya kuimarisha weledi na hivyo kuzuia matukiko kama yale ya kuuawa kwa Askari wa Jeshi hilo Wilayani Kibiti.

### 5.3 Kuimarisha usalama wa Barabarani

**Mheshimiwa Spika,** Wakati Wizara ya Mambo ya Ndani inawasilisha makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Taifa limepatwa na Mshituko mkubwa sana juu ya Ajali mbaya sana iliyotokea huko Karatu Mkoani Arusha na kusababisha vifo vya watoto wa shule ya Msingi Lucky Vicent ya jijini Arusha ambapo walimu wawili na dereva wagari na wanafunzi 32 wote walipoteza maisha papo hapo.

**Mheshimiwa Spika,** sio muhimu tena kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kuja na takwimu za idadi ya vifo na ulemavu unaotokana na ajali za barabarani. Takwimu ziko wazi kwamba watu wanapoteza maisha kila uchwao. Pamoja na Sheria kali za usalama wa Barabarani kutungwa, ni muhimu sasa masuala yanayohusu usalama barabarani yakaanza kufundishwa kuanzia shule za msingi mpaka katika vyuo vya elimu ya juu. Kwani usalama wa barabarani hauhusu gari peke yake bali inahusu pia namna sahihi ya matumizi ya barabara kwa kila mmoja wetu na watoto wetu.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayo taarifa kwamba, fedha na mafunzo ya Askari wa Usalama barabarani (Traffic) hayajafanyika kwa muda mrefu na hivyo Askari wengi wa barabarani wanafanya kazi kwa mazoea badala ya utaalamu. Hii ndio sababu kazi yao imekuwa ni ya kuvizia hadi kufikia kupanda juu ya miti na kamera za tochi huku wakiamini kuwa kosa la barabarani ni mwendo kasi peke yake. Hawana uwezo wa kufanya uchambuzi wa kina hata juu ya matatizo ya mifumo ya magari kwa undani.

**Mheshimiwa Spika,** Leo hii kitengo hicho cha traffic kinatumika kukusanya mapato kazi ya TRA badala ya kutumika kuelimisha jamii juu ya usalama barabarani jambo ambalo ndio dhima ya uanzishwaji wa kitengo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inayojivunia mapato yatokanayo na makosa ya barabarani, inakosa uhalali wa

kutuma salamu za rambirambi pindi ajali na vifo vinapotokea, kwa kuwa haitumii fedha hizo kupunguza ajali za barabrani. Imekuwa ni jambo la kawaida badala ya kutoa taarifa za kupungua kwa matukio ya ajali za barabrani, Jeshi la Polisi kanda maalumu ya Dar es Salaam, linajigamba kukusanya mapato ya makosa ya barabarani jambo ambalo linawavutia askari wa kikosi hicho kusahau kuwa wajibu wao sio kukusanya fedha bali wajibu wao ni kuhakisha usalama barabarani na kuzuia matukio ya ajali yasiongezeke.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaasa wananchi wawe makini katika chaguzi zinazokuja, kwani vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani ni sehemu ya majanga mengi yanayotokana na Serikali hii ya awamu ya tano kushindwa kusimamia ustawi wa Taifa.

### 5.4 Masilahi duni ya askari Polisi na Magereza

**Mheshimiwa Spika,** askari wetu wanahitaji mazingira bora na masilahi bora wawapo kazini. Nguzo ya kwanza ya ulinzi kwa askari ni yeye kuwa na amani, askari wasiokuwa na maslahi bora ni hatari kwa usalama wa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kucheza na masilahi ya askari wetu na kuanza kuwalipa mishahara vizuri pamoja na posho zote zilizoko kisheria kama ambavyo wanafanya kwa watumishi wengine wa umma kama Wabunge na Mawaziri.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipokea mara kwa mara taarifa za manyanyaso yanayotokana na urasimu na uonevu unaofanywa dhidi ya askari wetu. Hivi karibuni Askari magereza Anjela Masawe alishushwa cheo kazini na kuhamishwa kituo chake cha kazi kwa sababu ya kumuuliza waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Mwigulu Nchemba habari za posho zao (package), Askari huyu ambaye kituo chake cha kazi ilikuwa ni gereza kuu Arusha, sasa amehamishiwa gereza la Mang'ola kama adhabu.

**5.5 Kuzuia Msongamano Mahabusu na Wafungwa Na Bajeti Ya Maendeleo – Jeshi La Magereza**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia randama ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Fungu 29 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kubaini kuwa bajeti ya maendeleo iliyopelekwa katika Jeshi la Magereza na Serikali mpaka mwezi Februari, 2017 ni **asilimia 6 tu** ya bajeti yote ya Fedha za Maendeleo kwa ajili ya Jeshi hilo ambazo zilizoidhinishiwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 3,053,380,000 na ambapo fedha zilizotolewa ni shilingi 190,000,000 pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza nchini limenukuliwa likitoa lawama kwa Serikali kutokana na kuruhusu msongamano magerezani bila kuwa na juhudi zozote za kutatua shida hiyo. Ikumbukwe kuwa Magereza nchini yana uwezo wa kuhifadhi wahalifu 29,552 kwa siku lakini yanapokea wastani wa wahalifu kati ya 35,000 hadi 38,000. Katika Randama ya fungu 29 Jeshi la Magereza limeitupia Serikali lawama likisema kuwa ***“Msongamano huu unatufanya tusiweze kutoa huduma ipasavyo kutokana na fedha kidogo zinazotolewa na Serikali”***

**Mheshimiwa Spika,** Ufinyu wa Bajeti kama unavyosomeka kwenye randama limesababisha kutofanikiwa kwa masuala mbalimbali ya kimaendeleo ya Jeshi hilo kama ifuatavyo;

1. Ukosefu wa Nyumba za Maafisa na Askari
2. Upungufu wa vyombo vya usafiri
3. Upungufu wa watumishi
4. Madeni ya watumishi (Sh **bilioni 23.03** na Wazabuni Sh **billion 44.92**)
5. Ukosefu wa Ofisi stahiki za wakuu wa Magereza wa Mikoa
6. Uhaba wa madawa na vifaa tiba
7. Uhaba wa vitendea kazi

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza kwa mwaka wa fedha 2017/2018 limeomba fedha za bajeti ya maendeleo

Shilingi 7,254,742,000 sawa na ongezeko la asilimia 58 la bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaihoji Serikali, inawezaje kuleta hapa ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa asilimia 58 zaidi kuliko ile bajeti ya mwaka wa fedha unaoenda kuisha, kama sio kulihadaa jeshi la magereza kuwa watapatiwa bajeti kubwa wakati uwezo wa Serikali kutoa fedha zote haupo?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza vyema Sheria ya Parole, na utekelezaji wake uzingatie kuwaachia huru wafungwa ambao wameshatumikia vifungo virefu gerezani badala ya wale ambao wamehukumiwa miaka michache na wanaachiwa na Parole kila mara. Uzoefu unaonyesha kuwa wafungwa wa vifungo vidogo wanaochiliwa kwa parole ni wafungwa wanaorudiarudia makosa kulikoni wale ambao tayari wameshakaa magereza muda mrefu na hutamani uhuru kwa shauku kubwa. Endapo jambo hili litafanyika kila mara na kwa wakati litapunguza msongamano magerezani hasa wale wa vifungo virefu ambao kimsingi huwa tayari wamejifunza na kujirekebisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa bodi ya Parole, ifike mahali iwaachilie wafungwa wote waliofungwa wakati wa Nyerere na Wakati wa Mwinyi na hata wakati wa Mkapa ambao wana zaidi ya miaka 10 mpaka 15 magereza. Kwani ni imani ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa watu hao wameshajifunza kiasi cha kutosha. mtu amekaa jela miaka 25, na ana miaka zaidi ya 65 akipata msamaha kisha akawa huru, kweli mtu huyo anawezaje kuwa mhalifu tena?

**Mheshimiwa Spika,** lakini pia haki nyingine za mahabusu ni pamoja na maisha yao ya ndani ya kila siku, ni maisha ya huzuni kwao pamoja na wafungwa. Chakula sio kizuri , malazi ni ya shida kubwa , selo yenye uwezo wakuchukua watu 35 wanaweza kulala hata watu 80 , mawasiliano yao na ndugu zao ni tabu kwani mpaka leo Magereza Tanzania wanatumia kanuni zilizoachwa na mkoloni kuendesha masuala ya magereza.

**Mheshimiwa Spika,** kuna unyanyasaji wa aina mbalimbali ambao maneno hayawezi kutosha kuyaelezea katika hotuba hii unaotokana na tabia za askari na mfumo mbovu wa kanuni za uendeshaji magereza. Kwa mfano; *wafungwa na mahabusu* h*uvuliwa nguo zote na kupanuliwa makalio yao kwa ajili ya kupekuliwa mara watokapo na kuingia magerezani wakati hasa wakati wanakwenda mahakamani na wakati wa kurudi ikiwa ni pamoja na kutoka kwenye shughuli nyingine mbalimbali ambao mar azote wanakuwa chini ya ulinzi wa askari. Vitendo vinavyofanywa na Jeshi la Magereza hapa nchini kuwavua nguo mahabusu na wafungwa sio cha kibinadamu ni utekelezaji wa mikakati ya kishetani. Ni tendo la aibu sana kwa Wazee na Vijana wanapokusanyika kufanyiwa hivi hadharani, hata Askari wanaofanya kazi hii na wao wanatiwa huzuni bila sababu.*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Jeshi la Magereza kuacha mara moja udhalilishaji dhidi ya utu wa binadamu, na pia Serikali kutenga fedha za vifaa vya kisasa kwa ajili ya upekuzi wa mahabusu na wafunguwa katika magereza yote nchini kwa kutumia mbinu za kisasa ambazo hazitwezi utu wa binadamu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani Bungeni pia imetambua ugumu wa mawasiliano uliopo ndani ya Mahabusu na Magereza. Hivyo tunaitaka Serikali kuweka 'Simu Maalumu' (Call Box) ili kurahisisha mawasiliano baina ya ndugu, mawakili na mahabusu na wafungwa walioko magerezani. Mawasiliano jela kutoka kwa mahabusu au wafungwa kwenda kwa ndugu au jamaa ni magumu sana , Wakati wenzetu wa Kenya wamefikia mahali hata wafungwa na mahabusu kuruhusiwa kuonana na watoto wao, Kenya wameunda sehemu maalumu (Childrens corner)ambapo mahabusu au wafungwa hukutana na familia zao na kupanga mikakati ya maisha. Hapa kwetu Tanzania hata simu kupiga kuijulia hali familia ni jambo ambalo ni marufuku kubwa. Huu sio utu bali ni unyama uliopitiliza, Kama Mungu angekuwa hivyo, basi ninyi CCM

na vizazi vyenu asingekuwepo hata mtu mmoja kwa namna mnavyohuzunisha moyo wa Mungu kwa kutotenda kwenu haki. Rehema ni bora kuliko sadaka.

**Mheshimiwa Spika,** kuonesha umuhimu wa Mawasiliano magerezani, mfungwa mmoja rafiki yangu alihukumiwa kunyongwa mpaka kufa huko Babati. Neno la mwisho kwa familia kusikia ilikuwa baba yao amehukumiwa kunyongwa mpaka kufa , Mzee Kisingo alihamishiwa Gereza la Dodoma baada ya hukumu hiyo, na ndugu zake hawakumuona tena, alianza kutafuta utetezi hivyo na kwenda mahakama ya rufani na akashinda kesi akoondolewa adhabu ya kifo na kupunguziwa miaka aliyokaa gerezani na mwaka jana amepata msamaha wa Rais na mwakani 2018 mwezi wa tatu atakuwa nje, kwa miaka zaidi ya tisa hajawahi kuwasiliana na familia yake na familia inajua kuwa Baba yao alinyongwa, nilimuuliza Mzee Kisingo, unatoka mwakani ukikuta mkeo ameolewa utafanya nini? Mzee Kisingo alinijibu ***"Mungu ataniongoza siku hiyo kama nitalikuta jambo hilo"***

**Mheshimiwa Spika,** kuonesha umuhimu wa Mawasiliano magerezani, mfungwa mwingine ni Octvian aliyehukumiwa miaka thelasini jela, mke wake akaanguka mahakamani na kupoteza fahamu akiwa ni mjamzito na toka hapo hawakuwahi kuonana tena na mume wake. Octvian alihamishwa magereza mbali mbali na sasa yuko Gereza kuu Arusha , baada ya miaka zaidi ya kumi na tano siku moja akiwa kwenye kazi za nje alimuona mwanamke anafanana na mke wake, akumuomba askari amsogelee dada huyo , na kumbe alikuwa anakutana na mke wake ambaye naye alikuja Arusha kutafuta vibarua.

**Mheshimiwa Spika,** iko mifano mingi ambayo inathibitisha hoja yangu ya umuhimu wa mawasiliano ndani ya Magereza, hii ni michache sana katika kitabu changu nimeeleza mambo ya kuwasaidia binadamu kama hawa, ndio sababu nasema kwenda kwangu magereza ilikuwa ni kusudi la Mungu.

### 5.6 Njia Bora za Kupamba na Madawa ya Kulevya Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Wakati dhima ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ni *"Kujenga mfumo bora wa kudhibiti na Kupambana na Kupambana na dawa za kulevya nchini, kuendeleza ushirikiano katika hatua mbalimbali za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya na kujenga uwezo wa Taasisi na Asasi za kiserikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya"* inashangaza kuona Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda akibomoa mfumo huo kwa makusudi kwa kuamua kuwaficha watuhimiwa halisi wa biashara za dawa za kulevya kwa kutaja majina hadharani kwa makusudi jambo wataalamu wa upelelezi duniani wanasema kuwa ni kitendo cha kuharibu upelelezi kwa hatua za awali kwa kuwapa signal wahusika halisi kujificha na kukwepa mfumo kuwafikia kwa njia za Kitaalamu na sio za kutaja taja hovyo majina na kuharibu upelelezi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inalaani vikali njia zilizotumiwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda katika kukabiliana na madawa ya kulevya kwa kutaja hadharani majina ya watu ambao hakuwa na ushahidi kama kweli waliendesha biashara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Vita hii ya dawa za kulevya inapaswa kupiganwa kwa dhamira safi ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mzaha na vita hii kwa kuwa katika mwaka wa fedha unaoisha 2016/ 2017, Serikali haikutenga fedha zozote za Maendeleo kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuonesha kuwa Serikali bado haina dhamira ya kweli kupambana na biashara ya dawa za kulevya nchini, pamoja na utekelezaji wa Sheria hiyo kwa uteuzi wa Kamishna Mkuu wa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za Kulevya, bado kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa fungu 91 – Mamlaka yua Kudhibiti na

Kupamba na dawa za kulevya chini ya Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na watu wenye ulemavu) Serikali haijatenga fedha zozote pia kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo, hivyo ni muhimu Wizara ya Mambo ya Ndani ikatambua jambo hili na kuona namna linavyoweza kufanyiwa marekebisho haraka iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Jitihada za Serikali kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya zinapaswa pia kuangalia nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu sera na sheria zao katika vita hii, kwani wakati nchini Kenya mirungi ni zao la kibiashara na Serikali ya Kenya, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wametenga bilioni 2 za Kenya kwa ajili ya kusaidia wakulima wadogo wadogo wa zao hili. Hapa Kwetu Tanzania, mtumiaji wa mirungi akikamatwa adhabu yake ni miaka 30 mpaka kifungo cha maisha Jela. Kuna utata wa fikra katika jambo hili na katika Jumuiya.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni sio chuki dhidi ya Serikali iliyopo madarakani, bali ni msaada wa fikra mbadala ambao Serikali inapaswa kuuzingatia kwa kuwa taifa hili ni letu sote.

**Mheshimiwa Spika,** tunaweza tukataja mikakati mbalimbali ya kuelimisha umoja na mshikamano wa Taifa lakini ukweli unabakia kwamba, umoja na mshikamano hautajengwa kwa matangazo ya Luninga wala machapisho ya magazetini, isipokuwa upendo ukishamiri miongoni mwetu haki, utu, usawa vitakuwa ni sehemu ya miasha yetu. Kwa hiyo, kama tunafikiri kwa dhati usalama wa nchi hii ni lazima tukubali kwamba utu wetu ni bora kuliko rangi za vyama vyetu, utu wetu ni bora kuliko vyeo vyetu.

**Mheshimiwa Spika,** tabia ya hivi karibuni ya viongozi wakuu wa nchi kuanza kujenga utengano kati ya jamii, ni jambo la hatari linalopaswa kupigwa vita na kila mtu

mwenye akili timamu. Kauli za viongozi ni muhimu katika kujenga mshikamano wa Taifa kwani kama baba alivyo ndivyo watoto wanavyokuwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeongelea masuala ya DPP na ofisi ya DCI kwa kirefu. Ni muhimu tukatambua kwamba amani na usalama wa Taifa hili utajengwa kwa uhuru kamili wa mahakama zetu. Kwa sababu ya mfumo wa kikatiba wa uteuzi wa watendaji wa mahakama zetu,bado haupo huru kwa kiwango cha kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika historia moja ya sababu zilizopelekea mapinduzi yaliyosababisha machafuko Ufaransa ni wananchi kukosa imani na mahakama. Hivyo kuwa na mhimili imara wa mahakama jambo muhimu kwa ustawi wa amani katika Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kumalizia kwa leo, kwa sababu muda uliopo ni mdogo, naomba ninukuu maneno ya mwanaharakati aliyepinga utumwa Bw. Frederick Douglass aliyeishi kati ya mwaka 1818 hadi 1895 alipata kusema maneno haya, nitanukuu;

*"Where justice is denied, where poverty is enforced, where ignorance prevails, and where any one class is made to feel that society is an organized conspiracy to oppress, rob and degrade them, neither persons nor property will be safe."*

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili, Frederick Douglass anasema kuwa;

*"Mahali ambapo haki inakataliwa, mahali ambapo umasikini unatekelezwa, mahali ambapo ujinga unatawala, na mahali ambapo daraja moja la watu linafanywa lijisikie kuwa jamii imeundwa kwa njama ili kufanya ukandamizaji, unyang'anyi na udidimizaji, sio watu wala mali zitakuwa salama"*

**Mheshimiwa Spika,** Upendo, haki na usawa ndio silaha ya amani.

Naomba kuwasilisha;

………………………………………………..
Godbless Jonathan Lema (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
*Tarehe 09 Mei, 2017*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshasikiliza maoni yote, tuna muda mchache, moja kwa moja tutaanza na mjadala hapa…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Tutaweza kupata watu wawili kwa dakika tano tano na tutaanza na Mheshimiwa Ibrahim Raza na baadaye atafuata Mheshimiwa Khamis Mtumwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae miongozo tutachukua baadaye ngoja tumalize hawa kwanza.

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ni suala la utaratibu, ulisema ukimaliza utatoa nafasi?

**MWENYEKITI:** Ndiyo nitakupa, wewe kaa tu tuendelee na hawa kwanza.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI RAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa leo Bungeni nikiwa mzima wa afya. Vilevile nichukue nafasi hii kutoa mkono wangu wa pole wa rambirambi kwa wazee ambao walifiwa na watoto wao juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuelezea changamoto yangu katika Wizara hii Mambo ya Ndani ya Nchi, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya kuweka nchi hii katika hali ya utulivu na amani. Tukienda kwenye changamoto katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nitazungumzia upande wa Zanzibar. Kwa kweli Vituo vingi vya Polisi Zanzibar vipo katika hali mbaya sana vimekuwa kama magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kwenda Kituo cha Polisi ukastaajabu kwa sababu vitendea kazi kwanza hamna, Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, jengo limechaa, mapolisi wengi Zanzibar hawana *radio call* za kuwasiliana na viongozi wao na hawana magari. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie Zanzibar kwa jicho la huruma kwa sababu mapolisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa upande wa trafiki, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze kaka yangu Kamanda Mohamed Mpinga na timu yake nzuri kwa kazi wanayofanya kwa kweli wametusaidia sana katika Jiji letu la Dar es Salaam, sasa hivi madereva wanafuata sheria na nidhamu imekuwepo lakini bado kuna matatizo mengi sana hasa katika suala la kupaki magari sehemu ambapo hairuhusiwi. Kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mohamed Mpinga suala hili alitilie mkazo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala hili la mapolisi wanapotaka kwenda likizo wanaambiwa waende

halafu wakirudi ndiyo watapewa haki zao kwa maana ya posho zao. Mimi namuuliza Mheshimiwa Waziri wakati polisi anapokwenda likizo unamwambiaje aende likizo halafu akirudi ndiyo apewe marupurupu yake, inakuwa si haki. Polisi anapopangiwa kwenda nyumbani basi apewe haki zake zote aende akastarehe na mama watoto na watoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa kweli linawavunja nguvu Jeshi la Polisi kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Naomba Wizara hii walitupie macho Jeshi la Polisi kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na wanastahiki posho muda ukifika na kama kuna uwezekano posho zao ziongezwe kwa sababu wao ndio wanatulinda sisi na mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tukiwavunja nguvu Jeshi la Polisi hakuna litakaloendelea katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie Jeshi la Polisi kwa macho ya huruma kwa sababu wanafanya kazi ngumu na ya hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa maafande wetu wanapokwenda kwenye kazi maalum (*task force*) nashauri wapewe vifaa ambavyo vitawasaidia hususan mapolisi. Dar es Salaam kuna mapolisi ambao tunawaita Polisi Tigo kwa kweli zile *uniform* wanazovaa akitokea mtu yeyote mwenye nia mbaya na kuwapiga risasi basi inapenya tu kwa sababu hazistahili kutokana na kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika upande wa Uhamiaji, niwapongeze kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini naomba wazingatie suala la wakimbizi. Kuna hawa wakimbizi wanaotoka nchi jirani wanakuja nchini kwetu na kutuharibia amani yetu, kwa sababu wakija nchini kwetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raza, ahsante sana muda wako umemalizika.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI RAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mtumwa na muda ukitosha tutamalizia na Mheshimiwa Faida.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**WABUNGE FULANI:** Utaratibu huku.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Kiti chako kiwaelekeze Wabunge kwa mujibu wa Kanuni kama ulivyoondoa taarifa za Kambi za Upinzani kwa kufuata Kanuni ndiyo hivyo hivyo Wabunge wasiwe wanasoma wawe wanarejea.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Mheshimiwa Ester Bulaya. Mheshimiwa Mtumwa endelea.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi kwa kuniwezesha kuwa mzima wa afya na kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Mama Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kazi nzuri ya kusimamia Taifa letu hili. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu

Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kusimamia amani ya nchi hii. Kwa kweli bila amani hatuwezi kufanya jambo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linakabiliwa na changamoto mbalimbali nitaanza kuzungumzia makazi ya askari. Kwa kweli makazi ya askari ni duni sana pamoja na Mheshimiwa Waziri kuelezea kwamba wana mpango mzuri wa kujenga nyumba za askari. Hata hivyo, kiuhalisia ukiangalia zile nyumba za askari ambazo zipo hivi sasa zinatisha. Ukienda *central* tu hapo utakuta nyumba za askari zina mabati, ndani hazina *ceiling board* hata yule askari akinunua mayai akayaweka ndani baada ya wiki utaona yameshatoa watoto yaani zile nyumba zimegeuka *incubator. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo hizo nyumba za askari zilizopo ambazo hazina hata *ceiling board,* zimejegwa kwa udongo ambapo siku za mvua ukipata maji zinaporomoka. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri ni lazima aangalie hali hii kwani mazingira wanayoishi askari wetu si mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifika wakati wa usiku baridi iliyokuwemo ndani ya nyumba zile ni kama wapo katika mafriji. Wale ni binadamu, wanataka nyumba nzuri ili waishi kama binadamu wengine ili waweze kufanya kazi vizuri. Naomba sana Serikali kupitia Wizara hii waweze kuangalia hizi nyumba wanazojenga na hizi ambazo zipo ili kuziboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea posho za askari wetu hawa. Kwa kweli inasikitisha sana, askari wadogo hawapati posho stahiki na kwa wakati na hali hii inapelekea kuwa na imani potofu na duni. Ikiwa kama kuna matabaka ya kupata hizi posho stahiki au kucheleweshewa kupelekwa posho hizi kwa wakati itapelekea askari hawa kuvunjika moyo na hatimaye kutofanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa wakati wa bajeti tulimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba askari wanalipia umeme kwenye mifuko yao wenyewe kutoka katika mishahara yao. Mheshimiwa Waziri akasema hili atalisimamia lakini inafika hatua wanastaafu pesa za umeme ambazo wametumia kutoka kwenye mifuko yako hawajalipwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana sana Mheshimiwa Waziri na hili aliangalie aweze kuhakikisha askari hawa wanapewa posho zao *straight* kama ilivyo kwa Jeshi la Wananchi (JW). Kwa sababu wakipewa hivyo itapunguza malalamiko wakati wa kustaafu ya kutopewa posho au pesa ambazo wanazitumia kwa ajili ya kulipia nyumba au umeme. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja aweze kutuelezea vizuri mkakati huu kafikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu mafunzo mbalimbali ya Jeshi la Polisi. Ni ukweli usiopingika kwamba bila mafunzo Jeshi la Polisi haliwezi likafanya kazi vizuri. Ikiwa mafunzo haya yanatolewa kwa askari wa *headquarter* tu bila kuwashirikisha wale askari wadogo wadogo waliopo mikoani itakuwa ni vigumu askari hawa kufanya kazi kwa weledi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kuhakikisha kwamba askari wadogo nao wanakwenda mafunzo siyo waliopo *headquarter* tu mikoani mafunzo hamna, hivi sasa mafunzo yamepungua kabisa. Kama kutakuwa na upungufu wa bajeti basi Serikali ipeleke fedha kikamilifu ili mafunzo haya yaweze kupatikana vizuri zaidi kwa askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Vituo vya Polisi kama alivyosema Mhesimiwa Raza pale vipo katika hali ngumu. Katika Jimbo langu kuna Kituo cha Polisi kimoja tu, unapotokea uhalifu inakuwa ni shida sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba katika Shehia yangu ya Kilombero tungepata Kituo kimoja cha Polisi kwa sababu

anapotokea mhalifu inakuwa ni vigumu kumfikisha Kituo cha Mahonda ambapo ni mbali zaidi kutoka eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja hapa akasema kwamba viatu vyake vizuri sana kuliko vya wengine, ni kweli. Hata hivyo, askari wake viatu wanavyotumia ni vile vya *UN!* Namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi viatu vya askari wake viwe kama vyake. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida kwa dakika tatu.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo tukiwa katika hali ya afya njema. Pia napenda kutoa pole kwa wazazi wenzetu ambao wamepoteza watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda moja kwa moja kwenye makazi ya askari na vituo vya askari. Kama tunavyojua askari siyo vizuri kukaa uraiani kwa sababu askari hawa wana namna yao ya kuishi, wana siri zao na mambo yao ya kitaalam na ya kimaadili yao, siyo vizuri kuchanganyika yaani nyumba hiyo hiyo askari nyumba hiyo hiyo raia. Wao wanatakiwa watulinde sisi, wanatakiwa wawe na maeneo yao ya kuishi, lakini hawana nyumba. Kila nikisimama naongea kuhusu nyumba za askari hasa kule kwetu Pemba,

hakuna nyumba za askari, wengi wanakaa uraiani na ni maili nyingi kutoka wanakokaa na kazini. Wanachelewa kufika kazini kutokana na usafiri, si vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja Pemba, Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja Pemba, Pemba wanaijua, naomba nisiseme tena, naomba askari wajengewe nyumba na vituo vyao ni vibovu. Kituo cha Mkoani, Kengeja, Konde kote vituo ni vibovu vinavuja, mvua hizi zote zimo ndani kwenye vituo vile. Hivyo kweli jamani hatuwaonei huruma askari wetu, kwa nini tunawafanyia hivi askari? Naomba sana nisiseme tena kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee hali ya amani na utulivu. Tunawashukuru sana wananchi wa Tanzania na Serikali yetu hasa kwetu Pemba kwa sababu zamani hatukuwa tunaishi vile, vyama vyote tulikuwa na matatizo kusema ule ukweli, huyu anampiga huyu, huyu anamuua huyu, huyu hamziki huyu, huyu haendi dukani kununua kwa huyu, lakini sasa hivi hali ya amani Pemba imetulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana wananchi wa Pemba na kwa kweli tujitahidi kuzidisha ushirikiano wetu ili tuweze kuishi kwa amani na utulivu katika Kisiwa chetu cha Pemba. Siasa tuiweke nyuma ili tuweze kuleta amani na utulivu na watoto wetu waishi vizuri katika Kisiwa chetu cha Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee ajira za vijana katika Kisiwa changu cha Pemba. Kule Pemba kuna vijana wazuri tena wasomi, unajua wasomi wazuri wanatoka Pemba, nyie mnajua hilo? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Wasomo wazuri wanatoka Pemba, vijana ni wasomi, wana maadili na ni wachapa kazi, lakini wakati wa ajira vijana wa Pemba wanaachwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Faida.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Unanipa taarifa mimi au?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Nakwambia wewe Mwenyekiti taarifa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba mtambue uwepo wa Mtumishi wa Mungu, Mtume na Nabii Josephat Mwingira, yupo katika *gallery* ya Spika pamoja na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala jioni na tutaanza na Mheshimiwa Kangi Lugola, atufuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Katani Ahmad Katani halafu wengine wataendelea.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae na Mheshimiwa Katani Ahmad Katani.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majeshi yetu ya Polisi, Magereza, Uhamiaji pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni majeshi ambayo yamesahaulika, ni majeshi ambayo yanachukuliwa kama ni ya kawaida, ni majeshi ambayo yanadhaniwa watendaji walioko mle hawana *professionalism* ya aina yoyote. Ndiyo maana majeshi haya yamefanywa kama majeshi ya miujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Yesu peke yake Mwana wa Mungu aliye hai ambaye ni bingwa wa miujiza, ambaye alikufa akafufuka, ambaye alimfufua Lazaro, ambaye alitembea juu ya maji. Hivi kweli kama majeshi haya hatutawekeza, hatuwezi tukapunguza uhalifu katika nchi yetu, hatuwezi tukajenga nidhamu ya majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe kidogo Waheshimiwa Wabunge, hima himaaa, Tanzania sauti hii ukiona vyaelea vimeundwa, msidhani magwaride haya mnayofurahi jinsi majeshi wanavyopiga mguu chini, jinsi wanavyotoa sauti yao ya kutoa heshima ya utii kwa Amiri Jeshi Mkuu, mkadhani sauti hii imekuja hivi hivi. Sauti hii inatengenezwa na lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje askari wetu tunawapa shilingi 10,000, shilingi 10,000 hii aiache kwa familia, shilingi 10,000hii aende nayo kwenye lindo la benki, shilingi 10,000 hii aende nayo doria, asubuhi mpaka jioni haitawezekana. Ndiyo maana Waziri anapotuambia katika

ukurasa wake wa 21 katika hotuba yake kwamba Serikali inaendelea kuboresha maslahi ya watendaji wa vyombo vya usalama kwa kuwapatia *ration allowance* za kila mwezi. Mheshimiwa Waziri unasema unaendelea kuboresha *ration allowance* mbona kwenye kitabu chako humu hujaboresha, umeweka maneno tu yasiyoboresha? Tunahitaji uboreshe maslahi haya ili askari wetu waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari hawa mnaosikia wengine wanatekwa kwenye mabenki, wengine wanavamiwa kwenye doria, wakati mwingine wanakuwa kwenye *stress,* hajui leo familia yake itakula nini, hajui yeye atakula nini, anabaki askari wa kupiga miayo tu kwenye benki matokeo yake wanamnyang'anya bunduki. Tunahitaji kuboresha maslahi ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mafunzo, Mheshimiwa Mwigulu ulipokuwa Wizara ya Kilimo ulikuwa na kauli mbiu mkitaka mali mtaipata shambani. Sasa leo uko Wizara ya Mambo ya Ndani nataka nikushauri, ukitaka kupunguza msongamano magereza, siyo kujenga mabweni ni kupunguza uhalifu katika nchi yetu. Ukitaka kupunguza uhalifu katika nchi yetu lazima uzingatie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya miaka kumi sasa hakuna *traffic courses* kwenye Jeshi la Polisi, imebaki tu wewe askari kesho unapigiwa simu unakuwa *traffic* na ndiyo maana ghafla mnaona *traffic* anachoropoka kwenye vichaka kwa sababu hawana mafunzo ya aina yoyote. Mnagombana na askari *traffic* hawana mafunzo, tunataka mafunzo ya askari wa usalama barabarani wasomee magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya *CID*. Msongamano utaendelea kwa sababu upelelezi uko kiwango cha chini sana, kesi zinachukua muda mrefu kwa sababu ya kutokuwa na mafunzo katika kupeleleza, kwa sababu ya kutokuwa na fedha ya kutosha kwenye *Criminal Investigation Fund,* mfuko ambao unatumika kuwapatia watu wanaoleta taarifa, taarifa ni za kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *CRO* wenzangu ambao hamkupita kwenye Jeshi kama hilo maana yake mimi nimepita huko nina-*declare interest.* Pale mnapoita kaunta pale, pale ni *CRO* pale kulikuwa na mafunzo ya *CRO*, lazima anayekuwa *in charge* pale awe amefundishwa namna ya kupokea mashitaka, namna ya kujua hili ni kosa la jinai au ni kosa la *civil,* matokeo yake kunakuwa na malalamiko mengi ndani ya Jeshi la Polisi, kwa sababu hakuna kozi kama hizi za *CRO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Mwigulu kozi hizi zirudi na wafundishwe Askari ili wajue kupokea mashtaka, tunaposema watu wanabambikizwa kesi ni pamoja na kutokujua hii ni ya *criminal* au ni ya *civil* kwa sababu hawajapata mafunzo ya *CRO* muda mrefu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye vitendea kazi. Kwenye *PGO* lazima askari anapopanga ile *duty roster* pale kituoni, kunakuwa na askari wa *standby*...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola dakika tano zako zimemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Lijualikali yeye atapewa dakika kumi.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lugola. Mheshimiwa Peter Lijualikali dakika kumi.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa leo ni mara ya kwanza nasimama ndani ya Bunge lako kuzungumza tangu nimetoka Gereza la Ukonga, ambako nilikuwa natumikia kifungo batili cha miezi sita, nashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kilombero, kwa namna ambavyo wananipenda, wananiheshimu na

wanajua mchango wangu kwao, kiasi ambacho nilipokuwa nimefungwa hawakukata tamaa, walikuwa wanakuja kuniona, walikuja kwa wingi Idete, mpaka ikaonekana wanaweza wakavunja Gereza, maana walikuwa wengi sana, ikabidi nihamishwe. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukrani za pekee kwa Chama changu, Mwenyekiti wangu wa Chama Taifa Mheshimiwa Mbowe, Wakili wangu msomi Mheshimiwa Tundu Lissu, pia ninawashukuru watu wote waliokula njama, walionifanyia fitna na uhuni ili nifungwe, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru Wabunge wa CCM wakati Kiongozi wa Upinzani Bungeni (KUB) Mheshimiwa Mbowe anazungumza yanayonisibu gerezani na kutaka Bunge lichukue *attention* nawashukuru kwa kumzomea, ila mjue mlikuwa hamzomei Mwenyekiti, hamkuwa mnamzomea Mbowe ila mlinizomea mimi, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa ninawashukuru wafungwa wa Gereza la Ukonga na wale wa Gereza la Idete, maana naamini maisha yangu yalikuwa mikononi mwao. Wangeweza kufanya ubaya wowote lakini waliniheshimu, wakanitunza na niseme Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu programu ya *Parole* ambayo ni misamaha kwa wafungwa. Misamaha hii ambayo inatumika vibaya na vizuri. Gerezani nimekuta kuna wafungwa wazee ambao wamefungwa miaka ya 1970 mpaka leo bado wapo gerezani, lakini Serikali mmekuwa mkitoa msamaha kwa wafungwa wanaofungwa miezi sita, vifungo vidogo. Nataka nimwambie Waziri, nilimwambia tukiwa wawili na leo ninasema mbele ya Bunge, vifungo hivi vya miezi sita, wahalifu wakubwa wa Taifa hili, wanatumia vifungo vidogo kufanya uhalifu wanakuja gerezani, wanakaa kwa muda mchache, halafu wanatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mtu anajipa kesi ndogo ambayo anajua atafungwa miezi sita, anajua atakaa miezi mitatu, atapata msamaha. Anakuwa na kesi hiyo mahakamani, anakwenda anafanya tukio kubwa la mauaji au ujambazi ile kesi ndogo inamfunga, anakuwa amejikinga na lile tukio kubwa ambalo amelifanya mtaani. Waziri wa Mambo ya Ndani unatoa msamaha kwa huyu mfungwa pasipokujua umemsaidia kuficha kesi kubwa ambayo alikuwa nayo mtaani.

Kwa hiyo, mnawafunga watu kwa miezi michache mnawatoa, baada ya muda mfupi kumbe walitakiwa wapate msamaha watu wenye vifungo vikubwa, hii ingesaidia kuwafanya watu wenye vifungo vya muda mfupi peke yao waone kwamba hii siyo kinga.

Mheshimiwa Waziri, hili nilikwambia na leo nasisitiza *Parole* muwe mnaangalia vifungo, msijali kwamba hiki ni kikubwa mkaona hawa hawafai, hawa wenye vidogo basi ndiyo tuwatoe, vidogo vinatumika kuficha maovu makubwa. Kwa hiyo, naomba hili muangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukiwa Ukonga na magereza mengine, nimeshuhudia askari wakifanya njama pamoja na maafisa wa mahakama, wale *admission officers* wafungwa wanakosa kupata haki zao za kupata Hati za Hukumu pamoja na upande wa mashtaka, kunakuwa na uhusiano mzuri kati ya mahakama pamoja na askari wa *admission.* Mfungwa akiomba apate nakala ya hukumu akienda kule mahakamani anaambiwa muone askari fulani, askari yule anamwambia mfungwa lazima utoe hela, ndiyo upate hati ya mashtaka na mwenendo wa mashtaka. Hii maana yake ni kwamba askari wako lazima uwaangalie. Vitengo vya *Admission* vinatenda rushwa, vinazuia wafungwa kupata haki yao, naomba hilo Mheshimiwa Waziri uangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu hii programu mnasema ya urekebishaji. Mimi nilipokuwa gerezani nilitegemea ningeona huo urekebishaji mnaousema,

kwamba wafungwa mnawarekebisha kwa programu ambayo ni *tangible.* Nione kuna programu ya urekebishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nimekiona sasa sijui kama huu ndiyo urekebishaji wenyewe, nimeona marungu, mfungwa anapigwa marungu mpaka mguu unageuka. Unapigwa rungu mpaka mguu unashindwa kutoka.Nimeona wafungwa wanafanyishwa, labda niseme nilipoingia mara ya kwanza gerezani, askari wako walinikamata wakanipiga mitama, sijafanya chochote nimeingia hapo. Sasa sidhani kama Mbunge naweza nikafanyiwa hivyo wafungwa wa kawaida sijui wanafanywaje na siamini kama huu ndiyo urekebishaji au nilifanyiwa hivyo kwa sababu mimi ni Mbunge wa Upinzania labda, lakini kama hizo ndiyo programu za urekebishaji, vile ambavyo wafungwa wanafanyiwa mle ndani, wafungwa wanauwawa, wanapigwa risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mimi nimefanyiwa mambo ajabu kama hayo katika Gereza la Idete, askari ananiambia nitakuuwa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuambie wewe ni Waziri mpaka wa wafungwa, usifikiri kwamba wewe ni Waziri tu kwa watu ambao wako mtaani, nenda gerezani kasikilize vilio vya wafungwa. Wafungwa wana matatizo makubwa sana nenda kawasikilize, wanavyofanyiwa mambo ya ajabu mle ndani. Nilikwambia tukiwa wawili na leo nakwambia, nenda kasikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoamini kabisa mtu yeyote wa Mungu anajua kabisa vitabu vinasema waonee huruma wafungwa, wagonjwa, walemavu na wajane. Hizi kauli za wamenyeke tu, Mheshimiwa Rais anasema hawa wafungwa wamenyeke hawafai, wafanye kazi mpaka wachubuke,mimi nilifungwa kihuni, nimeonewa, sina kosa, lakini Rais alisema kwamba nimenyeke. Ningekuwa sina

Wakili msomi kama Mheshimiwa Tundu Lissu maana yake yake na mimi ningebaki ninamenyeka. Sasa kuna watu wangapi ambao nchi hii wanamenyeka kwa uhuni tu ambao wamefanyiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, wale wafungwa ni binadamu, wafungwa ni watu. Yeyote aliyepo hapa ipo siku chochote kinaweza kikatokea. Sheria mnazotunga hapa, wakati mimi nasema haya wewe umevaa *crown* upo juu unafikiri uko sahihi, ipo siku na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena kuhusu maisha ya askari. Mheshimiwa Waziri nikuulize, hivi leo ukiambiwa uchague, ukae kwenye choo chako au ukae kwenye nyumba wa Askari wa Magereza wa Idete wewe utachagua ukae wapi? Kati ya choo chako wewe Waziri, choo chako wewe Mbunge na chumba cha Askari wa Magereza uambiwe ukae kwa siku moja utakaa wapi?

**WABUNGE FULANI:** Chooni.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Utakaa chooni kwako. Nyumba ya askari wa nchi hii wa magereza ni mbaya choo chako ni kizuri. Wabunge vyoo vyenu ni vizuri, vyoo vya askari wenu, na hawa askari pamoja na yote haya mnayofanyiwa, bado sisi ambao tunaongea haya maneno mnatupiga virungu, Mungu anawaona ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza tangu mwaka 2012 mpaka leo*uniform* hawajapewa. Nimekuta askari wanajinunulia wenyewe *uniform.*Wananiambia Mbunge hii *uniform* nimenunua mwenyewe kwa fedha zangu na hivi unavyoona hivi haifanani na nguo za askari wengine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo *fair, package allowance* mnawapa askari wengine, wanajeshi wengine mnawapa *package allowance* leoMagereza wale mpaka leo hamjawapa, kwa nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali muda wako umemalizika.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini askari polisi msitumike vibaya na hawa jamaa, Mungu anawaona. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lijualikali. Tunaendelea na Mheshimiwa Katani ambaye amekubaliana dakika tano na Mheshimiwa Khatib Said na baadaye Mheshimiwa Jaku Hashim ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri vizuri, ninapenda kusema si ajabu Waziri mwenyewe akawa chanzo cha matatizo ya askari wa Jeshi la Polisi. Hili nazungumza wazi kwa sababu kuna matukio ambayo yametokea polisi wakiwa wanatimiza wajibu wao, baadaye wanatengua walichokiandika wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nazungumza sana kutokana na mgogoro ulioandaliwa na chama fulani ndani ya *CUF*. Tarehe 16 Novemba, 2016, nikiwa na Wabunge wenzangu wa *CUF* ambao ni Wajumbe wa Baraza kuu la Uongozi, tuliokwenda Newala kwa kibali cha polisi kwamba tunaruhusiwa kufanya mkutano wa ndani. Asubuhi tuko kwenye mkutano wa ndani, ghafla askari polisi wanakuja

na *defender* na washawasha wanakuja kutuondoa kwenye mkutano wa ndani, eti kuna mtu mwingine amewaambia kwamba haturuhusiwi kuendelea kufanya mkutano wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi haturuhusiwi kufanya mkutano wa ndani ni siku tano nyuma Ibrahimu Lipumba aliyekuwa Mwenyekiti wa *CUF* alifanya mkutano na wakamlinda. Tarehe 19 tulienda Mtwara...

**MHE.MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Mheshimiwa Katani, taarifa.

**MHE.MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza, kwamba analipotosha Bunge hili, eti kwamba mgogoro wa*CUF* umeanzishwa na chama fulani. Hili suala siyo la kweli, mgogoro wa*CUF* umeanzishwa na viongozi wakuu, tena ni kiongozi mkuu, Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi - *CUF*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani unapokea hiyo taarifa?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa, pia Kiti chako kisiyumbe. Kuna watu wameomba taarifa hapa umewakatalia mara kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa mnaowabeba, ndiyo pamoja na hawa wengine hawa. Tarehe 19 Novemba Katibu Mkuu wa Chama changu cha *CUF* alikwenda Mtwara, anapaswa kufanya kikao cha ndani, tumelipia ukumbi na kila kitu, mwisho wa siku tunaambiwa haturuhusiwi kufanya kikao cha ndani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukampigia Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, tukamwambia tatizo hili, lakini mwisho wa siku hatukupata maamuzi sahihi ya mambo haya. Mambo haya ya kihuni yanaendelea kufanywa na kundi hili la akina Lipumba na watu wake hawa akina Mheshimiwa Magdalena Sakaya, polisi wakiwa wanaendelea kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa *CUF* Taifa, Mheshimiwa Julius Mtatiro amekwenda Tanga katika vikao vya ndani, hakuna mgogoro, polisi wameendelea kuzuia wasifanye vikao vya ndani.

**MBUNGE FULANI:** Haki ipo wapi?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Polisi hawa pia wakati tuko mahakamani wanaona mtu anapigwa kwa kisu, yule aliyepiga mpaka leo hajakamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mabibo Mwenyekiti wetu wa Wilaya ya Kinondoni, Juma Mkumbi, ameitisha kikao na waandishi wa habari, wameingia wavamizi na bastola, hawajakamatwa mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio yote haya na Waziri ana barua ya chama ya kulalamika juu ya matukio haya ambalo Jeshi linaendelea kuwakumbatia hawa *mungiki*. Hata mkutano wa tarehe 21 Agosti, 2016, Lipumba kaingizwa kwenye mkutano na polisi kuvamia mkutano ambao mwenyewe Lipumba amekiri hakualikwa. Kama uliangalia kipindi kile cha 360 cha *Redio Clouds,* Lipumba mwenyewe anakubali hakualikwa, amevamia mkutano akiwa na*OC-CID* wa Magomeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mnakaa hapa mnazungumza, nikuombe Mheshimiwa Waziri, ulitia nia kubwa ya kutaka nafasi kubwa mwaka juzi ya Urais wa nchi hii, si ajabu Mungu kwa makusudi kabisa aliona bado na ndiyo haya unayoyafanya. Kwa sababu haiwezekani, watu

wanaofanya matukio wapo, tumesharipoti kesi nyingi, matukio anayoyafanya Lipumba anasindikizwa na polisi. Tumeomba juzi kwenda kufanya usafi Buguruni, Mbunge wa Temeke mmemzuia, Lipumba mlikuwa mnamlinda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri dhamana uliyopewa ni dhamana kubwa sana. Mwanadamu kuna muda anavumilia na kuna muda uvumilivu pia unashindikana. Mimi nasema hawa mnaowatumia, mmemtumia Sakaya anakwenda kushtaki watu polisi anasema tunataka kumshughulikia, watu ambao hatukuwepo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Said, dakika tano...

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dakika mbili umezitumia wakati anaongea huyu *mungiki* hapa.

**MWENYEKITI:** Dakika moja tu, imeisha imeshawekwa hiyo tunaendela na Mheshimiwa Khatib Said dakika tano.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu pekee kwa sababu ni dakika tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muongeaji anasema mwanadamu uvumilivu unapomuishia anakuwa ni afadhali mnyama kuliko mwanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukumuacha Lipumba na vibaraka wake na wanaomtumia kwa sababu

tunamuogopa, hapana. Tulimuacha kwa sababu Watanzania na dunia ijue ujinga wao na hao wanaomtumia kufanya ujinga ule. Watanzania waelewe ujinga wa Lipumba na hao wanaomtumia kudhihirisha ujinga wake. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya siasa vipo kwa mujibu wa sheria. Vyama vya siasa waasisi wa kuleta vyama hivi vya siasa mmojawapo ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mnamuita Baba wa Taifa na sisi tunakubali ni Baba wa Taifa, hawezi kutokea mjanja akamuona Baba wa Taifa aliyekubali vyama vingi vije nchi hii ni mjinga yeye ndiyo mwerevu, huyo ni zumbukuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme wazi kwamba mgogoro unaoendelea ndani ya Chama cha Wananchi *(CUF)*kwa kupandikizwa na watu tunaowajua, akiwemo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanzania, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni. Mheshimiwa Waziri umesema maneno makubwa sana nakuheshimu na katika Mawaziri kwenye Bunge hili ninaowaheshimu ni Mheshimiwa Mwigulu, lakini msaidizi wako hafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema Mheshimiwa Waziri hakuna ushirika wowote wa waovu utakaoweza kuishinda haki, nakubaliana na wewe sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Masauni umekuwa ukifanya mambo kadhaa kwa kushirikiana na hao mnaoona wanaweza kuiuwa *CUF,* lakini nikuambie hukuijua ilivyozaliwa na hutoishuhudia ikifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna matukio 13 ya utekwaji wanayofanyiwa watu wa *CUF* na bado watu wa *CUF* tumeendelea kudumisha amani na kuvumilia. Hivi niambieni yule mwendawazimu aliyetumwa na hawa akina

Maftaha juzi, akapigwa pale, kama siyo uvumilivu na ukomavu wa watu wetu, angekuwa hai leo? Angekuwa hai leo kama si ustaarabu? *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Wewe shika adabu yako, kaa chini.*(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Kaa chini.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tuendelee tafadhali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu wameendelea kuilinda...

**MWENYEKITI:** Tafadhali naomba utulivu Bungeni.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu, chama chetu, viongozi wetu wameendelea kuilinda amani na kuhakikisha damu haimwagiki kama anavyotaka Mheshimiwa Masauni imwagike ili apate sababu ya kufuta chama chetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Hamad Masauni juzi uliratibu kikao cha kuhakikisha Tanga Mwenyekiti wetu hafanyi kikao, wewe kwa kushirikiana na Mheshimiwa Maftaha pamoja na *mungiki* wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumevumilia vyakutosha, hatumuogopi Lipumba na ninakuambieni sasa tunamnyoosha Lipumba na watu wake…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kumnyoosha tunao, nia ya kumnyosha tunayo na sababu ya kumnyosha tunayo.*(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Uvumilivu umetuishia, na ninakuambia hawa *mungiki* kwetu hawajai kwenye mkono mmoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Hawa ni wadogo sana, Chama cha Wananchi ni kikubwa sana ndani ya nchi hii, tunawaambia ifike mwisho na wakome, tupo tayari kwa lolote, lakini tutamnyoosha Lipumba na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la mrundikano wa mahabusu mahakamani.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa sana kuhusu mrundikano wa mahabusu ndani ya magereza yetu. Hivi karibuni tunakwenda kwenye mfungo wa Ramadhani ilhali Masheikh wa Uamsho bado wakiwa gerezani wanaendelea kukaa bila kufikishwa mahakamani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, basi muda wako umemalizika. Mnashangilia sana muda unapita hamuoni.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, *mungiki* tutawanyoosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na baadaye Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis na Mheshimiwa Mkuchika ajiandae.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi bila kupoteza muda nichukue fursa hii kukupongeza wewe kwakuniruhusu kuchangia. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa muda mfupi kuwa Waziri katika Wizara mbili tofauti, hii ni kutokana na utendaji wake na umakini wake Mheshimiwa Waziri. Nikupongeze vilevile kwa timu ya *Singida United* kupanda daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Kamishna Hamdani Omar Makame kwa kutuongoza vizuri Zanzibar katika kipindi chake na nimtakie kila la kheri na mapumziko mema ya kikazi. Nitakuwa sijamfanyia haki Kamishna Johari Masoud Sururu wa*Immigration* Zanzibar kwa kazi anayoifanya Zanzibar, amekuwa makini katika utendaji wake bila ya kujali mvua, jua, usiku, mchana anapiga kazi, nimpongeze sana Kamishna Sururu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa sijamfanyia haki Kamishna Musa Ali wa Zanzibar, kwa kujenga vituo vingi Zanzibar vya polisi zikiwemo nyumba. Amejenga nyumba na vituo vya Polisi Paje katika Jimbo langu ninakotokea.Vilevile amejenga vituo cha polisi karibu saba kikiwemo cha Jambiani, Nungwi, Bumbwini, Kiboje, Meli Nne, Fumba, Jozani na Pemba – Chokocho. Mheshimiwa *IGP* huyu mtu nafikiri ni hazina kubwa sana unisikilize kwa makini Mheshimiwa *IGP,* amefanya kazi vizuri sana na kubwa zaidi

kujenga Kituo cha Afya Ziwani katika Makao Makuu ya Polisi, kituo cha kileo kabisa, huyu ni mtendaji kazi kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri hapa unisikilize kwa makini vinginevyo shilingi nitaizuia. Kuna mjenzi nimeshakwambia mara mbili/mara tatu, amejenga nyumba na Kituo cha Madungu anadai shilingi milioni 220, leo mwaka wa tano anahangaika,mpaka akapata maradhi anafanya mazoezi bila kutaka kupata ngazi kwenda na kushuka.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nitakuwa mkaidi sana kama hujamlipa haki yake na Mwenyezi Mungu kamjalia kapata maradhi ya mitihani sasa hivi. Mtu anadai shilingi milioni 220; ameshajenga vituo, leo miaka mitano na baya zaidi hata kwenda kukaguliwa hazijaenda kukaguliwa, hilo ni jambo la kusikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na *IGP* naomba mnisikilize, kumekuwa na kilio cha Wabunge humu ndani kunyanyaswa na wanaambiwa baada ya miaka mitatu muda wao wa Ubunge umekwisha, kuna Mbunge wa Ulanga yumo ndani humu, anaonesha kitambulisho kwa *traffic* anaambiwa wewe baada ya miaka mitatu Ubunge wako unaisha, siyo kauli nzuri hiyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalipigia kelele katika vikao vyetu siku zote. *Traffic* wamekuwa wameshika mpini, Mbunge hana thamani mbele ya *traffic.* Leo Mbunge wa Ulanga yule anaambiwa baada ya miaka mitatu na kitambulisho anatoa, hatuwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu hali za uchakavu wa nyumba, Mheshimiwa Waziri ulikuwemo Ziwani umeona askari wetu wanaishi vipi, mchana haendi kujisaidia, anakaa mtu upande huo huko anamwambia nitizamie mtu anakuja huko, ili apate kwenda chooni! Hali hairidhishi,

mazingira siyo mazuri wanayofanya askari, vitendea kazi havipo, tunafanya nini? Hali ya Ziwani ndiyo Makao Makuu ya Polisi hairidhishi.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile askari wanakaa muda mrefu kupandishwa vyeo, anafika miaka 15 mpaka mtu anakaribia kustaafu hajapanda cheo! Hii siyo halali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vituo vya polisi vimekuwa vichakavu sana, ulikaja Pemba, pia wale wanaojenga mbona hamuwalipi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nichangie kuhusu mahabusu.Polisi wanapata shida wanatoa pesa zao mfukoni kuwahudumia mahabusu.Pia hali ya bajeti Zanzibar kupiga doria, umekuwa mtihani vilevile mafuta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaku, dakika tano zimeisha.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sitaunga hoja mkono mpaka jamaa apate haki yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia, na baadae Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru au kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa umahiri wake anaouonesha Tanzania kuimarisha uchumi, uwajibikaji na maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sina budi kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, mama chapa kazi na tunakuona umevaa viatu vya Marehemu Dkt. Omar Ali Juma, umevaa viatu vya Dkt. Mohamed Shein,

tunakuona unavyoenda mbio na Muungano na Muungano utadumu. Mama unapofika Dodoma mwezi wa Ramadhani, usitusahau katika ufalme wako, *Inshallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie Ziwani Zanzibar katika Jimbo la Jang'ombe. Ziwani marehemu bibi zetu tulikuwa tunasikia wanaita Bomani. Mimi nazaliwa nimeliona Ziwani boma liko vilevile na mpaka leo liko vilevile, kama linatengenezwa matengenezo yake siyo makubwa. Isitoshe unapotaka kuingia bomani njia za panya zimejaa tele, ukaingia ndani na utatoka hakuna atakayekuona ingawa wao wenyewewanatumia milango, kuna milango mizuri na kuna ulinzi, lakini imekuwa ni bure wakati milango iko ya kuingilia na kutoka na humu kuna milango ya panya imekuwa haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu ya uzio, uzio uliojengwa toka ukoloni mpaka leo haujatengenezwa, Ziwa liko karibu na mitaa wanayokaa watu, wametengeneza njia za panya. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aende akaangalie na aweze kutuwekea imara ya boma letu ambalo tunaliamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia vijana wetu hawa ambao katika ukurasa wako wa 11, Mheshimiwa Waziri alizungumza udhibiti wa dawa za kulevya. Najua dawa za kulevya nikizungumzia 'unga' haliko kwenu, kuna kitengo kimeundwa, lakini nalileta kwenu kwa sababu mnao askari wa kutosha wa kusaidia kitengo kilichoundwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu bibi yangu niliwahi kumsikia akizungumza kuna Askari Kanzu ambao ni*CID.* Hawa askari kama mtawatumia wataweza kukisaidia hiki kitengo, kwa sababu hiki kitengo kinahitaji kipate watu na ninyi ndiyo mtakaoweza kuyapangua haya mafiga matatu, kwa sababu kuna mletaji, kuna msambazaji na kuna mlaji. Sasa hawa wote, hili figa hili kama hamkuweza ninyi kuliangalia mkalipangua kwa sababu *CID* anaweza kupenya sehemu zote akampata mletaji, akampata msambazaji, walaji tunawaona kwa sababu picha yao inaonekana, ili

muweze kukisaidia hiki kitengo tuweze kusaidia nguvu kazi ambayo inapotea katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu suala la *NIDA.* Unajua katika bajeti yenu ya mwaka jana, mlizungumza kwamba hiki kitengo mtakiboresha baada ya kupata vifaa kutoka Tume ya Uchaguzi. Vifaa mmevipata, lakini hakuna kinachotendeka. Hatuoni tena *NIDA* kazi inayoifanya, hatuoni kuangalia kuboresha maslahi ya watu, wafanyakazi wa*NIDA* mmewatoa/mmewapunguza, sasa kweli hivi vifaa mlivyopewa vikae ndani ni mapambo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vilivyopo mle ndani viweze kufanya kazi na wafanyakazi ni hawa vijana ambao tayari mmewatoa. Maana mmesema mtafanya utambuzi wa Watanzania, mtafanya usajili wa Watanzania, usajili hauko, upembuzi hauko, watu wanajiingilia na kutoka. Nataka Waziri utakapokuja uniambie, kwa nini mlipunguza wafanyakazi na wakati ulikuwa hujaimaliza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE.KAPT.MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwakunipa nafasi, nitangulie kusema kwamba, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kupongeza sana kazi nzuri inayofanywa na majeshi yetu. Kazi nzuri inayofanywa na askari waliopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, bila wao hapa Tanzania pasingekalika, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pole kwa ndugu zangu wa Rufiji, Kibiti, wajukuu zangu kwa mikasa wanayopata, wanauawa bila sababu, lakini kama mlivyosikia Jeshi la Polisi liko pamoja na ninyi jambo hili la muda litazimwa na majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pole kwandugu wanaohusika na msiba wa jana kule Arusha, niseme jambo moja, mchangiaji mwenzetu mmoja hapa asubuhi alisema kwamba itakuwa vizuri kama kila Mbunge akaonja jela, ili kuweza kujua mambo ya kule ndani. Nataka nimjibu kwamba Wabunge wa Tanzania ni waadilifu sana, tunajitahidi kila tunavyoweza ili tusiende jela na kwa sababu tulimpata mtu kaenda jela katusimulia, imetosha. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nijikite katika Jeshi la Zimamoto. Kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Jeshi la Zimamoto kama Jeshi bado ni change, ilikuwa ni Idara chini ya Jeshi la Polisi lakini baada ya kufanywa kuwa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Wizara mnatakiwa mlilee Jeshi la Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu gani mimi ni Mjumbe ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Nilipotembea Majeshi ya Zimamoto tumegundua matatizo mengi. Kwa mfano, iko Tume ya Majeshi inayopandisha vyeo, kuajiri ni Tume ya Majeshi, Magereza wamo, Polisi wamo, bado hamjawaweka Zimamoto. Sasa kama hawamo kwenye Tume watapandaje vyeo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kule Zimamoto ukimwondoa Thobias Andengenya ambaye ni Kamishna Jenerali wanaomsaidia wote *acting,*hizo bado tangu lilipoanza Jeshi pale mpaka leo wana *act?* Hii inawezekana kwa sababu Tume ya kuwapandisha haipo. Natoa kutoa rai watu wale hatua ichukuliwe haraka, tuwe na Makamishna siyo *acting. (Makofi)*

Suala lingine kuonesha kwamba sisi Wajumbe tuna mashaka kwamba pengine Waziri jicho haliangalii sana Jeshi hilo, asubuhi umetueleza hapa majengo mapya ya Polisi, Uhamiaji, Magereza, tukawa tunasubiri Zimamoto kimya, hata hela kumalizia Zimamoto ambayo tayari wameanza kujenga kule Dar es Salaam, kimya! Niishie hapo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie juu ya magereza. Leo bajeti ya magereza ni kubwa kwa sababu Magereza hawajitoshelezi kwa chakula. Tumetembelea kambi za magereza nyingi tu. Tumekwenda Songwe tumeona ardhi nzuri, eneo nzuri la kulima, walituambia tunaomba Waheshimiwa Wabunge iambieni Serikali itupe matrekta, itupe vifaa vya kilimo, tuna uwezo wa kulima na kugawa chakula kwa magereza mengine, badala ya kuomba hapa Mheshimiwa Waziri hela ya magereza ya chakula omba matrekta wale watu wako tayari kujilisha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni maeneo ya utawala. Leo Wilaya mpya zote zina matatizo ya kiutawala, kwa sababu hawana magereza hawana vituo vya polisi, hawana mahakama. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana inafanywa na magereza kubeba askari kutoka Wilaya mpya kuwapeleka Wilaya mama watuhumiwa kwenda kusikiliza kesi, gharama ile ya mafuta ni kubwa. Ushauri wangu ni kwamba maeneo mapya ya utawala yanapoanza izingatiwe kwanza magereza, kituo cha polisi, mahakama ni sehemu ya utawala. Mkuu wa Wilaya hawezi kukamilika kama hana kituo cha polisi, kama hana magereza, kama hana mahakama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkuchika.

**MHE.KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilidhani dakika zangu ni kumi kumbe tano. Naunga mkono hoja kwa kuombatu kwamba Uhamiaji wajenge kituo cha uhamiaji kule Newala na mmalizie kituo cha polisi ambacho mnasema kimefika asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkuchika. Tunaendelea na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi na mimi nitoe maoni yangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Pia ninamshukuru Mwenyenzi Mungu kutupa afya njema, sisi wote katika Bunge hili ili kuishauri Serikali.

Pili, niendelee kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Babati Mjini kwa msiba ambao tulipata wa wale watoto ambao walipata ajali na Watanzania wote niwape pole, siku ya leo ni mazishi pale mtaa wa Mrara, Mungu awatie nguvu, ni msiba mzito sana ambao kwa kweli ni kazi kuupokea katika mioyo yetu, lakini Mungu atupe faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, haya ninayochangia ni ambayo naona niyaseme kutoka moyoni mwangu. Naomba niseme neno moja la kiswahili kwamba Wabunge tuko hapa kwa ajili ya kusimamia Serikali, lakini kama hatutaacha unafiki toka moyoni, haya malalamiko ya wanajeshi na wananchi wetu hayawezi kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hili kwa sababu unafiki huu tusipouacha tutaendelea kusema Magereza ya Jimboni kwangu, Polisi wa Jimboni kwangu, Zimamoto wa Jimboni kwangulakini wenye matatizo ni sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii bajeti yake ni shilingi bilioni 930, lakini bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 40, kati ya shilingi bilioni 940 ndio za maendeleo. Waheshimiwa Wabunge tunaongea hapa kinafki, tunaongea tu kwa kupapasa wakati wa kupitisha vifungu tunaongeaongea tunakwenda kwenye *guillotine* haya hatuyaongei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufiki kwenye vifungu, hatuongei kwa dhati ya mioyo yetu na kama tukisimama kuisimamia Serikali niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na mimi tuache unafiki. Ikifika saa ya kupitisha vifungu tuitake Serikali waongeze fedha za maendeleo kwa sababu kila Mbunge analalamika kuhusu Polisi kwenye Jimbo lake, Magereza kwenye Jimbo lake, Polisi kwenye Jimbo lake, na Jeshi la Zimamoto kwenye Jimbo lake hawana magari, hawana maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifika kwenye kupitisha vifungu tunaenda mtu anatoa shilingi baadaye anarejesha kishkaji, wakati fedha hazipo huku kwenye maendeleo. Kwa hiyo, ni aibu Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo inalinda Tanzania, fedha za maendeleo shilingi bilioni 40 wakati wanajeshi wanakaa kwenye mabanzi, kwenye bati ndiyo nyumba zao. Unafiki huu utatupeleka pabaya. Mimi ninawaomba Waheshimiwa Wabunge leo, bajeti hii isipite wanongezewe fedha wanajeshi hawa na magereza na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe pole Mheshimiwa Waziri wetu Kivuli Mheshimiwa Godbless Lema, jana alibaguliwa kule Arusha na maeneo mengine. Nimtie moyo tu kwamba ubaguzi huu siyokwa sisi peke yetu, ubaguzi huu upo hata kwa wanajeshi wetu. Nitoe mfano, Jeshi la Magereza katika bajeti hii, hivi tunavyoongea nimeona kwamba Jeshi la Magereza hawajawahi kusikilizwa mambo yao. Niwape mfano, Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi Novemba, alizungumza kuhusu *duty free* hizi bidhaa ambazo zinapelekwa kwenye majeshi yetu, akasema hizi fedha badala ya kuwaletea vinywaji tutakuwa tunawaletea kila baada ya miezi mitatu shilingi 300,000. Ninavyoongea hapa Jeshi la Magereza hawajawahi kupewa fedha hizi, lakini majeshi mengine wamepewa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri utuambie kwa nini mnabagua Jeshi la Magereza. Jeshi la Polisi mmewapa Januari, Aprili mmewapa awamu mbili. Jeshi la Wananchi mmewapa mwezi wa Novemba, Desemba,

awamu mbili. Jeshi la Magereza hamjawahi kuwapa hizi fedha,kwa nini mnawabagua jeshi hili? Wakati Jeshi la Magereza ndiyo linakaa na wananchi ambao wanaonewa, wanabambikiziwa kesi, wanawalinda wahalifu, wanakaa na watu kule wanawavumilia. Wengine hawa mahabusu na wafungwa mnawapeleka kule.

Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikuambia hawana hata *uniform,* hawana hata nguo, mnawapeleka mnawafunga. Wafungwa wetu katika magereza nilifanya ziara katika Gereza la Babati, mtu mzima unakwenda pale unapewa suruali na shati la juu tu hakuna nguo nyingine yoyote ni mfungwa huyo! Jeshi hili wanakaa na watu hawa wasiokuwa na nguo mnawapa suruali tu na shati la juu, nguo zingine *pull neck* na nguo za ndani hamuwapi, halafu watu hawa hawapewi fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mnaita Jeshi la Magereza mnawapenda, mnawasikiliza, hata kwenye nyumba kwenye kitabu cha *development* nimekwenda, nyumba zote ambazo mnakwenda kujenga mnafanya *renovation* ni nyumba za polisi, sina tatizo na polisi wetu lakini Jeshi la Magereza mmewasahau kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie kwa nini ubaguzi huu mnaotufanyia sisi, sasa mnaupeleka kwenye majeshi yetu? Mtakuwa salama vipi? Wewe ni mfungwa mtarajiwa kaka yangu, kesho na kesho kutwa, utakuwa mahabusu pia, uko hapo tu wengine walikuwa hapo na wengine walishaondoka unafahamu, usicheze na Jeshi la Magereza wapelekeeni mahitaji yao na hizi pesa mlizowaahidi muapelekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo niliseme, hizi shilingi bilioni 40 ambazo ninasema tusipoacha unafiki, ndiyo hizi ambazo zinatakiwa ziende kwenye maendeleo. Wafungwa na mahabusu wapate magodoro. Gereza la Babati wafungwa wetu na mahabusu wanalala kwenye magodoro kama *slice* za mikate. Wanaunganisha

unganisha vipande vya magodoro halafu havitoshi wanalala chini. Ukitaka kwenda kupeleka pale mlolongo ni mrefu mpaka uende Magereza Makao Makuu. Mkuu wa Gereza pale hatakuruhusu kupeka hivyo vitu mpaka uandike barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mnaleta mlolongo kwa nini hamnunui vitu hivyo? Magodoro hamnunui, *uniform* hampeleki lakini pia hata chakula *ration* wanazokula hazitoshelezi! Mtuambie ni kwa nini hizi fedha za maendeleo msiongeze kwa sababu kila mmoja ni mfungwa na mahabusu mtarajiwa. Hakuna magodogo huko.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu alifika babati, alifika pale Jeshi la Polisi, nashukuru alienda pale rangi ikapigwa pigwa kwa sababu alienda pale, lakini nilimweleza masuala ya Gereza la Babati, hali ni mbaya na Magereza ya nchi nzima hali ni mbaya, hata magodoro hakuna. Ni vizuri tukakubaliana kwamba fedha hizi ziongezwe.Mfano, Jeshi la Magereza wanatakiwa nyumba 10,526 asilimia 71 hizi nyumba hazipo.Achilia mbali Magereza wanakokaa, lakini asilimia 71 ya Jeshi la Magereza hawana hizo nyumba.Polisi hawana hizo nyumba, Wilaya tano tu ndiyo mmeweka katika bajeti hii. Hivi kweli Waheshimiwa Wabunge tukae tu tunalalamika, kwamba jimboni kwangu, jimboni kwangu, nafikiri hili tulichukue kama Wabunge. Kwamba Wizara hii tunataka fedha za *development* angalau hata bilioni 200 ili tuache kelele za nyumba za Polisi wetu, tuache nyumba zetu za Magereza zijengwe, vinginevyo mnatuachia mzigo mkubwa sana na hili halitokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Magereza Wilaya moja kutokuwa na Gereza. Mfano, Babati pale tuko Makao Makuu ya Mkoa, lakini wenzetu wa Hanang' hawana gereza tunaletewa mahabusu, gereza la Babati sasa lina watu zaidi ya 400 wafungwa pamoja na mahabusu, wanakaa mahabusu wa Hanang' wiki tatu hawapelekwi Mahakamani, *OCD* wa Babati na wa Hanang' hawana mafuta, Polisi wetu hawa wamewaachia mzigo mkubwa

sana, kwenye ziara zao wakubwa wakija pale, wanawaambia watafute magari, wanaanza kuomba matairi yako wapi, mafuta yako wapi, hata fedha hawapeleki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanashindwaje kujenga Gereza Hanang' wanarundika pale, watu wanasukumana pale, chakula hakitoshi, hawapelekwi Mahakamani, wanakosa haki zao. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu, naomba nifahamu na atuunge mkono kwa kweli, siyo baadaye aseme hela hazitoshi wakati anajua Hanang' hakuna gereza, Babati msongamano ni mkubwa kwenye Gereza letu la Wilaya. Atuambie ni lini la Hanang' litajengwa ili wananchi wa Babati wanapoingia kwenye lile Gereza, wasisongamane kiasi hicho kwa sababu hizi fedha hazitoshi na yeye atuunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine suala la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto wanafanya kazi nzuri na wanakusanya...

**MHE.DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul naomba upokee taarifa kidogo.

**TAARIFA**

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa kwamba Mbunge wa Jimbo la Hanang' yuko hapa, Mheshimiwa Pauline Gekul ni Mbunge wa Jimbo la Babati aongelee mambo ya Babati...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la Magereza ya Hanang' aniachie mimi nina uwezo huo wa kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul unapokea hiyo taarifa?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Mary Nagu alikuwa Waziri kwa muda mrefu kweli, nataka nimpe taarifa kwamba, Wilaya ya Hanang' hakuna Magereza na haya mambo anayoyaombea taarifa hapa alipaswa ayaongee miaka 15 iliyopita alipokuwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul umepokea taarifa hiyo?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nisaidie tu kulinda muda wangu. Naomba nipokee taarifa ya Mheshimiwa Nagu ni dada yangu, naomba tu nikwambie dada ulikuwa haujalisemea ndiyo maana mpaka leo hakuna Gereza, kwa hiyo acha nikusaidie mdogo wako nikusemee. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Gekul muda wako umekwisha umepokea taarifa vizuri...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Haujakwisha Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naendelea.

**MWENYEKITI:** Umepokea taarifa vizuri muda mambo yamekwisha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Imetosha Mheshimiwa naomba ukae.

Tunaendelea na Mheshimiwa Pondeza, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji,wajiandae kwa dakika tatu tatu.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze

kushiriki katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nijielekeze kwenye maeneo ya Jimbo langu la Chumbuni ambalo lina matatizo ya Kituo cha Polisi ambayo bajeti ya mwaka jana niliyasema na kikaahidiwa kuwa nitapatiwa matengezo na nitapatiwa kituo katika Jimbo langu la Chumbuni Zanzibar, mpaka sasa hivi sijapata. Nilikuwa na kituo kimoja tu kidogo ambacho mpaka sasa hivi nacho hakifai kinavuja, kazi hazifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa zaidi ambalo nataka kulisema hapa leo ni vitendea kazi vya Jeshi la Polisi hususan Zanzibar. Polisi wetu hawana vifaa vya kutendea kazi sana hasa hasa Jeshi letu la *Traffic*. Unakuta Jeshi la *Traffic* wanaongoza magari kwa kutumia simu zao za mkononi. Redio hawana, hata *section* nne hazifiki, vitendea kazi ambavyo ni muhimu. Tumeshuhudia Zanzibar mara mbili ama mara tatu Viongozi wetu Wakuu wa nchi, madereva wanaingilia misafara yao kutokana na kutokuwepo kwa taarifa ambazo zinakuwepo kabla,hii yote ni kutokana na ukosefu wa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Jeshi la Polisi Zanzibar lina deni katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika vikosi vyake vya Jeshi la Kujenga Uchumi yaani *JKU* ni kitengo cha *NIDA* mamlaka ya Vitambulisho, wanadaiwa karibu milioni 172 ambazo hawajazilipa mpaka sasa hivi. Nataka kujua leo hapa lini watazilipa fedha hizi milioni 172 katika JKU ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho napenda ambacho napenda kushauri Jeshi letu la Polisi au Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, linaonaje likafikiria kuweka sheria hata wale ambao ni Makamishna wa Jeshi hili. Kwa mfumo uliopo nafahamu wapo Makamishna tisa, kuanzia Kamishna Kaniki, Kamishna Amdan, Kamishna Musa na wengine wapo tisa, wakistaafu anayefahamika kwa

mafao ni *IGP* peke yake. Kwa nini, Jeshi la Polisi lisiwe na mfumo kama Jeshi la Wananchi Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruhusa hii nami kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nichangie kwenye kituo changu cha Bububu.Kituo cha Bububu hakina Kompyuta, hakina *photocopy machine, copy* wanakwenda kutoa nje ya kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu matundu ya choo. Matundu ya choo hali ni mbaya katika kituo changu cha Bububu. Askari wanawake wanatoka nje wanakwenda kujisaidia na wao hawako salama, kwa sababu tunaijua Bububu ilivyo ni hatari. Tunamwomba Waziri kile kituo akitendee haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la watani zangu. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, katika Jimbo langu kulikuwa na uhalifu mkubwa sana, amejitahidi uhalifu ule umepungua kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kule sasa hivi wameanza kujikusanya vikundi wakiwa wanazungumza tunaita Zanzibar *drip,* wanasema uchaguzi upo kesho Maalim Seif anapewa nchi kesho. Tena niwahakikishieni kama ni

uchaguzi umemalizika na tusubiri mwaka 2020, baada ya miezi mitatu, minne tutakuwa na wagonjwa wa hali nyingi, wagonjwa wa wasiwasi na wagonjwa wa presha kwa sababu akikaa tu Maalim Seif kesho anapewa nchi. Uchaguzi umemalizika tufanyeni kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye kituo changu cha Polisi Bububu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Basi awe na heshima zake.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alijitahidi sana kwa sababu pale palikuwa na Mwekezaji, wameondoka na kituo kipo salama kwa sababu sisi wenyewe wananchi tulikuwa hatuko salama kwenye kituo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Waziri kwa hali aliyoichukua pale kwenye kituo akamwondoa yule mwekezaji na sasa hayupo, nashukuru kituo kimebakia salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantakaje.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia juu ya mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantumu Dau na Mheshimiwa Ali Hassan Omar ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi

Mungu mwingi wa rehema na vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu ndogo kwa hiyo siwezi kusema mlolongo mkubwa. Naipongeza hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba hii ambayo ni nzuri, aliyoipanga na haina mjadala, isipokuwa kuna mambo tu madogo madogo yaweze kuwekwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Polisi Daraja 'B' Mkokotoni Unguja kina asilimia 60 na haya ninayozungumza yamo katika hotuba hii. Kituo hiki kina asilimia 60 Mkokotoni tayari kimeshakuwa kimefanikisha, lakini kuna vituo humu nchini ambavyo havina hadhi na havina mashiko. Tukizingatia katika Mkoa wangu wa Kusini Unguja kituo hiki cha Paje ambaye hapa kidogo mwenye hili Jimbo alilizungumzia lakini hakulitoa sahihi sana. Kituo kile hakina hadhi na ukipita pale utahisi kama hiki siyo kituo cha Polisi, kama wenyewe watakuwa hawapo pale nje basi huwezi hudhani kwamba hiki ni kituo cha Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo pia hiki kilikuwa kimo ndani ya mgao kwamba kitengenezwe na kiwe kituo cha hadhi cha Wilaya ya Kusini, naomba kama hili suala kweli lipo basi hiki kituo kiweze kutengenezwa kwa sababu ukanda mzima ule ni ukanda wa watalii na watalii wote waliopo kile kituo hiki ndicho kinachohusika kuanzia Jambiani hadi Michamvi. Naomba kituo hiki kitengenezwe kuwa kituo cha hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantum. Tunaendelea na Mheshimiwa Ali Omari.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naungana na wote waliotoa rambirambi na naungana na wote walioongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze haraka mambo matatu, katika kifungu ambacho kinahusiana na umeme, mafuta na redio Zanzibar ni tatizo. Fedha zilizotengwa hazitoshi katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mkoa wa Mjini Magharibi una Wilaya tatu na una jumla ya vituo 14, Askari wanachangishana wenyewe katika vituo hivi. Kwa hiyo, hapa namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya maendeleo, niliahidiwa ukarabati wa nyumba za Polisi, ukarabati wa Makao Makuu ya Polisi na niliahidiwa uzio pamoja na nyumba mpya za Polisi lakini bado hayajafanyika. Hapa kuna kituo kimoja cha Mkokotoni hicho ambacho kimetajwa.Kwa hiyo, hiyo naomba katika miradi ya maendeleo waje watuangalie vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo hapa lilizungumzwa naona kwamba bora na mimi nigusie, haiwezekani ugomvi wa nyumbani kwako ukaenda ukamtumpia jirani yako. Wewe umeachia ushuzi katika nyumba yako, harufu ya ushuzi ule unamsingizia jirani, jitazameni ninyi wenyewe, CCM haishiriki katika mgogoro wa*CUF* na ndiyo maana tunasema la kuvunda halina ubani. Hiyo ni*sakaratul maut,* mtu anapokuwa katika *sakaratul maut* anakuwa mara nyingi hajitambui, kwa hiyo, hiyo mtambue ni *sakaratul maut* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu mlijue kilichowaponza ni tamaa zenu wenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mlihisi mnakuja kupokea mapesa kumbe ndiyo mmekwenda kukiua Chama. Kwa hiyo, ni ninyi wenyewe, mgogoro wenu wenyewe kwa

tamaa zenu wenyewe, msisingizie Chama cha Mapinduzi hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine ambalo ni muhimu mzingatie kwamba hayo mambo mliaza ninyi wenyewe ukaribishaji, utoaji, kumuingiza huyu kwenye Chama, kumtoa huyu mlifanya wenyewe, CCM imehusika wapi? Mjiangalie vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika hoja moja ambayo alizungumza hapa mtu haki za binadamu katika Magereza. Haki za binadamu katika Magereza ni lazima ziangaliwe pamoja na usalama ndani ya Magereza. Ndiyo maana hapa ikasemwa kwamba watu wanapekuliwa mabanda ya uwani, mabanda ya uwani lazima watu watapekuliwa, anaweza mtu akaingia na shazia ikahatarisha usalama, akaingia na msumari, anaweza mtu akaingia na silaha yoyote. Kwa hiyo, nimpe pole au kama nimpe hongera Mheshimiwa Lema kama na yeye yalimkuta haya ya kupekuliwa mabanda ya uwani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa King muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaya wenyewe unaweza ukaja ukamkuta mwanaume mwenzako anakuvalia *gloves* halafu anaanza kusema *mashallah,* lazima utakuja kusema hivyo hapa...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, naomba ukae tafadhali.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili nalizungumza maksudi ili watu waache kuota ndoto za kipuuzi na kutangaza hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza mjadala upande wa Wabunge. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika 25 na baadaye Mheshimiwa Waziri atamalizia kwa dakika 35.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kutumia fursa hii kumshukuru sana kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini kwenye majukumu haya muhimu. Naomba nitumie methali ya wahenga fupi tu ambayo inasema kwamba imani huzaa imani, mimi na Mheshimiwa Waziri ambaye kwa kweli amekuwa akinipa ushirikiano wa hali ya juu na msaada mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yangu, tutaendelea kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu muhimu wengi kweli wa kuwashukuru lakini kwa kuwa muda ni mfupi, naomba moja kwa moja niende katika hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mengi sana, wengine kwa kuzungumza na wengine kwa maandishi. Kwa muda huu inawezekana siyo hoja zote za Waheshimiwa Wabunge tutakazoweza kuzipatia majibu, lakini zile ambazo hazitapatiwa majibu kwa njia ya kuzungumza tutawapatia majibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya suala la usalama barabarani. Leo hii tunazungumzia changamoto ya usalama barabarani katika nchi yetu katika kipindi ambapo Taifa tumepata msiba mkubwa sana wa ajali ya basi lililojeruhi na kuua watoto na vijana wetu ambao walikuwa wana shughuli za masomo. Naomba Mwenyezi Mungu atupe moyo wa subira pamoja na wazazi wa watoto

hawa katika kipindi hiki kigumu. Wakati tukiendelea kuomboleza msiba huu mzito, inaweza ikawa vigumu sana kueleza kwamba katika eneo hili la usalama barabarani tumefanya kazi kubwa sana katika kipindi cha mwaka mmoja na tumefanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikisha azma yetu hii ya kupunguza ajali za barabarani kuna hatua kadhaa tulizichukua. Moja katika hatua ambazo tulichukua tulianzisha mkakati kabambe wa miezi sita ambao ulikuwa na lengo la kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia kumi. Kiukweli mkakati huo umefanikiwa kwa kiasi cha kuridhisha ingawa tumegundua changamoto nyingine za hapa na pale ambazo tutazifanyia kazi. Mkakati huu ulizingatia mambo makubwa matatu ambayo ni vyanzo vya ajali barabarani ambavyo vinasababishwa na makosa ya kibinadamu, ambapo mara nyingi makosa haya yanatokana na uzembe wa madereva wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni kwa asilimia ndogo ni changamoto ya miundombinu yetu na changamoto ya ubovu wa magari. Kwa hiyo, mkakati wetu ambao ulilenga maeneo 14 zaidi uliangalia maeneo hayo matatu. Leo hii nimesimama hapa mbele yako na mbele ya Waheshimiwa Wabunge kuelezea tathmini kwa ufupi ya mafanikio hayo ambayo tulilenga kupunguza asilimia kumi ya ajali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa mkakati ule wa miezi sita tumefanikiwa kupunguza kwa upande wa ajali za magari ambazo zinasababisha madhara makubwa, tumefanikiwa kupunguza ajali za vifo kwa asilimia nane, hatukufikia asilimia kumi lakini tumekaribia, asilimia nane. Katika ajali za majeruhi tumevuka viwango na kufikia asilimia 13. Kwa upande wa pikipiki tumefanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 17 zile ajali ambazo zinasababisha vifo lakini kwa majeruhi wa pikipiki hatukufanya vizuri sana na ajali ziliongezeka kwa asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ukiangalia utaona kwamba kwa kiwango kikubwa ajali hizi zimefanikiwa kupungua katika kipindi hiki cha miezi sita. Mkakati huo wa miezi sita ndiyo uliopelekea mafanikio ambayo leo hii tunajivunia kipindi cha mwaka mmoja wa kupunguza ajali kwa asilimia 7.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto mbalimbali ambazo tunakabiliana nazo, najua eneo hili limeguswa na Waheshimiwa Wabunge wengi, nitawataja baadaye ambao wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto ambazo tumekabiliana nazo kama ambavyo baadhi ya Wabunge waliochangia wamezungumza, moja ni changamoto ya sheria yetu tuliyonayo sasa hivi, ambapo baadhi ya mambo yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Kuna mambo machache ambayo nitayataja kwa haraka. Kwanza kunahitajika kuongeza ukali wa adhabu katika sheria yetu, vilevile kunahitajika kuongeza idadi na aina ya makosa ambayo hayamo katika sheria ya sasa hivi. Kwa hiyo, katika mambo 14 ambayo tumeyaangalia moja lilikuwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo tumeyaangalia na Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza kwa uchungu kabisa, kwamba kuna tatizo kuhusu Askari ya Barabarani, wengine wamefika mpaka kusema Askari wanakaa juu ya miti. Tuna changamoto moja ya kisheria, lakini kuna changamoto vilevile nyingine ya kimfumo wa nchi yetu. Tunapozungumza sasa hivi tunatumia mfumo ambao tumeingia mkataba na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wetu tulikusudia kwamba tuweze kutumia utaratibu wa nukta, kwamba mtu atakapokuwa amefanya makosa aweze kupunguziwa *points* na baadaye ikiwezekana leseni yake ipunguzwe. Mkakati huu umeshindwa kufanikiwa kwa sababu ya utaratibu wa huu mfumo tulionao. Tunatarajia baada ya mkataba huu kumalizika Juni tutaingia katika mfumo

ambao umeandaliwa na Jeshi la Polisi, mfumo huu tunatarajia kuoanisha na mfumo unaotumika *TRA* ili tuweze sasa kutumia utaratibu wa nukta na hii itasaidia sana kuweza kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya matumizi ya teknolojia ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza. Hili ni jambo ambalo katika mkakati wetu wa awamu ya pili tunatarajia kuanzisha na tutalipa kipaumbele ikiwemo utaratibu wa kuweza kuweka vidhibiti mwendo badala ya kutumia hizi tochi za sasa hivi ambazo zinatumika barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna mambo mengine ambayo yamezungumzwa kuhusiana na changamoto za Askari wetu wa barabarani. Nataka tu nichukue fursa hii kutoa takwimu za haraka kwamba kuna Askari wengi sana ambao katika kipindi cha mkakati huu katika mambo 14 tuliyoyazungumza kwamba tutahakikisha tunashughulikia wale ambao wanakiuka maadili wakati huo huo tunawapongeza wale ambao wanafanya vizuri. Kuna orodha ndefu ya Askari ambao wamefanya kazi vizuri na kuna orodha ndefu yaAskari ambao tumewapongeza ambapo mara nyingi hawa ambao wanafanya kazi nzuri ambao ndiyo wengi huwa hawaonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba tunatarajia kuanzisha awamu ya pili ya mkakati wetu wa kupunguza ajali, baada ya kuona mafanikio na upungufu ambao nimeuzungumza, sasa hivi tunajikita zaidi katika kuangalia utaratibu wa aina ya madereva waliopo nchini mwetu. Leo hii naomba nichukue fursa hii kukazia maagizo ya Mheshimiwa Makamu ya Rais aliyoyatoa juzi kuhusiana na kuhakikisha kwamba ukaguzi wa kina unafanyika kwa upande wa madereva ya mabasi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kutoa maagizo hapa kwa Jeshi la Polisi kuanza operesheni maalum ya kusaka na kukagua mabasi ya wanafunzi

pamoja na madereva ambao wanaendesha magari haya ili sasa hivi tuweze kuona kwamba eneo hili ambalo lilisahaulika kwa kiasi fulani, liweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hali ya usalama barabarani, naomba sasa niingie katika hali ya kisiasa kwa ujumla wake. Upande wa hali ya kisiasa nchi yetu ipo salama juu ya matukio na changamoto za hapa na pale, hali ya usalama kwa ujumla katika nchi yetu ni ya kuridhisha. Tumepita katika kipindi kigumu sana, katika kipindi cha mwaka mmoja nchi yetu imekumbana na majaribu mbalimbali na ninyi ni mashahidi. Tumeweza kuona matukio ya uhalifu ya aina yake ambayo yametokea kule katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, maeneo ya Mbagala na mengine ambayo yamehusisha mpaka uuaji wa Askari wetu. Yote haya ambayo yamejitokeza katika kipindi cha nyuma tuliahidi hapa Bungeni kwamba tutashughulika nayo na tumeshughulika nayo kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo inaendelea kujitokeza sasa hivi katika Mkoa wa Pwani, nina hakika tutafanikiwa kuweza kudhibiti hali ile na hali ya usalama iweze kurudi kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza vilevile jambo lingine la muhimu sana na la msingi kwamba katika kufanikisha lengo hili ni lazima wananchi watoe mchango mkubwa, wananchi ndiyo ambao wanakaa na jamii na wahalifu huko. Kwa hiyo, bila kulisaidia Jeshi la Polisi kazi hii inaweza isiwe na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama Zanzibar; Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia jambo hili, kimsingi ni kwamba hali ya usalama Zanzibar nayo ni shwari. Nilisikitika sana nilipofanya ziara kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge nilipotembelea Majimbo yao akiwemo Mheshimiwa Mwantakaje kuona kwamba katika Zanzibar ambayo naifahamu mimi kuna baadhi ya maeneo yalikuwa hawezi kupita raia. Nachukua fursa hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya

kuweza kuhakikisha maeneo yale yanaendelea kurudi katika hali ya kawaida na wananchi wanafanya kazi zao kwa usalama na amani. Kwa hiyo, hali ya usalama kwa ujumla katika nchi yetu inaendelea kuimarika na itazidi kuimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo limezungumzwa; suala hili la mgogoro wa Chama cha *CUF.* Hapa hatuwezi kupoteza muda kuzungumza migogoro ya Vyama vya Siasa, hiyo siyo kazi yetu. Jeshi la Polisi linafanya kazi yake kwa mujibu wa sheria, weledi na maadili. Kama kuna vyama ambavyo labda maji yapo shingoni migogoro yao imewashinda wenyewe kwa wenyewe wanatafuta mtu wa kumsuluhisha, siyo kazi ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi kazi yake ni kusimamia sheria, ndiyo maana nasema kwamba matukio ambayo yametokea ya ugomvi wa vyama vya siasa wenyewe kwa wenyewe hatuwezi tukaruhusu umwagaji wa damu wa raia yeyote. Kama mna migogoro yenu, mtafute njia sahihi ya kuirekebisha. Anapotokea mfuasi wa chama chochote, iwe ndani ya chama hicho hicho anawasilisha taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya mwelekeo wa uvunjifu wa amani, Jeshi la Polisi haliwezi kuruhusu hiyo hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana, kwamba leo asubuhi nimeangalia *TV Channel Ten,* nimeona kwenye taarifa ya habari ya *Channel Ten* leo hivi asubuhi kwamba Chama cha *CUF,* wamefanya mkutano wa hadhara uliovyoelezwa na Waandishi wa Habari kwa mujibu wa *TV* ya *Channel Ten*, wamefanya mkutano wa hadhara na mazingira yameonesha ni mazingira ya maandamano. Nataka nimuagize *IGP* hapahapa kulichunguza hilo jambo. Tumepiga marufuku mikutano ya hadhara isipokuwa kwa Wabunge wa Majimbo hayo, tumeona watu wamekusanyika wameenda kufanya mikutano ya hadhara, hilo jambo lazima lichunguzwe na hatua stahiki zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipo hapa kujibu hoja za Mheshimiwa Khatib maana marehemu Bibi yangu alinifundisha hadithi moja kwamba kama umeenda kuogelea baharini halafu akatokea mwendawazimu akachukua nguo

zako huwezi kumkimbiza, wewe utaonekana mwendawazimu zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Magereza. Katika jambo ambalo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambalo ni aibu kwamba kwa idadi ya nguvukazi ya wafungwa tulionao na kwa idadi ya rasilimali ya mashamba makubwa tuliyonayo katika maeneo ya Magereza haiwezekani hata siku moja, hatuwezi kukubali chini ya uongozi wa Wizara hii ikiwa Mheshimiwa Mwigulu ni Waziri na mimi Naibu Wake namsaidia, kuona kwamba jambo la Wafungwa kuendelea kula bure, hali ya kuwa tuna mashamba yenye nafasi ya kutosha na tuna rasilimali na nguvukazi ya kutosha. Tumejipanga vizuri katika hilo kuhakikisha kwamba utegemezi wa chakula katika Magereza yetu unapungua kama siyo kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya idadi ya Magereza yetu ni 129 ambayo yana jumla ya ekari zaidi ya 300,000. Miongoni mwa Magereza haya, ya kilimo ni 48 ambayo yana takribani ekari zaidi ya 150,000. Kuna mikakati kadhaa ambayo tumeichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; tumejaribu kuangalia uwezekano wa kuwavutia Wawekezaji waweze kushirikiana na Jeshi la Magereza kuzalisha. Nichukue fursa hii kuyapongeza sana mashirika yetu ya pensheni, leo tunapozungumza hapa Gereza la Mbigiri tayari wameshaingia mkataba na *NSSF* katika kuzalisha siyo tu miwa vilevile kuanzisha kiwanda cha sukari. Wakati jitihada hizo za kuvutia wawekezaji werevu zikiendelea, tunaendelea kuhakikisha kwamba Magereza ambazo zipo karibu na mito tunaanzisha kilimo cha umwagiliaji kama ambavyo tumefanya katika baadhi ya Magereza mfano, Idete, Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi tuna mpango katika kipindi chetu hiki cha mwaka mmoja unaokuja kuhakikisha kwamba tume-*earmark* Magereza 11 kwa ajili ya kuzalisha pamoja na mifugo katika kilimo cha mpunga,

mahindi na mawese. Matarajio yetu ni kwamba tuzalishe takribani tani 13,260 kwa kutumia Magereza hayo ambayo tumeyachagua. Mahitaji ya sasa hivi ya chakula kwa wafungwa ni takribani tani 10,740, tutakapozalisha tani 13,260 tuna uwezo wa ku-*cover* mahitaji yote ya wafungwa, wakati huo tukaweza kuwa na chakula cha ziada cha takribani tani 2,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutusaidia kupata matrekta 50 ambayo mchakato wake umeshaanza, kati ya hayo matrekta 50 yatakayopatikana yatasaidia kuhakikisha kwamba mpango wetu huu wa kuhakikisha kwamba Magereza yanajitegemea kwa kilimo unafanikiwa, leo hii matrekta matatu tayari yapo katika Gereza la Mbigiri kwa ajili ya shughuli za kilimo cha miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba wafungwa wafanye kazi, tumehakikisha kwamba tumefanya kazi hiyo na mafanikio yake ni makubwa sana. Siyo tu kwamba wafungwa hawa watashirikishwa katika kilimo, leo hii Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Magereza Ukonga, leo hii nimesimama hapa nikiwa nimefarijika sana, kwamba tumefanikiwa kuokoa takribani nyumba 80 za ziada kwa kuwatumia wafungwa, jambo ambalo pengine tungetumia utaratibu mwingine nyumba hizi 80 tusingeweza kuzipata kwa ajili ya nyongeza ya Askari wetu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo faida ya kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba wafungwa tunawatumia ipasavyo siyo tu kwa kuzalisha lakini kwa kusaidia kuwajengea uwezo ili waweze kwenda kujitegemea watakapotoka huko kwenye Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba hiyo haitoshi, tayari tuna programu mbalimbali za kurekebisha wafungwa katika Magereza yetu mbalimbali ambayo sina haja ya kuyataja kutokana na muda kwani yapo mengi. Katika bajeti yetu ya mwaka huu tumewekeza takribani shilingi bilioni 2.2

ambazo zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kuimarisha viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ushiriki wa Magereza katika uchumi wa viwanda hatuzungumzii viwanda vikubwa tu, mpaka viwanda vidogovidogo, tunapozungumzia viwanda vya karanga Mbigiri, lakini wenyewe ndani ya Magereza kuna viwanda kwa mfano, katika bajeti hii katika fedha hizi tunatarajia kuanzisha kiwanda cha *helmet* pale Ukonga, kiwanda cha useremala Isanga, Dodoma, kwenye kambi ya Kimbiji tunatarajia kununua mashine vilevile kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha mawese, pamoja na Gereza la Lindi - Machole ambapo kuna kiwanda cha chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba niende kwenye Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto jambo kubwa na la msingi ambalo tunaliwekea kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunapata kwanza vifaa vya kutosha ili tuweze kudhibiti majanga ya moto yanapotokea, pia vifaa hivi viweze kuenea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu hasa katika Wilaya ambapo huduma hii haijafika. Hivi sasa kuna huduma ya Zimamoto katika mikoa yote lakini kuna wilaya nyingi ambazo bado huduma hii haijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika kipindi cha mwaka mmoja tunajivunia mafanikio makubwa kwamba, tumeweza kuanzisha Zimamoto katika Ofisi za Wilaya takribani nne ikiwemo Ruangwa, Ukerewe, Ileje na Rungwe. Nilipokwenda Ruangwa na Rungwe tuliwaahidi kwamba tutawapatia gari. Bahati mbaya zile gari tulizoahidi zimepata changamoto lakini hii ahadi iko palepale, gari nyingine zitakapofika kipaumbele kitaelekea katika maeneo ambayo tumetoa ahadi ili yaweze kusogeza nguvu na jitihada ambazo tayari zimeoneshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi wakati mkakati huu wa kueneza huduma ya Zimamoto Wilayani unaendelea, tunaanza kupeleka huduma ya elimu katika wilaya zetu, kuhakikisha kwamba tunatafuta Askari kwa ajili ya kupeleka elimu ya kinga na tahadhari ya moto. Hilo jambo limekuwa likifanyika kwa mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali nchini na tunaomba Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katika bajeti hii tumetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari manne, kuna mkakati kabambe utakapofanikiwa wa kupata mkopo wa fedha zitakazosaidia kupata vifaa vya kisasa kupitia mkopo wa Benki ya *KBC* chini ya kampuni ya *Smart* ambayo mazungumzo yanaendelea vizuri. Tunatarajia katika mpango huu kununua magari 21 pamoja na vituo vitatu vya kisasa vya zimamoto na uokoaji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatarajia kuingia mkopo mwingine wa*Euro* milioni tano ambapo unatarajia kutolewa na Serikali ya Austria kupitia *Raiffeisen Bank* ambapo tunatarajia kununua magari pamoja na vitendea kazi vingine. Kwa hiyo, utaona kwamba kuna jitihada kubwa ambazo tumezichukua katika kuhakikisha kwamba tunaimarisha vitendea kazi katika Jeshi la Zimamoto pamoja na kuweza kusogeza huduma hizi karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA)*. Kabla sijazungumzia Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA),* kabla kengele yangu haijalia, naomba nichukue fursa hii kuwatambua kwa haraka, maana niwatendee haki Waheshimiwa Wabunge wametoa michango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hoja ya usalama barabarani ambayo Mheshimiwa Lucy Owenya,

Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Oscar R. Mukasa, Mheshimiwa Raza, Mheshimiwa Risala Kabongo, Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, hawa walichangia wengine kwa maandishi na wengine kwa kuzungumza hii hoja ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja ya hali ya kisiasa, Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Makilagi, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Faida, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Sofia Mwakagenda, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Mwantakaje pamoja na Mheshimiwa Ali King walichangia kwa kiasi fulani kwa maandishi na kwa kuzungumza hoja ya hali ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Magereza wachangiaji walikuwa ni wengi vilevile; Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Risala Kabongo, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Mkuchika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hii hoja ambayo nimemaliza nayo muda huu mfupi uliopita ya zimamoto; Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, wote hawa walichangia hii hoja ya zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hii hoja ambayo namalizia sasa hivi ya *NIDA,* kuna wachangiaji wawili ambao walichangia kwa maandishi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Bobali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge kutokana na michango yao mizuri, naomba sasa nimalizie kwa haraka hoja ya Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA).* Kuna hoja mbili kubwa ambazo zilizungumzwa. Moja, ni kwamba malengo hayajafikiwa, tulikuwa tuna *target* ya kufikia malengo ya kusajili watu zaidi ya milioni 22, mpaka mwezi wa Machi tumesajili zaidi ya watu milioni nane, wakasema kwamba inakuwaje hali hii inajitokeza wakati tayari tumeshapata *BVR* kutoka Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba *BVR* za Tume ya Uchaguzi zina changamoto zake. Kwanza *BVR* za Tume ya Uchaguzi zinatambua taarifa zisizozidi 40 wakati taarifa ambazo zinahitajika kutumika na mfumo wa *NIDA* ni taarifa 72, hilo moja. Hata *quality* ya picha na*fingerprints* kwa upande wa mfumo huu wa *BVR...*

*(Hapa muda kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kengele ya pili, naomba umalizie sentensi yako ya mwisho.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa namkaribisha Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhitimisha hoja baada ya kuwa tumepata michango toka kwa Kamati, kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani na kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwashukuru wote waliochangia, tukianza na maoni ya Kamati, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo mmetoka kuchangia hivi punde. Wizara tumeyapokea maoni yenu, tutayafanyia kazi na tutayachambua yale ambayo yanahitaji ufafanuzi wa kina zaidi, tuweze kuyajibu kwa maandishi. Kwa yale ambayo mmetupa ushauri ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ujumla wake kwa sababu hoja ni nyingi, niwaambie tu kwamba tumeyapokea na tutayafanyia kazi, kama ambavyo tumekuwa tukipokea ushauri kutoka kwenu mnapokuwa mmetimiza wajibu wenu wa kikanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja za jumla kabla sijaenda kwenye hoja mojamoja kati ya hoja ambazo zilijitokeza. Hoja ya kwanza ambayo imeongelewa kwa upana ni hii ambayo ilikuwa inahusisha mambo ya Vyama vya Siasa pamoja na Wabunge na ndugu yangu Mheshimiwa Lijualikali akasemea kwamba labda haya yanafanyika kwa Wabunge wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke kumbukumbu sawa; moja, vyama vingi vya siasa kwenye nchi yetu viko kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa sababu viko kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila Mtanzania kuwa kwenye chama anachokitaka si kosa. Mtu anapokuwa kwenye Chama chake siyo kosa. Ikumbukwe tu kwamba wakati vyama vingi vya siasa vinaanzishwa kilikuwepo chama kimoja tu, Chama cha Mapinduzi na kwa aina ya watu waliokuwepo na maoni

yaliyotolewa kulikuwepo na fursa pana zaidi ya kuwa na chama kimoja kuliko kuwa na vyama vingi, kwa maana hiyo Chama cha Mapinduzi kwa ridhaa yake ndiyo kilianzisha vyama vingi na kama Chama cha Mapinduzi kilianzisha vyama vingi na tangu vyama vingi vianzishwe Chama cha Mapinduzi hakijawahi kuyumba kuhusu ushindi wake, kuanzia ngazi ya vijiji mpaka ngazi ya Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, panatokea kamsukosuko kadogo mnaanza kutafuta mchawi, mara wanasema wanatumiwa mara wanasema wanatumwa na juzi nilimsikiliza Kiongozi wenu Mkuu akisema hao wanatumwa. Niwatoe hofu, Serikali pamoja na Chama haiwezi ikaanzisha yenyewe vyama vingi na yenyewe ikaanza kushiriki kuviondoa vyama hivyo, kwa sababu hata hivyo haijawahi kupata tishio lolote na uwepo wa vyama vingi bali imepata faida na uwepo wa vyama vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, katika mazingira haya, niwashauri kitu kimoja, ndugu yangu Mheshimiwa Khatib Said Haji, ndugu yangu Mheshimiwa Katani walioongea, panapokuwepo na misukosuko ni wakati wa kutulia, huu nimewapa tu ushauri kwa kifupi ni wakati wa kutulia. Pia panapokuwepo na mizozo inayotishia usalama wa raia litakuwa jambo la kushangaza kama watu ambao wana jukumu la kusimamia usalama wa raia wasipoingilia kati, wakiingilia kati hilo ndilo jukumu lao, kwa sababu leo hii kukitokea jambo ambalo linatishia watu kupigana halafu Polisi kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani wakawa wameshapewa taarifa wasiende watakuwa hawajatimiza wajibu wa kulinda usalama wa raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pande zozote zile, hata mechi tu za mchezo wa ndondo, wakiona pana tishio la

usalama wanaita Polisi wanaenda kuwasaidia. Kwa hiyo, ndugu zangu pande zote zinazoona mnatofautiana mkiona mna shida toeni taarifa ili polisi iweze kuingilia kati. Sisi tusipoingilia kati tutakuwa hatujatenda haki ya kuwahakikishia raia wa Tanzania usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira kama hayo, mambo ya aina hii, niwaombe msitafute mchawi nje yenu, tumieni Katiba yenu, tumieni taratibu zenu ili muweze kulimaliza jambo hilo na nchi yetu inufaike na malengo yaliyokusudiwa kwa ajili ya uwepo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, Mheshimiwa Katani ndiyo amenichekesha zaidi, anasema kulikuwepo na mkutano wa ndani kule kwao, mkutano wa ndani tu, halafu ndiyo anatolea mfano kwamba Waziri ulitamani mpaka Urais halafu hukuingilia kati ume-*prove failure.* Unajua kwa mtu anayetamani mpaka Urais kuingilia kitu ambacho *OCD* tu kinamtosha na yenyewe haijakaa sawa. Jambo ambalo lilikuwa la mkutano wa ndani la kibali cha mkutano wa ndani, hilo ni jambo ambalo Mkuu wa Polisi wa ngazi ya Kata ile anaweza kulimaliza na inapotokea limeshapita ngazi zote zile, basi utaratibu unaelekeza kukata rufaa kwa maandishi kwenda kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kupata rufaa hiyo ambayo inaelezea kwamba kuna jambo mahali fulani limeshindikana, mara zote inapotokea jambo limetokea la aina hiyo niwashauri kwamba tumieni taratibu, tumieni ofisi. Mara zote Polisi hawatungi sheria, Polisi wanasimamia sheria na pale ambapo sheria sisi wenyewe ndiyo tumepitisha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wala tusiwalaumu Polisi na kama tunaona zina kasoro basi tuzirekebishe ili wao wasimamie kwa urahisi bila kupata shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukaa kwenye Wizara hii nimekuja kuona kwamba lawama nyingi sana wanazopelekewa polisi hazitokani na polisi wenyewe. Kwa mfano, hata mambo haya yanayoongelewa sana ya kubambika kesi, mimi naweza nikawambia kwa kiwango kikubwa kesi za kubambikwa hazibambikwi na polisi ila wananchi wenyewe kwa kuhasimiana ndiyo wanaobambikiana kesi hizo. *(Makofi)*

Kuna Wilaya niliendа, tulijaribisha hata kufanya kura ya maoni, tulifanya kura ya maoni ya wazi ya kutafuta wahalifu; ili muweze kuona makundi yanayohasimiana yanavyoweza kubambikiana kesi. Baada ya kura ya maoni ile kupigwa kutafuta wahalifu wa CCM wote waliandika wahalifu ni wale wa CHADEMA, halafu wale wa CHADEMA waliandika wahalifu wote ni wale wa CCM. Leo hii ukienda Pemba ukiitisha kura ya maoni kutafuta wahalifu itakuja kwa muundo huo huo; na hata ukienda kwenye kesi nyingine kubwa, ndiyo maana wakati mwingine uchunguzi unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukakuta msikiti ambao hauna ugomvi, umetulia kabisa ibada zinaenda vizuri hamna kesi ya ugaidi, ukienda kwa wale waliogombana zinatokea kesi za ugaidi. Sasa polisi ambaye hasali pale amejuaje huyu ana kasoro hii na hii? Wengine ni wacha Mungu tu wanatumia muda mwingi sana kutimiza ibada zile lakini ndiyo hivyo kwa sababu ya maslahi mengine ya kiuongozi wala siyo ya kiibada yanatokea hivyo.

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunaongelea mambo ya polisi tuweke akiba tukizingatia kwamba wao wanatimiza sheria, lakini pia taarifa nyingi wanazozitumia kuchukua hatua zinatoka kwa wananchi na tukishalijua hilo tutawasaidia waweze kutimiza wajibu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokutana na ma-*RPC* niliwaambia wasitumie taarifa za mahasimu

wanaohasimiana kuwa ndiyo taarifa pekee za kujenga hoja katika kuandaa mashitaka hayo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Tutaendelea kulifanyia kazi, lakini makundi yanayohasimiana hayajengi hoja ya kuweza kujitosheleza. Hatutapuuza kitu lakini ile siyo njia pekee ya kuweza kujengea hoja na kumtia mtu hatiani. Hata tu ukimuuliza Ndassa kwenye michezo ni nani wanaocheza rafu yeye atakutajia wale tu anaohasimiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye hoja moja moja, nikianza na zile zilizotolewa kwenye Kamati. Serikali imepokea ushauri wa Kamati na utazingatiwa; na kama ambavyo tumekuwa tukifanyia kazi na tutaendelea kushauriana nanyi kuweza kuhakikisha kwamba yale yaliyotolewa na Kamati tunayafanyia kazi na majawabu yake mnayaona.

Kwa upande wa Zimamoto, hoja iliyotolea na Mheshimiwa Mkuchika tumeipokea, lakini si kwamba hatukuweka uzito, tuna mipango ambayo inaenda sambamba na hii ambayo imeonekena kwenye bajeti. Bajeti kubwa ya Serikali kuu itakapokuja itakuwa na dirisha ambalo Serikali inategemea kukopa fedha; na sisi tumeshafanya mazungumzo kama nilivyosema na wenzetu wa Ubelgiji pamoja na Australia ambapo tunategemea kupata zaidi ya *Euro* 22,000 kwa ajili ya manunuzi ya magari ya zimamoto na uokoaji. Kwa hiyo, pamoja na bajeti iliyotengwa, kuna njia zingine ambazo zinaenda sambamba ambazo ndizo tunategemea zituongezee nguvu za kupata magari hayo ambayo tunayahitaji.

Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia kwenye upande wa zimamoto, Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda pamoja na Mheshimiwa Japhet Hasunga

tumepokea hoja zenu, hoja zenu ni za msingi na niwahakikishie kwamba Serikali inazifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja zingine za mtu mmoja mmoja zilizotolewa, zimetoka hoja za masuala ya umeme aliyotoa Mheshimiwa Lucy, kuna hoja ilitolewa na Mheshimiwa Mtumwa kwa ajili ya kituo cha polisi, Mheshimiwa Raza na ndugu yangu Kangi Lugola; tumeyapokea na katika bajeti hii ni moja ya mambo ambayo tumeyazingatia sana haya yanayohusu maslahi ya askari wetu pamoja na haya ya vituo vya polisi na masuala ya umeme kama ambavyo Mheshimiwa Kiwelu aliulizia pamoja na Mheshimiwa Kangi Lugola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetolea ufafanuzi zaidi na tutawapa kwa maandishi kwa namba na kwa maelezo jinsi mafunzo ambavyo yameweza kufanyika kwa vikosi vyetu vyote ambavyo viko ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Jambo lingine ambalo liliongelewa ni lile linalohusu *package* kwa vikosi vingine vilivyosalia. Ameisema kwa kirefu Mheshimiwa Gekul na mara kwa mara amekuwa akiisemea Mheshimiwa Esther Matiko pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa.

Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ilikuwa ni utaratibu wa utoaji wa fedha kwa vipaumbele, haikuwa kuweka madaraja, ilikuwa ni utaratibu wa utoaji wa fedha kufuatana na upatikanaji wa fedha na mahitaji kwa sekta nzima kwa maeneo yote katika nchi yetu. Kwa mfano, fedha zinapopatikana kipaumbele cha kwanza kinakuwa ni mishahara ya watumishi wote kwa ujumla wao, ukishatoka hapo kunakuwepo na suala la Deni la Taifa na ukishatoka hapo kunakuwepo na mafungu madogo madogo kulingana na bakaa inayosalia.

Kwa hiyo, kwa utaratibu ule, ili na shughuli zingine ziweze kuendelea ilionekana ni vyema tuanze na kikosi kimoja kimoja kwa maana ya taasisi moja moja zilizoko kwenye

vikosi, hivyo ndivyo ilivyotokea wakapata wa kwanza wakaja wakapata Polisi na kwa sasa tunavyoongea mwezi huu watapata Magereza na baada ya hapo watapata na wengine. Niwatoe hofu jambo hili kila askari ana fedha yake; kwa hiyo hakuna wa kusema huyu aliyechelewa labda atakuwa amekosa, watapata kama wenzao waliokuwa wamepata na watapata *arrears* zao kama ambavyo ilitakiwa waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la Magereza alilisemea nadhani na mmoja wa wachangiaji kwamba nitembelee Magereza. Mimi nimeshatembelea Magereza mengi sana, yamebaki machache sana ambako sijaenda, na kote nilikopita nimeziona hizo hali zote. Ndiyo maana tunapotengeneza utaratibu wa utekelezaji wa mpango wetu tunazingatia yale ambayo tumeyakuta katika hali halisi za Magereza yale. Hata lile la Hanang nilifika na nimeona ujenzi ambao ulishaendelea lakini halijaanza kutumika kwa sababu sehemu ya jengo la utawala lilikuwa bado halijakamilika, na hicho ndicho ambacho tunaweka uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaitambua hiyo hoja ya kwamba mahabusu wanakuwa hawaendi kusikiliza kesi zao kwa sababu kwanza, panakosekana magari, lakini pili wakati mwingine mafuta yanakosekana; pia na ule umbali unasababisha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mary Nagu amelisema sana na amelililia sana na hata alishachangia sehemu ya ukamilishaji wa jengo hilo na mimi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tunatoa vipaumbele kwenye maeneo hayo. Hoja yako tumeipokea, kwamba watu hawa wanakosa haki zao, lakini niseme kwamba ni jambo ambalo tulishalipokea na mimi nilishafika katika ene hilo, na hiyo hoja ya kutokutumia angalau yale majengo ambayo yalishajengwa nilishaiona na niwahakikishie kwamba tutalipa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye maoni ya Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani; Mheshimiwa Lema ameulizia kwa nini Jeshi la Polisi linazuia mikusanyiko ya kisiasa

kwa sababu za kiintelijensia. Jeshi la Polisi halizuii mikutano ya kisiasa iwapo muhusika atafuata taratibu na kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge nilishalielezea kwenye *briefing* na nilishaelezea siku nilipokuwa najibu maswali hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baadhi yenu mmoja mmoja tulishaongea, kwenye hili la mikutano ya hadhara hatujataka utaratibu ambao uko duniani kote ila tumetaka utaratibu wa kimazoea na kwa sababu tunabeba utaratibu wa kimazoea tunasababisha jambo zima lionekane liko tofauti. Utaratibu uliopo kama taasisi zile za vyama vya siasa zingekuwa zinaangalia hata mataifa mengine yanafanyaje kile ambacho kingekuwa kinadaiwa hakikupaswa kiwe hiki ambacho kinadaiwa kwa sasa hivi. Kwa sababu hiki ambacho kinatokea ndiyo *common practice* katika mataifa yote ambako tunajifunza demokrasia ya vyama vingi. Naiunga mkono hiyo kwa sehemu hiyo ya kuhakikisha kwamba kila mtu kwenye anuani yake aende akafanye shughuli zake za kazi za watu wake ambako wanaweza wakamhoji na akafanya kazi za kwake za kisiasa.

Kwa maana hiyo kama jambo hili lingekuwa linajadiliwa kwa sehemu ya wale ambao jukumu lake si sehemu ile aliyochaguliwa ile ingekuwa ni mada nyingine, lakini ule utaratibu uliokuwa unatumika wa kiholela hata Watanzania wenyewe walikuwa hawaridhiki nao na ni utaratibu ambao umewagharimu sana Watanzania katika baadhi ya maeneo na ninyi ni mashahidi. Hata hivyo utaratibu huu ambao umekuwa ukitumika katika maeneo mengine umesababisha mpaka vifo. Kwa maana hiyo hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais alilitolea dira, ndio utaratibu ambao na maeneo mengine unatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Lema alisema kwa nini Jeshi la Polisi linafanya kazi ya kukusanya mapato na tozo wakati hiyo ni kazi ya *TRA.* Tuna mapato ambayo yanakusanywa na *TRA,* lakini vile vile kuna sehemu ya mapato ya Serikali yanayojulikana kama maduhuli yanakusanywa na taasisi mbalimbali za Kiserikali kufuatana na *convenience* ya kuweza kukusanya mapato hayo. kwa

mfano mapato kidogo yanayoweza kukusanywa na Jeshi la Polisi ni *convenience* kwamba hawa watu wametapakaa maeneo mengi wanaweza wakaifanya kazi hiyo kwa ufanisi kuliko kutumia *TRA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameelezea suala la Wakili Mwale ambalo amesema kwamba kesi yake imechukua muda mrefu. Niseme tu kwamba nimelipokea na kwa sababu ni eneo ambalo na mimi napanga kuzungukia, ni maeneo ambayo tumekuwa tukizungukia kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ni jambo ambalo tunalipokea, tutafuatilia undani wake tujue imefika wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hata *DPP* amezunguka maeneo tofauti tofauti akiwa na Dkt. Mwakyembe, na wakati mwingine tumezunguka tukiwa wote watatu kama Wizara, kuna baadhi ya maeneo ambayo tuliyatolea ufafanuzi na kuna baadhi ya maeneo ambayo tulichukua hatua kwa watu ambao walikuwa na matatizo ya aina hiyo..

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni hoja ambayo tumeipokea, tutakaa na kaka yangu tulione na tufuatilie, tujue undani wake umefikia wapi; lakini na kile ulichosema kwa huyu tuweze kuangalia na wengine ambao wanaangukia kwenye mkumbo huo ili waweze kupata haki zao na waweze kuendelea na maisha yao, tumeipokea na tutaifanyia kazi. Kwa Wabunge wengine ambao mmepokea hoja za aina hiyo, tunaweza tukapenyezeana lakini na sisi tutazungukia katika maeneo tofauti tofauti ili tuweze kuchukua hatua na watu hawa waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la askari wa usalama barabarani *(traffic)* kupata mafunzo na wengine elimu ya usalama barabarani tumeshalisema na kuna hatua ambazo tumesema tutazichukua ili kuweza kuhakikisha kwamba watu wetu wanaendelea kuwa na mafunzo na wanafanya kazi kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilisemwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwamba Jeshi la Polisi nchini litahakikisha kwamba amani na utulivu vinakuwepo. Hili ni jambo la kipaumbele kwa Wizara yetu na tumesema hata katika haya maeneo ambayo katika siku za hivi karibuni kumetokea na rabsha za hapa na pale, niwahakikishie kwamba kazi inaendelea kwa ufanisi mkubwa sana, kazi inayoendelea ni kubwa sana na kwa sababu ya mazingira ya kiusalama hatusemi mipango tunayoifanya na hatusemi hatua tunazochukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo miwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mnaotokea katika maeneo hayo na maeneo mengine kuweni na uhakika kwamba Serikali iko kazini, Wizara ya Mambo ya Ndani iko kazini, Jeshi la Polisi liko kazini na niwahakikishie kwamba ni suala la muda tu. Wale ambao wameamua kujipima kwenye hilo, mimi niwatangazie kwamba wameshindwa kabla hata hawajaanza na tutashughulika na mmoja mmoja mpaka tutampata wa mwisho anayeshughulika na mambo hayo. Mpaka sasa zoezi hilo linaendelea vizuri na watakuwa wanajihesabu na wengine wanawaona wakiwa huko magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutamvumilia hata mmoja asababishe maisha ya wananchi wetu yawe ya hekaheka. Kwa hiyo, tutashughulika na mmoja mmoja lakini na yoyote yule ambaye atashirikiana na wahalifu na yeye tutamuunganisha na wahalifu. Hatutaruhusu watu wetu washindwe kufanya shughuli za uzalishaji kwa sababu ya watu ambao hawataki amani katika suala la aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja za maandishi, Mheshimiwa Mwikabe alisema askari wana madai mengi ya likizo, safari na kuistaafu. Nilielezea kwenye hotuba, kazi kubwa sana imefanyika ya malipo, na ukiangalia malipo ya madai ndiyo utaona kwamba Magereza hatuwabagui, kwenye madai yale tuliyolipa, Magereza tumewalipa fedha nyingi kulikoa hizi taasisi nyingine ambazo ziko Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, tunatoa tu

vipaumbele vinavyolingana lakini panapotokea pana mtiririko wa fedha ambao hautoshi kuwalipa wote kwa pamoja tunafanya kwa namna hiyo.

Ndugu yangu Mheshimiwa Njalu alisemea kuhusu malalamikoa ya askari kuhusu nyongeza ya mishahara na posho; tumeweka yale mapendekezo niliyoyasoma wakati nawasilisha bajeti leo hii mapema.

Waheshimiwa Wabunge wengine wameelezea kwa kirefu, Mheshimiwa Mponda, Mheshimiwa Mtulia, mama yangu wa Iringa, ndugu yangu Mheshimiwa Kakoso wa Mpanda na ndugu yangu Mheshimiwa Shangazi tumepokea hoja zenu. Hii aliyoisemea Mheshimiwa Kakoso aliisema pia Mheshimiwa Kadutu, ameisema pia ndugu yangu Mheshimiwa Mbogo wa Nsimbo, jambo hilo kwa ngazi ya Serikali tumelipokea kuhusu uamuzi uliofanyika siku zilizopita wa kuwapa uraia ndugu zetu wapendwa wa kutoka Burundi na nchi nyingine, lakini baada ya kuwapa wakaendelea kukaa wamoja katika eneo lao moja ambalo baadhi yao wasiojua vizuri misingi ya nchi yetu, wanatengeneza kanchi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipokea, tunaendelea kujadili kwa ngazi ya Serikali kuangalia utaratibu ni upi mzuri ambao utawafanya baada ya kuwa wameshakuwa Watanzania wasichukue hata kimoja kilicho kibaya kutoka katika Mataifa yao yaliyosababisha hata wakatoka kule walikokuwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumelipokea na baada ya kuwa tumeshamaliza bajeti kwa ngazi ya Serikali tutajadiliana na ninyi tutawahusisha na Kamati tutaihusisha kwa sababu ilishatembelea hata hayo maeneo ili tuweze kuona njia muafaka na ya kudumu ya watu hawa ambao walipata uraia. Kwa sababu hawatakuwa watu wa makazi yenye taswira ya kiukimbizi lakini wakiwa ndani ya nchi. Hivi ilivyo sasa, sheria wanazozitumia wanazitumia ambazo ni

za makazi ilhali walishakuwa raia kwa kupewa uraia. Kwa hiyo, hilo tumelipokea na niwahakikishie kwamba tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Ndugu yangu Mnyika ameongelea kuhusu vituo vya polisi katika Wilaya yake; nilisemee tu kwamba tayari tuna hatua ambazo tunazichukua. Maeneo yale ya mji ni moja ya maeneo ambayo tunaweka vipaumbele kwa sababu uhalifu unapotokea katikati ya Jiji unahamia pembeni. Kwa hiyo, hivi tunavyoongea pale Madale kuna kituo kimekamilishwa cha Daraja B, Kiluvya pana kituo kimekamilishwa na Mburahati ambacho ni cha *Class A.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya aina hiyo pia ameisemea Mheshimiwa Bonnah kwa upande wa Segerea; tumeipokea na yenyewe tutaipa uzito unaostahili na baada ya Bunge kuwa limeisha tunategemea kufanya tathmini kujua hayo maeneo ambayo yameshauwa na watu wengi yanastahili kuwa na vituo lakini kwa mazingira yalivyo yanaendelea kutokuwa na vituo na hivyo kusababisha matatizo.

Ndugu yangu Mheshimiwa Dau ametoa hoja yake na ndugu yetu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ametoa na yeye maoni yake kwa maandishi. Mheshimiwa Adadi nikuhakikishie tu kwa kuwa wewe ni *dictionary* inayotusaidia kwenye taasisi hii na kumbukumbu nzuri kwenye taasisi hii, hoja yako ambayo umeitoa tumeipokea. Tunawapongeza sana wananchi wa Muheza kwa kukuchangua kwa kweli umekuwa *dictionary* inayotusaidia katika Wizara yetu, tutaifanyia kazi hoja yako kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida Bakar ulipewa dakika chache sana lakini mambo uliyoyaongea yamekuwa na msingi sana na yatatusaidia sana, tumeyapokea. Ni kweli Jeshi la Polisi katika maeneo ya Pemba wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana na mimi nilishafika huko, tumeyazingatia yote uliyasema, tunayapa uzito. Juu ya hoja yako uliyotoa katika eneo lake itatupa fursa ya kuifanyia kazi na kuwapa faida na maeneo

mengine. Kwa sababu kuna maeneo mengine yanayofanana na huko ulikotolea mfano na mimi nilijionea nilipofika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uhamiaji hoja zilizotolewa zilikuwa ni Serikali iendelee kutekeleza mpango wa kuwarudisha makwao wahamiaji haramu walioko magerezani ili kupunguza gharama za kuwahudumia na kupunguza msongamano. Jambo hili lina matatizo lakini tumeendelea kulijadili. Waheshimiwa Wabunge hata ninyi mtakubaliana nami kwamba lina matatizo. Moja wengi wa wahamiaji haramu tulionao kwenye magereza yetu kimsingi ni wapitaji haramu, kwa sababu wengi wao nia yao huwa si kukaa Tanzania; ndiyo maana unakuta wengine walishapita, wanakaribia kupita wanakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tatizo lake ni kwamba tumeingia kwenye mikataba ya kimataifa ya kutokufanya biashara ya usafirishaji wa binadamu. Kwa hiyo, hilo ambalo linatokea, linatupa shida ya namna ya ku-*facilitate* upitaji wao kwa sababu ya mikataba hiyo kwamba tupo kwenye mstari mwembamba sana wa kuonekana tumewasaidia wapite kwa sababu hawakai kwetu, lakini vilevile kwa wakati ule ule iwe hatujavunja hilo sharti la kuwa tumeshiriki kurahisisha usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa mazingira kama hayo tunajadiliana tuone ipi ni njia muafaka na hili litajadiliwa kwa ngazi ya nchi wanakotoka hawa watu ili kuweze kuonekana ni namna gani ambavyo tunaweza tukalifanya. Lakini sasa hivi Serikali inaendelea na juhudi za kuwaondosha nchini kwa taratibu zilizopo. Zoezi hili limekuwa likitekelezwa punde fedha zinapopatikana kwa sababu linahitaji fedha kuweza kuwasafirisha watu hawa. Kwa hiyo, juhudi hizo za kuwaondoa kwa utaratibu huu ambao hautatufanya tuonekane tumevunja mikataba hiyo na tuonekane ni sehemu ya nchi inayofanya biashara za kusafirisha wanadamu tuwe tumelikwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ilikuwa kwamba Serikali iwezeshe bajeti ya Fungu 93 kwa kufanya makisio ya doria ili kubaini na kuwaondosha wahamiaji haramu, jambo hilo limezingatiwa na bajeti imeongezewa. Lingine ilikuwa kuhusu hati za kusafiria; Serikali ipo katika mpango wa kutoa *passport* mpya za kielektroniki ambapo kwa mujibu wa makubaliano ya Wakuu wa Nchi wa Jumuiya za Afrika Mashariki, *passport* za ki-diplomasia zitakuwa na rangi nyekundu kwa nchi zote za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu yangu Mheshimiwa Hamidu na ndugu yangu Mheshimiwa Zainab waliongelea kuhusu masuala ya Msumbiji na Mtwara. Raia wa Msumbiji wanaoishi katika Mkoa wa Lindi na Mtwara ni wahamiaji walowezi na hivyo kisheria hawana haki ya kupiga kura. Aidha, katika Katiba yetu pamoja na sheria haviruhusu uraia wa nchi mbili, kwa maana hiyo ili kuondoa utata walowezi wote hao wanaoishi bila vibali hawatambuliki. Hata hivyo Serikali inaendelea na zoezi la kuwatambua ili kuweza kuwapatia kibali kinachoitwa *Settled Migrants Spars* ambapo kitawawezesha kisheria kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwa upande wa *NIDA,* alisema kwa kuandika Mheshimiwa Upendo Peneza pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Pondeza. *NIDA* anasema iliandaliwa shilingi bilioni 172 kwa upande wa JKU Zanzibar na Serikali ielezee hili deni litalipwa lini, nimelipokea.

Mheshimwia Mwenyekiti, jambo lingine alilolisema ndugu yangu Jaku, nimuombe wala asishike shilingi, jambo lake tulishalipokea, tumelifanyia kazi kwa kiwango kikubwa. Isipokuwa ni kwamba kiserikali kuna *procedure* ambazo ni lazima zifuatwe hasa mambo yanapokuwa ya kimalipo. Lazima uhakiki ufanyike na uhakiki ukishafanyika kuna taratibu za kuweza kuanza kulipa. Kwa maana hiyo taratibu ambazo zinahusisha fedha pamoja na kuielewa vizuri hoja yake, lakini lazima taratibu zingine za uhakiki ilikuwa ni lazima zifanyike ndipo taratibu hizo za malipo ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuhakikishie kwamba baada ya kuwa taratibu za uhakiki wa malipo, uhalali wa deni zitakapokuywa zimeshafanyika malipo yatafanyika. Yeye nimpongeze kwa kufuatilia kwa umakini na kwa ukaribu hoja zinazohusu wapiga kura wake; na siku akiwa na uchaguzi aniambie tu nitawasemea wapiga kura wake kwamba Jaku anapokuwa Bungeni hana mchezo na akipewa hoja za wapiga kura wake huhakikisha kwamba anazifanyia kazi kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi kama nilivyosema wameandika hoja zao kwa maandishi na hapa tulipo tunazo nyingi sana ambapo ni wengi sana. Kwa mujibu wa kanuni zetu nisingeweza kuwataja mmoja mmoja, lakini niwahakikishie kwamba hoja zenu kwa ujumla wake tumezipokea, tunawashukuru na tunazifanyia kazi na nyingine tutazitolea ufafanuzi kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pia hoja alizotoa Janet Mbene, tutazifanyia kazi na kuhakikisha kwamba tunatoa majibu. Amesemea ndugu yangu Ritta Kabati suala la gereza nililielezea na wakati ule wala asishike shilingi. Huo ndio uamuzi wa Serikali, mapendekezo hayo aliyoyatoa ndicho tutakachofanya na ameyasema. Ameandika ndugu yangu Oliver tutayafanyia kazi yale yote na wengine wote ambao sijataja ambao wako kwenye orodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi wa hoja hizi, naomba kutoa hoja, ahsante sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, naona hoja imeungwa mkono. Katibu tuendelee.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI**:

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* …….................Shs. 12,905,920,800/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Matumizi tunaanza na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, na hapa kuna majina, Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Peter Serukamba, tutaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema na Mheshimiwa John Mnyika. Tuanze na Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ABDALAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi sitaki kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri ila nina swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale upande wa Uhamiaji kuna vijana wetu walipata matatizo kwa sababu ya kugonga viza bila utaratibu na yule mtu aliyekuwa anasababisha, ambaye ni raia wa Burundi lakini ana uraia wa Marekani, Uhamiaji wakamkamata wakampeleka mahakamani na akathibitika ana matatizo. Amehukumiwa kulipa shilingi 2,200,000 na kupiga *PI* ya kutoka nchini, lakini amelipa shilingi 2,200,000 Afisa Upelelezi wenu wa Uhamiaji pale Ilala akamruhusu aendelee na yuko uraiani. Nataka unijibu mtu akipigwa *PI* anarudi mtaani au anaenda kwao alikotoka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Bulembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala hili Mheshimiwa Bulembo aliwahi kunieleza, ninataka tu

nimthibitishie hapa kama nilivyokuwa nimemuahidi kwamba tumelifanyia kazi vya kutosha kabisa. Bahati nzuri kutokana na hizi harakati za maandalizi hapa sikuweza kukutana naye mchana, lakini naomba nitumie fursa hii hapa hapa kumjulisha tu kwamba tumeshakubaliana na Kamishna wa Jenerali wa Uhamiaji baadaye tukae ili tuweze kumaliza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bulembo naomba vuta subira na bahari nzuri hujashika shilingi basi jambo lako limekaa vizuri.

**MHE. ABDALAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema sishiki shilingi, lakini sheria inasema nini? Pamoja na kwamba tutaongea, amepigwa mtu *PI* anarudije uraiani wakati watoto wetu waliogonga viza wameshafukuzwa kazi? Kwa nini tunamuona mtu wa nje ni bora zaidi na ameshavunja sheria lakini watoto wetu wanapata matatizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivi alivyoiweka Mheshimiwa Bulembo ndivyo ilivyo sheria inasema mtu akipigwa *PI* ni *Prohibited Immigrant,* hapaswi kuwa nchini. Kwa hiyo kama hivyo ulivyosema ndivyo nikitoka hapa nitafuatilia nione ili niweze kuchukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida ya shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu *IGP* na Kamishna Jenerali wanafanya kazi nzuri sana. Pale Mpwapwa kuna Gereza la akina mama ambalo limekamilika na ninashukuru sana kwamba Mheshimiwa Waziri anakwenda kulifungua kesho. Hata hivyo swali langu ni kwamba kuna nyumba zilijengwa mwaka 1992 na walijenga Askari Magereza wenyewe. Bahati nzuri wakati Waziri Mkuu akiwa Mheshimiwa John Malecela na Waziri wa Mambo ya Ndani ni Mrema niliomba bati 200 nikasaidiwa, lakini nyumba zile hazijakamilika mpaka sasa. Waziri ananiahidi nini kuhusu kukamilisha nyumba zile za Askari Magereza gereza la Mpwapwa?.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu Lubeleje kwa kufuatilia jitihada hizo. Sisi kama Wizara tunahamasisha sana matumizi ya nguvu kazi tulizonazo katika ujenzi wa nyumba na mabweni ya magereza pamoja na majengo mengine yalioko kwenye taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ambalo amelisemea na lilishafika hatua hiyo tunategemea kuhakikisha panapokuwepo na upatikanaji wa fedha tufanye ukamilishaji wa majengo yote hayo ambayo yalishatumia nguvu kazi ya askari wetu kwa kujitoa, pamoja na wadau wengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje tumelipokea jambo hilo na nikuhakikishie tu kwamba tutatao kipaumbele punde tutakapokuwa tumeshapata fedha kukamilisha majengo hayo ambayo vijana wetu wameshaonesha jitihada hizo pamoja na wadau likiwemo hilo la kwako ambalo umelisemea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje ameridhika, tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri hatonijibu vizuri natarajia kutoa shilingi. Kama kuna tatizo sasa tunalo kubwa ni ajali za barabarani. Kama Taifa hatuwezi kila siku tunaomboleza halafu hatufanyi jambo lolote. Duniani sasa zipo *technologies* za kuhangaika na kupunguza ajali barabarani ambapo huhitaji kwenda chini ya uvungu, magari yote yanapimwa kwa mitambo, inajulikana hili gari haliwezi kutembea unaambiwa gari lisiende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko ajali nyingi zimetokeo kama vile kwa sababu gari lime-*fail break* limeuwa watu, lakini huu ni mwaka wa tisa watu wa Polisi mnajua hamtaki kufaya. Nataka uniambie Mheshimiwa Waziri, nimekusikia umeisema leo kwenye *speech* yako; ni lini sasa tutaitumia *private sector* washindane *competitively?* Kwamba ambaye atakuja na *best technology* tumpe; na Serikali haitatumia

hata shilingi moja, ili tuokoe maisha ya Watanzania hawa ambao wanakufa kila siku Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Serukamba na nimuombe asishike shilingi kwa sababu kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amezungumza katika hotuba yake katika mambo ambayo tutayapa kipaumbele katika kipindi cha mwaka huu ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Baraza la Usalama Barabarani juzi tumekaa na tumeweza kuunda kamati ndogo ya kuangalia utaratibu mpya hata wa kuweza kutoa *stickers* lakini pia na kuweza kuangalia uwezekano kwa maana ya Jeshi la Polisi kwa ujumla wake, wa utaratibu gani utumike ili kuweza kupata wadau sahihi ambao wanaweza wakatoa huduma hii kwa ufanisi. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Serukamba avute subira wakati jambo hili tunajipanga nalo katika mwaka huu wa fedha, tunatarajia kwamba tutakwenda nalo vizuri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana naomba nishike shilingi ili tujadili jambo hili kwa sababu moja tu, Mheshimiwa Waziri anasema kutumia Baraza la Usalama Barabarani.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi, Baraza la Usalama Barabarani wanachofanya wanauza kadi tu, wanauza *sticker* tu hakuna anayekagua magari. Kila mwaka sisi kazi yetu ni kununua *sticker* tu. Sasa kweli unachokwenda kufanya ni kwenda kuuza *sticker* tu wakati Watanzania wanakufa kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Waheshimiwa Wabunge tulijadili ili kama Bunge litoe maelezo kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Cecilia, Mheshimiwa Saada Mkuya na Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bashe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adadi.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bashe!

**MWENYEKITI:** Wanatosha hao kwanza.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Bashe!

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nianze kumuunga mkono mtoa hoja, Mheshimiwa Peter Serukamba juu ya suala zima la mikakati ya Serikali, kuitaka Serikali ituambie namna gani ya kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea wakati Polisi wanafanya *operation* ya leseni *fake* barabarani mbona kuna baadhi ya magari huwezi ukayaona tena? Lakini ile imekuja kama zimamoto tu, wanafanya *operation* ya leseni *fake* tu, aina moja tu ya mkakati wao lakini unakuta magari mengi tu kabisa utasikia yamewekwa pembeni na ajali zinapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ambalo analisema Mheshimiwa Serukamba, kama hatutakaa vizuri, hatutakwenda vizuri bado kila siku tutakuwa tunaendelea kuomboleza. Serikali ituambie hapa wana mkakati gani hasa wa ziada wa kuhakikisha kwamba wanakomesha au kupunguza kama si kumaliza kabisa ajali za barabarani? Kwa sababu ajali za barabarani zinaendelea kupoteza maisha ya watu kuliko baadhi ya magonjwa mengine hapa Tanzania; kila siku ni kuombeleza.

Mheshimiwa Waziri tuambie una mkakati gani wa ziada mbali na leseni *fake* ili tupunguze majanga haya? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSINGWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Kimsingi Serikali haijajipanga vizuri katika kupunguza hizi ajali za barabarani na inasikitisha sana tunajifunza kwa njia ngumu sana. Ukiangalia ajali tokea MV Bukoba inaonekana hakuna somo tulilolipata na hatujachukua hatua zozote za hata kuwa na vyombo vya uokozi. Ni kama vile haya majanga yanavyotokea, hatujui kwamba kuna siku yatatokea na kwamba kuna siku watu watakufa. Tumeona hata watoto juzi wale wa Arusha wamebebwa kwenye gari la Polisi kama mizigo ya kuni, ni kwa sababu hatuna maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja anayoisema Mheshimiwa Serukamba ni hoja ya msingi sana ambayo ni lazima Serikali ituambie ina mkakati gani wa makusudi na ina mpango gani, tuachane na haya mambo ya sticker. Haya mambo ya *sticker* mara nyingi unaweza ukachukua *sticker* yako hata ukiwa nyumbani na gari halijakaguliwa. Ukienda nchi za wenzetu magari huwa yanaenda yanajaribiwa mpaka lionekane kwamba linafaa kutembea barabarani; kitu hicho hapa Tanzania hakipo. Ningeomba Serikali itoe *commitment* ni namna gani na ina mkakati gani wa kuhakikisha magari yanayotembea barabarani yana sifa za kutembea barabarani.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba, lazima Serikali itoe *commitment.* Haya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni majibu ambayo ni biashara kama kawaida.

**MHE. CECILLIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Ukiangalia takwimu kwenye kitabu

cha Waziri inaonyesha kabisa ajali zinazidi kuongezeka. Katika mwaka 2016 ajali zilizosababisha vifo ni 2,840 idadi ya watu waliokufa ni 3,381 majeruhi 9,549. Kwa takwimu hizi sisi kama Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi kwa kweli hatuwezi kuendelea kuona wananchi wetu wanakuwa majeruhi, wanakuwa na vilema na wengine wanakufa wakati wananchi hao wanaolipa kodi wanatakiwa wahudumiwe na Serikali. Ni wakati sasa kuona tunahitaji *commitment* ya Wizara, namna gani wanaenda kukagua haya mabasi au vyombo vyote vya usafiri vinapita barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali yaani mapaka itokee shida ndipo wanaanza kusema. Mheshimiwa Waziri amejibu hapa anasema anafuata agizo la Makamu wa Rais lililotolewa jana baada ya kupoteza idadi kubwa ya Watoto hawa waliofariki juzi.

Kwa nini Serikali inafanya kazi kwa matukio? Itokee shida kwanza ndipo mnaanza kuchukua hatua; kwa nini msichukue hatua mapema kabla ya tatizo hili halijatokea? Kwa hiyo na mimi namuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Serukamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niende kwenye takwimu. Takwimu bado zinaonesha hizi ajali za barabarani zinaongeza idadi ya vifo hapa Tanzania, bado hatuko kwenye usalama zaidi. Kwa mfano, nikiangalia katika *context* ya Zanzibar, nataka kulinganisha na tukio ambalo lilitokea juzi ambalo lilichukua maisha ya wanafunzi, watoto wetu. Kwetu Zanzibar mabasi hususani yale ambayo yanabeba wanafunzi Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, yana-*factor* tatu, kwanza ni mabasi mabovu, mabasi ambayo yametumika, shule zote ambazo zinatoa huduma za usafiri kwa Zanzibar mabasi yake ni mabasi mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni mabasi ambayo yanabeba wanafunzi kupita kiasi. Hatujawahi katika kipindi cha karibuni kupata *incidence* kama ilitokea juzi, ni mbaya, lakini tunaona kila dalili, Mungu apushie mbali; hizi *incidence* zinaweza zikatokea karibuni. Vilevile la tatu, mabasi haya ya wanafunzi yakimaliza kuweka wanafunzi yanafanya biashara ya usafari barabarani.

Kwa hiyo, yote hayo yanaweza yakasababisha kwa namna moja ama nyingine ajali. Kwa hivyo tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze mkakati wa kuangalia kwa ujumla wake kupunguza kabisa idadi ya vifo vinavyotokana na ajli za barabarani, lakini pia kuangalia kwa umakini zaidi huduma za usafiri ambazo zinatolewa na hizi shule zinazotoa huduma hizo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba tuu kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Kwa kweli suala la kuingiza *the private sector* kwenye suala hili ni lamsingi sana, na ndiyo hoja ya Mheshimiwa Serukamba hiyo. Hata hivyo tutasema maneno mengi sana, Jeshi la Polisi kwa ujumla wake linafanya kazi nzuri sana lakini hawana fedha na vitendea kazi. Ni wajibu wa Bunge hili tuwasaidie kupata fedha za kutosha tuzi-*ring fence* fedha hizo, wapate bajeti ya kufanyia kazi. Mazingira ambayo polisi wanafanyia kazi kwa kwa kweli wakati mwingine ni hatarishi sana, lakini kama Serikali, nadhani kwa hoja ya Mheshimiwa Serukamba kwamba tujaribu kushirikisha. Pale ambapo Serikali inashindwa kibajeti basi turuhusu *private sector* isaidie kuwezaa kuleta nini hiyo taaluma au utalamu huo wakuweza kupunguza hizi ajali barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tusiangalie suala la ajli ya watoto iliyotokea huko Karatu, lakini angalia barabarani kila siku, barabara zetu vilevile zina tatizo, ni nyembamba mno. Kunapotokea *heavy trafficking* ajali zinakuwa za mara kwa mara. Tutalaumu madereva,

tutalaumu vyombo vya usafiri lakini tunahaja ya kuangalia suala hili kwa upana zaidi, ahsante sana.

**MHE. BALOZI ADADI M. BALOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Ni hoja ya msingi sana tukichukulia maanani ajali ambazo zinaendelea kutokea kwenye hii nchi sasa hivi. Suala la kushirikisha sekta binafsi ni suala muhimu sana. Serikali haiwezi kufanya mambo yote, haiwezi kuwa na hela zote za kufanya mambo. Sasa hivi tunataka kutengeneza jeshi la kisasa, lakini bila kushirikisha sekta binafsi hatuwezi. Sasa hivi barabara zetu ni mbovu sana, sasa hivi kuna vyombo vya kisasa ambavyo vinaweza vikatumika kama tunavyoona kwenye nchi za wenzetu kwamba zina-*control speed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufanya hivyo kwa vyote, ni lazima sasa ufike wakati ambapo sekta binafsi zinahitajika zihusishe. Sekta binafsi zitengeneze hizi barabara, sekta binafsi zilete vyombo vya kisasa ambavyo vinaweza ku-*control speed.* Kama tukisema Serikali kwa Serikali haiwezi kufika hiyo, tutakaa miaka na miaka. Sasa hivi tumekuwa na suala la *CCTV cameras* hapa imekuwa ni gumzo tu, kila siku inazungumzwa *CCTV cameras* zitawekwa.

Kwa hiyo, mimi nasema Mheshimiwa Waziri lazima aonyeshe *commitment* sasa hivi, kwamba kweli sasa hivi watakuwa tayari kuhusisha sekta binafsi kuweza kuleta maendeleo kwenye haya majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mabadiliko tumeleta mapendekezo, Kamati imeleta mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani lakini mpaka sasa hivi Sheria hiyo haijaletwa hapa. Nimeshaongea na Waziri, nimeshaongea na *Attorney General,* na hiki ni kitu muhimu. Hawa wanafunzi ambao wamefari naamini kabisa kwamba wangekuwa wamefunga mikanda si ajabu baadhi yao wengi wangekuwa hai mpaka leo.

Sasa Mheshimiwa Waziri, kwanza tunataka hiyo *commitment* na pili u-*commit* kwamba hayo mapendekezo

ya Sheria ya Usalama Barabarani ambayo yako kwenye *pipeline* yataletwa kabla Bunge hili halijamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja au Naibu Waziri, Wajumbe wanataka mkakati wa Serikali

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi maelezo yangu ambayo nimeyatoa mwanzo hayana tofauti sana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nadhani sikuwa nimeeleweka vizuri tu. Nilichokisema, kwamba kwanza kuna vitu viwili vinachanganywa hapa, Baraza la Usalama Barabarani limetambua kwamba utaratibu wa *stickers* kama njia ya ukaguzi haukidhi mahitaji yetu, hauko sawa, hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunakiri, mimi binafsi nilifanya ziara ya ghafla kwenye baadhi ya vituo vya mabasi kikiwemo Ubungo, Kibaha na nikagundua kwamba kuna mapungufu vilevile ya ukaguzi kwa sababu jeshi la polisi lenyewe linazidiwa. Kwa hiyo, katika haya mambo mawili hatujatofautiana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekit, tulichotofautiana ambacho mimi nimekieleza sijaeleweka vizuri, nimesema kwamba Baraza la Usalama Barabarani kama chombo ambacho kina dhamana baada ya kubaini mapungufu hayo kimeandaa kamati ambayo inafuatilia kwa kina ili iweze kushauri utaratibu muafaka wa kuweza kuchukua ikiwemo hizo hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumza za kushirikisha sekta binafsi. Si kwamba tumepinga kwamba utaratibu uliopo una mapungufu na ndiyo maana nikasema katika mkakati wetu wa miezi sita, nashangaa kwamba Waheshimiwa Wabunge wanazungumzia takwimu za kuongezeka kwa ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotoba yake amezungumza ajali zimepungua kwa asilima

7.2 na katika mkakati ambao tumeufanya wa miezi sita nimeeleza, nimechambua takwimu ambazo zimeonyesha upungufu wa ajali kwa kiwango kikubwa sasa hizi namba nyingi sijui zimepatikana wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nilichotaka kusema ni kwamba nilichokizungumza ni kwamba kwa kutambua mapungufu hayo katika eneo hili, baada ya kutekeleza mikakati yetu ya kuchambua ndiyo maana sasa Baraza linakaa ili tushauri namna bora ya kuweza kuondoka nalo na kwa kuzingatia na maoni ya Waheshimiwa Wabunge basi nadhani tutakuwa tumefikia mahala pazuri zaidi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi, labda Waziri angesimama angetoa *commitment*, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri anapiga siasa tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongea jioni hii, basi la Ally's likitokea Mwanza kwenda Tabora limepata ajali watu 26 wako mahututi. Tutaacha watu wanakufa mpaka lini tunakuja kurekodi tu? Tunachosema ili gari itembee barabarani tujiridhishe *technicaly* kama iko sahihi, kwa sababu magari mengine limekaa miaka 25 bado liko barabarani na linabeba watu. Wanao kufa hawa jamani ni ndugu zetu, unakuja tu unasema tutaangalia, tutaunda kamati.

Mimi naomba Mheshimiwa Waziri simama toa *commitment,* nendeni mkafanye kazi, mhakikishe tunawashirikisha sekta binafsi ili kuanza kukagua haya magari *road worthiness* yake, lakini tunakaa hapa tunasema tunaunda kamati, mimi naomba hiyo *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hamna namna tunaweza tukatofautiana na Waheshimiwa Wabunge kwenye jambo zito la aina hii, kwa sababu halihitaji utafiti kujua kwamba watu wetu

wanapotea sana kwenye ajali. Wizara imechukua jitihada nyingi sana na sababu ambazo zimekuwa zikisababisha ajali mojawapo ni mwendo kasi, nyingine ni uzembe, nyingine ni miundombinu lakini mojawapo kubwa ndiyo hii anayoisema Mheshimiwa Serukamba. Kwa hiyo hatuwezi tukabishana, sisi kama Serikali hatuwezi tukabishana kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na Waheshimiwa Wabunge wametoa na *way out* (mapendekezo) kwamba kama Serikali haiwezi ikawa na fedha za kufanya mradi huo mkubwa basi itumie hata *private sector* na kwa njia ambayo iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba tumelipokea jambo hilo na tutatumia timu ambayo kwenye kikao walishaitengeneza, tutatumia timu yetu ya wataalam ya *cooperation soul.* Halafu tuende kwenye mchakato wa kuweza kupata wazo zima na kwenda kwenye utaratibu wa utekelezaji kwa maana ya kupata watu wa kutengeneza mradi huo ambao utatuhakikishia magari yote mabovu yanaondoka barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Serukamba hoja yako hiyo, hata Watanzania tu wakisikia tumebishana kwa zaidi ya dakika tano kwamba umetoa wazo ambalo litaondoa magari yanayosababisha ajali halafu sisi tukakataa hawatatuelewa vizuri. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunakubaliana kwamba ni tatizo, lakini la pili tunakubaliana na mapendekezo hayo ya kuanza hizo hatua kwa hilo lililopo tu alichokuwa anakisemea Naibu Waziri ni utaratibu tu wakwenda kwenye mchakato huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *commitment* ya Serikali kwamba tunapokea jambo hilo na katika mwaka wa fedha huu, huu baada ya kuwa tumemaliza maswala ya bajeti tutaenda kwenye utaratibu wa kuweza kutekeleza mapendekezo hayo. Na kwa sababu Bunge lako Tukufu lina kawaida ya kukutana tutaendelea kuwapa taarifa Kamati kwa bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati naye ametoa hayo maoni.

Kwa hiyo, tutaendelea kutoa hizo taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa mapendekezo haya yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa maana hiyo kwa uzito wa jambo hili nimuombe Mheshimiwa Serukamba wala asitoe shilingi kwa sababu hatupaswi kubishana kwenye jambo hili ambalo linagharimu maisha ya ndugu zetu, tunapaswa kukubaliana ili kuondokana na tatizo hilo ili watu wetu waweze kuishi, watu wetu wanataka kuishi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri amepokea *commitment,* kwa hiyo tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa sana la ubambikwaji wa kesi, lakini wakati Mheshimiwa Waziri anajibu alisema kwamba kesi nyingi ambazo amezifanyia utafiti inaonekana ni kesi kati ya mahasimu na mahasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba asilimia 70 ya watu walioko magereza, mahabusu ama wafugwa ni watu ambao wamebambikiwa kesi na ndiyo sababu katika hoja yangu ya hotuba yangu nilielezea Ofisi ya *DPP* kama chanzo, nikaelezea kukosekana kwa fedha kwa ajili ya upelelezi ndani ya Jeshi la Polisi kama chanzo. Vilevile nikaelezea kama makosa ya jinai ambayo hayana dhamana yamekuwa chanzo kikubwa. Pamoja na hayo lakini hata viongozi wa kisiasa, Wabunge wamekuwa wakidhalilishwa, wakibambikiwa kesi, wakifanyiwa kila dhihaka. Sasa nataka kusikia na kufahamu kutoka kwa Waziri ni nini kinafanyika ili kuepusha mambo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukienda hata polisi leo mtu anakaa l*ock-up* mpaka siku 60 siku 40. Mimi ni Mbunge nilipelekwa mahakamani baada ya kuwa nimeenda ku-*apply habeas corpus.* Kuna watu niliwakuta wapo kituo cha polisi zaidi ya siku 40, *police bail* haifanyi kazi tena siku hizi. Polisi watakukamata, hata kama kosa linahitaji dhamana kwenye kituo cha polisi watakupeleka mahakamani ukapatie dhamana mahakamani, kesi

ambayo kimsingi ama kosa ambalo kimsingi lingeweza kuwa na *access ya police bail.* Naomba sasa Waziri atupe maelezo ni jitihada gani zinafanyika na Serikali dhidi ya polisi wanaobambikia watu kesi na dhidi ya mambo ambayo nimeyasema hapa? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimetoka kulifafanua kwa kirefu. Kama nilivyosema, kwanza hatuwezi tukakataa kwamba kuna watu ambao wana makosa, watu walioko kule kuna watu wana makosa na ni wengi tu. Kwa bahati nzuri watu wetu wakikaa gerezani wengi huwa wanabadilika na kuwa wakweli, huwa wanasema ukweli. Mimi nilivyozungukia magerezani kuna wakati unawainua watu kwa nyakati tofauti tofauti unamuuliza, wengi wanakiri kwamba hili nilifanya, hili nilifanya katuombee tu msamaha kwa Mheshimiwa Rais, wapo waliofanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili ambalo la inapotokea kwamba mtu amebambikwa kesi, kwa upande wa Jeshi la Polisi Waheshimiwa Wabunge mimi ni wahakikishie kwamba nilipofika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nimejua taasisi zetu hizi za vyombo ni moja ya taasisi ambazo zinafanya kazi kwa nidhamu kubwa sana na hata uchukuaji wa hatua hawacheleweshi. Kwa mfano, ikidhihirika askari amefanya kosa wanachukua hatua hata kabla ya kuwa imefika kwa Waziri, ni taasisi ambazo ziko *well structured.* Hivi tunavyoongea kwa wale waliodhihirika kwamba wamefanya makosa, nimetoa kwenye takwimu, utaona kwamba pale ni zaidi ya 20 walichukuliwa hatua na ni katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha huu tunaoongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hapo tu hata maeneo mengine wana adhabu za kwao ambazo na wenyewe wanaweka hatua za kuonyana, hizo hata hatuziandiki kwa mfano akifanya jambo ambalo si kubwa sana lakini ni kosa la kimaadili ambalo wamejiwekea kwenye taratibu zao na wenyewe huwa wanapeana maonyo. Kuna wakati mwingine wanawekwa *lockup*, kuna wakati mwingine

wanashushwa vyeo, kuna wakati mwingine anyimwa *privilege* zikiwepo za kwenda kusoma, zipo na adhabu na zingine ambazo hata hatujaziandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo mimi nilichukue hilo kwa sababu pia hatuwezi tukakataa, kwamba kuna watu wanaobambikwa kesi, nilichukue hilo na niweke *commitment* kama nilivyosema kwamba tutashirikiana na kaka yangu wa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria kama ambavyo katika kipindi kilichopita tulizungukia tukawasikiliza kwa pamoja, huku tukiwa na *DPP* tuliweza kutoa uamuzi kwa watu wengine walikuwa watoto walioko chini ya miaka 18 tukachukua uamuzi kwa watu ambao umeelezea mazingira kama hayo. Ni wajibu wetu, ni jukumu letu, kama kitu *seriously* ambacho ni *concern* ya Waheshimiwa Wabunge na sisi tutoe kama *commitment* kwamba baada ya shughuli za Bunge tutaendelea kuzungukia maeneo kwa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si kuzungukia tu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia wamekuwa wakielekezwa na Waziri mwenye dhamana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasikiliza wale watu, kuzungukia kwa sababu wako kwenye kila kanda. Waziri kufika kila eneo inaweza ikachukua muda mrefu zaidi wako kila kanda kuweza kuhakikisha kwamba wanawasikiliza na kila mmoja anaandika kwamba suala lake lilikuwaje ili liweze kuchukuliwa kama *issue specific* kuweza kuchukua hatua inayostahili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lema na kwa kuwa hiki unachokisema umeshuhudia sina haja ya kubishana na wewe hata mimi umeshanipa dondoo tutalifanyia kazi kwa hizi tasisi nilizosema ikiwepo Wizara ya Katiba na Sheria, *DPP* pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) naongeza muda wa nusu saa. Mheshimiwa Lema tuendelee.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi namuona Mheshimiwa Waziri anajaribu wakati mwingine kusema kitu labda hakielewi. Kuna mgogoro

mkubwa sana kati ya Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mgogoro ambao hata Mheshimiwa Rais aliutaja siku ya sheria.

Kwa mujibu wa Katiba *AG* hana mamlaka yoyote dhidi ya watu wote wenye mashitaka yanayohusu mienendo ya makosa ya kijinai.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anaponiambia kwamba atawasiliana na Ofisi ya *AG* ili waweke *committement* ya pamoja ya kwenda kuwasaidia watu walioko magereza na walioko mahabusu, mimi naona kama jambo hili si sawa sawa. Watu wanaozea jela, watu wanateswa, wanakaa kwenye vituo vya polisi muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shilingi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kulijadili jambo hili, nashukuru. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Halima, huku upande wa pili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa AG, Mheshimiwa Zitto Kabwe tuanze na hao kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Bashe humtaki?

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri wakati anajibu, lakini nadhani labda Mheshimiwa Waziri maeneo anayoishi ni kule ambako Watanzania wa kawaida hawaishi. Sisi tunaoishi mtaani, Mbagala, kule Temeke, Polisi imekuwa na tabia za kawaida kabisa kila ikifika jioni kupita mtaani kukamata watu na kuwabambikia kesi. Wanawakusanya, wanafika sehemu wanawaambia njooni tuelewane, wanachukua elfu hamsini hamsini wanaondoka. Imekuwa ni tabia ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini alichokisema Mheshimiwa Waziri, kuhusu hizi adhabu zinazotolewa wanaopewa ni polisi wadogo wadogo wa huku chini, tatizo kubwa ambalo Watanzania wanalalamika, wanamlalamikia *DPP* na yule Mwanasheria Mkuu wa Serikali; hawa ndio tatizo. Kuna watu wako Mahabusu zaidi ya miaka mitatu minne hawana dhamana; lakini pia kama Serikali ingekuwa inafanya *performance Audit* kwa *DPP*, mimi naamini *DPP* aliyeko sasa hivi angekuwa ameshaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kesi ngapi *DPP* amepeleka Mahakamani na Serikali imeshindwa? Hapa tu mnashindwa kujua kwamba kesi zaidi ya asilimia 80 au 90, kama mnafanya *performance Audit,* ambazo Serikali mmeshtaki mmeshindwa. Kama mmefikia hivyo, kwa nini hamtaki kujua kwamba hawa watu wanabambikiwa kesi? Kwa hiyo, naunga mkono hoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri hayajaridhisha, tunaomba Mheshimiwa Waziri, asiangalie hizi adhabu wanazopewa hawa ma *WP*, hawa wadogo wadogo wa chini huku. Tatizo liko kule juu na hawa ndio tatizo na yule pale ndiye tatizo lingine namba moja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lema, ambayo ameizungumza katika muktadha wa mambo matatu. Kwanza, amezungumzia suala la kesi za kubambikiwa, pili amezungumzia suala la watu wako Mahabusu kwenye makosa ambayo yanatakiwa kupewa dhamana, lakini tatu amezungumzia watu wako mahabusu kwa muda mrefu kwa kigezo kwamba upelelezi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni jukumu la Serikali. Badala ya kutoa majibu kiujumla walieleze Bunge hili Tukufu, ni lini itaundwa Kamati maalum ambayo itakuwa ina jukumu la kupita magerezani na kwa muda gani kazi hiyo itakamilika na kwa bajeti gani ambayo wanatarajia kuitumia, ili muda huo ukikamilika walete taarifa hapa Bungeni ili Bunge lijue ni

wafungwa gani, mahabusu gani wameachiwa kwa sababu gani na kwa nini pelelezi zinachelewa kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha Mheshimiwa Waziri atujibu kiujumla jumla bila kutoa *commitment* ya Serikali hapa kwenye Bajeti ijayo itashikwa shilingi lakini matatizo ni yale yale. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mwigulu akisimama hapa atuambie kwa uwazi kabisa, hizo Kamati watakazounda ama hiyo Kamati itakayoundwa, itafanya kazi kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wanaumia magerezani, tujiweke kwenye miguu ya familia na wazazi ambao vijana wako magerezani kwa makosa madogo madogo. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba Mwenyekiti utuongoze katika hili; kwa sababu bajeti yake mwenyewe ya kujenga magereza ndio tunaambiwa 40 bilioni bajeti ya Wizara nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna uwezo wa kupanua magereza lakini kwa nini tunaacha kwenye magereza kunakuwa kuna watu ambao makosa yao yanadhaminika? Mheshimiwa Waziri amelia hapa bajeti ndogo Wabunge wanamsaidia kulia bajeti ndogo na tunajua hata kama kuna nyongeza itakuwa finyu, aji-*commit* hapa tupunguze vijana wetu ambao wako kule ndani kwa makosa madogo madogo yasiyokuwa na tija. Aji-*commit* hapa suala la watu ambao wana kesi upelelezi umechelewa ni lini utakamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo ambalo kwanza nimeona ni la kijasiri na kishujaa sana ni

pale Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alipokubali dhahiri shahiri kwamba mambo hayo baadhi yake yapo na kwamba yeye anakubali kuchukua hatua ya kuendelea kufuatilia na kuona yanapewa ufumbuzi kwa kiwango kikubwa. Hilo nimeona ni jambo ambalo ni jema na kubwa sana ambalo hata Mheshimwa Lema, amekiri, si rahisi sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niseme tu kwamba kubambikwa kwa kesi; mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa na nilikuwa naenda sana magerezani, hiyo hali ipo lakini si tu kwa polisi kuwabambikia kesi wananchi, hata wananchi wenyewe hasa wale matajiri, kubambika kesi huo mchezo upo na wanaleta hata mashahidi wa uongo kiasi kwamba hata yule askari anayeandika kesi au Mwanasheria kwa sababu ushahidi unakuwepo lakini ni ushahidi ambao umekuwa na rushwa ndani yake, inakuwa ni ngumu namna hata ya kutatua kesi kama hiyo. Hata hivyo, wakati mwingine ni kweli ni suala la miundombinu yetu; unakuta wakati mwingine magereza yaliko na sehemu za mahakama ni mbali jambo ambalo sasa hivi Serikali imekuwa ikiendelea kutatua. Kwa mfano pale Nkasi hakukuwa na Mahakama, sasa hivi Mahakama imeshaweka na kupunguza adha za usafiri na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, nakiri suala la kukaa gerezani wakati huna hatia, ni jambo linaloumiza. Kwa hiyo sisi Serikali lazima tuungane kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri kufanya mazingira yote ya upatikanaji wa haki, kuwa ni mazuri na wananchi wetu wasipate shida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, suala hili ni zito na Serikali inalipa uzito unaostahili. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ziara atakazozifanya kutembelea magereza na hatua mbalimbali,

si yeye na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapana, ni yeye na Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, mtu yeyote kukaa gerezani au mahabusu kwa muda mrefu bila jambo lake kusikilizwa si jambo linalofurahisha wala kupendeza. Kwa hiyo, Serikali inalichukua suala hili kwa uzito mkubwa kabisa. Hata hivyo, tuzingatie kabisa kwamba mambo haya yanafanywa na binadamu, na wanadam waliozaliwa na mwanamke wana kasoro na zikitokea wanahitaji kusaidiwa na kuhurumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maneno ya maandiko matakatifu wasiokwenda Kanisani hawawezi kuyaelewa. Kwa hiyo zipo sababu ambazo zinazofanya upelelezi uchelewe, uzembe pia upo lazima tukiri, kukosa umakini kupo, lakini pia rushwa ipo, vile vile pia ziko kesi ambazo ni *complex.* Kwa hiyo, nashukuru kwamba Sheria ya *National Prosecution Services Act* nadhani Sheria Namba 27 ya Mwaka 2008yenyewe imeweka utaratibu ambao ni muhimu tukaufanyia kazi kwa umakini sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Case Flow Management Committees* katika ngazi ya wilaya na katika ngazi ya mikoa. Niahidi kwamba baada ya Bunge hili tutaona ni jinsi gani, hizi *Case Flow Management Committees* za wilaya na mikoa zifanye kazi. Hizi zinawajumuisha, wadau mbalimbali ndani ya wilaya ambao ni Mahakama, Polisi, Magereza *State Attorney In Charge, PCCB*, Tanganyika *Law Society,* kama kesi inahusu Idara ya Wanyamapori na kadhalika; ili tuone kamati hizi zifanye kazi ili tupunguze watu kukaa gerezani muda mrefu kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ngazi ya Taifa tunayo *National Criminal Justices Forum* ambayo imeanzishwa na kifungu cha 27 cha Sheria ya *National Prosecution Services Act,* ambayo nayo sasa ina wadau wengi kabisa, tuone jambo hili ambalo limeletwa mbele yetu na Waheshimiwa Wabunge tulipeleke kwenye hii *National*

*Criminal Justices Forum* ya Kitaifa, lijadiliwe, liwekewe mikakati, ili tulitafutie ufumbuzi unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngazi ya Mahakama wamekuwa na utaratibu wa ku- *clear* hizi *backlog of cases* ingawa baadhi yetu humu ndani ya Bunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba umalizie muda umemalizika, naomba umalizie.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kwa hiyo ukiangalia afua zote hizo zitatusaidia katika jambo hili na ningeomba katika jambo hili, badala ya kuwa wagombezi tuwe wagombozi. Kuna tofauti kati ya mgombezi na mgombozi na mimi kwa hili ningependa wote tushirikiane tuwe wagombozi na si wagombezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameyasema hayo vizuri, lakini kuna mambo naomba niyatolee ufafanuzi kidogo. Moja; mnatambua kwamba lipo tatizo la ubambikizaji wa kesi, lakini pia si wote waliopo magerezani au wanaodaiwa kubambikizwa kesi wamebambikizwa kesi, wengine wakishtakiwa tu wanasema wamebambikizwa. Mmoja wa Mawakili wa Serikali ambao wametembelea magerezani sana ni mimi nilipokuwa kwenye *level* hiyo ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kurudi chini, kwa hiyo nataka liwekwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo naweza kusema, ni kwamba Sheria yenyewe ya *National Prosecution Services Act* imeweka utaratibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kila robo mwaka inatembelea magerezani, yaani kila baada ya miezi mitatu twende magerezani na tumekuwa tukienda lakini yaliyoko magerezani, hayawezi utatuzi wake ukamtegemea Ofisa wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali peke yake, ni masuala *crosscutting (mtambuka);* kwa hiyo na hapa na sisi pia tunahusika; lakini pia Waheshimiwa Wabunge nyinyi ni *just of peace* Sheria ya magereza

inawaruhusu kwenda kule magerezani, kwa hiyo naomba tushirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, licha ya kuja kusema hapa Bungeni, mmetumia vizuri haki yenu ya kuyasema haya Bungeni ucheleweshaji upelelezi; lakini pia tunaweza tukawa tunatumia utaratibu wa kawaida una-*draw attention* hiki kitu unakipeleka kwa yule mhusika pale. Kwa mfano Arusha tuna Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale. Kama umewa-*engage* wale lakini hawasaidii, basi mnishirikishe hata mimi basi au mumshirikishe Mkurugenzi wa Mashtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ambalo ningeweza kusema, ni hili la haya madai kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashindwa kila kesi, si ya kweli. Juzi tu hapa Waziri alipokuwa anatoa hotuba yake, ameeleza kesi ngapi zimeshugulikiwa; na ambao mnafahamu na hata jana tu tulipokuwa tunahitimisha ile hoja, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, amezungumza juu ya kesi zilizofunguliwa kuhusu Sheria ya *Cyber Crimes Act* na Sheria nyingine kwamba huko Mahakamani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshinda; zikiwemo na kesi hata hizi za uchaguzi. Kwa hiyo ziko kesi nyingi, lakini masuala ya kushinda kesi hayawezi kutegemea Mwanasheria Mkuu wa Serikali, basi vinginevyo, Mahakama haitakuwa na mamlaka. Mahakama iko pale sasa kila siku tukipeleka kesi tunashinda sasa sisi ndio tumekuwa Mahakama...

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa AG.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kushauri, Mheshimiwa Lema, amefanya kazi nzuri sana kwenye hili suala na Serikali imejieleza vizuri sana, tupeni fursa tukayafanyie kazi haya. Naomba Mheshimiwa Lema arudishe hiyo shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa AG, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana wajumbe waliochangia wameelezea vizuri sana na wametoa ufafanuzi ulio mzuri sana; na kwa maana hiyo hata hiki alichomalizia Mwanasheria Mkuu hata mimi mwenyewe nina mtazamo ule ule. Waheshimiwa Wabunge, ni kipimo cha utawala bora, panapokuwepo na kesi ya mwananchi *against* Serikali na mwananchi akashinda na tena mnatakiwa mpongeze kwa maana hiyo kwamba mwananchi wa kawaida anaweza akapata haki yake, vinginevyo kama kila mwananchi akishakuwa na kesi na Serikali na Serikali inashinda ujue wananchi wale haki zao zitakuwa zinapokwa pokwa sana. Hili ni jambo la kuipongeza Serikali; kwamba pale panapopelekwa mahali kwenye mhimili mwingine unaruhusu mwananchi apate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu alichokisema Mheshimiwa Lema, kama ambavyo wenzangu wameelezea, hayo ni mambo yenye uzito kwa sababu mtu asiye na hatia, kubambikwa kesi ama kukaa mahabusu muda mrefu, kwanza kihaki tu si kitu kizuri, lakini sisi kama Wizara pia na mimi kama Mchumi, ni hasara kubwa sana tunapokuwa na mahabusu wengi, kwa sababu kwanza mahabusu hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunapokuwa na mahabusu ambao hawakuwa na makosa tukawaweka magerezani kukaa na wenye makosa kuna wakati tunaandaa wahalifu wajao, kwa sababu wale ambao wako nao mle, hasa wale wanaojua huenda wasitoke wanawafundisha wale wenye uwezo wa kutoka kwenda kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nilivyoongea na Wakuu wa Polisi wa Mikoa niliwaelezea utaratibu wa kumaliza kesi zile ambazo kiuchunguzi wameona kabisa hazistahili watu kwenda magerezani, ikiwemo na ya watoto wadogo,

pamoja na na watu wenye makosa ambayo kwa kweli yanaweza yakashughulikiwa kwa ngazi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Lema ni Waziri Kivuli na Mheshimiwa Adadi ni *dictionary* kwenye *sector* hii hata yeye tutamkaribisha katika baadhi ya maeneo ambayo ni nyeti tutakapozunguka kama Kamati Kibunge. Mheshimiwa Waziri Kivuli tutamkaribisha na ataona yale ambayo tunayafanyia kazi na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nimhakikishie, katika maeneo ambako tulitembea kwa umoja wetu niliona matokeo yake na matunda yake kuna watu ambao waliweza kupata haki zao ambapo zingepotea kwa kutokufanya hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapopata changamoto au hoja kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge hivi, tunaporudi ofisini tunaelekeza pia wale ambao wanatusaidia waweze kuzingatia haya ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli yakawa na uzito wake. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Lema tumeshalipokea kwa uzito mkubwa, wala asichukue shilingi, *commitment* ya Serikali tunalibeba na tutalifanyia kazi kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godbless Lema, hitimisha hoja yako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli Waziri na Mawaziri wengine wamekuwa *so honest* kwenye jambo hili na mimi shilingi yangu narudisha kwenye *wallet*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lema, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Ally Salehe.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante moja kati ya *core function* za polisi ni kulinda raia, mali zao na wenyewe, lakini kwa bahati mbaya, kule Zanzibar sio raia wote wanaolindwa, ni nusu raia wanalindwa na wengine hawalindwi. Hii inatokana na ukweli kwamba,

kuwa mpinzani Zanzibar ni kama vile tayari wewe una nusu ya hatia. Tangu nije Bungeni hapa, nime-*raise issue* hiyo mara ya nne. Mara ya mwisho niliuliza swali la Mheshimiwa Muhammed Amour na nikamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba nitakuletea watu ambao wamekamatwa, wamefikishwa vituo vya polisi, wameteswa, wamenyanyaswa, wamenajisiwa, tukutane uwanja wa amani, akaniambia kwamba hana taarifa kwamba watu hao wameripoti, kwa hivyo hakuna kile kitu kinaitwa *RB* au *IR* katika vituo vya polisi, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya Muungano, nimeweka orodha na hii hapa nimei-*produce* tena ya watu wote wenye *RB* tulioweza kukusanya, mamia kwa mamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwanza amelidanganya Bunge kusema kwamba hajui kwamba kuna watu wana *RB* wakati mimi hapa ninazo zaidi ya mia mbili hilo la kwanza, lakini pia katika hili Mheshimiwa Waziri amewadhalilisha, amewaonea, amewafedhehesha wale ambao wamenyanyaswa wamekwenda vituo vya polisi hawatambui kabisa kama wapo watu hawa,.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha pili ni kwamba watu hawa wengine; kwa mfano juzi Mheshimiwa Waziri Masauni alisema hapa kwamba viongozi waandamizi wa *CUF* ndio wanaohusika katika kuchoma nyumba ya Kamishna wa Polisi Zanzibar. Kwa taarifa ya Bunge hili ni kweli tukio hili la kukamatwa wao walikamatwa tarehe 16 Machi lakini kilichofanya ni kupelekwa Madema na mpaka leo hata kesi haijafunguliwa. Kwa hivyo, Waziri anathibitisha vipi anaaminisha vipi Bunge kwamba watu hao ndio waliochoma au wamehusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka ni kujua kutoka kwa Serikali au Mheshimiwa Waziri msimamo wa Wizara juu ya jambo hili ambalo tumelipigia kelele kwa muda mrefu sana juu ya watu kuonewa na kwa bahati mbaya wanaoshiriki wanashirikiana pia na vikosi vya Serikali. Picha

zipo, ushahidi upo wa hawa watu wa vikosi vya Serikali kuhusika na polisi wanaohusika.

Kama sikuridhika ile shilingi ya Mheshimiwa Lema nitaitoa mimi sasa, naitoa kwenye *wallet* yake. Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikuombe kama utaridhia Mheshimiwa Ally Saleh atafute muda mimi baada ya kuwa nimeshapitisha bajeti, yeye pamoja na wenzake tukae ili wanipe undani tu wa jambo hili. Nadhani hiyo itakuwa jambo zuri sana. Hata hivyo, nikipata kauli zinahusisha watu kuteswa na hasa hasa yakitokea kwa misingi ya uvyama huwa nasononeka kwa sababu kama ambavyo nilisema wakati najibu; vyama vya siasa katika nchi yetu viko kwa mujibu wa Katiba na viko kwa mujibu wa sheria na mtu kuchagua chama chochote si kosa kwa sababu imeruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vyama vyetu pia si kinga anapotokea mtu amefanya kosa, kama mtu amefanya kosa hawezi akapata kinga ya Chama chake kwa sababu ndio utaratibu wa kisheria. Kwa maana hiyo, kama kuna mambo yametokea ambayo hayahusishi makosa, sisi tutayafanyia kazi, lakini kama mambo yametokea na ni ya kimakosa Waheshimiwa Wabunge sisi ndio tuliotunga sheria, ni lazima sheria ifuate mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira haya anayoyasemea Mheshimiwa Ally Saleh ambayo yana *complexities* mimi nimwombe aridhie pamoja na mdau mwingine tutapata muda tukae, tujadiliane tupate undani wake na sisi kama Serikali tupo kwa ajili ya wananchi, tutachukua hatua ili kuweza kuhakikisha wananchi wanafurahia uwepo wao katika nchi yao. Kwa maana hiyo kwa hili ambalo amelisemea nilipokee lakini aridhie tutafute fursa ofisini tukae tujadiliane jambo la aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kawaida si azma ya Serikali na si jambo la Serikali kuonea watu kwa misingi ya vyama vya siasa, hilo si jambo la Serikali

na Serikali haitafanya hivyo kwa sababu ni Serikali ya chama hiki hiki ndiyo iliyoanzisha vyama vingi. Kama nilivyosema vyama vingi vina faida yake katika nchi yetu na hata ninyi mnavyoona tunavyokaa hapa mnaona faida yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nilipotembelea Pemba niliongea ongea nikawaambia siku nikizungukia huko nitawaambia wananchi wa Zanzibar, nitawaambia Wananchi wa Pemba, kwamba wao wanapokaa kule wanabaguana hata maduka ya kununua bidhaa, wanabaguana kwa misingi ya vyama. Wao kule kwa misingi ya kutuchagua sisi wanapoteza muda kwa sababu sisi wakimaliza kutuchagua jioni ile ile huwa tunakunywa *juice* moja ya baridi moja ya moto tukishangilia wao kutuchagua, sasa kwa nini wao wakae na uadui?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sisi kama viongozi tuendelee kuwaunganisha wananchi na tukishawaunganisha hata hivi vitu vya kushtakiana kwa misingi ya vyama na watu kunyanyaswa kwa misingi ya vyama ambacho chanzo chake kitakuwa kinatokana na wananchi wenyewe vitakuwa vimekwisha.

Mheshimiawa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe ndugu yangu wala asichukue shilingi, aridhie tutatafuta muda na wadau ambao wana taarifa za aina hiyo tukae kiofisi kwa sababu niko kwa ajili ya kushughulikia mambo hayo. Hiyo ndiyo kazi aliyonituma Mheshimiwa Rais kwa niaba yake kufanya ili Serikali iweze kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh umeridhia?

**MHE. ALLY S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhia, *we gave him time, a lot of time*, mimi mwenyewe nimemwambia mara nyingi na amekuwa hasa Mheshimiwa Masauni amekuwa akileta kauli ambazo si nzuri kabisa. Kwa sababu hiyo basi ili Bunge lione kwamba kuna ukubwa wa tatizo, kuna watu wengine hawa-*appreciate* tatizo hili, tukisema wanaona kama tunapiga kelele, kama tunatetea watu wahalifu, hatutetei wahalifu kuna uonevu mkubwa

sana unaofanyika. Kwa hivyo mie nazuia shilingi naomba kutoa hoja ili jambo hili lijadiliwe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, jamani Waheshimiwa kutokana na muda itabidi niwachague wachache sasa maana mnaongea sana, hamfanyi *briefing*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Adadi...

**MHE. MUSSA BAKARI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mussa Mbarouk.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yusuf, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa *AG* wa mwisho.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatosha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda tatizo, tunaomba tuendelee na hao. Tunaanza na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ZITTO Z. KABWE**: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Ally Saleh kwa maelezo ambayo ameyatoa kuhusiana na jambo hili; na linaendana kabisa na jambo la ubambikiaji wa kesi ambalo Mheshimiwa Lema alilizungumza katika hoja yake ambayo aliitoa hapo kabla. Wale ambao wamebambikiwa kesi na wako kwenye magereza au wameteswa wako nyumbani ni rahisi kuwaona na ni rahisi kuweza kuwafuatilia mambo yao na kuweza kuona namna ya kuyatatua, lakini kuna ambao wamebambikiwa kesi wameitwa majambazi, wameuawa haki zao watu wa namna hii zinapatikana namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 mwezi Septemba mwaka jana, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na leo nimerudia kumwandikia kwenye mchango wa maandishi kwa ufupi. Suala la ndugu Ally Kalindo Swai,

ambaye alikamatwa stendi ya ubungo Dar es Salaam ametoka kumsindikiza mkewe anasafiri kwenda Morogoro, amekamatwa tarehe 2 Septemba. Tarehe 3 Septemba akampigia simu mkewe kumwambia nimekamatwa niko kituo cha polisi cha Chang'ombe naomba urudi toka hiyo safari ya Morogoro urudi Dar es Salaam utazame watoto.

Tarehe 4 Septemba *RPC* wa *Dar es Salaam Zonal Police Commander* wa Dar es salaam akatangaza kwamba Polisi wamevamia majambazi wamewaua, miongoni mwa watu waliouawa ni huyu Ally Kalindo Swai. Alikamatwa, polisi walikaa naye na hawakumpeleka mahakamani kama taratibu zinavyotakiwa, lakini akawa *presented* kama ni jambazi ambaye ameuawa pamoja na majambazi wengine, mtu wa namna hii kesi yake...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto muda umemalizika

**MHE. ZITTO Z. KABWE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie, mtu wa namna hii kesi yake...

**MWENYEKITI:** Muda sio rafiki Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ZITTO Z. KABWE**:... kwa hiyo naomba, na nilishapeleka kwa Mheshimiwa Waziri toka Septemba na leo nimemkumbusha, hajalijibu, jambo kama hili lilifanyiwa *enquiry* likachunguzwa; kwa sababu hawa ambao Mheshimiwa Lema aliowasema na Mheshimiwa Ally Saleh amewasema wanaweza wakafidiwa wapo hai, hawa ambao wamekufa kwa kubambikiwa, kesi hali zao zinakuwaje? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa vile muda si rafiki nampa fursa Mheshimiwa Waziri aweze kuhitimisha hapo ili tuingie kwenye kanuni inayohusika. Naomba uwe *brief,* muda si rafiki.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua hiki kitabu cha bajeti ya Mheshimiwa Ally Saleh cha maoni ya upinzani ambacho

ndiyo nilikuwa narekodi sasa hivi yale ambayo alikuwa amezungumza. Kwa wale ambao watakumbuka ukiangalia hiki kitabu hayo ambayo yeye mwenyewe anayaita kwamba ni ushahidi naomba niyasome kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 42 kuna orodha ya watu ambao ameweka hapa, ambao anasema wamemzomea Mheshimiwa Dkt. Shein, Rais wa Zanzibar. Ukiangalia ukurasa wa 55 inasema kuna watu ambao wameshukiwa wamechoma moto nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimwamba Mheshimiwa Ally Saleh kama kuna matukio ya ushahidi tuletee hakuleta, kinyume chake ameleta orodha kwenye kitabu ambayo ni orodha ya watu waliofanya makosa ya kumzomea Mheshimiwa Rais na ya kuchoma moto mikarafuu, sasa watu kama hao unatarajia wafanywe nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na muda naomba ukae, kwa mujibu wa kanuni ya 104 muda si rafiki kwa hiyo tunaingia kwenye *guillotine*.

**MHE: ALLY S. ALLY:** Mwenyekiti bila ku-*conclude* hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh naomba uvumilie tu huu muda si rafiki na nilishatoa nusu saa kwa mujibu wa kanuni ya 104(2) nafunga mjadala tunaendelea na *guillotine*.

**MHE: ALLY S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *no, no, no*, mimi nataka tuunde Tume ya Kibunge...

**FUNGU 51 - WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Kif.1001 – *Administration and HR Mgnt*...Sh. 12,905,920,800/=
Kif.1002 – *Finance and Accounts*...............Sh. 447,182,000/=
Kif.1003 – *Policy and Planning*.......................Sh. 535,840,000/=
Kif.1004 – *Probation and Community Services Div*..............................Sh. 2,671,997,200/=

Kif.1005 – *Government Comm. Unit*..........Sh. 141, 599,000/=
Kif.1006 – *Management Information System Unit*........................ Sh. 223, 269,000/=
Kif.1007 – *Internal Audit Unit*.................... Sh.179,103,000/=
Kif.1008 – *Procurement Mgnt Unit*................Sh. 217,154,000/=
Kif.1009 – *Complaints Division*.................. Sh. 142,075,000/=
Kif.1010 – *Legal Division*..........................Sh. 406, 570,000/=
Kif.4001 – *Refugees Unit*...........................Sh. 697,156,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 14 – JESHI LA ZIMA MOTO NA UOKOAJI**

Kif. 3001 – *Fire and Rescue Service*...........Sh.19,487,640,000/=
Kif. 3002 – *Fire and Rescue Services Training Inst*.............................Sh. 493,511,000/=
Kif. 3003 – *Fire Safety*............................. Sh. 140,000,000/=
Kif. 3004 – *Operations*..........................Sh. 1,177,336,000/=
Kif. 3005 – *Dar es Salaam Regional Office*.....Sh. 667,301,000/=
Kif. 3006 – *Arusha Regional Office*..............Sh. 398,700,000/=
Kif. 3007 – *Dodoma Regional Office*...........Sh. 310, 900,000/=
Kif. 3008 – *Mwanza Regional Office*............Sh. 510,300,000/=
Kif. 3009 – *Mbeya Regional Office*................Sh.233,100,000/=
Kif. 3010 – *Kinondoni Regional Office*...........Sh.485,100,000/=
Kif. 3011 – *Mara Regional Office*................Sh. 242,500,000/=
Kif. 3012 – *Kigoma Regional Office*..............Sh. 213,700,000/=
Kif. 3013 – *Pwani Regional Office*................Sh. 390,100,000/=
Kif. 3014 – *Manyara Regional Office*............Sh. 235,300,000/=
Kif. 3015 – *Geita Regional Office*................ Sh. 181,300,000/=
Kif. 3016 – *Temeke Regional Office*..............Sh. 546,300,000/=
Kif. 3017 – *Singida Regional Office*..............Sh. 220,900,000/=
Kif. 3018 – *Tabora Regional Office*...............Sh. 310,900,000/=
Kif. 3019 – *Iringa Regional Office*.................Sh. 309,800,000/=
Kif. 3020 – *Rukwa Regional Office*...............Sh. 184,900,000/=
Kif. 3021 – *Ruvuma Regional Office*.............Sh. 264,100,000/=
Kif. 3022 – *Kagera Regional Office*.............. Sh. 246,100,000/=
Kif. 3023 – *Mtwara Regional Office*............ Sh. 256,900,000/=
Kif. 3024 – *Lindi Regional Office*................. Sh. 224,500,000/=
Kif. 3025 – *Njombe Regional Office*............ Sh. 184,900,000/=

Kif. 3026 – *Shinyanga Regional Office*..........Sh. 302,100,000/=
Kif. 3027 – *Ilala Regional Office*..................Sh. 542,700,000/=
Kif. 3028 – *Kilimanjaro Regional Office*.........Sh. 350,500,000/=
Kif. 3029 – *Morogoro Regional Office*...........Sh. 354,100,000/=
Kif. 3030 – *Katavi Regional Office*...............Sh. 177,700,000/=
Kif. 3031 – *Tanga Regional Office*...............Sh. 336,100,000/=
Kif. 3032 – *Simiyu Regional Office*...............Sh. 166,900,000/=
Kif. 3033 – *Songwe Regional Office*..............Sh. 138,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 28 - JESHI LA POLISI**

Kif. 1002 – *Finance and Accounting*...........Sh. 1,645,402,000/=
Kif. 2001 – *Police Main force*................Sh. 267,851,438,000/=
Kif. 2002 – *Police Marine*........................Sh. 1,832,469,000/=
Kif. 2003 – *Railway Police division* ............Sh. 1,609,174,000/=
Kif. 2004 – *Police Signals Branch* ............. Sh. 1,944,283,000/=
Kif. 2005 – *Police Zanzibar*..................... Sh. 7,504,448,000/=
Kif. 2006 – *Police Air Wing*..................... Sh. 1,978,666,000/=
Kif. 2007 – *TAZARA Police*......................Sh. 1,920,248,000/=
Kif. 2008 – *Field Force Unit*.....................Sh. 1,583,614,000/=
Kif. 2009 – *Traffic Police*.......................... Sh. 934,298,000/=
Kif. 2010 – *Police Airport*...................... Sh. 2,188,139,000/=
Kif. 2011 – *Police Dog and Horse*............. Sh. 979, 681,000/=
Kif. 2012 – *DSM Special Zone*................. Sh. 8,818,614,000/=
Kif. 2013 – *Police Ilala*..........................Sh. 9,774,738,000/=
Kif. 2014 – *Police Kinondoni*.................. Sh. 10,821,269,000/=
Kif. 2015 – *Police Temeke*.......................Sh. 7,929,513,000/=
Kif. 2016 – *Police Arusha*.......................Sh. 11,893,683,000/=
Kif. 2017 – *Police Iringa*.........................Sh. 7,043,555,000/=
Kif. 2018 – *Police Kilimanjaro*.................Sh. 10,881,888,000/=
Kif 2019 – *Police Kigoma*........................Sh.9, 366,169,000/=
Kif. 2020 – *Police Kagera*..................... Sh. 12,067,516,000/=
Kif. 2021 – *Police Lindi*..........................Sh.6,613,628,000/=
Kif. 2022 – *Police Mwanza*.....................Sh.12,174,212,000/=
Kif. 2023 – *Police Mara*........................ Sh.8,825,794,000/=

Kif. 2024 – *Police Tarime – Rorya*..............Sh.6,119,724,000/=
Kif. 2025 – *Police Mbeya*.....................Sh.11,760,627,000/=
Kif. 2026 – *Police Mtwara*......................Sh.8,944,974,000/=
Kif. 2027 – *Police Morogoro*................ Sh.12, 873,550,000/=
Kif. 2028 – *Police Manyara*................... Sh.8,217,561,000/=
Kif. 2029 – *Police Singida*..................... Sh.8,571,506,000/=
Kif. 2030 – *Police Pwani*....................... Sh.9,284,496,000/=
Kif. 2031 – *Police Ruvuma*.................... Sh.7,276,263,000/=
Kif. 2032 – *Police Rukwa*................ .......Sh.6,057,587,000/=
Kif. 2033 – *Police Shinyanga*............ .......Sh.6,026,438,000/=
Kif. 2034 – *Police Tabora*.......................Sh.7,744,180,000/=
Kif. 2035 – *Police Tanga*.........................Sh.9,345,413,000/=
Kif. 2036 – *Police Mjini Magharibi*......... Sh.12,114,031,000/=
Kif. 2037 – *Police Kusini Unguja*.............. Sh.5,642,672,000/=
Kif. 2038 – *Police Kaskazini Unguja* .......... Sh.4,544,204,000/=
Kif. 2039 – *Police Kusini Pemba*...............Sh.4,111,016,000/=
Kif. 2040 – *Police Kaskazini Pemba*...........Sh.4,183,950,000/=
Kif. 2041 – *Police Dodoma*....................Sh.9,313,995,000/=
Kif. 2042 – *Police Geita*....................... Sh.6,818,219,000/=
Kif. 2043 – *Police Katavi*...................... Sh.4,112,429,000/=
Kif. 2044 – *Police Njombe*.....................Sh. 5,103,458,000/=
Kif. 2045 – *Police Simiyu*.......................Sh.4,711,320,000/=
Kif. 3001 – *Police College Moshi*............ Sh.4,541,923,000/=
Kif. 3002 – *Police College*.................... Sh.1,782,176,000/=
Kif. 4001 – *Police Vehicles*
*Maintenance Unit*. .................Sh.2,878,848,000/=
Kif. 5001 – *Police Medical Unit* ...............Sh.2,015,616,000/=
Kif. 6001 – *Police Building Brigade* ............Sh.2,810,912,000/=
Kif. 7001 – *Criminal Investigation*
*Division*...........................Sh.7,619,771,000/=
Kif. 7002 – *Stock Theft Prevention Unit*..........Sh.506,299,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 29-JESHI LA MAGEREZA**

Kif. 1001 – *Prisons Headquaters*............... Sh.8,180,824,496/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*..............Sh.176, 600,000/=
Kif. 2001 – *Parole Department*................Sh.1,113,887,764/=
Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation*.................. Sh. 157,780,302,712/=
Kif. 2003 – *Resettlement of Offenders*........Sh. 4,743,239,880/=
Kif. 2004 – *Prisons Arusha*.......................Sh. 824,585,828/=
Kif. 2005 – *Prisons Dar es Salaam*........... Sh. 1,949,239,120/=
Kif. 2006 – *Prisons Dodoma*..................... Sh. 787,111,424/=
Kif. 2007 – *Prisons Kigoma*........................ Sh. 442,899,392/=
Kif. 2008 – *Prisons Tanga*......................... Sh. 768,032,432/=
Kif. 2009 – *Prisons Kagera*......................Sh. 614, 477,180/=
Kif. 2010 – *Prisons Mwanza*.........................Sh. 959,448,920/=
Kif. 2011 – *Prisons Tabora*....................... Sh. 615, 127,340/=
Kif. 2012 – *Prisons Mbeya*......................... Sh. 766,676,984/=
Kif. 2013 – *Prisons Singida*...................... Sh. 495, 586,892/=
Kif. 2014 – *Prisons Coast*........................Sh. 788,374,556/=
Kif. 2015 – *Prisons Lindi*.......................... Sh. 570,634,424/=
Kif. 2016 – *Prisons Manyara*...................Sh. 436, 415,504/=
Kif. 2017 – *Prisons Mtwara*....................... Sh. 617,223,272/=
Kif. 2018 – *Prisons Ruvuma*.....................Sh. 483, 430,328/=
Kif. 2019 – *Prisons Rukwa*........................Sh. 592,595,132/=
Kif. 2020 – *Prisons Mara*.........................Sh. 599,379,308/=
Kif. 2021 – *Prisons Iringa*.........................Sh. 577,448,492/=
Kif. 2022 – *Prisons Kilimanjaro*................... Sh. 650, 813,492/=
Kif. 2023 – *Prisons Morogoro*...................Sh. 1,453,202,208/=
Kif. 2024 – *Prisons Geita*........................................Sh. 0/=
Kif. 2025 – *Prisons Katavi*.....................................Sh. 0/=
Kif. 2026 – *Prisons Njombe*...................................Sh. 0/=
Kif. 2027 – *Prisons Simiyu*.....................................Sh. 0/=
Kif. 2028 – *Prisons Shinyanga*...................Sh. 498,734,680/=
Kif. 3001 – *Prisons Staff College*..............Shs. 3,596,000,764/=
Kif. 3002 – *Prisons Driving School*.............. Sh. 595,960,620/=
Kif. 3003 – *Prisons Trade School*..................Sh. 993,569,264/=
Kif. 3004 – *Prisons College Kiwira*..............Sh. 1,835,360,236/=
Kif. 4001 – *Prison Building Brigade*.........Shs. 1,319,178,368/=
Kif. 4002 – *Prison Industries*......................Sh. 625,886,988/=
Kif. 4003 – *Prison farms*.............................Sh. 1,671,355,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 93 - IDARA YA UHAMIAJI

Kif. 2001 – *Immigration Zanzibar*.............Sh. 5,674,844,000/=
Kif. 2002 – *Immigration Head Quarter*.....Sh. 43, 560,858,211/=
Kif. 2003 – *Immigration Ilala*................... ..Sh. 20,609,800/=
Kif. 2004 – *Tz Regional Immigration Training Academy*....................Sh. 136,337,589/=
Kif. 2005 – *Immigration Kinondoni*.......... ....Sh. 24,080,000/=
Kif. 2006 – *Immigration Temeke*..................Sh. 21,840,000/=
Kif. 2007 – *Immigration Arusha*.................. Sh. 33,500,000/=
Kif. 2008 – *Immigration Dar es Salaam*.......... Sh. 24,350,000/=
Kif. 2009 – *Immigration Dodoma*................Sh. 26,400,000/=
Kif. 2010 – *Immigration Geita*.................. ..Sh. 29,190,000/=
Kif. 2011 – *Immigration Iringa*....................Sh. 30,550,000/=
Kif. 2012 – *Immigration Kilimanjaro*.............Sh. 28,600,000/=
Kif. 2013 – *Immigration Kigoma*............. .....Sh. 29,950,000/=
Kif. 2014 – *Immigration Katavi*...................Sh. 39,400,800/=
Kif. 2015 – *Immigration Kagera*..................Sh. 30,570,000/=
Kif. 2016 – *Immigration Lindi*.....................Sh. 27,180,000/=
Kif. 2017 – *Immigration Mwanza*..................Sh. 31,241,750/=
Kif. 2018 – *Immigration Manyara*.................Sh. 26,782,850/=
Kif. 2019 – *Immigration Mbeya*..................Sh. 67,358,000/=
Kif. 2020 – *Immigration Morogoro*...............Sh. 28,700,000/=
Kif. 2021 – *Immigration Mtwara*..................Sh. 31,510,000/=
Kif. 2022 – *Immigration Mara*.....................Sh. 26,995,000/=
Kif. 2023 – *Immigration Njombe*.................Sh. 25,400,000/=
Kif. 2024 – *Immigration Coast*...................Sh. 30,500,000/=
Kif. 2025 – *Immigration Ruvuma*.................Sh. 30,410,000/=
Kif. 2026 – *Immigration Rukwa*...,,,.............Sh. 29,450,000/=
Kif. 2027 – *Immigration Simiyu*....................Sh. 26,310,000/=
Kif. 2028 – *Immigration Singida*..................Sh. 23,800,000/=
Kif. 2029 – *Immigration Shinyanga*...............Sh. 25,420,000/=
Kif. 2030 – *Immigration Tanga*....................Sh. 30,680,000/=
Kif. 2031 – *Immigration Tabora*..................Sh. 27,280,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 14 - IDARA YA ZIMAMOTO

Kif. 3001 *Fire and Rescue Services*.......... Shs. 3,500,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 28 - WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI - POLISI

Kif. 2001 – *Police Main force*......................Sh. 941,123,000/=
Kif. 2005 – *Police Zanzibar*........................Sh. 200,000,000/=
Kif. 2020 – *Police Kagera*.........................Sh. 300,000,000/=
Kif. 2022 – *Police Mwanza*........................Sh. 515,000,000/=
Kif. 2023 – *Police Mara*...........................Sh. 535,000,000/=
Kif. 2026 – *Police Mtwara*........................Sh. 132,500,000/=
Kif. 2041 – *Police Dodoma*...................Sh. 2,100,000,000/=
Kif. 2044 – *Police Njombe*........................Sh. 530,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 29 -JESHI LA MAGEREZA

Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation*..........................Sh. 54,742,000/=
Kif. 4001 – *Prison Building Brigade*............Sh. 5,000,000,000/=
Kif. 4002 – *Prison Industries*.....................Sh. 2,200,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 51 - WIZARA YA MAMBO YA NDANI

Kif.1001 – *Administration and HR Mgnt*...Sh. 20,000,000,000/=
Kif. 4001 – *Refugee Unit*.......................................Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 93 - IDARA YA UHAMIAJI.**

Kif. 2002 – *Immigration Mainland*........... Shs. 4,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Mheshimiwa Waziri Taarifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa na wenzetu wawe wanatoa fursa ya kusikiliza kwa sababu ndo kazi yenyewe ya kuongea na kusikilizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba kutoa taarifa Kamati ya matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, natangaza rasmi kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani yamepitishwa na Bunge hili. Pia nichukue fursa hii kuwapa hongera na pongezi kubwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya ndani kwa

kuweza kupitishiwa Bajeti yao pamoja na timu yao yote ya Watendaji.

Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mbalimbali ambayo mmetoa kwenye hoja ya Wizara hii katika kuchangia katika bajeti hii ya Wizara. Naamini kwamba Serikali itatumia hekima na kuchukua yale ambayo yana tija kwa Taifa na kuyafanyia kazi. Niwaombee heri wote ambao mmechangia mambo mazuri na naiombea Serikali iweze kuyatekeleza hayo kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bada ya kusema hayo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.16 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*